**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA NANE**

**Kikao cha Sita - Tarehe 2 Februari, 2015**

*(Mkutano Ulianza Saa tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:**

Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala Katika Kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari, 2015.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSYA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):**

Taarifa ya Mwaka wa Shughuli za Kamati za Kudumu

ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari, 2015.

**MHE DIANA M. CHILOLO (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MASUALA YA UKIMWI):**

Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI katika kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari, 2015.

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri Samuel Sitta, anakaimu nafasi ya Kiongozi wa Shughuli za Bunge hapa ndani, kwa sababu Kiongozi wa Shughuli za Bunge yuko safari. Nakutakia kazi njema. *(Makofi)*

Na. 53

**Kutunga Sheria ya Kutambua Dodoma Kuwa Makao Makuu ya Nchi**

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE** aliuliza:-

Ibara ya 212 (c), (d) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 inaitaka Serikali kutunga Sheria ya kutambua Mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi, lakini mpaka sasa haijfanya hivyo:-

(a) Je, ni sababu zipi zinazoifanya Serikali ishindwe

kuleta Bungeni Muswada wa Sheria iiyokusudiwa?

(b) Je, ni kwa nini Serikali inaendelea kujenga majengo mapya ya Wizara na Taasisi za Serikali Dar es Salaam?

(c) Je, ni lini Serikali itaandaa na kuweka wazi Ratiba ya Mpangilio wa Wizara na Taasisi za Serikali kuhamia Dodoma kwa awamu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje, Mbunge wa Chilonwa lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika,mchakato wa kuandaa Muswada wa Sheria unapitia katika hatua kadhaa kabla ya kuletwa Bungeni. Baadhi ya hatua hizo ni kuandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri; kupata maoni ya wadau; kupata maoni ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri; kupata maoni ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu *(IMTC);* kupata maamuzi ya Baraza la Mawaziri na hatimaye Muswada unaletwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Waraka wa Baraza la Mawaziri wa kutunga sheria ya kutambua Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi uko katika hatua ya kupata maoni ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri.(b) Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka wa fedha 2010/2011, Serikali ilitoa agizo la

kuzuia ujenzi wa majengo mapya katika Jiji la Dar es Salaam.

Agizo hilo lilitolewa mara baada ya Serikali kupitia Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu kukamilisha kuandaa mapitio ya mpango kabambe wa Mji wa Dodoma ambao umewezesha kutenga eneo maalum lenye ukubwa wa hekta 8,033 kwa ajili ya Mji wa Serikali.

(c) Mheshimiwa Spika, kupitia Sheria ya kutambua Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi inayotarajiwa kutungwa, Serikali itaweka utaratibu mahsusi kupitia kanuni zitakazotungwa na Waziri mwenye dhamana ya Ustawishaji Makao Makuu kwa lengo la kuharakisha na kuwezesha utekelezaji wa sheria ikiwemo ukomo wa muda ambao Serikali itahamia Makao Makuu ya Nchi. *(Makofi)*

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mchakato ambao Serikali umeueleza katika jibu hili si sababu za msingi za kucheleweshauletaji wa Muswada huu kwa miaka mitano tokea agizo lililoko kwenye Ilani ya Uchaguzi. Hata hivyo nataka kuuliza kama ifuatavyo:-

Kwa sababu kero moja kubwa kwa hapa Dodoma ni migongano na mivutano kati ya Manispaa na *CDA* kutokana na kukosekana kwa sheria ambayo inaeleza bayana mpangilio pamoja na majukumu ya uendelezaji wa Mji wa Dodoma.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuharakisha kuleta Muswada wa Sheria hii kabla ya Uchaguzi Mkuu ili kuondokana na kero hiyo ya wananchi wa Dodoma.

La pili, Mheshimiwa Waziri anasema kwamba mpango kabambe wa Mji wa Dodoma sasa

umeshakamilika, lakini tunashuhudia bado mipango ya ujenzi wa majengo ya Wizara za Serikali unaendelea kule Dar es Salaam. Nataka kujua ni Wizara zipi za mwanzo sasa zimepangwa kuanza kujengwa Dodoma baada ya mpango kabambe kukamilika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, sisi wote tuliokaa hapana kwamba tunafanya mkutano huu hapa ni matokeo ya Ilani ambayo imezungumzwa hapa. Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania halikutani Dar es Salaam, linakutana hapa tunataka kuwa *concrete*. Kuwa *concrete* ni kusema Zimbabwe, Tanzania, Kenya. Ukishasema hivyo ni mtaani ndio umekuwa *concrete*. Tunakutana hapa kwa sababu iko azma ya Serikali inayosema kwamba tunataka tuhamie Dodoma na hili analolisukuma hapa Mheshimiwa Chibulunje, mimi nalielewa msingi wake.

Mheshimiwa Spika, Manispaa hii ya Dodoma tunayozungumza hapa ina watu laki tano. Ukisema leo unawaleta watu wote hapa ukisema wanahama Serikali nzima inakuja hapa hesabu laki tano zidisha mara kumi. Nenda kasome *Rio-de-Janeiro* nenda kasome kule Abuja nenda kaangalie Lilongwe walivyofanya kule, nenda Malaysia kote walikofanya kule.

Kwetu sisi tumetumia utaratibu unaoitwa *a step by step approach* kwamba tunakwenda kwa hatua kwa hatua. Kilichofanyika hapa na mimi nataka nisimame hapa kwa niaba ya Serikali ni kuweka miundombinu ambayo itabeba jukumu jipya la kupafanya Makao Makuu ya Serikali hapa Dodoma na kitu hiki kimefanyika. Ame-*quote* hapa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kwamba imetamka kwamba tupeleke Makao Makuu.

Jana mimi nilikuwa nafuatana na watu wangu wa Siha wako hapa na Mwenyekiti wa CCM. Tumetembelea Makao Makuu mapya yanayojengwa pale. Unaiona wazi

wazi kabisa ile dhamira ya kwamba tunataka kuhamia Dodoma. Nataka niseme hapa kwamba ziko Wizara na mimi hapa Mkuu mkiondoka hapa nyie mnakwenda Dar es Salaam mimi siondoki nabaki hapa hapa. Ofisi ya Waziri Mkuu iko hapa inakaa pale na Wabunge wote huwa wanakuja pale.

Kwa hiyo, dhamira ya Serikali ni kwamba inataka kuhamia Dodoma na kwamba inatia mushkeli mimi siioni kwa maoni yangu. Sasa *Referral Hospital* ya Dodoma pale tumeifanya imekuwa *Referral* badala ya kuwa Hospitali ya Mkoa au ya Wilaya na kazi hii imefanyika vizuri.

Kwa maneno mengine sasa tumefika mahali ambapo unaiona nchi kabisa unaweza ukasema sasa tuhamie Dodoma na ndiyo maana nakubaliana na Mheshimiwa Chibulunje kwamba hiki anachokizungumza hapa ni sahihi kwa wakati wake. Nimesema habari za Baraza la Mawaziri, nimesema kuhusu vikao mbalimbali na Miswada hii yote imeshafanyiwa kazi. Sauti hii ni msisitizo tu mama yangu na wala usiwe na wazi wasi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho anasema kwamba kule Dar es Salaa mwako watu bado wanaendelea kujenga mle. Mimi naomba, mimi hapa ni mtumishi wa Bwana anipatie ushahidi, anipatie na majengo hayo. Isije kuwa mtu anajenga tu ka-*research unit* halafu ikaambiwa ndiyo Wizara inajengwa hapo. Kinachozungumzwa hapa ni Makao Makuu na Waziri Mkuu alisema hapa ndani kwamba hakuna tena kujenga majengo mengine kule Dar es Salaam majengo yote yaendelee kujengwa hapa.

Mheshimiwa Spika, mimi nataka niseme hivi tunaipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri ya kusimamia kwa maana yake tumekwenda hatua kwa hatua ili tuweze kufikia pale. Watoto wa shule waweze kupata shule, maji yaweze kupatikana, barabara *ring roads* tayari tumeshazijenga. Mimi kwa sababu niko TAMISEMI najua kinachofanyika. *World Bank* wametusaidia kujenga barabara

hizi ni msongamano ulioko Dar es Salaam hutegemei kwamba utapatikana *flying-overs,* sasa hivi ukaanza kujengwa, tumefika mahali pazuri kwa hiyo tunaweza tukaendelea. *(Makofi)*

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa katika majibu ya Mheshimiwa Waziri imeonyesha kwamba Serikali ina dhamira ya kweli ya kuhamia Dodoma na kama alivyosema Mheshimiwa Waziri *step by step*. Sasa kwa nini Serikali isiandae Bajeti Maalum ya *step by step* ya kuhamia Dodoma ambayo tutaipitisha hapa Bungeni na tuweze kuiratibu kwa ajili ya Serikali kuhamia hapa Dodoma? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa na yeye ameona hiyo hoja ya *step by step* kwamba ni hoja ya msingi.

Mheshimiwa Spika, kwa vile wewe mwenyewe una-*restrict* hapa kutoa majibu mafupi mafupi na mimi naheshimu sana kiti. Ndiyo nitafanya kifupi sana. Kwenye hili nataka niseme kwamba sisi kama Serikali na Kaimu Waziri Mkuu yuko hapa anasikia hilo ni jambo zuri, jambo jema kwa sababu linakwenda katika hili jambo tunalipokea na ushauri huo ni mzuri na tutaufanyia kazi.

**SPIKA:** Huyo anaitwa Kaimu Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Kwa kuwa imeshachukua miaka 43 tangu azimio hili limepita kuhamia Dodoma na kwa sababu mpaka sasa hivi

halijafanikiwa. Je, Serikali haioni sasa umefika wakati wa kufikiria uamuzi huo yaani ku-*review*?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, sasa hapa tuelewane vizuri. Yaani kwenye swali la nyongeza hapa mimi nifanye maamuzi hapa niseme kwa niaba ya Serikali tutafikiria upya kubadilisha hii azma, yaani ananitakia mema kweli hapa Mheshimiwa Akunaay. Niseme hivyo na watu wote na viongozi wote wananisikiliza waseme wewe pale asubuhi ulipoamka ulikuwa unakunywa pombe na mimi situmii pombe.

Mheshimiwa Spika, namwelewa Mheshimiwa Akunaay anachosema. Namuelewa kabisa anachozungumza hapa. Hapa habari ya kwamba tunarudi kule Misri haturudi tunakwenda nchi ya ahadi Dodoma ndiko tunakokwenda. Yaani kwamba tunabadilisha hapa mimi sijui *unless you are imagining of a highly hypothetically developed institution*. Mimi hivi hivi kwamba unaniambia hapa njibu.

Mheshimiwa Spika, ninachosema tu tusikate tamaa kama Mheshimiwa Akunaay kama unavyoeleza kwamba kuna haja ya kuona kwamba tunakaa tunatafakari, kutafakari kwa namna nzuri ya kutufikisha katika kwenda Dodoma. Dodoma hii ilikuwa na mantiki yake umeniambia niseme kwa ufupi. Tulisema hapa ni katikati, tuliposema hapa ni katikati tukasema sasa unafikaje.

Kuna barabara inatoka kule kwako Mheshimiwa Spika, inakuja hapa. Kuna barabara inatoka Singida inakuja hapa, kuna barabara zinatoka Tabora kule kwa Mheshimiwa Sitta nazo zinakuja hapa. Kuna barabara zinatoka Dar es Salaam nazo zinakuja hapa.Usingeweza ukasema twende

Dodoma halafu baadaye hatuwezi tukafika Dodoma wote watatushangaa pale.

Kwa hiyo mimi naomba tuamini kwamba Serikali inaposema inahamia Dodoma *I, for one I convinced* kwamba hii azma itatekelezwa. Kwa hiyo tutasimama hapo. Kwa hiyo tusonge mbele katika kwenda.

**SPIKA:** Kwanza ni vizuri mmechelewa, mngewahi mngejenga vijumba vidogo vidogo kama vilivyopo huko, kumbe dunia haiendi hivyo. Mimi naona hata misongamano ya barabara tumeijua. Kwa hiyo sasa hapa ni kukwepa hayo yote. Mimi nadhani kuchelewa nako kulikuwa na faida. Tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 54

**Mikopo Kwa Wafanyabiashara Walemavu**

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR** aliuliza:-

(a) Je, ni wafanyabiashara walemavu wangapi walipatiwa mikopo kupitia Fedha za Mabilioni ya Kikwete kwa Tanzania Bara na Visiwani toka mfuko huo uanzishwe?

(b) Je, wafanyabiashara hao ni wenye ulemavu gani?

(c) Je, wanatoka sehemu gani na wanafanya biashara gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, naomba nifanye

marekebisho madogo kama ifuatavyo. Noamba *figure* ile iliyo katikati ya *paragraph* ya kwanza inayosomeka na iliyokolezwa *figure* 46.64 isomeke 43.69.

**SPIKA:**Mheshimiwa Waziri kwa sababu sisi hatuna hiyo nakala. Sasa wewe soma ukifika hapo urekebishe kama ulivyotaka.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, baada ya marekebisho hayo kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a), (b) na (c) yote kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa kuwawezesha wananchi kiuchumi maarufu kwa jina la Mabilioni ya JK ulikuwa na madhumuni ya kuwawezesha wananchi kiuchumi na kuongeza ajira kwa wanawake na vijana vijijini na mijini kwa kuwapatia mikopo bila kujali maumbile yao. Chini ya mpango huu, mikopo ilitolewa katika awamu mbili kupitia benki na asasi za kifedha zilizoteuliwa na Serikali baada ya kukidhi vigezo ambapo jumla ya shilingi bilioni 43.96 zilitolewa na kuwanufaisha wajasiriamali 74,593. Kwa upande wa Tanzania Bara, wananchi waliohitaji mikopo hiyo walitakiwa kujaza fomu ambazo hazikuwa na kipengele kinachoainisha iwapo mwombaji ni mtu mwenye ulemavu au siyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na utaratibu huu, imekuwa vigumu kutoa takwimu za watu wenye ulemavu waliopata mikopo, aina ya ulemavu walionao, sehemu wanakotoka na aina ya biashara wanazofanya.

Napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri, na Serikali imelipokea kama changamoto ya kufanyia kazi ambayo itatuchochea kubuni upya utaratibu wa utoaji mikopo hiyo kwa kuzingatia vigezo

vya ziada kwa watu na makundi maalum wakiwemo wenye ulemavu wa viungo.

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba mkopo huu hauna vigezo maalum. Hli inasababisha watu wenye ulemavu wengi sana hasa wanaoishi vijijini kukosa mikopo hii. Kwa sababu si watu wengi wenye ulemavu ambao wanafuatiliwa kule vijijini ili kupata mikopo hii.

Pia Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba wataweka vigezo, nashukuru sana kwamba sasa wataweka vigezo kwa sababu watu wenye ulemavu watawekewa vigezo vyao ili na wao wafaidike na mkopo huu.

Je, Mheshimiwa Waziri ataniambia vigezo hivyo vitaanza lini ili watu wenye Ulemavu waweze kupata huduma hii? Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, nirekebishe kidogo kwamba hakuna vigezo kabisa mikopo iliyotolewa ilikuwa na vigezo kwa sababu ilipita katika mabenki na mabenki nayo yana vigezo vyake kwa hapa ambalo limejitokeza ni kwamba vigezo vile vilikuwa ni vigumu sana na masharti mengi yalikuwa ni magumu haswa kalengwa wakiwemo walemavu.

Kwa hiyo, nilichofikiri hapa ndicho ambacho nimesema kwamba tutakachokifanya sasa hivi ni kurejea vigezo vile azungumze na mabenki na Taasisi zote ambazo

zitashirikiana na sisi ili angalau vigezo vile viwe rahisi kuwezesha walengwa wapate mikopo hii kuliko ilivyotokea kwamba mikopo walioipata walikuwa ni wale wenye uwezo ukidhi vigezo vinavyotakiwa na mabenki. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM S. SALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi ninaomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri swali la nyongeza kwa kuwa mkopo huu wa Mheshimiwa Rais Kikwete na kwa Zanzibar ilikuwa ni kwa Rais Mstaafu Aman Karume, kuna watu walionufaika na mikopo lakini watu hawa hawakurejesha marejesho. Je, Serikali iliwachukulia hatua gani wapate kunufaika na zile pesa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, Zanzibar walipata milioni mia sita (600,000,000/=) na wakaongeza milioni mia sita (600,000,000/=) zikawa bilioni moja na laki mbili. Sasa siyo Zanzibar tu hata Tanzania Bara ziko changamoto ambazo zimejitokeza katika mikopo hii kwanza kuna fedha zingine bado hazijatumika.

Kwa hiyo tunachokifanya sasa Serikali imechukua hatua. Mkaguzi Mkuu wa Ndani amefanya Ukaguzi kuhusu fedha zote zilizotolewa.

Sasa Taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani kwa Tanzania Bara itatumika kujua ni nani alipata mkopo wa fedha na fedha kiasi gani zilizotolewa na ni nani ambaye hajaresha.

Sasa kwa upande wa Zanzibar ninafikiri itabidi hatua kama hiyo hiyo ichukuliwe na Serikali ya Zanzibar ili kujua ni nani hajarejesha hatimaye zichukuliwe hatua za kuwafanya wale ambao hawajaresha warejeshe. Kwa sababu wakirejesha ndiyo mkopo ule unaweza ukazunguka ili na wengine waweze kupata.

Na. 55

**Kukaimu Nafasi ya Mtendaji Kijiji/Mtaa/Kata**

**MHE. PAULINE P. GEKUL** aliuliza:-

(a) Je, pale inapotokea Mtendaji wa Kijiji, Mtaa ua Kata amefariki, kujiuzulu au kuhamishwa Kituo cha kazi ni nani Kisheria anapaswa kukaimu nafasi hiyo?

(b) Je, ni katika siku ngapi nafasi hiyo inatakiwa kujazwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, vyeo vya Maafisa Watendaji wa Vijiji, Mitaa na Kata ni vyeo vya Kimuundo kwa maana ya kuajiriwa inapotokea Mtendaji wa Kijiji au Mtaa au Kata amefariki, kujiuzulu, kustaafu au kuacha kazi. Taratibu za kiutumishi zinamtaka Mkurugenzi wa Halmashauri husika kumteua mtumishi mwingine miongoni mwa Watumishi katika Kata, Kijiji au Mtaa husika ambaye ni mwajiriwa wa Serikali kukaimu nafasi hiyo wakati taratibu za kuajiri Mtendaji wa kudumu zinafanyika.

Aidha, Mkurugenzi anaweza kumchagua Mtendaji Kata au Kijiji au Mtaa ambaye eneo lake la Utawala liko karibu na Kata, Mtaa, Kijiji kukaimu nafasi iliyoachwa wazi. Anayekaimishwa nafasi hiyo ni lazima awe ni Mtumishi wa Umma yaani ameajiriwa na Serikali.

(b)Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa katika sehemu (a) ya jibu hili nafasi iliyoachwa wazi itajazwa kwa kuajiri Mtendaji mwingine. Kwa utaratibu wa sasa Watendaji wa Vijiji na Mtaa wanaajiriwa na Halmashauri zenyewe baada ya kupata kibali kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Aidha, Watendaji wa Kata bado ajira zinafanyika kupitia Sekretarieti ya Ajira iliyoko chini ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Muda ambao utatumika kumwajiri Mtendaji wa Kjiji au Mtaa au Kata utategemea na kukamilika kwa taratibu za ajira ikiwemo kupatikana kwa kibali kutoka Utumishi na uwepo wa fedha katika Bajeti kutekeleza azma hiyo. *(Makofi)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL**: heshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kuwa kuna tatizo kubwa sana katika Halmashauri zetu hususani Halmshauri ya Mji wa Babati, pale ambapo Vyama Vya Upinzani wanashinda katika Mitaa Uenyeviti, Watendaji hao wamekuwa wakihamishwa na kulaumiwa kuwa wao ndiyo wamesababisha hayo wakati ni wananchi wamefanya maamuzi.

Je, Serikali ipo tayari kuongea na Mkurugenzi kuacha kuwasumbua watendaji kwa kuwa ni wananchi ndiyo wanaofanya maamuzi kuwa ni nani awe Mwenyekiti wa Mtaa?

Swali la pili, kwa kuwa baadhi ya Watendaji wanaowahujumu Wenyeviti wa Mtaa wa Vyama Vya Upinzani pale wanaposhinda wakikataa kuandaa mikutano ya Kisheria kila baada ya miezi mitatu. Serikali ina kauli gani kwa Wakurugenzi ambao wamekuwa wakiwalinda hawa Watendaji wanaosumbua Wenyeviti wetu?

Kwa mfano, Mwenyekiti wa Mtaa wa Maiskama pale Babati amekuwa akisumbua kwa muda mrefu Mtendaji huyo

haitishi, hashirikiani na Mwenyekiti wa Mtaa wa Maisaka Kati. Waziri una kauli gani kwa Wakurugenzii wanaowalinda Watendaji hawa wanaowakwamisha Wenyeviti wetu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, Ninaomba kujibu swali la Nyongeza la Mheshimiwa Pauline Phillipo Gekul, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Hii inayozungumzwa hapa ni *allegations* ambazo anazisema Mheshimiwa Mbunge. Anazungumza kwamba inafika mahali Wapinzani wameshinda pale halafu unamwandikia Mtendaji kumhamisha.

Mimi sina rekodi hiyo na wala siifahamu rekodi hiyo na kama ipo au kama kuna ushahidi tuletewe hapa. Mimi ninavyofahamu Mtendaji wa Kijiji au Mtendaji wa Kata anaposimama atasimama katika nafasi yake kufuata Sheria na Kanuni zilizowekwa. *(Makofi)*

Kama kuna *incidence* ambayo Mheshimiwa anaijua ambayo ilipelekea mazingira haya kwa sababu siwezi kum-*dismiss* Mheshimiwa Mbunge hapa tutamwomba atueleze vizuri ili tuweze kushauriana na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini mimi ninasema kwa hapa nilivyo sasa hivi, ninayo rekodi eti umemwondoa Mtendaji kwa sababu Upinzani umeshinda.

Kwa hiyo mwondoe hapana mimi ninafahamu maeneo mengine sana wameshinda Wapinzani na Watendaji wake ni wale wale wameendelea. *(Makofi)*

Kama kumekuwa kuna *coincidence* yaani kumetokea tukio halafu kulikuwa kuna zoezi inawezekana ni kitu cha namna hiyo, lakini siwezi kujua hapa kuwa ni mazingira gani. Kwa hiyo, Mheshimiwa atatusaidia na tutampa ushirikiano unaotosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hili la pili analozungumza iko pale imetamkwa kuwa kila baada ya miezi mitatu uta-*pin on the board* taarifa ya Mapato na Matumizi ya kijiji na utaeleza pale utaiweka pale ili wananchi waende kwenye Mkutano Mkuu wazungumze jambo hili linalozungumzwa hapa. Kwa hiyo yuko *right* kabisa na ndivyo inavyotakiwa.

Sasa kwamba kuna mtendaji amekaa pale halafu anajua hapa kuna hizi *politics* hizi tulishaachana nazo hizi wakati tunapomaliza Uchaguzi Mkuu. Tunacho address siyo Chama, tunaaddress *Developments,* tuna *addres* maendeleo tunachoangalia pale tunaangalia *background* ya mtu kuwa ametokea wapi *is not an issue*. Wananchi wanachohitaji wanahitaji maji, wanahitaji barabara. Wanataka kujua hela zao zimetumikaje.

*That is the bottom line,* ndicho wanachoangalia pale wala hatutaangalia haya mambo mengine hii siyo *issue* sana. Katika mazingira haya yetu tunayokwenda nayo tunaangalia zaidi maendeleo na hii ndiyo *spirit* ambayo tunataka kuijenga lakini kama kuna mahala popote ambapo kuna tatizo Mbunge karibu tutashirikiana na kusaidiana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jitu Vrajial Soni, swali la nyongeza ninawaita wale niliowaona mara ya kwanza tu siyo wanaosimama baadaye.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mimi nilikuwa ninataka kumwuliza Naibu Waziri.

Je, kama ndiyo hivyo, hamwoni kwamba hizi nafasi kwa kukaimishwa na Mtumishi mwingine katika sehemu husika kama ni kijiji au Kata, hamwoni kuwa inaleta udhaifu kwa sababu huyo Mtumishi mwingine hana elimu wala hana uzoefu wa kufanya kazi ya Mtendaji wa Kijiji au Kata? Anatakiwa kufanya na ile kazi ambayo yeye atakuwa na

nafasi mbili ya kukaimu na ile ya kwake ambayo anaifanya kama mratibu, kama ni wa Afisa Kilimo basi, ile kazi yake pia itakuwa ina pwaya?

Je Serikali haioni kwamba kuwe na mfumo bora zaidi wa kuboresha huu mfumo wa kuleta Watendaji mara tu anapostaafu au wanapoondoka kwenye kituo cha kazi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jitu Vrajial Soni, Mbunge wa Babati Vijijini, kama ifuatavyo:-

Hivi anavyosema anavyoeleza ndiyo *the ideal situation*. Ndivyo inavyotakiwa kuwa umpate mtu ambaye eneo hilo analielewa. Mtendaji wa Kata na ndiyo maana serikali imeanzisha Chuo Kile cha Hombolo. Hombolo tunataka mtu aende pale ambaye amebobea katika eneo hili. Sasa unakwenda pale Mwanga Mtendaji wa Kata Mungu amemchukua au hayupo tena na nafasi ile ipo wazi unafanyaje pale?

Huwezi kuiacha ile nafasi ikabaki hivi kwa sababu kuna masuala ya Sheria yanayopita pale na mipango ya Sheria inayopita pale na bajeti na vitu vingine. Unachofanya pale unamchukua yule wa karibu, unamchukua na kumweka pale, au huyu wa kijiji una mu-*elemet* kidogo unamfanya Akaimu na ndiyo maana ninajenga yale mazingira kuonyesha jinsi unavyofanya yaani pale lazima kuwe na Serikali iwepo pale.

Mheshimiwa Spika, haiwezi ikabaki tu hivi ikiwa *vaquum* halafu wakaingia watu mle na kufanya wanavyotaka. Twende tukaweke maabara pale hakuna cha maabara kwa sababu hakuna Mtendaji anayesimamia unawaweka hawa wote hapo unawapanga hapa. Lakini

sasa kwa maana ya kujibu swali lako Mheshimiwa Jitu Soni, ambaye ninakuona hunisikilizi unachoweza kufanya katika mazingira haya ni kuandaa kada ambayo iko pale ili inapotokea uweke pale. *(Makofi)*

Sasa hatuna utaratibu tu kwamba una kaa kwamba una *library* au una kundi limekaa hapo pembeni tunachofanya ni hiki cha kuchukua yule aliyepo karibu, aliyeko jirani na wakati mwingine tunamchua Mtendaji wa Kata ambaye ni wa jirani au Mtendaji wa kijiji aliyeko jirani akakaimu hapo wakati huo tukifanya mipango kamili ya kumweka mtu mwingine katika eneo hilo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tuendelee na swali linalofuata Wizara ya Kazi na Ajira Mheshimiwa Professor Kulikoyela Kahigi, atauliza swali hilo, majina makubwa tu.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru lakini kabla ya kuuliza swali langu, kwa ruhusa yako ninawaomba kuwapa pole Wana Bukombe wale ambao wamekutwa na matukio ya hivi karibuni ambayo yametikisa amani na utulivu.

Ninawaomba polisi ambao wanafanya uchunguzi wafanye hivyo kwa weledi na kwa kuzingatia Utawala Bora. Baada ya hapo ninaomba swali langu Namba 56 lijibiwe.

Na. 56

**Kuboresha viwango vya Pensheni kwa Watumishi**

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI** aliuliza:-

Pensheni ni miongoni mwa haki ambazo kila amtu

ambaye amefanya kazi kwa muda mrefu (miaka 15 na kuendelea ) anastahili kupata:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia pensheni ya kila mwezi Wahadahiri wa Vyuo Vikuu waliokuwa wa SS waliostaafu kabla ya Machi, 2011?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia pensheni wazee wote nchini waliofikia umri wa kustaafu (yaani miaka 60)?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Professor Kulikoyela Kahigi, Mbunge wa Bukombe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Suala la Wahadhiri wa Vyuo Vikuu waliokuwa katika utaratibu wa SS SS na kustaafu kabla ya Machi, 2011 bado linashughulikiwa na kwamba mazungumzo kati ya Mwajiri Chuo Kikuu na Serikali yanaendelea.

(b) Serikali ipo kwenye mchakacho wa utafiti na majadiliano ili iweze kuanzisha programu ya Pensheni wote yaani *universal pansion.*

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru na ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri, ni mazuri kwa sabau ni mafupi hayana blabla, lakini siyo mazuri kwa kuwa amejibu swali, maswali hayajajibiwa. Kwa sababu swali la pensheni kwa ajili ya Wahadhari wa Vyuo Vikuu limekuwa likijadiliwa toka miaka ya 90 na sasa ni miaka zadi ya 20 mazungumzo yanaendelea kati ya Serikali na hao Waadhiri na wengine wanaendelea kufa.

Sasa ninaomba Naibu Waziri anijibu kuna mpango yaani ratiba iko. Je, yaani *time line* ikoje kwamba haya

mazungumzo yataisha lini ili hawa Wahadhiri wapate haki zao za kimsingi kwa sababu wamefanya kazi na wengine wamewafundisha hata hawa Mawaziri waliomo humu Bungeni.

Swali la pili, ni kweli kwamba Serikali imekuwa katika mchakato wa kuandaa mpango wa pensheni kwa wazee wote nchini lakini mwanzoni mwa Bunge hili tuliahidiwa na Waziri Mkuu kwamba huu mchakato ungeisha hivi karibuni sasa utaisha lini huu mchakato?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira ninapenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Professor Kulikohela Kahigi, kama ifuatavyo:-

Mpango huu wa *Seniour Staff Supper Annuation Scheme* ulioanzishwa na kuendeshwa na Wahadhiri wa Chuo Kikuu na ambao mwaka 1978 *PPF* ilipokuwa inaanzishwa wakaombwa wajiunge na *PPF* wakakataa kwa maandishi limechukua muda mrefu, na katika kikao cha Baraza la Mawaziri mwaka 2011 baada ya majadiliano ya muda mrefu iliamuliwa kwamba wale waliokuwa bado wanaendelea kufundisha mwaka 2011 mafao yao sasa yahamishiwe *PPF* na waanze kuchangia na Serikali inachangia. na mpaka sasa Serikali inapeleka fedha *PPF* na mpaka 2010 Juni tayari Serikali imelipa.

Mheshimiwa Spika, hao wataendelea kulipwa kwa mujibu wa maagizo ya Baraza la Mawaziri lakini Baraza la Mawaziri lilikataa kuwa wale waliosataafu kabla hawajafikiriwa na Serikali kwa sababu walikataa mpango ule wa kuja *PPF* na kwakaendelea na mpango wao ule na walilipwa ilivyostahili kulingana na mpango wao ulivyokuwa walipokuwa wanastaafu na mpango wa SSSS kama ulivyokuwepo, walilipwa bila ya kupunjwa kulinaga na mpango huo. Kwa hiyo, Serikali ilisema haitajighulisha lakini

kumeendelea kuwapo na *appeals* Serikalini na hizi *appeals* ndiyo zinaangaliwa na kujadiliwa kama nilivyosema.

Suala la pili, mpango wa pensheni kwa wazee wote ni lini utaanza. Tumelijibu mara nyingi hapa kwamba bado tunaendelea na utafiti na kubwa zaidi ni kuangalia vyanzo vya mapato. Baada ya kuangalia kwamba Bajeti ya Serikali hakuna mashahidi wazuri wanaojua ufinyu wa Bajeti ya Serikali kama nyie Wabunge akiwemo Professor. Kuna maeneo ambayo tunashindwa kuyahudumia kutokana ufinyu wa fedha, mpango huu unahitaji fedha nyingi sana. Kwa hiyo, Bajeti ya Serikali itakuwa ni ngumu kwa kipindi kifupi. Kwa hiyo tunajarinu kuliangalia, je tunaweza kupata vyanzo vingine?

Kwa hiyo, mambo tunayoangalia ni hayo sasa mpaka hapo tutakapokuwa na uhakika wa vyanzo kwa sababu hatuwezi kuanza mpango utakuwa siyo endelevu mpaka hapo tutakapokuwa na uhakika wa vyanzo na kuweka utaratibu wa mpango huu ndipo utakapoanza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jafo, swali la nyongeza ninawaona niliowaona mwanzo wanaodandia maswali hakuna.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, katika suala zima la pensheni mtu anapofanya kazi anategemea baada ya kustaafu aweze kupata pensheni ya uzeeni. Lakini imetokea wazi kwamba kuna wafanyakazi zaidi ya 300 wa Kampuni ya Mgoodi ya Bulyanh'ulu wameachishwa kazi baada ya kupata madhara wakiwa kazini, lakini kwa bahati mbaya sana watu hawa wamekuwa wakihangaika kwa muda mrefu sana katika ofisi mbalimbali ikiwepo ofisi yako Mheshimiwa Waziri.

Hivi sasa wengine hali zao ni mbaya hata hali ya kutibiwa inakuwa ni changamoto kuwa kubwa na mwenye mgodi anashindwa kuhudumia watu wale na kuwaachisha

kazi Watanzania wale. Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya kadhia hii wanayoipta juu ya Taifa lao?

**SPIKA:** Professor aliuliza Maprofessor wa Chuo Kikuu tena hawa migodi tena na wewe unajua siyo lenyewe lakini hebu jibu tu.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jafo, kama ifuatavyo:-

Suala la wafanyakazi wa Bulyah'ulu limechukua muda mrefu na limekuwa na utata mwingi. Suala hili limekuwa likijadiliwa na likiwa linashughulikiwa na wenzetu wa OSHA. Taarifa nilizo nazo hata wiki iliyopita kulikuwa na Kikao pale OSHA kujaribu kuona ni namna gani suala hili litafikia mwisho. Lakini kwa kweli ni suala refu na siwezi kuelezea kila kitu hapa. Lakini limekuwa kwenye mchakato na makosa yamekuwepo kwa pande nyingi katika masuala haya yanayohusu wafanyakazi wa Bulyanhulu.

**SPIKA:** Tuendelee na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Suleimani Said Bungara, atauliza swali hilo na kwa niaba yake Mheshimiwa Kidawa.

Na. 57

**Matumizi ya Kiswahili- Mahakamani**

**MHE. AMINA MWIDAU (K.n.y. MHE. SELEMANI SAIDI BUNGARA)** aliuliza:-

Mahakama zetu kuanzia ngazi ya Wilaya hadi Mahakama ya Rufaa hutumia kiingereza kuendesha mashauri Mahakamani na kufanya wateja wengi washindwe kukidhi matakwa ya Mahakama kama vile kuandaa Nyaraka za kesi na kuwafanya kukosa haki zao za msingi hasa pale wanapokosa uwezo wa kuweka Wakili:-

Je, Serikali haioni umefika wakati sasa Mahakama zetu

kutumia Kiswahili kuendeshea mashitaka na kuandika hukumu ili kuwawezesha Watanzania wengi kuelewa na kufuatilia mashauri Mahakamani?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Said Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu umuhimu wa Mahakama zetu kuendesha mashauri kwa lugha ya Kiswahili na kila mara imekuwa ikisisitiza hilo. Matumizi ya lugha Mahakamani ni suala la kisheria ambapo *Kif. 13(1)* cha Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura ya kumi na moja kinaeleza kuwa, lugha ya Mahakama za Mwanzo itakuwa ni Kiswahili.

*Kif.13(2),* kinaeleza kuwa lugha ya Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi ni kiingereza au Kiswahili au lugha nyingine yoyote ambayo hakimu anayeendesha kesi ataelekeza. Isipokuwa kumbukumbu na hukumu ya Mahakama itakuwa katika lugha ya kiingereza.

Mheshimiwa Spika, kati ngazi ya Mahakama Kuu, Kanuni za Lugha za Mahakama, Kanuni ya pili inaeleza kuwa, "Lugha itakayotumika Mahakama Kuu ni Kiingereza au Kiswahili au Lugha nyingine yoyote ambayo Jaji anayeendesha shauri husika ataelekeza itumike. Lakini kumbukumbu za shauri na hukumu zitakuwa katika ludha ya Kiingereza.

Pia Kanuni ya 5 ya Kanuni za Mahakama za Rufani, inaelekeza kwamba, Lugha ya Mahakama ya Rufani, itakuwa ni Kiingereza au Kiswahili, kama Jaji atakavyoelekeza au Jaji anayesikiliza atakavyoelekeza, lakini hukumu, amri au uamuzi

wa Mahakama utakuwa kwa Lugha ya Kiingereza.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, matumizi ya Lugha ya Kiswahili katika ngazi zote za Mahakama zetu yanaruhusiwa, kwa sababu ni matakwa ya kisheria. Ili kuhakikisha kwamba uamuzi wa Mahakama unaeleweka kwa pande zote, Kif.313(1) cha sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura ya 20 kinaeleza kuwa: "Pale ambapo mshtakiwa anataka nakala ya hukumu, nakala hiyo kama inawezekana itatafsiriwa katika lugha anayotaka mshatakiwa bila ya kuchelewa na bila malipo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwidau swali la nyongeza.

**MHE. AMINA MOHAMED MWIDAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na ufafanuzi mzuri wa Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali la nyongeza.

Kutokana na usumbufu wanaoupata Watanzania wengi ambao hawajui Lugha ya Kiingereza na kwakuwa lugha ya sheria kwakweli ni ngumu ukichanganya na Kiingereza pia kinawachanganya zaidi.

Je, Serikali haioni kuna kila sababu ya kuleta sheria hiyo Bungeni ili iweze kufanyiwa marekebisho, ili kumbukumbu na hukumu sasa ziwe zinapatikana katika Lugha ya Kiswahili?

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna haja sasa hata ya hukumu ambazo zinatolewa katika Mahakama zetu kuandikwa katika Lugha ya Kiswahili, ili haki iweze kutendeka na ionekane inatendeka.

Lakini tayari kama Serikali tumeshaanza kuchukua hatua. Nakumbuka Mheshimiwa Profesa Kahigi hapa aliuliza

swali Bungeni. Changamoto ambayo tunayo sheria zetu nyingi zipo katika Lugha ya Kiingereza.

Kwa hiyo, tunakosa ile misamiati, istilahi ya kisheria katika lugha ya Kiswahili. Tumeshaanza kufanya mashauriano na Taasisi ya TUKI ya Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam, ili tuweze kutengeneza au ku-*develop* istilahi na misamiati ambayo itaweza kutumika katika Mahakama zetu. Lakini pia tumeshafanya mawasiliano na Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA), tunaendelea kushauriana.

Mheshimiwa Spika, lakini wewe mwenyewe ni shahidi sasa hivi, Miswada yote ambayo tunaileta sasa hivi katika Bunge lako Tukufu, inakuja katika lugha mbili, Kiswahili na Kiingereza. Kwa hiyo, tayari tumeshaanza kuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba nijenge uelewa kwa Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau kwamba Katiba inayopendekezwa Ibara ya nne, inasisitiza kwamba lugha ya Taifa itakuwa ni Kiswahili, na itatumika katika Mawasiliano yote rasmi Serikalini. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tuipigie kura ya ndiyo Katiba inayopendekezwa, ili tuhakikishe kwamba Kiswahili kinatumika katika Mahakama zetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kama mnaleta fujo tusiendelee. Mheshimiwa Sabreena sijawahi kukusikia toka tumeingia.

**MHE. SABREENA HAMZA SUNGURA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa Watanzania wengi hususani walio vijijini, Kiswahili chenyewe ni shida. Kuna Watanzania wengine hata Kiswahili hawajui wanatumia lugha za kimila.

Lakini kwa kuwa hata lugha yenyewe ya Kiingereza, kwa mtu anajua lugha ya kiingereza ya kawaida, kiingereza cha sheria huwa ni kigumu hata kwa mtu anayejua Kiingereza cha kawaida.

Je, Serikali sasa haioni, kama katika kumbukumbu

zetu kuendelea kutumia lugha ya sheria ya Kiingereza ni kuwanyima Watanzania haki?

**SPIKA:** Ungeuliza tena swali la mwisho, hawakusikia vizuri.

**MHE. SABREENA HAMZA SUNGURA:** Mheshimiwa Spika, naomba nirudie. Kwa kuwa Watanzania wengi hususan walioko vijijini wengine Kiswahili hawafahamu wanatumia lugha za kimila na kwa kuwa Kiingereza kinachotumika Mahakamani, ni Kiingereza cha sheria, hata kwa wale wanaojua Kiingereza cha kawaida wakati mwingine inakuwa ngumu kwa wao kuweza kutafsiri.

Sasa Waziri, amesema katika mawasiliano, Katiba mpya inashauri kwamba watu watumie Kiswahili. Lakini kinachozungumziwa hapa, ni kwenye kumbukumbu sahihi zinazobaki Mahakamani.

Kwa nini kisitumike Kiswahili, ili kuwatendea haki Watanzania?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri nadhani umeelewa, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nimejibu katika swali la msingi kwamba, lugha zinazotumika Mahakamani, Kiswahili pia ni lugha rasmi inaruhusiwa.

Lakini tatizo linakuja katika hukumu. Matakwa ya kisheria kwamba hukumu iandikwe katika lugha ya Kiingereza. Lakini nikasema, kipo kifungu katika sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai ambacho kinasema hukumu itapatikana katika lugha ambayo mshtakiwa anaomba. Kwa hiyo, bado ipo nafasi ya kuweza kuhakikisha hukumu pia inatolewa katika lugha ya Kiswahili.

Lakini nikuthibitishie Mheshimiwa Sabreena, lengo letu

ni kweli. Kiswahili kitumike katika ngazi zote za Mahakama ikiwemo pia katika mwenendo wa kuendesha mashauri lakini pia na kutoa hukumu. Mheshimiwa Jaji Mkuu hilo amekuwa akilisititiza, na sisi kama Serikali ambao tunasimamia sera tutaendelea kulisisitiza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tuendelee na swali linalofuata Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo.

Na. 58

**Ahadi ya Ujenzi wa Mahakama ya Wilaya- Iramba**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Ni muda mrefu sasa tangu Serikali itoe ahadi ya kujenga Mahakama ya Wilaya ya Iramba ikijibu swali langu hapa Bungeni.

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo, hasa ikizingatiwa kuwa hadi leo Mahakama hiyo inatumia jengo la Mahakama ya Kata kwa miaka mingi?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge Viti Maalum, Singida, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa jengo la Mahakama ya Wilaya Iramba upo katika mpango wa ujenzi 2014/2015. Hata hivyo mradi huu haujatekelezwa kutokana ukosefu wa fedha za Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, aidha ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Iramba utatekelezwa pindi Mahakama

itakapopatiwa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Diana Chilolo, swali la nyongeza.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri ni fupi sana. Na wala haliwafurahishi wananchi wa Wilaya ya Iramba.

**SPIKA:** Ndio jibu zuri hilo, zuri kabisa! Nampongeza Naibu Waziri.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, na kwa kuwa swali hili nimeshaliuliza hapa Bungeni mara nyingi na Wilaya hiyo ni Wilaya kongwe.

Mheshimiwa Naibu Waziri, haoni sasa kuna wakati wa kuwaambia, kuwapa muda maalum wa kutekeleza ujenzi wa Mahakama hii kuliko kuacha jibu lina eleaelea? Ambalo halina mwisho? Ni lini pesa zitapatikana?

Swali la pili, kwa kuwa Mkoa wa Singida, una Wilaya zingine tatu ambazo hazina Mahakama za Wilaya. Wilaya ya Mkalama ambayo ni mpya, Wilaya ya Singida Vijijini ambayo ni Wilaya Kongwe haina Mahakama ya Wilaya wala Mahakimu hakuna. Wilaya ya Ikungi mpya, haina Mahakama wala haina Hakimu. Rufaa za kutoka katika Mahakama za Mwanzo, Mkalama zinaenda Wilaya ya Iramba.

Rufaa za Mahakama za Mwanzo za Ikungi, na Singida Vijijini zinaenda Singida Mjini, kiasi kwamba Mahakimu hao wa Wilaya wanalimbikiziwa makazi mengi zaidi ya uwezo wao.

Je, kwa kuwa Mahakama ya Iramba ya Wilaya inafanya kazi kwenye Mahakama ya Mwanzo. Kwa nini Wilaya hizi tatu na zenyewe zisipelekewe Mahakimu wa Wilaya, wafanye kazi kwenye Mahakama za Mwanzo kama

inavyofanyika Iramba?

**SPIKA:** We swali lenyewe umelirefusha. Haya majibu tunaomba. Maswali yako vizuri sana amejibu kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme, niliona ni busara kusema kwamba ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Iramba haujaanza kutokana na kuwa, hatujapata fedha za Bajeti ya Maendeleo.

Hilo ndio jibu ambalo nitaendelea kulisema kwamba, katika zile bilioni 40 ambazo tulizitenga, au Bunge lako Tukufu lilipitisha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ya Mahakama hadi sasa hakuna fedha ambayo tumepata.

Lakini naomba nikuthibitishie Mheshimiwa Diana Chilolo kwamba, Wizara ya Katiba na Sheria itaendelea kushauriana na Wizara ya Fedha. Mheshimiwa Waziri wa Fedha yupo hapa, kuhakikisha kwamba ile miradi yote ya Maendeleo ambayo imepangwa kufanywa katika mwaka wa fedha 2014/2015 inatekelezwa kabla ya kumalizika muda. Mheshimiwa Chilolo naomba nikuthibitishie kwamba bado tunao muda kabla ya kumaliza mwaka wa fedha huu.

Swali la pili, ni kwa nini sasa tusipeleke Mahakimu, katika hizo Wilaya tatu za Mkalama, Singida Vijijini na Ikungi. Naomba nikuahidi kwamba hili suala nitalifuatilia pamoja na Mahakama, kuona ni jinsi gani sasa, zile kesi ambazo zipo katika Wilaya husika, basi zinapangiwa Hakimu ambaye ataweza kuzisikiliza, katika kuhakikisha kwamba kunapatikana haki kwa wakati na mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Dkt. Ndugulile nilikuona.

Wengine walisimama baada.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia fursa ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Katika utoaji wa haki katika Mahakama za Mwanzo kuna Wazee wa Baraza. Ambao kwa muda mrefu sasa wamekuwa wanalalamikia malipo ambayo wanapaswa kupata. Kwa muda mrefu wameambiwa wawe wanafanya uhakiki wa mashauri ambayo wameyasikiliza, taarifa hizo wamezipeleka. Lakini mpak hivi sasa wengi hawajalipwa.

Ni lini, Serikali itawalipa Wazee hawa wa Baraza?

**SPIKA:** Naelewa kwamba Wazee wanakaaga kwenye Mahakama. Lakini hilo swali lingine, naomba ujibu Mheshimiwa Waziri wa Ardhi kwa niaba.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kwa niaba ya Wizara wa Katiba na Sheria kumtaarifu tu Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, amekuwa akifuatilia sana suala hili na ninapenda kumpa tu taarifa kwamba mpaka kufikia Juni, malipo yote ya Wazee wa Baraza nchi nzima yamekwishafanyika na hakuna madai mpaka Juni, 2014. *(Makofi)*

Na. 59

**Mradi wa kupeleka Maji Kagongwa na Isaka**

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE** aliuliza:-

Zipo ahadi nyingi za kupeleka maji katika Miji Midogo ya Kagongwa na Isaka ikiwa ni pamoja na ahadi ya Rais mwaka 2008 na pia Kauli ya Serikali kuwa mradi huo uunganishwe na ule wa kupeleka maji Tinde, Nzega hadi

Tabora kitu ambacho kitachelewesha utekelezaji wa miradi ya awali:-

(a) Je, kwanini Serikali isitekeleze kwanza ahadi ya Rais ya mwaka 2008 ndipo ahadi nyingine zifuate?

(b) Je, ni lini hasa huu mradi wa Kagongwa na Isaka kutoka Kahama utaanza?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kutatua tatizo la maji Isaka ambalo ni kubwa kabla ya mradi wa Ziwa Victoria kukamilika?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Ezekiel Mgolyo Maige (Msalala) lenye sehemu A, B, C kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza ahadi hiyo, Wizara imeagiza Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kahama - Shinyanga (KASHWASA) kufanya kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na kuandaa vitabu vya Mzabuni kwa mradi wa maji safi wa Miji Midogo ya Kagongwa, Isaka na Tinde pamoja na kusimamia ujenzi wa mradi huo kama ulivyofanya kwenye mradi wa kupeleka maji safi katika Mji wa Ngudu. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Septemba mwaka huu 2015.

Katika mwaka huu wa fedha 2014/2015, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 8 kwa ajili ya kuanza kutekeleza mradi huo.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa dharura katika kutatua tatizo la maji katika Mji wa Isaka, Serikali kupitia Halmashauri ya Msalala katika Bajeti ya mwaka 2014/2015, imetenga kiasi cha shilingi milioni 21. Hadi sasa kazi zilizofanyika kupitia Bajeti hiyo ni ununuzi wa *pump* mpya,

kusafisha kisima kinachotoa huduma katika Mji wa Isaka, ununuzi na ufungaji wa mabomba na viungio kwa ajili ya kuboresha mtandao wa usambazaji wa maji.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Maige swali la nyongeza.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake.

Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwenye Bajeti ya mwaka huu Serikali ilitenga shilingi bilioni 8 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Hivi sasa tunavyozungumza ni miezi saba imekwishakupita. Nilitaka kujua katika hizi bilioni 8, ni kiasi gani cha fedha kimetoka na kimetumika kwa shughuli gani?

Swali la pili, kwa kuwa tatizo la maji kwenye Miji midogo ya Kagongwa na Isaka ni kubwa. Hivi sasa Mji mdogo wa Kagongwa ulikuwa kwenye ule mradi wa Vijiji kumi katika kila Wilaya na maji hayapo kabisa kwa sababu kisima kilichokuwepo kimekauka pamoja na kwamba mvua zinanyesha. Isaka hali kadhalika maji hakuna kabisa.

Nilitaka kujua kwanini Serikali, isiingilie kati badala ya kuiachia Halmashauri ya Mji wa Kahama pamoja na Mji wa Msalala, kwa kuleta uwakala wa uchimbaji visima, ili waje wachimbe visima vingine vya nyongeza. Kwa mfano, pale Kagongwa vikichimbwa Visima viwili ama vitatu, pamoja na Isaka vikichimbwa Visima vingine viwili au vitatu, naamini angalau kwa muda tatizo linaweza kuwa limeisha.

Kwanini Wizara isiingilie kati kwa kuja kuchimba wenyewe kupitia wakala wake wa Visima?

**SPIKA:** Ahsante sana. Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimhakikishie kwamba nimeshaongea na Wizara ya Fedha na wakati wowote watatupatia hizo fedha na siye tutazileta.

Lakini tumeshatanguliza fedha kwa ajili ya kufanya hiyo *survey* ambayo nimeisema. Ili mradi uweze kuanza mwezi Septemba, 2015.

La pili, kwa kuwa mimi na yeye tulishafika Isaka na kuona matatizo na amekuwa na mazungumzo na mimi na Waziri mara kwa mara, ombi lake tumelipokea tutatuma wataalamu wakapime Kagongwa na Isaka ili tuweze kuchimba Visima kama alivyopendekeza.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ezekiah Wenje.

**MHE. EZEKIAH D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, matatizo ya maji yapo karibia kila kona ya nchi yetu, na hata Jiji la Mwanza kuna matatizo ya maji maeneo mengi.

Sasa kuna taarifa kwamba Serikali ilipata fedha kutoka kwa wafadhili kwa ajili ya kuleta mradi wa maji mkubwa maeneo ya Bugarika, Nyashana na Nyegezi Calfornia.

Ningependa tu kujua kwamba, je, hizi fedha zipo na mradi huu utaanza kutekelezwa lini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tumetiliana saini mkataba wa kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji katika Jiji la Mwanza, na katika maeneo hayo ambayo Mheshimiwa Ezekiah Wenje ameyataja. Pia kushughulikia Mji wa Lamadi, Magu, pamoja na Misungwi.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Godbless Blandes, swali la nyongeza.

**MHE. GODBLESS BLANDES:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mwaka jana meheshimiwa Rais alipotembelea

Wilaya ya Karagwe, akiongozana na Mheshimiwa Waziri wa Maji, Profesa Jumanne Maghembe, aliona adha kubwa sana ya matatizo la maji katika Miji ya Lushaka na Wilaya ya Karagwe kwa ujumla. Aliahidi kwa upendo mkubwa sana, kwamba angeipatia Wilaya ya Karagwe maji haraka iwezekanavyo, kutoka Ziwa Liwakajunju.

Mheshimiwa Spika, nafahamu kwamba *study* tayari imeshafanyika, nilitaka nijue je, ni lini mradi huo unaanza kutekelezwa ili wananchi wa Karagwe wapate maji safi na salama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu. Ingawa maswali yenyewe mapya kabisa.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa Rais akiambatana na Waziri wa Maji alitoa ahadi hiyo. Yeye kama anavyokiri ni kwamba tayari *study* imeshafanyika. Hivi sasa tunachosubiri tu ni utekelezaji na tutatekeleza mara tutakapopata fedha.

**SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata la Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu.

Na. 60

**Miradi ya Maji Moshi Vijijini**

**MHE. BETTY E. MACHANGU** aliuliza:-

Tangu Serikali ianze mpango wa miradi ya maji kwa Vijiji Kumi (10) kila Wilaya ni miaka kumi imepita wakati wananchi wa Wilaya ya Moshi Vijijini wakikabiliwa na tatizo kubwa la maji katika Vijiji vya Tela, Mande, Mawanjeni, Matala na Makuyuni- Himo licha ya kwamba Vijiji hivyo

vilishatangaza tenda na mkandarasi alikuwa tayari tangu, Juni, 2014.

Katika Mkutano wa Sekta ya Maji wa mwezi Septemba, 2014 Halmashauri iliagizwa kusaini mkataba kwa sababu fedha yao ilifikia kikomo *(ceiling)*, wananchi wakiwa walishapewa ahadi ya utekelezaji wa mradi huo.

(a) Je, Serikali inatoa tamko gani katika ahadi yake ya "*Big Results Now*" kwa wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi Vijijini?

(b) Vijiji vingine vya Kirima Juu, Kirima Chini na Boro ambavyo mradi unaendelea kusuasua. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha za kutosha ili mradi huo uweze kukamilika?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2013, Wizara ya Maji imetekeleza mpango wa Serikali wa Tekeleza kwa Matukio Makubwa Sasa yaani *(Big Results Now) (BRN)*. Nia ya Serikali katika mpango huu ni kukamilisha miradi yote nchini inayotekelezwa chini ya *BRN,* ikiwemo Halmashauri ya Moshi Vijijini. Hadi Desemba 2014, miradi 498 imekamilika na watu wapatao milioni 4.9 wanapata huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mpango huo, Halmashauri ya Moshi Vijijini inatekeleza jumla ya miradi kumi na mbili (12) katika Vijiji vya Korini Kaskazini, Korini Kusini, Tella, Mande, Makami Juu, Makami Chini, Matala, Mawanjeni, Kirima Juu, Kirima Kati, Boro na Kilimo Makuyuni. Kati ya Vijiji hivyo, miradi katika Vijiji vya Korini Juu na Korini Chini imekamilika na watu wapatao 9,679 wanapata huduma ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mpango huo Halmashauri ya Moshi Vijijini inatekeleza jumla ya miradi 12 katika vijiji vya Korini Kaskazini, Korini Kusini, Tela, Mande, Makami Juu, Makami Chini, Matala, Mawanjeni, Kilima Juu, Kilima Kati, Bolo, Kilimo na Makuyu. Kati ya vijiji hivyo miradi katika vijiji vya Korini Juu na Korini Chini imekamilika na watu wapatao 9,679 wanapata huduma ya maji. Ujenzi wa miundombinu katika vijiji vitatu Kilima Juu, Kilima Kati na Bolo unaendelea vizuri ambapo ujenzi wake umefikia asilimia 80.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Januari, 2015 Serikali imeshapeleka jumla ya shilingi milioni 494.2 katika Halmashauri ya Moshi Vijijini kupitia Programu ya Maji Vijijini na itaendelea kutuma fedha ili kukamilisha ujenzi wa miradi katika vijiji vyote kwa kadri fedha zitakavyopatikana.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, ninasikitika sana kwa majibu ya Naibu Waziri wa Maji, kwa sababu majibu hayo niliyapata mwaka 2012 na yanakuwa ni yale yale.

Mheshimiwa Spika, hawa watu wa Matala na Mawanjeni wamekuwepo tangu wakati wa uhuru hawajapata maji, unaweza ku-*imagine* watu ambao wapo kwenye Mkoa wenye Mlima wa Kilimanjaro ambao unaaminika unatiririsha maji.

Mheshimiwa Spika, Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza na mojawapo ninahitaji kauli ya Serikali kwamba kumekuwepo na sintofahamu inayosababisha wanasiasa kuwaambia wananchi kwamba hawana haja ya kuchangia katika miradi ya maji hususani kwenye kuchimba mtaro. Naomba kauli ya Serikali katika hili, ni nani anatakiwa achimbe hii mitaro.

Pili, kuna mradi wa maji wa kijiji cha Mbokomu ambao umekuwa tayari lakini bado haujafunguliwa kwa fursa ya wananchi kutumia, naomba Serikali itoe ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme tu kwamba mimi nimefanya ziara Moshi Vijijini, na nimepita bahati mbaya tu yeye alikuwa na udhuru hakuwepo, maeneo haya mengi mimi nimepita, nimejionea na majibu haya tunayoyasema nafikiri tu angekuwa na yeye amepita angeweza kuona mabadiliko. Ipo miradi iliyokamilika na mingine ambayo haijakamilika kama anavyosema, tutapeleka pesa ili ikamilike.

Mheshimiwa Spika, suala la kuchangia wananchi wanapaswa kuchangia kwa maana kila kijiji kuna asilimia tano ya kuchangia kwa ajili ya ujenzi, hilo ni jambo la kisheria na ndiyo masharti yenyewe ili mradi huo wa vijiji kumi uweze kutekelezwa.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, mwaka jana nilimuomba Naibu Waziri asinijibie hapa Bungeni suala la maji Himo aje na kweli akawa muungwana akafika, hebu niambie wananchi wa Himo, Matala na Mawanjeni pamoja na Makami Juu na Makami Chini ambao wapo kwenye huu mradi ziara yako ile hebu waambie ni nini unategemea kwamba kwa kuja kwako ile miradi itakuwa imekwishaanza. Sasa ulienda kufanya nini, niambie ulichokifanya kule ambacho kitakuwa na manufaa kwa watu wa Vunjo? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikiri kwamba ni yeye ndiye aliyenishawishi kwenda na bahati mbaya sikumkuta alikuwa na udhuru.

Kwa hiyo, nilifika kwa yale maombi aliyoyaleta yeye hapa, nimefika Himo bahati mbaya sana alikuwa na udhuru, lakini moja ya jambo kubwa ilikuwa ni kufuatilia mradi huu unatekelezwa na mimi nimewaahidi kwamba tutakapopata fedha miradi ile itakamilika.

Mheshimiwa Spika, kubwa kwa pale Himo kulikuwa na vituo vya maji ambavyo vingine vilikuwa vimefungwa kwa sababu tu ya ubadhirifu wa wale watu waliokuwa wanauza yale maji, nikaamuru vifunguliwe ili wananchi wako

wasihukumiwe kwa sababu ya kosa la mtu mmoja. Moja ya kazi kubwa ni hiyo niliyoifanya. Nakushukuru.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu wa vijiji kumi katika Jimbo langu umekuwa ukisuasua sana. Ipo miradi iliyokwama kwa sababu hakuna fedha, Serikali haileti fedha katika mradi wa Ngaramtoni, mradi wa Musa, Bwawani pamoja na Nduruma.

Mheshimiwa Spika, Waziri ana kauli gani kwa sababu sasa mwaka wa fedha huu unakaribia kuisha, uhai wa Bunge hili unakaribia mwisho wake na ahadi kwa mfano ya Mheshimiwa Rais pale Ngaramtoni baada ya kusikia kilio cha wananchi hadi leo jaribio la kutekeleza halijaonekana pale, ninakushukuru.

**SPIKA:** Kweli lala salama, haya Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninashukuru kwamba maeneo yote aliyoyasema nimefika. Nilikuwa huko Ngaramtoni anakosema, Kisongo, Nduruma nimeona ile miradi ambavyo inaendelea kutekelezwa. Hata jana nilikuwa na mazungumzo naye, zipo fedha ambazo zipo mbioni tutazipeleka na nimeahidi kwamba wakati wa kuzindua ile miradi mimi au Waziri tutakwenda kwa sababu wananchi hawa wana hamu sana kuona mradi huu unatekelezwa.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tuendelee na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa David Silinde atauliza swali hilo.

Na. 61

**Gharama za Huduma za Simu za Mkononi**

**MHE. DAVID E. SILINDE** aliuliza:-

(a) Je, kwa nini inatokea kampuni moja ya simu kudai kuwa wao wanatoa gharama za chini uliko nyingine wakati *TCRA* wanasema gharama za simu kwa kampuni zote (*tariffs*) ni sawa?

(b) Je, inakuwaje pale kampuni moja inapowatangazia wananchi kuwa wao wanatoza muda halisi wa matumizi aliyotumia?

(c) Je, *TCRA* inafanya nini kukabiliana na hujuma hiyo dhidi ya watumiaji wa simu za mkononi?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, napenda kuwataarifu Waheshimiwa Wabunge kuwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania haipangi gharama za simu bali hupanga bei ya ukomo wa maunganisho *(inter-connection)* ya mawasiliano kati ya mtandao mmoja na mwingine. Hivyo, bei hizi za ukomo wa maunganisho ni sawa kwa makampuni yote ambayo kwa sasa ni kiasi cha shilingi 30.58 kwa dakika. Kwa kuwa gharama za ndani za mtandao mmoja hupangwa na mwenye mtandao ni wazi bei zitatofautiana.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika sehemu (a) kila mtoa huduma za mawasiliano anatakiwa kutoza gharama za mawasiliano kulingana na bei elekezi

iliyopangwa na mamlaka ya mawasiliano Tanzania. Hivyo, Kampuni kuwatangazia wananchi kuwa inatoza muda halisi wa matumizi ina maanisha kuwa inatoza kulingana na gharama ambayo imepangwa na kampuni husika lakini kwa kuzingatia bei elekezi, ikiwa kampuni inatoza gharama za maunganisho zaidi ya zile zilizodhibitiwa na *TCRA* hatua stahiki kwa mujibu wa sheria huchukuliwa dhidi ya kampuni hiyo.

(c) Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inasimamia ipasavyo udhibiti wa huduma za mawasiliano kulingana na sheria zilizopo ikiwa ni pamoja na kudhibiti hujuma mbalimbali. Katika kuimarisha udhibiti ikiwa ni pamoja na hujuma dhidi ya watumiaji wa simu za mkononi, kuna kitengo maalum ndani ya Mamlaka ya Mawasiliano kinachoshughulika na malalamiko mbalimbali ya wateja yanayohusiana na huduma za mawasiliano.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imekiri na imesema kabisa kuna kitengo maalum kinacho-*deal* na hujuma mbalimbali. Kwa miaka mitatu kuanzia mwaka 2010 mpaka mwaka 2013 kumekuwa na tatizo la vocha bandia ambapo wananchi wameumia kwa kuibiwa na Serikali imepata hasara kwa kukosa kodi stahiki.

Mheshimiwa Spika, kampuni ya *Vodacom* imeisimamisha kazi kampuni ya *Shivacom* kutengeneza vicha kwa kashfa ya kutengeneza vocha *fake* za dola milioni 350. Je, Serikali inatoa kauli gani?

(b) Kwa kuwa kampuni za simu zinafanya kazi vilevile ya huduma za kifedha, kwa mfano mwaka 2011 mpaka sasa hivi kampuni moja tu ya *Vodacom* fedha zinazopita kwenye mitandao ya M-PESA ni zaidi ya trilioni kumi kwa mwaka. Je, kwa nini Serikali isilete hiyo taarifa Bungeni ili tuweze kujua *cooperate tax* na mwenendo mzima wa fedha hizi ikiwemo

ambazo tumekuwa tukisikia wizi unaotokana na mitandao hii ya simu?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, suala la vocha bandia binafsi kama Serikali hatujalisikia, ambacho tunafahamu ni kwamba kama kuna mgogoro wa kibiashara kati ya kampuni ya simu na wale waliowapa kazi ya kutengeneza vocha basi dhuluma au wizi unafanywa kwa kampuni ya simu kwa mtu aliyepewa kazi ya kutengeneza vocha kwa kutengeneza vocha ambazo ni zaidi ya makubaliano.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mgogoro kati ya *Vodacom* na *Shivacom* ni mgogoro wa kibiashara kati ya makampuni mawili na sisi tunavyojua na kwa taarifa iliyopo Serikalini ni kwamba hatujapata malalamiko ya mteja kuja Serikalini kusema kwamba amepata vocha *fake*.

Mheshimiwa Spika, swali la pili linalohusu kodi. Swali la pili alilouliza Mheshimiwa Silinde linahusu pesa nyingi zinazopita kwenye mitandao. Ni kweli kwa miaka ya hivi karibuni kumekuwa na ongezeko kubwa la matumizi ya pesa zinazopita kwenye mitandao. Kwenye mtambo mpya na tulijibu juzi wakati tunajibu taarifa ya Kamati ya Miundombinu kwamba kwenye Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwenye ule mtambo wa kudhibiti huduma ya mawasiliano *(Telecoms Traffic Monitoring System)* katika hatua ijayo tumeweka kifaa au tumeongeza uwezo wa mtambo ule kuweza kubaini miamala inayopita kupitia kwenye mitandao ya simu.

Kwa maana hiyo Serikali itakuwa na uwezo kuanzia sasa wa kujua kiwango cha miamala hiyo na kodi inayopaswa kulipwa kwa makampuni ya simu. Huko nyuma hatukuwa na uwezo wa kiteknolojia wa kufahamu hivyo.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, tarehe 16 Mei, 2014 Wizara ilinijibu hapa, ilinipa majibu kwa barua kwamba kufikia Disemba 31

itakuwa imepeleka mnara wa simu katika Kata ya Mwakijembe, lakini mpaka tunaposema hakuna chochote kilichofanyika.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Kata hii ipo mpakani na nchi jirani ya Kenya, na eneo tunalolizungumzia ni eneo ambalo wenzetu wanapata matatizo sana ya mapambano na magaidi, nini kauli ya Serikali kwa sababu ya kiusalama kuhakikisha kwamba eneo hili linakuwa na mawasiliano ya simu kwa haraka?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tulimuandikia barua Mheshimiwa Kitandula kumueleza tarehe ambayo kampuni ya simu ya *Vodacom* ingeweza kuanza kujenga mnara kwenye Kata ya Mwakijembe.

Mheshimiwa Spika, barua ile tuliiandika kutokana na barua sisi tuliyoipata kutoka Kampuni ya *Vodacom* na mkataba tuliowekeana wa wao kutuahidi sisi tarehe ambayo wangeanza ile kazi. Yalijitokeza matatizo mbalimbali na siyo eneo la Mheshimiwa Kitandula tu, bali katika maeneo mengi kwamba ahadi tulizopewa na makampuni ya simu za kupeleka mawasiliano kwenye maeneo kadhaa ahadi zile hazikutimia kwa wakati kutokana na matatizo yaliyojitokeza katika kampuni ambazo zilipewa kazi ya kujenga minara hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua kadhaa katika kurekebisha hali hiyo ikiwemo kuziita kampuni za simu na kuziagiza kwamba ziajiri kampuni nyingine za ziada *(sub-contracting)* za kujenga minara ili kazi hiyo iende haraka.

**SPIKA:** Jamani muda umekuwa kinyume kwetu, Mheshimiwa Meshack Jeremiah Opolukwa swali linalofuata na badala yake Mheshimiwa Dkt. Mbassa.

**Kuweka Minara ya Mawasiliano Kata ya Meatu**

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA (K.n.y. MHE. MESHACK J. OPULUKWA)** aliuliza:-

Mawasiliano ya simu katika Kata ya Mwanjolo, Imalaseko, Bukundi, Ng'hoboko, Mwamalole katika Wilaya ya Meatu ni muhimu sana:-

Je, kwa nini mpaka sasa mipango ya kuweka minara ya mawasiliano katika Kata hizo imekuwa ya kusuasua.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Meshack Jeremiah Opulukwa, Mbunge wa Meatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kupitia mfuko wa mawasiliano kwa wote Serikali iliingiza Kata ya Bukundi katika awamu ya kwanza ya mawasiliano yaani *(World Bank Phase I)* ambapo kampuni ya simu ya *TTCL* tayari imekamilisha ujenzi wa mnara katika Kata ya Bukundi kwa gharama za Dola za Kimarekani 195,700 tangu mwezi Septemba, 2014.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Mwanjolo iliingizwa katika zabuni ya awamu ya kwanza 'A' ambapo kampuni ya simu ya *TTCL* imepata zabuni ya kufikisha mawasiliano. Mradi huu unatarajiwa kukamilika tarehe 30 Aprili, 2015. Kata za Imalaseko, Mwamalole na Ng'hoboko zimeingizwa katika zabuni ya awamu ya pili 'A' iliyotangazwa tarehe 28 Novemba, 2014 na mwisho wa kurudisha zabuni hiyo ni tarehe 16 Februari, 2015.

Aidha, kampuni ya simu ya Viettel nayo imeingia makubaliano na Serikali kupitia mfuko wa mawasiliano kwa

wote kufikisha huduma ya simu katika vijiji vya Kata za Imalaseko, Mwamalole, Ng'hoboko kupitia awamu ya kwanza ya kufikisha mawasiliano ya Viettel yenye vijiji 1557 itakayokamilika ifikapo mwezi Julai, 2015.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri hususani kwa hili lililofanyika katika Kata ya Bukundi, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza kwa kuwa sasa hivi inaonekana kuna kampuni mbili *TTCL* nah ii ya Viettel je, kampuni hizi zitafanyakazi katika eneo moja au moja imekuwa *sub-contracted* na kampuni nyingine?

Swali la pili, kwa kuwa suala la mawasiliano ni muhimu sana na katika Jimbo langu la Biharamulo Magharibi kuna Kata ya Nemba haina mawasiliano sambamba na mapori ya Kimisi pamoja na Kasindaga ambako kuna ujambazi wa kutosha hakuna mawasiliano, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga minara maeneo hayo kurahisisha mawasiliano? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la Kata ya Bukundi katika Jimbo la Meatu pamoja na kwamba kampuni ya *TTCL* imepeleka mnara bado vilevile kampuni ya Viettel na yenyewe itapeleka mnara kwa sababu haidhuru kwenye eneo moja kuwa na mtandao zaidi ya mmoja, na sisi ndivyo tunavyotaka kwamba Watanzania wawe na fursa zaidi ya kuwa na mitandao zaidi ya mmoja katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maeneo ya Jimbo la Biharamulo ikiwemo Pori la Kimisi tunaelewa umuhimu wa mawasiliano katika maeneo hayo na hasa maeneo kama kwenye Pori la Kimisi ambapo kuna matukio mengi ya ujambazi na yanashindwa kudhibitiwa kwa sababu watu wanapopata adha inakuwa ni vigumu kuita polisi kwa sababu hakuna mawasiliano. Serikali itayaangalia maeneo

hayo kwa jicho la huruma na kuomba makampuni yaharakishe kupeleka mawasiliano katika maeneo hayo.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini Mheshimiwa Hussein Nassor Amar atauliza swali hilo, kwa niaba yake Mheshimiwa Omary Badwel.

Na. 63

**Manufaa ya Bulyanhulu Gold Mine 'BARRICK'**

**MHE. OMARY A. BADWEL (K.n.y. MHE. HUSSEIN N. AMAR)** aliuliza:-

Tarehe 23 na 24/5/2012 kulitokea milipuko ya baruti zaidi ya nane kwenye Mgodi wa Bulyanhulu Goldmine 'Barrick'wakilipua miamba ili kuvuna dhahabu:-

(a) Je, wananchi wa Wilaya ya Nyang'hwale watanufaika na kitu gani toka kwa *Barrick?*

(b) Serikali ilitoa ahadi kuwa ifikapo Mei, 2012 umeme utakuwa umewashwa vijiji vya Nyang'hwale, Wilaya ya Nyang'wale lakini hadi sasa umeme huo haupo, je, Serikali inatoa kauli gani kwa kutotekeleza mradi huo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali namba 63 la Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'wale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mgodi wa Bulyanhulu uliopo Wilayani Kahama una manufaa yafuatayo ya kiuchumi na kijamii:-

i. Malipo ya kodi mbalimbali na mrabaha;
ii. Ajira kwa Watanzania;

iii. Malipo ya tozo za Halmashauri;
iv. Miradi ya huduma za jamii inayotekelezwa kwenye vijiji vinavyozunguka mgodi; na
v. Manufaa yanayotokana na ununuzi wa bidhaa na huduma za ndani yanayofanywa na mgodi.

Kwa mfano katika kipindi cha kuanzia mwaka 2001 mpaka 2013 Mgodi wa Bulyanhulu umelipa mrahaba wa jumla ya shilingi bilioni 124.3. Kodi mbalimbali jumla ya shilingi bilioni 277.03 na ushuru wa huduma kwa Halmashauri husika shilingi bilioni 4.15. Pia mgodi unaajiri takribani Watanzania 2,300 nje ya wale walioajiriwa na wakandarasi wanaotoa huduma katika mgodi huo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya huduma za jamii mgodi wa Bulyanhulu umekarabati barabara ya Mwasabuka, Kata ya Mwigio yenye urefu wa kilomita moja. Wanaendelea na taratibu za kumpata mkandarasi kwa ajili ya kujenga maabara ya kisasa yenye miundombinu yote katika sekondari ya Nyijundu iliyopo katika Kata ya Nyijundu, wamepeleka kitanda maalum kwa ajili ya kujifungulia akina mama katika hospitali ya Karumwa na wamesaidia vikundi mbalimbali vya wajasiriamali.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2005 mpaka 2011 mgodi umetumia takribani shilingi bilioni saba kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya jamii. Aidha, mwaka 2013 pekee mgodi ulitumia takribani bilioni 227 kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa za huduma toka kwa wagavi wa nchini mwetu.

Mheshimiwa Spika, upelekaji wa umeme katika Wilaya ya Nyang'hwale unahusisha miradi miwili. Mradi wa kwanza umetekelezwa chini ya ufadhili wa *MCC (Millennium Challenge Corporation)* chini ya mkandarasi *Symbion LLC* ambapo vijiji vya Nyang'hwale na Nyarubele tayari vimepata umeme.

Mheshimiwa Spika, mradi mwingine unatekelezwa na *REA* chini ya Mkandarasi *MS Nakuroi Investment Company*

*Limited,* ambapo Mkoa wa Geita ikiwemo Wilaya ya Nyang'hwale na vijiji Busorwa, Nyang'olongo, Idemtemwa, Kayenze, Nyangakagwe, Kakora na Mkorani vipo kwenye mradi. Katika vijiji vya Nyakagwe, Kakora na Mkorani njia kuu ya umeme ya msongo wa kilovolti 33 yenye urefu wa kilomita 6.5 imejengwa.

Aidha, njia ya msongo wa kilovolti 0.4 yenye urefu wa kilometa 10 inatarajiwa kuanza kujengwa mwezi Februari 2015. Mradi mzima unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2015 ambapo wateja 130 wanatarajiwa kuunganishiwa umeme na gharama ya mradi inakadiriwa kuwa shiliingi bilioni 17.3.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Serikali inaendelea na mpango wake kabambe wa kupeleka umeme vijijini lakini nina masikitiko makubwa kwa sababu mpango huu wa Serikali imeonekana katika baadhi ya Wilaya kumekuwa na upendeleo. Wilaya zingine zinapewa vijiji vingi na Wilaya zingine vinapewa vijiji vichache kwa mfano katika Mkoa wa Dodoma wenye Wilaya saba ambapo Wilaya sita ya hizo zimepewa vijiji kuanzia 30 mpaka 56. Lakini Wilaya ya Bahi imepewa vijiji vinne tu na kuonesha kwamba ni upendeleo mkubwa. Sasa nilitaka nijue Serikali lini itafuta upendeleo wa Mkoa wa Dodoma na Wilaya ya Bahi iweze kupata haki yake?

Lakini swali Mheshimiwa Spika, wananchi wa Bahi wametambua kutengwa kwao huko kwa maana ya suala la umeme kwa miaka saba mfululizo sasa hawajahi kuona hata nguzo moja ikishuka katika Wilaya ya Bahi.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua hivyo walimlalamikia Mheshimiwa Rais kwenye mkutano wa hadhara alipokuja Bahi mwaka jana tarehe 1 mwezi wa tisa na Mheshimiwa Rais katika huo huo wa hadhara alimpigia simu aliyekuwa Waziri wa Wizara hiyo na kumtaka kurekebisha kasoro hii katika Wilaya ya Bahi.

Sasa nilitaka nijue kufuatia agizo la Mheshimiwa Rais miezi mitano imepita, Wizara hii ya Nishati na Madini imechukua hatua gani katika kutekeleza agizo la Rais ili wananchi wa Bahi waweze kupata umeme kama vijiji vingine? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE):** Mheshimiwa Spika, wiki nilizungumzia juu ya suala la Wilaya ya Bahi, na nikazungumzia juu ya suala la Gairo. Nimekwenda TANESCO Dodoma kwa ajili ya suala la Bahi, na nimekwenda Gairo. Nimebaini Upungufu na nimewataka watalaam wa Morogoro na Dodoma waandike taarifa kwa wakubwa zao ili huu upungufu uliopo urekebishwe. Kweli upo upungufu Bahi walitengewa vijiji vinne na hakuna kilichofanyika na nimeamuru kwamba kirekebishwe.

Mheshimiwa Spika, kwa waliopata zaidi mtapata zaidi na zaidi, wale mliopata kidogo tutawainua mpaka wote mfikiwe, kitendawili hiki kitatatuliwa tutakapoweza kuondoa vikwazo na vikwazo mojawapo ni rasilimali. Naomba niwaombe wananchi wa Gairo na wananchi wa Bahi ambao mlikuwa mmetengwa au hamkufanyiwa stahili yenu hilo suala linarekebishwa. Sasa suala kwamba mlitengwa miaka saba basi ugonjwa umepata dawa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa nina maswali manne muda wa dakika ni tano tu, kwa hiyo sina namna ya kuongeza. Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya swali linalofuata. Kwa niaba yake aah upo.

Na. 64

**Utekelezaji wa mpango wa *REA* awamu ya kwanza**

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA** aliuliza:-

Serikali bado haijatekeleza mpango wa umeme vijijini *(REA)* awamu ya kwanza, katika vijiji vilivyopangwa.

(a) Je, ni sababu gani za msingi zimepelekea hali hiyo?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani kwa baadhi ya wakandarasi ambao wameshindwa kumaliza kazi ya kuweka umeme vijijini awamu ya kwanza?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba nijibu swali namba 64 la Mheshimiwa Mhonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya awamu ya kwanza ya Wakala wa Nishati Vijijini inahusisha miradi midogo 41 iliyotekelezwa katika Mikoa 16 ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Pwani, Morogoro, Dodoma, Singida, Mbeya, Rukwa, Tabora, Kagera, Kigoma, Mwanza, Shinyanga na Mara. Miradi hiyo inahusisha ujenzi wa kilometa 1,825 za njia ya umeme kwa msongo wa kati wa kilovolti 33 *medium voltage* na kilometa 1,043 za njia za umeme wa msongo mdogo za usambazaji, ufungaji wa transfoma 443 na kuunganisha wateja wa awali 22,000. Mradi huu unatekelezwa katika vijiji vyote vilivyopangwa. Hadi kufikia Desemba 2014 utekelezaji wa mradi huu ulikuwa umekamilika kwa kiwango cha asilimia 96. Kazi iliyobaki ni kuwaunganisha wateja.

Mheshimiwa Spika, Wakala umepokea maombi ya nyongeza kutoka kwenye vijiji vingine vilivyoko jirani na miradi inayoendelea. Wakala unaandaa utaratibu wa kuingiza maombi haya ya nyongeza kwenye mpango wa umeme vijijini utakaofuata baada ya awamu ya pili kukamilika.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika miradi ya *REA* awamu ya kwanza ni kampuni moja tu ya Symbion ambayo haikukamilika kazi zake kwa wakati. Serikali ilikaa na mkandarasi na kupitia mpango wa utekelezaji wa miradi aliyopewa na kumwelekeza kukamilisha kazi zilizobaki

haraka iwezekanavyo. Aidha, wakala kwa kushirikiana na TANESCO unandelea kuhamasisha wananchi ambao hawajatandaza nyaya kwenye nyumba zao kukamilisha haraka ili mkandarasi akabidhi mradi kwa TANESCO.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Ahsante Mheshimiwa Spika kunipa nafasi niulize maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, lengo la kuanzisha Wakala wa Umeme Vijijini ilikuwa kuwasaidia wananchi wa vijijini ili nao wapate umeme ili uchumi uongezeke kwao na Taifa kwa ujumla. Hata Mheshimiwa Rais jana katika hotuba yake amesema kwamba kabla hajaondoka atahakikisha kwamba vijiji vingi vinapatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa lililojionyesha ukiangalia hata ripoti zilizotolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na vilevile Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ameonyesha kwamba pesa hazitolewi kwa wakati. Sasa kwa kuwa kila anayevunja sheria huchukuliwa hatua na Serikali imevunja sheria kwa kutumia pesa ambazo tulizitungia sheria zitumike zaidi ya kupelekwa katika Wakala wa Umeme yaani *REA* je, hatua gani zitachukuliwa kwao?

Swali la pili, *REA I* na *REA II* walitengewa zaidi ya bilioni 880 na mpaka sasa hivi wameshapokea shilingi bilioni 321 tu. Sasa nataka kujua mpaka Juni 2015 *REA II* inatakiwa nayo iwe ishakamilika. Hiyo *deficit* ya shilingi bilioni 500 na zaidi itatoka wapi ili kukamilisha miradi hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE):** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa sana Mhonga.

Namshukuru alivyonukuu maelezo ya Mheshimiwa Rais na ungeendelea ukasema ni Sura ya Nne Ibara ya 63 (c) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ndiyo inatamka hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri anayehusika na fedha juzi amezungumza kwa kina namna gani pesa zile zinazotozwa

kwa ajili ya umeme zitakavyokuwa *ring-fenced* na zile pesa ambazo zitawekewa wigo zitakavyoheshimika. Nina imani katika yeye kwamba hiyo itatekelezwa, siwezi kuzungumza zaidi.

Swali la pili, bakaa ya shilingi bilioni 500 itatoka wapi? Leo asubuhi nilikuwa kwenye *televisio* ya TBC nimelizungumza kwamba ile pesa iliyotengwa kama ikiheshimika na itaheshimika nina imani na Mheshimiwa Waziri. Lakini juzi hapa Waheshimiwa Wabunge mkiongozwa na Kamati ya Nishati mlizungumza haja ya kutafuta vyanzo vingine na mimi nikadakia nikawaambia naweza nikakusanya shilingi bilioni 120 mpaka shilingi bilioni 152 kwa miezi mitatu.

Waheshimiwa Wabunge, kama mkinikubalia na hii tozo ikakubalika, ikaheshimika ina maana *REA* wanaweza kukopesheka na kuwapa imani wakandarasi kazi itafanyika. Bakaa ya shilingi bilioni 500 si tatizo kwa sababu mbali na pesa hizo kuna vyanzo vingine vya Serikali. Mimi nina taarifa kwamba Serikali inahangaika kuangalia vyanzo vingine kusudi pesa ije tuweze kutekeleza.

**SPIKA:** Acheni maneno, tendeni vitendo. Wizara ya Ujenzi Mheshimiwa Sylvestry Koka atauliza swali hilo. Mimi nina dakika tatu maswali matatu, haiwezekani.

Na. 65

**Ujenzi wa barabara za waenda kwa miguu na baiskeli katika barabara ya Dar es Salaam - Morogoro**

**MHE. SYLVESTRY F. KOKA** aliuliza:-

Ajali nyingi zimekuwa zikitokea katika maeneo ya Kibaha Mjini kutokana na kutokuwepo kwa njia ya waenda kwa miguu, baiskeli na pikipiki kwenye barabra ya kutoka Dar es Salaam kwenda Morogoro.

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kutengeneza barabara hizo ili kuepusha ajali zinazotokea mara kwa mara

na kutishia maisha ya wananchi wa Kibaha Mjini katika barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sylvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Dar es Salaam – Morogoro sehemu ya Ubungo hadi Mlandizi ulizingatia uwepo wa njia za waenda kwa miguu kwa kupanua mabega ya barabara kwa meta mbili hadi tatu kwenye maeneo ya miji ukiwemo mji wa Kibaha. Hivyo njia za waenda kwa miguu zilizopo zinakidhi vigezo vya kuepusha ajali na kulinda maisha ya watumiaji wa barabara zikitumika inavyotakiwa hususan waenda kwa miguu, waendesha baiskeli na pikipiki.

Mheshimiwa Spika, uwepo kwa kituo kikuu cha mabasi Kibaha Mjini, soko pembezoni mwa barabara, mizani ya kupima uzito wa magari na kituo cha ukaguzi wa mazao ya misitu ndiyo chanzo cha msongamano mkubwa wa magari hususan wakati wa mabasi yanaingia na kutoka kwenye stendi kuu na hivyo kusababisha kutokea kwa ajili za mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha hali ya usalama kwa watumiaji wa barabara katika eneo la barabara kuu Kibaha, Serikali imeamua kujenga mizani mpya ene la Vigwaza ambapo magari yatapima yakiwa katika mwendo.

Aidha, Halmashauri ya Mji wa Kibaha inaendelea na maandalizi ya kuhamisha kituo kikuu cha mabasi pamoja na kuondoa soko ambalo lipo pembezoni mwa barabara kuu.

**MHE. SYLVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya zamani inayopita kuanzia Picha ya Ndege, Kwa Mathias, Kibaha, Kongowe, Visiga hadi Mlandizi ni barabara muhimu ambapo ikitokea msukosuko wowote katika barabara kubwa hutumika kupita na wasafiri wanaotumia barabara hii muhimu. Lakini kilichojitokeza siku za karibuni Serikali imewawekea wananchi alama ya "X" ambao wamejenga pembezoni mwa barabara hii. Lakini hakuna mpango wowote wa kuihudumia barabara hii muhimu imeendelea kutelekezwa na kuendelea kubomoka. Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha barabara hii inaendelea kutengenezwa ili kuwahudumia wananchi na inawaambia nini hawa waliowekewa alama ya "X"?

Swali la pili, barabara ya Kwa Mathias hadi Msangani ambayo kimsingi ilikuwa ni barabara ya lami na inayotoa huduma kwa wananchi wa Msangani na Vikosi vya Jeshi vya Nyumbu pamoja na Msangani imetelekezwa na leo hii imebakia vumbi tupu. Bajeti ya mwaka 2013/2014 zilitengwa fedha kwa ajili ya kuanza kuitengeneza katika kiwango cha lami. Lakini hadi leo hakuna kilichofanyika. Serikali ina mpango gani kuweka lami barabara hii muhimu?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa koka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa anaongelea habari ya barabara hiyo inayokwenda Picha ya Ndege kwa maana kwamba kuna alama za "X" zimewekwa kwenye barabara hiyo. Alama za "X" ambazo zimewekwa kwenye barabara hiyo ni kujulisha tu kwamba wananchi wale wako kwenye eneo la hifadhi ya barabara ambayo kwa mujibu wa sheria. Kuna "X" za aina mbili kuna "X" nyekundu na kuna "X" za kijani. Kwa wale ambao wana alama za "X" nyekundu maana yake wanatakiwa waondoke kwenye eneo la hifadhi ya barabara na wale ambao kwenye "X" za kijani maana yake ni kwamba Serikali itawafidia pale itakapofanya maendelezo ya eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la pili, nijibu tu kwamba barabara ya Mathias - Msongani si kwamba Serikali imetelekeza barabara hiyo, kama anavyosema kwamba kwenye mwaka wa fedha 2014/2015 kuna fedha zimetengwa kwenye bajeti ina maana Serikali ina nia thabiti ya kuitengeneza barabara hiyo, tutaweza kufanya hivyo pale fedha zitakapopatikana.

Na. 66

**Kujenga vyuo vya VETA vya Wilaya na Mkoa – Kagera**

**MHE. GOSBERT B. BLANDES** aliuliza:-

Ni sera ya Serikali kujenga vyuo vya VETA kila Wilaya hapa nchini japokuwa katika Mkoa wa Kagera hakuna chuo cha VETA cha Mkoa:-

Je, ni lini Serikali itajenga vyuo vya VETA kila Wilaya na VETA Mkoa wa Kagera?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mbunge wa Karagwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya uchambuzi wa Stadi zitakazofundishwa katika Wilaya 43 ikiwemo Wilaya ya Misenyi. Katika mwaka wa fedha 2013/2014 na 2014/2015, Serikali imeendelea na maandalizi ya ujenzi katika Wilaya tano ambazo ni Chunya, Kilindi, Namtumbo, Ukerewe na Ludewa. Pia imeendelea na maandalizi ya ukarabati wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Wilaya ya Karagwe na Korogwe.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa bajeti Serikali haijaweza kutimiza azma yake ya kujenga Vyuo vya Ufundi Stadi katika kila Wilaya. Hivyo, Serikali ilifikia uamuzi

wa kutumia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vikiwemo Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi wa Gera kilichopo Wilayani Misenyi na Rubondo Wilayani Biharamulo. Vyuo hivi vilianza kutoa mafunzo ya ufundi stadi sanjari na mafunzo ya maendeleo ya jamii chini ya usimamizi wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Aidha, vyuo hivyo vimeanza kutoa mafunzo ya ufundi stadi katika fani za ufundi magari, uashi na ushonaji ambapo kuanzia mwaka 2013 kila chuo kinapokea idadi ya wanafunzi wapatao 50 kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kagera una chuo cha VETA ambacho kipo Rwamishenyi chenye hadi ya chuo cha Mkoa baada ya hivi karibuni kufanyiwa ukarabati na upanuzi wa madarasa na karakana ya kutosheleza kutoa mafunzo pamoja na kuongeza walimu wenye sifa.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ingawa bado hayajatosheleza. Kwanza nina maswali mawili.

Swali la kwanza amezungumzia kwamba Mkoa wa Kagera unacho Chuo cha VETA cha Mkoa ambacho kiko Rwamishenyi. Sijui kama Mheshimiwa Naibu Waziri amefika pale. Kale ni kachuo kadogo sana kenye hadhi pengine ya Wilaya. Mkoa wa Kagera unazo Wilaya nane ikiwepo Karagwe, Kyerwa, Ngara, Bukoba Vijijini, Muleba, Bukoba Mjini na Misenyi. Tunapozungumza VETA Mkoa chuo hicho hakina hadhi hata kidogo. Nataka kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, je anafahamu kwamba chuo hicho ni kidogo kiasi hicho na kuna mpango sasa hivi nafahamu wa kujenga Chuo cha VETA Mkoa wa Kagera katika maeneo ya Kahororo pale Bukoba Mjini. Je, taarifa hizo anazo, kama anazo kinaanza na kitakamilika lini? Swali la kwanza hilo.

Swali la pili, Mheshimiwa Spika, naomba ninukuu majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, anasema kwamba; "kwa mwaka 2013/2014 na 2014/2015 Serikali imeendelea na maandalizi ya ukarabati wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Karagwe na Korogwe Tanga." Imeendelea na maandalizi miaka miwili kukarabati vyuo hivi vya Karagwe, Ngara, Chuo

cha Iremera, Korogwe. Haya maandalizi yanaendelea kwa miaka miwili ya fedha, yatakamilika lini maandalizi haya tunataka vyuo vikarabatiwe?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kumshukuru Mheshimiwa Blandes kwa kuuliza swali ambalo ni muhimu sana kwa wananchi wa Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Spika, naomba nikiri kwamba Chuo kilichopo Mkoa wa Kagera kama Chuo cha VETA Mkoa ni kweli nakubali kwamba hakina hadhi japo mimi mwenyewe sijafika lakini nimekuta mezani kwamba Wizara yenyewe imekiri kwamba hakina hadhi. Lakini naomba niwapongeze Wabunge wote wa Mkoa wa Kagera wakiongozwa na Mheshimiwa Blandes kwamba kilio chao cha kutafuta na kulilia kwamba wapate VETA ya Mkoa sasa Serikali ya Chama cha Mapinduzi imesikiliza kilio kile na tarehe 26 Oktoba, 2014 Mheshimiwa Rais alikwenda China na alipofika China jambo la kwanza aliomba Serikali ya China iwajengee wananchi wa Mkoa wa Kagera chuo cha VETA na Serikali ya China ilikubali kujenga chuo mkoa wa Kagera na tarehe 26/01/ 2015, majuzi tu, Balozi wa China nchini Tanzania alikwenda Mkoa wa Kagera na alioneshwa hekta 10.4 ambako chuo hiki kitajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na ninaomba kabisa niwaambie wananchi wa Mkoa wa Kagera kwamba mimi mwenyewe nitakwenda kumshika Balozi vizuri niende Mkoa wa Kagera nikaone ni wapi chuo hiki kitajengwa. Isipokuwa ninaomba nitoe wito na nitoe maagizo leo kabisa, Manispaa ya Mkoa ya Bukoba Mjini imempa Balozi mpaka sasa hivi hekta 10.4 tu na VETA Mkoa tunahitaji hekta 35 na kuendelea. Kwa hivyo, Manispaa ya Bukoba Mjini kuanzia leo ikae na itafute ardhi haraka ili nitakapompeleka Balozi pale mahali ambapo Chuo kinajengwa tukute hekta 35 zimetengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali lake la pili kuhusu Karagwe kama Chuo cha VETA Wilaya; ni kweli, imekuwa ni muda mrefu sana Serikali inajitahidi kuzungumzia

Karagwe, lakini naomba nimpe habari njema sasa kwamba Serikali imeshatenga bilioni mbili kwa ajili ya kukarabati kile chuo cha Karagwe na zipo tayari zinangoja kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, na ni vyema Mheshimiwa Blandes ukafahamu kwamba mimi mwenyewe ninakuja Karagwe sasa kuhakikisha chuo hiki kinajengwa na ninaomba upokee kwamba hilo ni tamko la Serikali. *(Makofi)*

Na. 67

**Kufungwa kwa Ubalozi wa Uingereza Nchini**

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB** aliuliza:-

Tanzania imekuwa na ushirikiano na Uingereza kwa muda mrefu tangu Uhuru wa Tanganyika mwaka 1961 mpaka sasa:-

(a) Je, kwa nini Ubalozi wa Uingereza nchini umefungwa na kusababisha usumbufu mkubwa wa *VISA* nchini na wananchi kulazimika kufuata huduma hiyo Nairobi – Kenya au Afrika Kusini?

(b)Je, uamuzi wa Tanzania kuwa na Ubalozi nchini Uingereza umesaidia vipi kuendeleza na kuimarisha uhusiano wetu wa Kidiplomasia?

(c) Je, Serikali inatoa kauli gani kwa wananchi wake ambao wamekuwa wakipata usumbufu mkubwa kutokana na maamuzi hayo ya muda mrefu na Serikali kukaa kimya bila ya kuwafahamisha wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa KImataifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, awali ya yote nichukue fursa hii kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa Ubalozi wa Uingerereza hapa nchini haujafungwa na kutokana na mahusiano mazuri yaliyopo kati ya nchi zetu mbili, hatutarajii Ubalozi huo kufungwa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli huduma ya viza kwenda Uingereza zimehamishiwa sasa kwa wakala ambao Ofisi zao zipo katika jengo la *Viva Towers,* ghorofa ya pili, barabara ya Ali Hassan Mwinyi, Jijini Dar es Salaam, ni kupitia Wakala huyo ndiyo taratibu zote za viza zinafanywa hapa nchini. Kutokana na maelezo ya Ubalozi wa Uingereza, pamoja na kuwa viza zinashughulikiwa nje ya nchi, muda wa wastani wa kuomba na kupata viza ni siku 18 kabla ya safari. Usumbufu unajitokeza pale tu mtu anapokuwa na safari ya ghafla na haraka.

(b) Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Tanzania kuwa na Ubalozi nchini Uingereza umesaidia kukuza uhusiano mzuri wa kidiplomasia na Uingereza. Uhusiano ambao umetuwezesha kushirikiana katika nyanja za elimu, biashara, utalii na uwekezaji. Wanafunzi wa Tanzania wamekuwa wakinufaika na ufadhili wa Serikali ya Uingereza katika mafunzo ya elimu ya juu, hususan shahada ya Uzamili na Uzamivu. Aidha, ifahamike kuwa Serikali ya Uingereza ni mbia mkubwa wa biashara kwa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje inayojikita katika Diplomasia ya Uchumi, Tanzania inaendelea kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo nchini kupitia Ubalozi wa Tanzania uliopo London. Aidha, Serikali ya Uingereza ni moja ya wadau wakubwa ambao wamekuwa wakitoa misaada kupitia Umoja wa Ulaya na pia moja kwa moja kwenye bajeti yetu.

(c ) Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Serikali inaendelea kufanya jitihada kuhakikisha kuwa usumbufu wa upatikanaji wa viza ya Uingereza na nchi nyingine unapungua kwa kiasi kikubwa. Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa bado

inaendelea kuzisihi nchi hizo kupunguza masharti yao ya viza kwa Watanzania, ili wananchi wa Tanzania waendelee kufaidika na uhusiano mzuri tulionao na nchi hizo. Kadhalika, wakati jitihada zikiendelea, natoa wito kwa wananchi wa Tanzania wenye dhamira ya kwenda Uingereza kufanya maombi yao ya viza mapema, ili kuepuka usumbufu. Ahsante.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Muyuni kwa kushirikiana bega kwa bega na Mwakilishi wake na vilevile alipojibu swali hili kwa msingi wa hoja. Naomba kumuuliza maswali mawili madogo Dkt. Mahadhi Juma Maalim:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa amekiri katika swali la msingi kuwa Serikali ya Tanzania ina uhusiano mkubwa na Uingereza. Huduma hizo kutolewa na mawakala badala ya kutolewa na Ofisi yenyewe, huoni inajenga sura mbaya kwa Watanzania hasa ukizingtia Uingereza ilikuwa ni koloni la Tanzania? Je, inaleta picha gani kwa Watanzania?

**SPIKA:** Umesemaje?

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, la pili…

**SPIKA:** Yaani Uingereza ilikuwa koloni letu sisi?

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, aaah! Tulikuwa tumetawaliwa na Uingereza. Na ninaomba kurekebisha Mheshimiwa.

Mheshimiwa Spika, la pili kwa kuwa watu wengi hawafahamu Uingereza kuwa Ofisi yao imefungwa na wengine kwenda Nairobi au *South Africa,* ni lini watakaa kikweli kweli hasa kulitatua tatizo hili na huduma hizi zikapatikana hapa? Na kama msemo wa kiswahili unaosema fimbo ya mbali haiui nyoka?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, maswali yake yenye sehemu (a) na (b) ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli mara nyingi huduma za utolewaji viza zinafanyika katika Ubalozi unaohusika, lakini wenzetu hawa Waingereza kutokana na sababu kubwa mbili, moja ilikuwa ni kujaribu kubana matumizi, lakini na ya pili walikuwa wanajaribu kuweka huduma hizi kwa pamoja kwa ajili ya kuweza kudhibiti zaidi wageni wanaoingia hasa katika kupambana na masuala haya ya *terrorism*.

Kwa hiyo, mwanzo huduma hizi walizihamishia Nairobi na ni kuanzia mwaka jana tu mwezi wa nane ndiyo wameamua kutoa huduma hizi kupitia kwa wakala ambaye kama nilivyojibu katika jibu la msingi kwamba sasa huduma hizo zinapatikana *Viva Towers* na baadaye wamehamishia huduma katika nchi zote za Afrika Mashariki na Kati, wanashughulikia maombi hayo kwa pamoja Pretoria.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa wale wananchi ambao bado hawana taarifa hiyo bado tunawasihi, hawana haja ya kwenda Nairobi wala Pretoria, huduma hizo sasa zinapatikana kupitia kwa wakala. Ni uamuzi wa nchi yenyewe, tumekuwa tukiendelea kuwanasihi, lakini kwa kuangalia mazingira yao ndiyo wameona wafanye hivyo, isipokuwa kwa wale wenye *passport* za Kidiplomasia, kama Waheshimiwa Wabunge, maombi hayo yanapitia Wizara ya Mambo ya Nje na yanashughulikiwa Nairobi na inakuwa kuna uwezekano wa kupata viza katika muda mfupi kidogo.

Mheshimiwa Spika, nafikiri nimejibu maswali yote mawili kwa pamoja.

**SPIKA:** Ahsante, muda umekwisha. Tumeshakula sana muda wa zaidi ya dakika 20, sio sahihi. Kwa hiyo, naomba niwatambue baadhi ya wageni tulionao ndani ya Bunge hili.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 15 wa Mheshimiwa Alhaji Mohamed Missanga wa Singida Magharibi ambao ni jopo la Masheikh wakiongozwa na Sheikh Ahmad Zubeir kutoka Dodoma. Naomba Masheikh wote wasimame walipo hapo! Ahsante. Ahsanteni sana na karibuni sana, nadhani mtatusaidia katika mambo Fulani fulani, ahsante sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kutoka Jimbo la Siha, wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Siha Ndugu Oscar Themi. Yuko wapi huyu Mheshimiwa Themi? Yuko pale! Yupo na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Ndugu Jonathan Nassari, ahsante, yuko Katibu wa CCM Wilaya ya Siha Ndugu Allen Kingazi halafu ipo na Sekretarieti ya Chama Wilaya ya Siha na wengine wote wasimame kutoka Siha!

Hee, kumbe wamekuja wote? Hee, haya. *(Makofi)*

Ahsanteni sana ninyi watu wa Siha. Mbunge wenu huwa anapandisha sauti anasema ni kusisitiza tu mambo, kwa hiyo, lakini anafanya kazi nzuri. *(Kicheko/Makofi)*

Tunao wageni wengine katika msafara huo ambao ni Waheshimiwa Madiwani 15 kutoka Wilaya ya Siha. Naomba Waheshimiwa Madiwani wasimame. Ahaa, ahsante sana.

Kuna viongozi na watendaji tisa wa *CCM* Wilaya. Wasimame hao wengine. Pia tuna Wenyeviti 15 wa CCM Kata! Ahsante. *(Makofi)*

Tuna Makatibu 15 wa…, ndiyo hao hao wa CCM Kata nafikiri. Makatibu 15 wa CCM Kata! *(Makofi)*

Halafu kuna vijana wa makundi mbalimbali ambao ni bodaboda, vicoba, wakulima na wafugaji kutoka Siha. Naomba na wao pia wasimame. *(Makofi)*

*Okey,* ahsante sana. Naona Mheshimiwa Naibu Waziri kawaleta nyie wote hapa kuondoa fitna, haya. *(Makofi)*

Tuna wageni wengine 15 wa Mheshimiwa Agripina Buyogera, Mbunge na Mheshimiwa Moses Machali ambao ni viongozi wa NCCR-Mageuzi kutoka Mkoa wa Kigoma na Taifa ambao ni Ndugu Danford Kagabo – Kamishna wa NCCR Mageuzi Mkoa wa Kigoma, yuko wapi? Yuko upande ule. *(Makofi)*

Wapo Wenyeviti wa Wilaya na Majimbo manne yenye Wabunge wa NCCR-Mageuzi Kigoma. Na wenyewe wasimame! Ahsanteni. *(Makofi)*

Kuna Makatibu wa NCCR-Mageuzi kutoka Majimbo manne yenye Wabunge na wenyewe pia wasimame? Ahsante. *(Makofi)*

Kuna Mheshimiwa Fidelis Kumbo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza. Mheshimiwa Fidelis, ahsante. *(Makofi)*

Kuna Mheshimiwa Isaac Rashid ni Diwani wa Kata ya Kasulu Mjini. Mheshimiwa Diwani ahsante. *(Makofi)*

Tuna Ndugu Deo Meck – Kaimu Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana NCCR-Taifa. Huyo asimame na yeye, ahsante. *(Makofi)*

Halafu tuna Katibu wa Mheshimiwa Agripina Buyogera, jina lake halikutajwa, asaimame. Ahsante sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, ambao ni wanafunzi 47 kutoka Chuo cha Biashara *(CBE)* Dar es Salaam wakiongozwa na Spika wao, Ndugu Elias Gratian. Hawa wanafunzi wapo humu ndani? Ooh, *okey!* Ahsante, karibuni sana na Mheshimiwa Spika, karibu. Ahsante, ahsanteni sana naomba msome kwa bidii. *(Kicheko/Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Ismail Aden Rage na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah ambao ni Madiwani sita kutoka Manispaa ya Tabora Mjini pamoja na watumishi

watano kutoka Manispaa hiyo wakiongozwa na Mstahiki Meya, Mheshimiwa Dewji Gulam na Naibu wake Mheshimiwa Salum Msamazi. Waheshimiwa Madiwani wasimame kwanza. Ahsante nashukuru, ahsante sana.

Halafu na watendaji watano wasimame na baadaye Mheshimiwa Mstahiki Meya na Naibu wake wasimame.

Ahsanteni sana, karibuni. Tunawatakia kazi njema. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Martha Mlata ambaye ni Mwalimu Daines Lopa. Mwalimu Lopa yuko wapi? Ahsante sana. *(Makofi)*

Tuna wageni waliopo kwa ajili ya mafunzo ambao ni wanafunzi 20 na walimu 10 kutoka *Rabi English Medium School* ya Dodoma. Naomba wanafunzi hawa wasimame walipo! Ahsante.

Eeh, kumbe wadogo wadogo tu! Ahsante nashukuru. Karibuni sana, tunaomba tu, tunashukuru kwa ulezi wa watoto. Ahsanteni sana, mmevaa Jamhuri! Ahsante, karibuni. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya kazi sasa, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Saidi Mohamed Mtanda, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo tarehe 2 mara baada ya kuahirisha Kikao hiki nadhani saa 7.00 mchana, watakuwa na Kikao chao katika Ukumbi Namba 227.

Halafu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI…, watu mnaongea wakati sisi tuko Bungeni. Mheshimiwa Naibu Waziri pale. Tuko Bungeni, hatuko mitaani.

Eeh, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa

7.00 mchana kutakuwa na Kikao katika Ukumbi wa Msekwa C.

Halafu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Richard Ndassa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.00 mchana kutakuwa na Kikao chao katika Ukumbi Namba 121.

Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Pindi Chana…

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dunstan Kitandula anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.00 mchana kutakuwa na Kikao katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Naona Kamati mbili ziko Pius Msekwa, mtajua namna ya kugawana maeneo.

Halafu kuna chama kinaitwa TAPAFE, Mwenyekiti wa chama hicho, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, anaomba niwatangazie Wajumbe TAPAFE, ni chama kingine. Mwenyekiti wa Chama cha Wabunge Marafiki wa Mazingira na Uhifadhi, ndiyo TAPAFE hiyo, Mheshimiwa Hilda Ngoye, anaomba niwatangazie wanachama hao kushiriki chakula cha jioni pamoja na ugeni wa Chama cha *Climate Parliamentary Tanzania* kitakachoandaliwa *New Dodoma Hotel* leo Jumatatu saa 2.00 usiku. Kwa hiyo, chama hiki na ugeni wao watakuwa na chakula hiyo saa mliyotaja hapo, saa 2.00 usiku.

Halafu Ofisi inatangaza kwamba niwajulishe Wabunge… ooh, *I am sorry!* Sikuambiwa, wananiandikia tu! Kumbe kuna Mheshimiwa Mwenzetu, Ritta Mlaki, amefiwa na mama yake mzazi tarehe 1 Februari, huko Dar es Salaam na mwili wa marehemu utasafirishwa tarehe 4 Februari

kwenda Moshi kwa mazishi yatakayofanyika tarehe 5 Februari kule kwao kijiji cha Maili Sita. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina.

Katibu tuendelee.

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira na Taarifa ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, Pamoja na Mapendekezo na Maoni Yaliyomo Kwenye Taarifa Hizo Kama Ilivyosomwa Bungeni

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira!

**MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 117(15), Toleo la 2013, ninaomba kuwasilisha taarifa ya kazi zilizofanywa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira katika kipindi cha mwaka 2014 ili iweze kujadiliwa na Bunge lako Tukufu na kutolewa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati hii kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu ya Kamati kwa kipindi chote cha mwaka 2014, mawazo na ushauri wao, umewezesha Kamati kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira yameainishwa katika Kanuni za Kudumu za Bunge, Nyongeza ya Nane, Kifungu cha 6(8), Toleo la mwaka 2013 kama ifuatavyo:-

(i) Kushughulikia Bajeti za Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi;

(ii) kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi;

(iii) Kushughulikia taarifa za kila mwaka za utendaji za Wizara zilizo chini ya Kamati hii; na

(iv) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizi kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kutokana na muda na ukubwa wa taarifa hii, naomba taarifa yote hii iingizwe katika *Hansard* kama ilivyowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kufanyika kwa mwaka 2014. Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwa mwaka 2014, ilipanga kufanya kazi zifuatazo:-

(i) Kufanya mikutano mbalimbali ya Kamati na watendaji wa Wizara husika ili kujadili na kutathmini shughuli za Wizara husika na kutoa mawazo, ushauri pamoja na maelekezo;

(ii) Kufanya ziara katika sehemu mbalimbali nchini ili kuona utekelezaji wa miradi ya maendeleo na shughuli zilizo chini ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati;

(iii) Kupitia na kujadili taarifa za utendaji za Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, Wizara ya

Maliasili na Utalii na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; na

(iv) Kuchambua bajeti za Wizara husika, kuchambua Miswada ya sheria, Maazimio ya Bunge ya kuridhia Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizotekelezwa na Kamati kwa mwaka 2014. Mikutano na Wizara ya Maliasili na Utalii. Kamati ilikutana na Wizara ya Maliasili na Utalii kupokea taarifa mbalimbali kama zilivyoainishwa hapa chini. Mgogoro wa mpaka kati ya shamba la uwekezaji *(eko-energy)* la Bagamoyo na Hifadhi ya Taifa ya Saadan.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Taifa ya Saadan ilianzishwa mwaka 2005 kwa Tangazo la Serikali GN. Na.281. Lengo la kuanzisha Hifadhi hii ilikuwa ni kuunganisha maeneo ya Hifadhi katika mifumo ya ikolojia moja ili kuwa na Ikolojia mseto na timilifu. Mambo yaliyozingatiwa na Serikali katika kuanzisha hifadhi hii ni pamoja na:-

(i) Kuhifadhi maeneo muhimu kwa mtawanyiko wa wanyamapori *dispersal areas,* eneo la mazalia *(breeding sites)* na mapito ya wanyama *(migratory routes);*

**SPIKA:** Wale wanaotoka watoke waache amani ndani ya ukumbi siyo kelele tena. Mheshimiwa Mwenyekiti, endelea tafadhali.

**MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA:**

(ii) Kuhifadhi eneo la mazalia ya kasa wa kijani;

(iii) Kulinda na kuhifadhi msitu wa mikoko na baianuai ya mto Wami ambayo ni mazalia ya samaki na malisho kwa ndege wahamao; na

(iv) Kulinda na kuhifadhi tembo hasa shoroba zinazotumiwa na tembo au ndovu kuhama kati ya maeneo ya Selous, Mikumi, Wami Mbiki na Saadan na kulinda na kuhifadhi matumbawe na majani ya bahari.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2008, mwekezaji anayejulikana kama Bagamoyo *Eko Energy Tanzania Limited* alimilikishwa eneo linalopakana na Hifadhi ya Taifa ya Saadan kwa hati na 120397 ambayo ilimega eneo la hifadhi na hivyo kukiuka mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Saadan kama ilivyoainishwa katika Tangazo la Serikali Na. 281 la mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, Bagamoyo *Eko Energy* Tanzania *Limited* walipewa eneo hilo kwa ajili ya kilimo cha miwa ili kuzalisha sukari na umeme. Kampuni hii inadai kwamba sehemu ya ardhi hekta 3,441 ziko ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Saadan na hivyo waruhusiwe kutumia eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kusikiliza maelezo toka Wizara ya Ardhi na Wizara ya Maliasili, imebaini kwamba chanzo cha mgogoro ni Serikali yenyewe, kwamba Wizara zake katika kutekeleza majukumu yake katika baadhi ya maeneo hazishirikiani.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Kamati. Kamati inaishauri Serikali yafuatayo:-

(i) Wakati Wizara hizi mbili za Serikali zikijadili jinsi ya kutatua tatizo hilo, Sheria ya Hifadhi iheshimiwe na mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Saadan kwa mujibu wa GN. Na. 284 ya mwaka 2005 ilindwe na kuheshimiwa; na

(ii) Serikali kama inajiridhisha kwamba umuhimu wa kilimo cha miwa ni bora zaidi kuliko sababu zilizopelekea Serikali yenyewe kutangaza eneo la Saadan kuwa Hifadhi ya Taifa basi Serikali ilete mbele ya Bunge lako Tukufu Azimio la Serikali la kutaka kubadili

mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Saadan kama sheria inavyotaka.

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa mipaka ya msitu wa Kazimzumbwi. Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya mgogoro wa mipaka katika msitu wa Hifadhi ya Kazimzumbwi wenye ukubwa wa eneo la hekta za mraba 4,862 ambao ulitangazwa kuwa Hifadhi ya Msitu mwaka 1954 kwa Tangazo la Serikali Na. 306 na Ramani Na. Jb196. Msitu huu ni muhimu kwa maisha ya wakazi wa Jiji la Dar es Salaam kwa kuwa ndiyo chujio la hewa safi inayotumika katika Jiji na viunga vyake na chanzo kikuu cha maji yanayotiririka katika Mto Mzinga.

Mheshimiwa Spika, malalamiko ya wananchi wa Kitongoji cha Nzasa, Wilaya ya Ilala kuhusu mipaka ya msitu wa Hifadhi Kazimzumbwi ni ya muda mrefu na jitihada mbalimbali za kutatua mgogoro huu zimehusisha vyombo mbalimbali ikiwa pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu, ambayo ilitoa maagizo ya jinsi ya kumaliza mgogoro huo ambao sasa umeisha na wananchi waliokuwa wamevamia msitu huo wameondoshwa.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Kamati. Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

(i) Serikali iwachukulie hatua za kinidhamu watendaji wote wa Wizara ya Ardhi pamoja na wale wa Manispaa ya Ilala walioshiriki kwa namna moja au nyingine katika kutoa tafsiri potofu ya mipaka ya Msitu huu hali iliyopelekea wananchi kuvamia hifadhi hiyo muhimu na kufanya uharibifu mkubwa; na

(ii) Mipaka ya Hifadhi ya Msitu wa Kazimzumbwi iimarishwe kwa kuweka alama za kudumu na doria maalum iendelee kufanyika kuzunguka hifadhi hiyo kuzuia wananchi kurudi tena ndani ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa mipaka ya Pori la Akiba la Mkungunero. Tarehe 19/12/2014, Kamati ilitembelea Pori la Akiba la Mkungunero na Vijiji vinavyopakana na Pori hilo vya Kimotorok kilichoko katika Wilaya ya Simanjiro na Irkuishbor kilichoko katika Wilaya ya Kiteto. Hali ya mgogoro uliopo kati ya Pori la Akiba la Mkungunero na wananchi wanaopakana na Pori hilo kwenye Mikoa ya Dodoma na Manyara ni mkubwa na unahatarisha amani katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Kamati. Kamati inaishauri Serikali ichukue hatua za haraka kumaliza kabisa mgogoro huo ikiwa pamoja na kutambua hatua ya Vijiji 5 vya Tarafa ya Makami Wilaya ya Kiteto ya kuanzisha Hifadhi yao ya Jamii iliyoridhiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii mwaka 2011. Wizara ikamilishe haraka mchakato wa kurejesha eneo la kilomita za mraba 50 la Vijiji viwili pamoja na Kijiji cha Irkiusholbor vilivyoko katika Wilaya ya Kiteto kutoka katika eneo la Pori la Akiba la Mkungunero kwa sababu eneo hilo liliingizwa kimakosa.

Mheshimiwa Spika, uchimbaji wa madini ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Manyara. Sheria Na. 5 ya Wanyamapori ya mwaka 2009 hairuhusu uchimbaji wa madini ndani ya Hifadhi za Taifa isipokuwa kwa *strategic minerals* tu. Madini hayo ni Urani, Gesi na Petroli. Hata hivyo, leseni zilizotolewa kwa makampuni yanayochimba madini katika hifadhi hii ni batili.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kutembelea Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara na kujionea uharibifu mkubwa unaotokana na uchimbaji huo wa madini. Kamati imeelezwa kwamba makampuni hayo yalipewa leseni kihalali kabla ya eneo hilo halijaingizwa ndani ya Hifadhi za Taifa lakini ilipewa kibali maalum cha kuendelea kuchimba hadi muda wa leseni hizo kumalizika ambazo zote zilitakiwa kumalizika mwezi Februari mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilielezwa kwamba kati ya leseni 8 ambazo ukomo wake ni mwezi huu, leseni moja *PML* 0012658 ya Bwana Ahmed Saad ukomo wake ni mwaka 2020 kinyume kabisa cha utaratibu. Kamati inaitaka Serikali

kulieleza Bunge lako Tukufu ni kwa taratibu na sheria gani ilimpa mamlaka Kamishna wa Madini kutoa leseni hii kwa miaka 12 badala ya miaka mitano kama sheria inavyotaka.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inaitaka Serikali kusitisha mara moja leseni hii na kuwachukulia hatua stahiki watendaji wa Wizara ya Nishati na Madini waliohusika na utoaji wa leseni hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpaka wa Bologonja. Kufuatia taarifa kwamba mpaka wa Bologonja unaotenganisha nchi ya Kenya na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini pia unatenganisha Hifadhi ya Masai Mara kwa upande wa Kenya na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kwa upande wa Tanzania utafunguliwa. Kamati ilifanya ziara katika eneo hilo kuona hali halisi na ukweli wa fununu hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishuhudia shughuli za utalii zikiendelea vizuri katika eneo hilo la mpaka. Mpaka umefungwa na hakuna mtalii anayeingia kupitia lango hilo. Watalii wengi waliohojiwa kama wangependa lango hilo lifunguliwe walikataa kwa sababu ambazo walizitaja. Aidha, walisema kufunguliwa kwa lango la Baragonja kutaharibu sifa ya miaka mingi ya Serengeti kuwa ni hifadhi pekee Barani Afrika na duniani kote ambako mtalii anaweza kuona wanyama wakubwa, *the big five* bila ya kuwepo msongamano wa magari na watalii. Waliipongeza Sera ya Uhifadhi ya Tanzania ya kupokea wageni wachache lakini mapato makubwa tofauti na nchi jirani ambayo Sera yake ni watalii wengi mapato kidogo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kutofungua mpaka wa Bologonja kwa maslahi ya uhifadhi endelevu na kulinda mapato makubwa yanayopatikana hivi sasa kwa faida ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kesi dhidi ya tozo kwa watalii wanaolala katika hoteli zilizoko katika Hifadhi za Taifa. Septemba 12, 2014, Mahakama Kuu, Kanda ya Arusha ilitoa Hukumu ya kesi iliyokuwa imefunguliwa na makampuni

yapatayo 17 ambayo yanamiliki hoteli ndani ya Hifadhi za Taifa ya kuanza kutoza tozo mpya kwa mfumo wa "*Fixed Rate*" badala ya mfumo wa zamani wa "*Concession Rate*". Katika Hukumu hiyo, Mahakama iliiagiza Wizara ya Maliasili na Utalii kutoa tangazo katika Gazeti la Serikali kuhusu kuanza kutumika kwa tozo mpya. Ni miezi takribani sasa minne tangu kutolewa kwa hukumu hiyo, Wizara ya Maliasili na Utalii haijatekeleza hukumu hiyo ya Mahakama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na kutotekelezwa kwa hukumu hiyo, *TANAPA* kwa maana ya Hifadhi za Taifa Tanzania na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, zinapoteza mapato yanayofikia karibu shilingi bilioni mbili kila mwezi. Tangu kufunguliwa kwa kesi hiyo mwaka 2011 hadi Septemba 2014, Shirika la Hifadhi za Taifa na Mamlaka ya Hifadhi za Ngorongoro yamepoteza kwa pamoja takribani shilingi bilioni 80 kutokana na kukosa malipo yanayotokana na tozo hiyo. Kamati iliitaka Wizara ya Maliasili na Utalii iwe imeshatoa Tangazo hilo katika Gazeti la Serikali ifikapo tarehe 28 Januari, 2015. Kamati inataka Serikali itoe maelezo ya sababu za msingi za kutotekeleza maagizo haya ya Kamati hadi leo tunapowasilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, ziara katika Hifadhi ya Taifa ya Arusha. Kamati ilifanya ziara katika Hifadhi ya Taifa ya Arusha na kupokea taarifa kuhusu mgogoro baina ya Hifadhi ya Taifa ya Arusha na Wakala wa Misitu Tanzania. Chimbuko la mgogoro huu ni Tangazo la Serikali Na. 280 la 2005 ambalo liliongeza mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Arusha kwa kuongeza Misitu ya Hifadhi ya Meru na Ngurudoto. Tangazo hilo la Serikali lililenga kudhibiti uharibifu mkubwa wa Misitu ya Asili ya Mlima Meru na Ngurudoto ambayo ulitishia kuharibu kabisa ikolojia ya eneo hilo na vyanzo vya maji hasa kwa Jiji la Arusha.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusikiliza maelezo ya pande mbili na kutembelea eneo la mgogoro, Kamati iliishauri Serikali kukazia yaliyomo katika GN. Na.280 lakini kuleta Azimio la mabadiliko madogo ya mpaka ya *GN* hiyo ya kuondoa maeneo ya Chuo Kikuu cha Sokoine na Chuo cha Misitu cha Olmotonyi na eneo lingine lote likijumuisha

msitu wa kupanda libaki ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Arusha kulinda ikolojia na vyanzo vya maji vya Jiji la Arusha. Wakati hayo yakiendelea, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha Shirika la Hifadhi la Taifa Tanzania linatekeleza jukumu lake la kulinda mipaka ya Hifadhi ya Arusha kwa mujibu wa GN. Na.280.

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Kamati ilipokea taarifa kuhusu mgogoro wa mpaka kati ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na wananchi wanaozunguka hifadhi hiyo. Kamati inashauri Serikali yafuatayo:-

(i) Kuendeleza mazungumzo kuhusu utatuzi wa mgogoro huo na yahusishe wadau wote na Serikali ichukue hatua madhubuti na za haraka kumaliza mgogoro huo; na

(ii) Kutokana na umuhimu wa eneo la ardhi oevu kuwa katika Bonde la Usangu na ambalo liko ndani ya mpaka wa Hifadhi ya Taifa kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 281 la mwaka 2008, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kuwa GN. Na.281 ya 2008 pamoja na mipaka yake yote inaheshimiwa.

Mheshimiwa Spika, kupotea kwa Shoroba za Wanyamapori. Wakati Kamati hii ikiwa katika ziara ya Kanda ya Kaskazini, ilibaini kuwa shoroba za wanyamapori zimeanza kuzibwa na zingine zimezibwa kabisa hivyo kuzifanya baadhi ya Hifadhi za Taifa na Mapori ya Akiba kugeuka visiwa. Kwa mfano, Kamati ilijionea ongezeko la shughuli za kilimo na makazi kwenye shoroba ya wanyamapori ya Tarangire inayounganisha hifadhi hiyo na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Hifadhi ya Taifa ya Manyara na Hifadhi ya Tarangire. Ushoroba huo umekaribia kuziba kabisa hali itakayowafanya wanyama washindwe kuzunguka kama ilivyo kawaida yao ya asili.

Mheshimiwa Spika, shoroba nyingine zimekufa kabisa hizo ni pamoja na ushoroba unaounganisha Hifadhi ya Taifa

ya Mlima Kilimanjaro na ile ya Arusha hadi Hifadhi ya Taifa ya Mikumi. Hali hii imezua tatizo la *inbreeding* katika hifadhi ya Arusha jambo ambalo litapelekea kutoweka kabisa kwa baadhi ya wanyama katika maeneo hayo isipodhibitiwa. Kwa kuzingatia athari hizo, Kamati inashauri Serikali kufanya yafuatayo:-

(i) Kuandaa mkutano wa wadau utakaojadili na kupata ufumbuzi kuhusu uhifadhi wa shoroba za wanyamapori; na

(ii) Kuandaa utaratibu wa kuhifadhi shoroba kwa mujibu wa Sheria ya Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, ziara katika Msitu wa Mikoko wa Kijiji cha Tongoni – Tanga. Ikiwa Mkoani Tanga Kamati ilitembelea eneo la kijiji cha Tongoni ambacho pamoja na shughuli nyingine kinajihusisha na uhifadhi wa mikoko. Wananchi wa Tongoni walieleza Kamati kwamba kazi ya kuhifadhi mikoko ina changamoto nyingi kubwa ikiwa pamoja na kudhibiti majangili wa mikoko na uhaba wa vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Kuimarisha upandaji wa miti mbadala utakaowapatia wananchi miti kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ili waachane na matumizi ya mikoko.

Mheshimiwa Spika, ziara katika Hifadhi ya Taifa Mkomazi. Kamati ilifanya ziara kwenye Hifadhi ya Taifa Mkomazi kwa lengo la kuona maendeleo ya mradi wa faru weusi. Ikiwa Mkomazi Kamati ilibaini yafuatayo:-

(i) Mradi wa Faru Weusi katika Hifadhi ya Taifa Mkomazi unaendeshwa kwa kutegemea rasilimali fedha, vifaa na utaalamu kutoka kwa wahisani wenye nia njema na uhifadhi wa faru. Hata hivyo, jitihada hizi za wahisani zinakwamishwa na kodi ambayo hutozwa

kwa vifaru vinavyotolewa bure na wahisani kwa Taasisi yenye uwezo mdogo wa kifedha;

(ii) Kodi pia imekuwa ikitozwa kwa kila mnyamapori kwa maana ya faru anayetolewa kama msaada kwa Tanzania. Faru wote waliotolewa kama msaada nchini, Serikali ya Tanzania imewatoza kodi na kila faru ametozwa kodi ya *Import Duty* kati ya dola 300 na dola 400 kila mmoja. Kodi hii imekuwa ikilipwa na anayetoa msaada kwa maana ya wahisani jambo ambalo limewaumiza sana na wahisani wengine wanampango wa kusitisha kutoa misaada hiyo; na

(iii) Aidha, silaha, vifaa vya kutengeneza barabara na magari yanayoingizwa nchini kwa msaada wa wahisani kwa ajili ya uhifadhi wa faru pia hulipiwa *VAT* na *Import Duty*.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha na kitendo cha Serikali kuzuia bandarini magari 8 aina ya *Land Rover* yaliyotolewa na Jumuiya ya Nchi za Ulaya kwa ajili ya uhifadhi wa faru pamoja na silaha kwa ajili ya kupambana na ujangili ambazo zilizuiliwa bandarini kwa zaidi ya mwaka mmoja zikidaiwa kodi. Hii ni aibu kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kufuta mara moja kodi zote zinazotozwa kwa wanyama faru wanaoletwa nchini kama msaada pamoja na kodi ya vifaa vinavyotolewa na wahisani kwa ajili ya uhifadhi wa faru kama magari, magreda, silaha na mavazi ya Askari.

Mheshimiwa Spika, madai ya Stahiki ya Askari walioshiriki Operesheni Tokomeza. Baada ya kusimamishwa kwa Operesheni Tokomeza, Askari walioshiriki zoezi hilo walianza kudai posho zao ambazo walipaswa kulipwa baada ya zoezi kusimama. Madai ya msingi ya Askari hao wote walioshiriki kwa maana ya Polisi, Usalama wa Taifa, Jeshi ni posho ya siku 13 kati ya siku 31 za awali zilizokuwa

zimepangwa kabla ya kuongezwa kwa muda wa operesheni tokomeza. Takriban shilingi billion 3.9 zilikuwa zimekusanywa kutoka hifadhi ya Taifa Tanzania *TANAPA*, Wakala wa Misitu Tanzania, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Mfuko wa Taifa wa Wanyama Pori.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia madai hayo ya Askari yamekuwa ya siku nyingi na ambayo yanawakatisha tamaa kuendelea na kazi za kuzuia ujangili, Kamati inaitaka Wizara kuwasilisha mbele ya Kamati matumizi ya fedha hizo kwa maana ya shilingi bilioni 3.9. Aidha, Kamati inaitaka Serikali sambamba na kutoa taarifa ya matumizi ya shilingi bilioni 3.9, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali afanye Uchunguzi Maalum *(Special Audit)* wa jinsi pesa hizo zilivyotumika. Kamati inaikumbusha Serikali kutekeleza Maazimio yote yaliyoazimiwa na Bunge lako Tukufu kuhusu Operesheni Tokomeza.

Mheshimiwa Spika, mikutano na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kamati ilikutana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na kupokea taarifa kuhusu utekelezaji wa shughuli mbalimbali zinazofanywa na Wizara pamoja na taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, ardhi ni rasilimali ya msingi na ya muhimu ambayo shughuli zote za kijamii, kiuchumi na kimaendeleo zinafanyika juu yake. Kwa sababu hiyo, aridhi inatakiwa kumilikiwa kiserikali, kimila kwa sheria, kanuni na taratibu zinazokubalika. Kwa kuzingatia thamani na umuhimu wa ardhi, ni vema Serikali ikasimamia Sheria zake za Ardhi kwa manufaa ya maendeleo ya kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa asilimia 80 ya wananchi wa vijijini wanategemea ardhi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kwa kuwa mara nyingi migogoro huanza pale viongozi wa vijiji wanapoingia mikataba mibovu na watu binafsi, makampuni na wawekezaji ni dhahiri kwamba Serikali isipokuwa makini katika suala la kumilikisha ardhi kwa wananchi, wawekezaji wa ndani na wa nje na kutoa elimu kwa Viongozi wa Vijiji, Wilaya na Maafisa Waandamizi wa

Wizara ya Ardhi, nchi na wananchi wataendelea kuwa maskini na watwana katika ardhi yao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi. Moja ya changamoto kubwa ya Wizara hii ni kuongezeka kwa migogoro ya mipaka ya ardhi baina ya watumiaji mbalimbali wa ardhi. Kwa mfano, migogoro kati ya wakulima na wafugaji ambayo imeenea katika kila kona ya nchi hii, migogoro baina ya wawekezaji na wanavijiji na taasisi za Serikali na wananchi na kadhalika, migogoro hii na mingine imesababisha katika maeneo mengine mauaji ya raia wasiokuwa na hatia na uharibifu mkubwa wa mali za wananchi.

Mheshimiwa Spika, moja ya madhumuni ya kuanzishwa kwa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi ilikuwa ni kupanga matumizi ya ardhi ili kuondoa migogoro baina ya watumiaji wa ardhi. Mipango hii ya matumizi ya ardhi huongoza utendaji wa sekta zingine kama vile kutenga maeneo ya uwekezaji, kilimo, makazi ya wanyamapori, misitu, vyanzo vya maji, malisho ya wanyama na shughuli zote zinazotumia ardhi zisigongane.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa tunapotoa taarifa hii, sehemu kubwa ya ardhi ya nchi yetu bado haijaandaliwa mipango ya matumizi bora ya ardhi. Kati ya vijiji 11,000 vilivyoko nchini ni vijiji 1000 ndivyo vina mipango au matumizi bora ya ardhi. Hali ni mbaya zaidi katika Miji Mikuu ya Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali iangalie upya utendaji wa majukumu ya Tume hii kwa lengo la kuongeza nguvu lakini pia Serikali iiwezeshe kwa fedha ili iweze kutekeleza malengo yake.

Aidha, Kamati inaishauri Serikali itwae mara moja maeneo ya mashamba makubwa yaliyotekelezwa machache wapewe wananchi na mengi yaingie katika orodha ya ardhi ya akiba. Mashamba mengi...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge mashamba makubwa yaliyofanya nini?

**MHE. JAMES D. LEMBELI - MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, nitarudia aidha, Kamati inaishauri Serikali itwae mara moja maeneo ya mashamba makubwa yaliyotekelezwa...

**WABUNGE FULANI:** Yaliyotelekezwa! *(Kicheko)*

**MHE. JAMES D. LEMBELI - MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA:** Yaliyotelekezwa, machache wapewe wananchi na mengi yaingizwe katika orodha ya ardhi ya akiba ya Serikali. Mashamba mengi yaliyotelekezwa yamegeuka kuwa maficho ya majambazi, chanzo cha ugomvi kati ya wenye mashamba na wananchi na mengine yamekuwa vyanzo vya mapato, rushwa kwa baadhi ya watendaji na viongozi kwa kuyakodisha au kuratibu mipango ya kuyauza kinyemela kwa wamiliki wengine.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Kamati. Miji mingi hapa nchini imeendelea kukua kwa kasi kubwa bila ya kuwa na uwiano na taratibu za mipango miji. Ukuaji huu umechangia kuwepo kwa makazi yasiyo rasmi na ujenzi holela hasa katika maeneo ya mijini. Sheria ya Mipango Miji Na.8 ya mwaka 2008 na Sera ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 zinasimamia ukuaji wa miji na majiji na zinatoa dira juu ya namna gani miji ipangwe kulingana na miundombinu ya maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kusimamia na kutekeleza Sheria ya Mipango Miji kwani mbali na changamoto ya ukuaji wa kasi ya miji kumekuwepo pia na ukaidi wa makusudi wa wananchi kutotii sheria.

Mheshimiwa Spika, ziara katika Wilaya ya Mafia. Kamati ilifanya ziara katika Wilaya ya Mafia, tarehe 22 kutembelea mashamba makubwa ya Utumaini na

Ngombeni. Aidha, Kamati ilipokea taarifa ya Wilaya iliyobainisha migogoro iliyopo katika mashamba hayo baina ya wananchi na wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa ushauri ufuatao kuhusu ziara hii ya Mafia. Ili kumaliza mgogoro uliopo kati ya shamba la Utumaini, Kamati inashauri Serikali yafuatayo:-

(i) Sheria ya Ardhi ifuatwe; na

(ii) Serikali ifute hati miliki mara moja ya shamba la Utumaini na ligawiwe kwa manufaa ya matumizi ya wananachi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mikutano na Ofisi ya Makamu wa Rais. Kamati ilikutana na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na kupokea taarifa kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Mazingira katika migodi ya dhahabu. Katika utekelezaji wa Sheria ya Mazingira Kamati ilibaini mgongano wa taasisi ambao unakwamisha utekelezaji wa Sheria ya Mazingira. Kamati pia inasikitishwa na bajeti finyu ya mazingira inayotolewa kila mwaka hali ambayo inaifanya Wizara hii na Baraza la Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*) kushindwa kufuatilia na kusimamia Sheria ya Mazingira kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya mifuko ya plastiki. Kamati ilipokea taarifa kuhusu utekelezaji wa agizo la Serikali kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya *plastic* nchini. Kamati inaishauri Serikali kujifunza kutoka nchi nyingine kama India na Dubai jinsi zilivyofanikiwa katika udhibiti wa matumizi ya mifuko ya plastiki badala ya kupiga marufuku.

Mheshimiwa Spika, ziara katika mgodi wa North Mara. Kamati ilitembelea mgodi wa North Mara kukagua utekelezaji wa Sheria ya Mazingira. Kamati iliridhishwa na hatua zilizochukuliwa na mgodi kutekeleza Sheria ya Mazingira. Kamati imeshauri elimu zaidi kuhusu utunzaji wa mazingira ya maeneo yanayozunguka migodi itolewe kwa wananchi ambao ndiyo wadau wakubwa. Aidha, Kamati inaishauri Serikali ya Wilaya Tarime kuchukua hatua za haraka kuzuia

ujenzi wa nyumba zinazojulikana kama tegesha katika eneo la mita 200 ambalo mgodi wa North Mara umepewa. Aidha, Kamati imeagiza tathmini ya eneo hilo ifanyike haraka na fidia zilipwe kwa wananchi ili kuepusha migogoro inayoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, ziara katika mgodi wa Bulyankhulu. Kamati ilifanya ziara katika mgodi wa dhahabu wa Bulyankhulu. Kamati iliridhishwa na hatua zinazochukuliwa na mgodi huo katika kutekeleza Sheria ya Mazingira, kutekeleza maagizo ya Kamati ilipotembelea mwaka 2012. Yaliyotekelezwa ni pamoja na kujenga maeneo ya kukusanya taka za plastiki sambamba na kujenga vizuizi vya udhibiti uvujaji wa mafuta ya mitambo kuenea katika mazingira.

Mheshimiwa Spika, ziara katika kiwanda cha Falcon cha kuchakata taka za plastiki. Kamati ilifanya ziara katika kiwanda cha Falcon kilichoko Mwanza. Kamati ilijionea jinsi plastiki zinavyochakatwa na kutoa bidhaa za plastiki zinazotumika kutengeneza meza, milango, madawati na hivyo kupunguza matumizi ya mbao katika kutengeneza samani za majumbani. Kamati inaishauri uongozi wa kiwanda cha Falcon kuongeza ufanisi wa kukusanya taka za plastiki. Aidha, Kamati imeshauri uwezekano wa kiwanda kama hiki kujengwa jijini Dar es Salaam ambako kuna taka nyingi.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Mafanikio ya Kamati yangu katika kutekeleza shughuli zake kwa mwaka 2014 yametokana na ushirikiano wa karibu sana na Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Maliasili na Utalii, pamoja na Taasisi na Mashirika yote yaliyoko chini ya Wizara hizi. Mashirika ya Kitaifa na Kamataifa pamoja na wadau wetu, napenda kuwashukuru wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa shukrani kubwa kwa ushirikiano tulioupata kutoka kwenye ofisi yako. Napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas

Kashililah, pamoja na Katibu wa Kamati hii Ndugu Gerald Magili kwa kuratibu shughuli zote za Kamati na kipindi chote cha mwaka 2014.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, nachukua fursa hii kuwashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwa kutoa maoni, ushauri pamoja na ushirikiano wao kwenye Kamati.

**SPIKA:** Mheshimiwa ni kengele ya pili, ndiyo umemaliza muda wako.

**MHE. JAMES D. LEMBELI - MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA KWA KIPINDI CHA MWAKA 2014 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni Na. 117(15), Toleo la 2013, naomba kuwasilisha taarifa ya kazi zilizofanywa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira Kwa kipindi cha Mwaka 2014, ili iweze kujadiliwa na Bunge lako tukufu na kutolewa maamuzi.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati hii kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu ya Kamati kwa kipindi chote cha Mwaka 2014 mawazo na ushauri wao umewezesha Kamati kufanya kazi zake kwa

ufanisi mkubwa. Aidha, napenda kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. James Daudi Lembeli, Mb | - Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Abdulkarim E. H. Shah, Mb | - M/ Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Zakia Hamdan Meghji, Mb | - Mjumbe |
| 4. | Mhe. Muhamad Amour Chombo, Mb | - Mjumbe |
| 5. | Mhe. Esther Amos Bulaya, Mb | - Mjumbe |
| 6. | Mhe. Amina Andrew Clement, Mb | - Mjumbe |
| 7. | Mhe. Al-Shymaar John Kwegyr , Mb | - Mjumbe |
| 8. | Mhe. Waride Bakari Jabu, Mb | - Mjumbe |
| 9. | Mhe. Michael Lekule Laizer, Mb | - Mjumbe |
| 10. | Mhe. Suzan Limbweni Kiwanga, Mb | - Mjumbe |
| 11. | 11. Mhe. Kisyeri Werema Chambiri, Mb | - Mjumbe |
| 12. | Mhe. Sylivester Mhoja Kasulumbayi, Mb | - Mjumbe |
| 13. | Mhe. Haji Khatib Kai, Mb | - Mjumbe |
| 14. | Mhe. Benedict Ole-Nangoro, Mb | - Mjumbe |
| 15. | Mhe. Mwanakhamis Kassim Said, Mb | - Mjumbe |
| 16. | Mhe.John John Mnyika, Mb | - Mjumbe |
| 17. | Mhe.Gr ace Sindato Kiwelu,Mb | - Mjumbe |
| 18. | Mhe.Clara Diana Mwatuka, Mb | - Mjumbe |
| 19. | Mhe.Dkt Mary Machuche Mwanjelwa, Mb | - Mjumbe |
| 20. | Mhe.Dkt Henry Daffa Shekifu, Mb | - Mjumbe |
| 21. | Mhe.Salim Abdallah Turky Mb | - Mjumbe |
| 22. | Mhe. Abuu Hamoud Jumaa, Mb | - Mjumbe |
| 23. | Mhe. Dkt. Dalaly Kafumu, Mb | - Mjumbe |

## 2.0 MAJUKUMU YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, majukumu ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira yameainishwa katika Kanuni za Kudumu za Bunge, Nyongeza ya Nane Kifungu Na.6 (8) Toleo la 2013 kama ifuatavyo:-

- Kushughulikia Bajeti za Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira, Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

- Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira, Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

- Kushughulikia Taarifa za kila Mwaka za utendaji za Wizara zilizo chini ya Kamati hii.

- Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizi kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) (b) ya Katiba.

**3.0 KAZI ZILIZOPANGWA KUFANYIKA KWA MWAKA 201**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, kwa Mwaka 2014, ilipanga kufanya kazi zifuatazo:-

- Kufanya mikutano mbalimbali ya Kamati na watendaji wa Wizara husika ili kujadili na kutathmini shughuli za Wizara husika na kutoa mawazo, ushauri pamoja na maelekezo.

- Kufanya ziara katika sehemu mbalimbali nchini ili kuona utekelezaji wa miradi ya maendeleo na shughuli zilizo chini ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati

- Kupitia na kujadili Taarifa za utendaji za Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira, Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

- Kuchambua Bajeti za Wizara husika.

- Kuchambua Miswada ya sheria, Maazimio ya Bunge ya kuridhia Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge.

## 4.0 KAZI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI KWA MWAKA 2014

### 4.1 Mikutano na Semina na Wizara

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata nafasi ya kufanya mikutano na Semina mbalimbali kwa lengo la kuongeza upeo na uelewa wa Wajumbe wa Kamati katika maeneo yanayohusu Sekta zinazosimamiwa na Kamati hii. Aidha Kamati ilipata fursa ya kufanya ziara katika maeneo mbali mbali ya nchi yanayosimamiwa na Wizara husika na katika nchi za nje pia.

#### 4.1.1 Mikutano

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2014, Kamati ilikutana na kufanya Mikutano na Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira kama ifuatavyo:-

#### 4.1.2 Mikutano na Wizara ya Maliasili na Utalii

Kamati ilikutana na Wizara ya Maliasili na Utalii na kupokea taarifa mbalimbali kama zilivyoainishwa hapa nchini.

#### 4.1.3 Mgogoro wa mpaka kati ya shamba la uwekezaji (eko-energy) la Bagamoyo na Hifadhi ya Taifa ya Saadan

**Mheshimiwa Spika,** Hifadhi ya Taifa ya Saaadan ilianzishwa mwaka 2005 kwa Tangazo la Serikali GN na 281. Lengo la kuanzisha Hifadhi hii ilikuwa ni kuunganisha maeneo ya Hifadhi katika mifumo ya ikolojia moja ili kuwa na Ikolojia mseto na timilifu. Mambo yaliyozingatiwa na Serikali katika kuanzisha hifadhi hii ni pamoja na;

i. Kuhifadhi maeneo muhimu kwa mtawanyiko wa wanyamapori (dispersal areas), eneo la mazalia (breeding sites) na mapito ya wanyama (migratory Routes)

ii. Kuhifadhi eneo la mazalia ya kasa kijani (green Turtle)

iii. Kulinda na kuhifadhi msitu wa mikoko na estuary ya mto Wami ambayo ni mazalia ya samaki na malisho kwa ndege wahamao.

iv. Kulinda na kuhifadhi Tembo hasa shoroba zinazotumiwa na tembo kuhama hama kati ya maeneo ya selous, Mikumi, Wami mbiki na Saadan.

v. Kulinda na kuhifadhi matumbawe (coral reefs) na majani ya bahari (sea grass).

vi. Kuhifadhi Palahala (sable antelope).

vii. Kuongeza ulinzi wa mimea ya **Alalia zanzibarica.**

viii. Uhifadhi wa msitu **wa zaraninge** ambao ni makazi muhimu ya mbega Mweusi na Mweupe (Black and white **colobus** monkey).

**Mheshimiwa Spika,** Mwaka 2008, mwekezaji anayejulikana kama Bagamoyo Eko Energy Tanzania Limited alimilikishwa eneo linalopakana na Hifadhi ya Taifa ya Saadan kwa hati na 120397 ambayo ilimega eneo la hifadhi na hivyo kukiuka mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Saadan kama ilivyo ainishwa na Tangazo la Serikali Na. 281 la mwaka 2005.

**Mheshimiwa Spika,** Bagamoyo Eko Energy (T) Limited walipewa eneo hilo kwa ajili ya Kilimo cha miwa ili kuzalisha Sukari (bioethanol) na umeme. Kampuni hii inadai kwamba sehemu ya ardhi ya shamba hilo lenye ukumbwa wa hekta

3,441 ambazo ni sehemu ya Hifadhi ya Taifa ya Saadan.Madai ya Eco Energy kwamba imevamia eneo lake kwa maana ya nani kavamia mwenzake hayana msingi. Hifadhi ya Saadan ilianzishwa mwaka 2005, inakuwaje Eco Energy aliyepewa hati ya kumiliki ardhi hiyo mwaka 2008 adai kavamiwa? Baada ya kupata maelezo kutoka Wizara zinazohusika hasa wizara ya Ardhi na wizara ya Maliasili na Utalii Kamati iligundua kwamba katika suala hili hapakuwa na ushirikiano baina ya Wizara hizi mbili za serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya Kamati kusikiliza maelezo toka kwa Wizara ya Ardhi na Wizara ya Maliasili, Kamati imebaini kwamba chanzo cha mgogoro ni Serikali yenyewe, Kwamba Wizara zake katika kutekeleza majukumu yake katika baadhi ya maeneo kutoshirikiana. Kama kungekuwa na ushirikiano Wizara ya Ardhi wakati ikijua eneo hilo linasimamiwa na Sheria nyingine ya nchi isingefaa kutoa hati juu ya ardhi ambayo tayari inasimamiwa na sheria nyingine.

**Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali yafuatayo:-

- Wakati wizara hizi mbili za serikali zikijadili ijinsi ya kutatua tatizo hili, sheria ya uhifadhi iheshimiwe na mipaka ya hifadhi ya Saadan kwa mujibu wa GN 281 ya 2005 ilindwe na kuheshimiwa.

- Serikali kama inajiridhisha kwamba umuhimu wa kilimo cha miwa ni bora zaidi kuliko sababu zilizopelekea kutangaza eneo la Saadan kuwa hifadhi ya Taifa basi Serikali ilete mbele ya Bunge lako tukufu Azimio la Serikali la kubadili mipaka ya hifadhi ya Taifa ya Saadan kama sheria inavyotaka.

### 4.1.4 Mgogoro wa mipaka ya msitu wa Hifadhi Kazimzumbwi

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Mgogoro wa mipaka katika msitu wa hifadhi kazimzumbwi wenye ukubwa wa hekta 4,862 ambao ulitangazwa kuwa hifadhi ya Msitu mwaka 1954 kwa Tangazo la Serikali Na. 306 na Ramani Na. Jb 196. Msitu huu ni muhimu kwa maisha ya wakazi wa jiji la Dar es Salaam kwa kuwa ndio chujio la hewa inayotumika katika jiji na viunga vyake na chanzo kikuu cha maji yanayotiririka katika mto mzinga.

**Mheshimiwa Spika**, malalamiko ya wananchi wa kitongoji cha Nzasa kuhusu mipaka ya msitu wa hifadhi Kazimzumbwi ni ya muda mrefu na jitihada mbalimbali za kutatua mgogoro huu zimehusisha vyombo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu, ambayo ilitoa maagizo ya jinsi ya kumaliza mogoro huo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza maagizo ya Waziri Mkuu na kwa hatua ilizochukua kuwaondoa wavamizi wote ndani ya Msitu wa hifadhi wa kazimzumbwi, hatua ambayo itanusuru Msitu huu na kuuwezesha kurejesha uoto wake wa asili ambao ni muhimu kwa maisha ya wakazi wa jiji la Dar ES Salaam na maeneo mengine yaliyoko karibu na msitu huu.

**Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa** Spika**,** Pamoja na pongezi hizo Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

- Serikali iwachukulie hatua za kinidhamu watendaji wote wa Wizara ya Ardhi pamoja na wale wa Manispaa ya Ilala walioshiriki kwa namna moja au nyingine katika kutoa tafsiri potofu ya mipaka ya Msitu huu hali

iliyopelekea wananchi kuvamia hifadhi hiyo muhimu na kufanya uharibifu mkubwa.

- Mipaka ya Msitu huo iimarishwe kwa kuweka alama za kudumu na doria maalum iendelee kufanyika kuzunguka hifadhi kuzuia wananchi kurudi tena ndani ya hifadhi.

- wananchi waelimishwe juu ya umuhimu na faida ya msitu wa hifadhi kazimzumbwi kwa wananchi wanouzunguka jiji la Dar Es Salaam.

- Wakala wa Misitu nchini waandae Mkakati maalum wa Kupanda miti ya asili ili kurudisha uoto wa asili katika maeneo yaliyoharibiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia inaishauri Serikali kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi wa Manispaa ya Ilala waliohusika kugawa viwanja kwa wananchi katika maeneo ya msitu wa hifadhi wakati wakijua ni kinyume cha sheria.

### 4.1.5 Mgogoro wa mipaka ya pori la Akiba la Mkungunero

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 19/12/2014 Kamati ilitembelea Pori la Akiba la Mkungunero na Vijiji vinavyopakana na Pori hilo vya Kimotorok kilichoko katika wilaya ya Simanjiro na Irkuishbor kilichoko katika wilaya ya Kiteto. Kamati ilipokea na kujadili taarifa iliyowasilishwa na Wizara kuhusu mgogoro wa mipaka katika pori hilo. Kamati pia ilizungumza na wananchi wa vijiji hivyo.

**Mheshimwa Spika**, Hali ya mgogoro uliopo kati ya Pori la Akiba la Mkungunero na wananchi wanaopakana na Pori kwenye mikoa ya Dodoma na Manyara ni mkubwa na unahatarisha amani katika eneo hilo na maafa makubwa yanaweza kutokea

wakati wowote kama serikali haitachukua hatua za haraka za kumaliza mgogoro huo.

**Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali ichukue hatua za haraka kumaliza mgogoro huo ikiwa pamoja na kutambua hatua ya vijiji 5 vya taarifa ya Makami ya kuanzisha hifadhi yao ya Jamii (WMA) iliyoridhiwa Wizara ya Maliasili na Utalii mwaka 2011.

- Wizara ikamilishe haraka mchakato wa kurejesha eneo la kilomita 50 za mraba la Vijiji viwili pamoja na kijiji Irkiusholborr vilivyoko katika Wilaya ya Kiteto kutoka katika eneo la Pori la Akiba la Mkungunero kwa sababu eneo hilo liliingizwa kimakosa

- Wizara ya Maliasili na Utalii kila inapofanya zoezi la kuhakiki ama kuweka mipaka ya hifadhi ni lazima ishirikishe Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi lengo likiwa ni kumaliza tatizo la migogoro ya mipaka kama ilivyo sasa.

**4.1.6. Uchimbaji wa Madini ndani ya hifadhi ya taifa ya manyara**

**Mheshimiwa Spika**, Sheria namba 5 ya hifadhi hairuhusu uchimbaji wa madini ndani ya Hifadhi za Taifa isipokuwa kwa strategic minerals tu. Madini hayo ni Urani, Gesi na Petrol . Hivyo leseni zilizotolewa kwa Makampuni yanayochimba madini katika hifadhi ni batili.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kutembelea Hifadhi ya Taifa ya ziwa Manyara na kujionea uharibifu mkubwa unaotokana na uchimbaji

huo wa madini. Kamati ilielezwa kwamba makampuni hayo yalipewa leseni kihalali kabla ya eneo halijaingizwa ndani ya hifadhi na kupewa kibali maalum cha kuendelea kuchimba hadi muda wa leseni kumalizika ambazo zote zilikuwa zinafikia ukomo mwezi Februari mwaka huu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeelezwa kwamba kati ya leseni hizo 8 ambazo ukomo wake ni mwezi Februari mwaka huu, leseni moja PML 0012658 ya Ahmed Saad ukomo wake ni mwaka 2020 kinyume cha utaratibu.Kamati inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako tukufu ni kwa taratibu na sheria gani imempa mamlaka Kamishina wa madini kutoa leseni kwa miaka 12 badala ya miaka mitano kama sheria inavyotaka.

Aidha**,** Kamati inaitaka Serikali kusitisha mara moja leseni hii na kuwachukulia hatua stahiki watendaji wa Wizara ya Nishati na Madini waliohusika na utoaji wa leseni hii wakati wakijua ni kinyume cha sheria.

**4.1.7 Mpaka wa Bologonja**

**Mheshimiwa Spika**, Kufuatia fununu kwamba mpaka wa Bologonja unaotenganisha nchi ya Tanzania na Kenya hifadhi ya Masai Mara kwa upande wa Kenya na hifadhi ya Taifa ya Serengeti kwa upande wa Tanzania utafunguliwa. Kamati ilifanya ziara katika eneo hilo kuona hali halisi na ukweli wa fununu hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilishuhudia shughuli za utalii zikiendelea vizuri. Kamati ilipata fursa ya kuhoji baadhi ya watalii waliokuwepo katika eneo hilo kama waliingia kupitia lango hilo. Aidha wengi wa watalii waliohojiwa kama wangependa lango hilo lifunguliwe walikataa kwa kusema kwamba hali hiyo ingefungua mlango kwa maelfu kupita lango hilo na kuingia Serengeti kwa siku moja na kurejea Masai Mara ambako kuna hotel nyingi.

Aidha kufunguliwa kwa lango la Bologonja kutaharibu sifa ya miaka mingi ya Serengeti kuwa ni hifadhi pekee barani Afrika ambayo mtalii anaweza kuona wanyama wakubwa (The big 5) bila ya kuwapo msongamano wa magari na watalii. Walipongeza Sera ya uhifadhi ya Tanzania ya kupokea wageni wachache lakini mapato makubwa tofauti na Nchi jirani anbayo Sera yake ni watalii wengi mapato kidogo.

Kamati inaishauri Serikali kutofungua mpaka wa Bologonja kwa maslahi ya uhifadhi endelevu, kulinda mapato makubwa yanayopatikana hivi sasa kwa faida ya Taifa letu na vizazi vilivyopo na vijavyo.

**4.1.8 Kesi dhidi ya tozo kwa watalii wanaolala katika Hoteli zilizoko katika Hifadhi za Taifa**

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 12 Septemba, 2014, Mahakama Kuu Kanda ya Arusha ilitoa Hukumu ya kesi iliyokuwa imefunguliwa na baadhi ya wamiliki wa Hoteli zilizoko katika hifadhi za Taifa dhidi ya TANAPA kupinga TANAPA kuanza kutoza tozo mpya kwa mfumo wa "Fixed Rate" badala ya mfumo wa zamani wa "Concession Rate".

Katika Hukumu hiyo Mahakama iliiagiza Wizara ya Maliasili na Utalii kutoa Tangazo katika gazeti la Serikali kuhusu kuanza kutumika kwa tozo mpya. Ni miezi takriban minne sasa tangu kutolewa kwa hukumu hiyo Wizara ya Maliasili na Utalii haijatekeleza hukumu hiyo, hali ambayo inasababisha TANAPA na Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro kuendelea kupoteza mapato yanayofikia shilingi za Tanzania billion mbili kila mwezi. Tangu kufunguliwa kwa kesi hiyo mwaka 2011 hadi Septemba 2014 shirika la Hifadhi za Taifa limepoteza karibu shilingi billion 80 kutokana na kukosa malipo ya Tozo hiyo. Kamati iliitaka Wizara ya Maliasili na Utalii iwe imeshatoa Tangazo katika Gazeti la Serikali ifikapo tarehe 28 Januari, 2015. Kamati

inataka Serikali itoe maelezo ya sababu ya kutofanya hivyo.

### 4.1.9 Ziara Katika Hifadhi ya Taifa ya Arusha

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ziara katika hifadhi ya Taifa ya Arusha na kupokea taarifa kuhusu mgogoro baina ya hifadhi ya Taifa ya Arusha na Wakala wa Misitu Tanzania.Chimbuko la mgogoro huu ni Tangazo la Serikali (GN) Na. 280 la 2005 ambalo liliongeza mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Arusha kwa kuongeza Misitu ya hifadhi ya Meru na Ngurudoto (**"Declaration of Arusha National Park to Include Ngurudoto and Meru Forest Reserve"**). Tangazo hilo la Serikali lililenga kudhibiti uharibifu mkubwa wa Misitu ya Asili ya mlima Meru na Ngurudoto ambayo ulitishia kuharibu kabisa ikolojia ya eneo hilo na vyanzo vya maji kwa jiji la Arusha na maeneo yanayozunguuka mlima Meru.

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia tangazo hilo kuliibuka mgogoro baina ya taasisi hizo mbili huku hifadhi ya Taifa ya Arusha ikishindwa kabisa kusimamia GN namba 280.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusikiliza maelezo ya pande zote mbili na kutembelea eneo la mgogoro Kamati iliishauri Serikali kukazia yaliyomo katika GN namba 280 lakini kuleta Azimio la mabadiliko madogo ya mipaka ya GN 280 ya kuondoa maeneo ya Chuo Kikuu cha Sokoine na Chuo cha Misitu cha Olmotonyi na eneo lingine lote likijumuisha msitu wa kupanda libaki ndani ya hifadhi ya Taifa ya Arusha kulinda ikolojia na vyanzo vya maji vya jiji la Arusha. Wakati hayo yakiendelea Kamati ilishauri serikali kuhakikisha TANAPA wanatekeleza jukumu lao la kulinda mipaka ya hifadhi hiyo kwa mujibu wa GN namba 280.

### 4.1.10 Hali ya Misitu Nchini

Kamati ilipokea Taarifa kuhusu Hali ya Misitu Nchini. Kamati ilitoa ushauri uliogawanyika katika maeneo yafuatayo:-

(a) Kuujengea Wakala uwezo wa kimfumo, kitaasisi na kiutendaji.

(b) Kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za misitu na nyuki.

(c) Kuongeza kasi ya upandaji miti.

(d) Udhibiti wa uvamizi wa misitu ya hifadhi na utatuzi wa migogoro ya mipaka.

Aidha Kamati inaishauri Serikali:-

(a) Kuanzisha mchakato wa kuipandisha hadhi Wakala wa Misitu Tanzania, kutoka Wakala wa Misitu Tanzania kuwa Mamlaka Kamili (automomous organisation). Hatua hii itaisaidia Wakala wa Misitu Tanzania kuwa na uwezo wa kufanya maamuzi ya kiutendaji kwa haraka na; kuongeza kasi ya kuajiri watumishi, kutumia sehemu kubwa ya mapato yake kuliko ilivyo sasa na kuendeleza rasilimali za misitu na nyuki.

(b) Kuanzisha mfumo wa kusimamia rasilimali zilizopo kwenye maeneo yanayomilikiwa na Halmashauri za Wilaya na Vijiji. Mfumo utakaoanzishwa utawezesha usimamizi wa eneo kubwa la misitu ambalo takwimu zinaonyesha kuwa lipo chini ya Halmashauri na Vijiji (53% ya eneo la lote la misitu), eneo ambalo hivi sasa linakabiliwa na jangwa kutokana na usimamizi mbovu wa Halmashauri

(c) Katika kipindi cha mpito kuelekea kuwa mamlaka kamili, Serikali iweke mfumo wa kuhakikisha Wakala wa Misitu Tanzania inabakiza kiasi kikubwa cha mapato yake ili kuongeza kasi ya uhifadhi, upandaji miti na ushirikishwaji na utoaji elimu kwa jamii. Hatua hii itasaidia pia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika kupunguza gesi ukaa inayotokana na uharibifu wa misitu.

(d) Kuanzisha utafiti unaolenga kuboresha uhifadhi wa vinasaba na athari za upandaji wa miti ya misaji.

### 4.1.11 Mgogoro wa mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha

Kamati ilipokea taarifa kuhusu mgogoro wa mpaka kati ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na wananchi wanaozunguuka hifadhi hiyo. Kamati inashauri Serikali yafuatayo:-

(a) Kuendeleza mazungumzo kuhusu utatuzi wa mgogoro huo na yahusishe wadau wote na Serikali ichukue hatua madhubuti na za haraka kumaliza mgogoro huo.

(b) Kutokana na umuhimu wa eneo la ardhi oevu kuwa katika Bonde la Usangu na ambalo liko ndani ya mpaka wa hifadhi kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 281 la mwaka 2008, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha GN namba 281 ya 2008 pamoja na mipaka yake yote inaheshimiwa.

### 4.1.12 Mgogoro wa Mpaka Hifadhi ya Taifa ya Tarangire

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea Hifadhi ya Taifa ya Tarangire kwa lengo la kujionea maeneo yenye mgogoro wa mipaka. Ikiwa Tarangire Kamati ilitembelea kijiji cha Kimotorok kilichoko wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara na kuzungumza na wananchi wa kijiji hicho juu ya namna ya umaliza mgogoro huo. Aidha Kamati ilitemeblea kijiji cha Ayamango kilichopo katika wilaya ya Babati ambacho kipo ndani ya hifadhi na wananchi tayari wamelipwa fidia lakini wanasubiri eneo la kuhamia.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu maeneo haya matatu tuliyoyatembelea Kamati inashauri:-

- TANAPA na wananchi wa Kimotorok wakae pamoja na wajadili jinsi gani watamaliza mgogoro huo njia pekee iwe kuanzisha Wildlife Management Area (WMA) ambayo itasimamiwa na wananchi wenyewe. Aidha mipaka ya Hifadhi na ile ya Kijiji ibainishwe.

- Ardhi mbadala ipatikane haraka ili wananchi wa kijiji cha Ayamango wanaopaswa kuhama wahamie huko.

### 4.1.13 Kupotea kwa Shoroba za Wanyamapori

**Mheshimiwa Spika,** wakati Kamati ikiwa katika ziara ya Kanda ya Kaskazini ilibaini kuwa shoroba za wanyamapori zimeanza kuzibwa na zingine kuzibwa kabisa hivyo kuzifanya baadhi ya Hifadhi za Taifa na Mapori ya Akiba kugeuka visiwa. Kwa mfano, Kamati ilijionea ongezeko la shughuli za kilimo na makazi kwenye shoroba ya wanyamapori ya Tarangire inayounganisha Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Hifadhi ya Taifa ya Manyara na Hifadhi ya Tarangire.

Ushoroba huu umekaribia kuziba kabisa hali itakayowafanya wanyama washindwe kuzunguka kama ilivyo kawaida yao ya asili.

**Mheshimiwa Spika,** hali hii ni hatari kwa uhifadhi. Shoroba nyingine ambazo zimekufa kabisa ni pamoja na ushoroba unaounganisha hifadhi ya Kilimanjaro na ile ya Arusha hadi Mikumi. Hali hii imezua tatizo la "inbreeding" katika hifadhi ya Arusha jambo ambalo litapelekea kutoweka kwa baadhi ya wanyama katika maeneo hayo isipodhibitiwa. Kwa kuzingatia athari hizo, Kamati inashauri Serikali kufanya yafuatayo:-

(a) Kuandaa mkutano wa wadau utakaojadili na kupata ufumbuzi kuhusu uhifadhi wa shoroba za wanyamapori.

(b) Kuzitambua na kuzitangaza shoroba za wanyamapori zilizopo.

(c) Kuandaa utaratibu wa kuhifadhi shoroba kwa mujibu wa sheria ya wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009.

#### 4.1.13.1 Ziara katika Msitu wa Mikoko wa Kijiji cha Tongoni - Tanga

**Mheshimiwa Spika,** ikiwa Mkoani Tanga Kamati ilitembelea eneo la kijiji cha Tongoni ambacho pamoja na shughuli nyingine kinajihusisha na uhifadhi wa mikoko. Wananchi wa Tongoni walieleza Kamati kwamba kazi ya kuhifadhi mikoko ina changamoto nyingi kubwa ikiwa ni kudhibiti majangili wa mikoko na uhaba wa vitendea kazi.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa miti ya mikoko ni muhimu kwa ustawi wa maisha ya wananchi wanaoishi katika maeneo ya mwambao wa Pwani kimazingira na kiuchumi, Kamati inaishauri Serikali-

(i) Kuhamasisha upandaji wa miti mbadala utakaowapatia wananchi miti kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ili waachane na matumizi ya sasa ya Mikoko.

### 4.1.14 Ziara Katika Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Amani (Amani Nature Reserve)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilitembelea eneo la Amani Nature reserve tarehe 30/1/2014 ambapo ilipata fursa ya kuongea na uongozi na wananchi wa eneo hilo. Lakini jambo kubwa ni ujangili wa wanyama na mimea ndani ya hifadhi pamoja na uchimbaji wa madini ndani ya hifadhi.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na umuhimu wa hifadhi ya Amani Nature Reserve kwa Taifa letu na ambayo inakabiliwa na changamoto nyingi ili iendelee kuwapo, Kamati inaishauri ya fuatayo:-

(i) Kuajiri watumishi wa kutosha kulingana na mahitaji.

(ii) Kupiga marufuku uchimbaji wa madini ndani na pembezoni wa msitu wa Amani.

(iii) Kuimarisha ushirikiano baina ya uongozi wa hifadhi na serikali za vijjji.

### 4.1.15 HIFADHI YA TAIFA MKOMAZI

**Mheshimwia Spika,** Kamati ilifanya ziara kwenye hifadhi ya Taifa Mkomazi kwa lengo la kuona maendeleo ya mradi wa faru weusi. Ikiwa mkomazi Kamati ilibaini yafuatayo.

**Kodi/ushuru kwenye vifaa vya uhifadhi**

Mradi wa Faru Weusi katika Hifadhi ya Taifa Mkomazi unaendeshwa kwa kutegemea rasilimali fedha, vifaa na utaalamu kutoka kwa Wahisani wenye nia njema kwa uhifadhi. Hata hivyo juhudi hizi za wahisani zinakwamishwa na kodi ambayo hutozwa kwa vifaa vinavyotolewa bure na Wahisani kwa Taasisi yenye uwezo mdogo kifedha.

Kodi pia imekuwa ikitozwa kwa kila (mnyamapori) faru anayetolewa msaada kwa lengo la kuongeza idadi yao ili kufikia ***'viable population'*** ambayo imependekezwa kitalaam. Faru wote waliotolewa kama msaada kwa Serikali ya Tanzania wamekuwa wakilipiwa kodi *(Import Duty)* kati ya USD 300-400 kila mmoja. Kodi hii imekuwa ikilipwa na anayetoa msaada jambo ambalo limewaumiza sana wahisani.

Aidha, silaha, vifaa vya kutengeneza barabara na magari yanayoingizwa nchini kwa msaada wa Wahisani kwa ajili ya uhifadhi hulipiwa kodi **(VAT & Import Duty).** Hali hii inakwamisha uhifadhi na pia imekatisha tamaa Wahisani na kama Serikali itaendelea kusimamia msimamo huo, basi tusahau kuhusu mnyama faru kutamalaki Tanzania ambapo ilikuwa na Faru inaokadilia kufikia 200,000. Ieo hii Tanzania inao Faru wasio zidi 30 wengi ni hao waliotolewa kama msaada na kutozwa kodi. Aidha Kamati imesikitishwa na kitendo cha serikali kuzuia bandarini magari 8 aina ya Land Rover yaliyokuwa yametolewa na Jumuiya ya Umoja wa Ulaya(EU) kwa ajili ya uhifadhi wa faru pamoja na silaha kwa ajili ya

kupambana na ujangili ambazo zilikuwa zimezuiliwa bandarini kwa zaidi ya mwaka zikidaiwa kodi. Hii ni aibu kwa nchi yetu.

**Ushauri wa Kamati**

Kamati inaishauri Serikali

- kuandaa na kuwasilisha kwa Kamati taarifa ya kina kuhusu changamoto zinazokabili uhifadhi wa Faru nchini ili iweze kuishauri Serikali ipasavyo .

- Kufuta kodi zote zinazotozwa kwa wanyama faru wanaoletwa nchini kama msaada pamoja na kodi ya vifaa vinavyoletwa nchini kwa ajili ya uhifadhi wa faru kama magari, magreda, silaha na mavazi ya askari.

**4.1.16 Madai ya Stahiki ya askari walioshiriki**

**Operesheni Tokomeza-**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusimamishwa kwa operesheni tokomeza Askari walioshiriki zoezi hilo walianza kudai posho zao ambazo walipaswa kulipwa baada ya zoezi kusimama. Madai ya msingi ya Askari hao (wote walioshiriki) ni posho ya siku 13 kati ya siku 31 za awali zilizokuwa zimepangwa kabla ya kuongezwa kwa muda wa operesheni.Takriban **Tsh. Billion 3.9** zilikuwa zimekusanywa kutoka TANAPA, Wakala wa Misitu Tanzania, Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro na mfuko wa wanyama Pori. Fedha hizi kimsingi zilikuwa zimehifadhiwa makao makuu ya wizara ya maliasili na Utalii. Kimsingi madai ya Askari hayo hayahusishi siku za Operesheni tokomeza zilizoongezeka.

**Ushauri wa Kamati**

**Mheshimwia Spika,** kwa kuzingatia madai hayo ya Askari yamekuwa ya siku nyingi na yanawakatisha tamaa kuendelea na kazi ya kuzuia ujangili, kamati inaitaka Wizara kuwasilisha mbele ya Kamati matumizi ya Fedha hizo **(Bilion 3.9).** Aidha, Kamati imeitaka Wizara sambamba na kutoa taarifa ya matumizi **(Bilion 3.9)** Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali afanye uchunguzi maalum ( Special Audit) wa jinsi pesa hizo zilivyotumika.

**4.1.17 Hali ya Ujangili nchini**

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwaka 2013 hali ya ujangili wa mnyama ndovu au tembo ilikadiriwa kufikia 30 kwa siku. Kiwango hicho kilikuwa cha juu ambacho kilikuwa hakijawahi kufikiwa hapa nchini. Kufuatia hali hiyo, serikali ilichukua hatua ya kuzuia kutokomeza kabisa kwa mnyama ndovu nchini kwa kuanzisha operation tokomeza ambayo pamoja na madhara yaliyojitokeza ilisaidia kuanza kupangua kwa kesi ya ujangili wa tembo nchini.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya operesheni Tokomeza Serikali iliendelea kuchukua hatua zaidi kwa lengo la kutokomeza kabisa tatizo hilo. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuajiri askari zaidi wa wanyamapori ambapo askari wa wanyamapori zaidi ya 500 waliajiriwa na wengine 300 kama vonuntea, kuboresha vitendea kazi vya askari ikiwa pamoja na ununuzi wa silaha za kisasa, magari, mahema na kuendesha operesheni za mara kwa mara. Kutokana na jitihada hizi mafanikio makubwa wamepatikana ambapo silaha zipatazo 2000 zilikamatwa.

Mheshimiwa spika, mbali ya kupongeza hatua iliyofikiwa Kamati inaishauri Serikali kuendelea na

harakati za kupambana kwa nguvu zote na ujangili lakini iangalie upya maslahi ya watumishi hasa askari.

Kamati inaitaka Serikali kuweka wazi haraka iwezekanavyo taarifa ya hali ya ujangili nchini ili wananchi na wadau wa uhifadhi nchini ambao kwa namna moja au nyingine ni washirika wa vita hii, wafahamu kwa lengo la kuzidisha mapambano pale ambapo mambo hayaendi vizuri.

## 5.0 MIKUTANO NA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

### 5. 1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na kupokea taarifa kuhusu utekelezaji wa shughuli mbali mbali zinazofanywa na Wizara pamoja na Taasisi zake.

**Mheshimiwa Spika,** ardhi ni raslimali ya msingi na ya muhimu ambayo shughuli zote za kijamii, kiuchumi na kimaendeleo zinafanyika juu yake. Aidha, ardhi ni raslimali adimu ambayo hushindaniwa na watu na hivyo kuifanya iwe na thamani kubwa.

Kwa sababu hiyo ardhi inatakiwa kumilikiwa Kiserikali na Kimila kwa sheria, Kanuni na taratibu zinazokubalika. Kwa kuzingatia thamani na umuhimu wa ardhi, ni vyema Serikali ikasimamia sheria zake za ardhi kwa manufaa ya maendeleo ya kila mtanzania na kuhakikisha ardhi ya nchi yetu haiuzwi/kumilikishwa ovyo kwa wawekezaji kutoka nje, na hata wakimilikishwa, wamilikishwe kwa masharti.

Nchi kama ya Falme za Kiarabu imepata mafanikio makubwa kwa kutumia ardhi yake kwa manufaa ya wananchi wake na taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa asilimia 80 ya wananchi wa vijijini wanategemea ardhi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi, na kwa kuwa mara nyingi migogoro huanza pale viongozi wa vijiji wanapoingia mikataba mibovu na watu binafsi, makampuni na wawekezaji, ni dhahiri kwamba Serikali isipokuwa makini katika suala la kumilikisha ardhi kwa wananchi, wawekezaji wa ndani na nje na kutoa elimu kwa viongozi wa vijiji, wilaya na maafisa waandamizi wa Wizara ya Ardhi, nchi na wananchi wataendelea kuwa maskini na watwana katika ardhi yao wenyewe. Aidha migogoro ya ardhi inayoendelea nchini hivi sasa isipotafutiwa ufumbuzi nchi yetu itaingia katika machafuko ambayo hayana msingi.

**5.2 Migogoro ya ardhi**

**Mheshimiwa Spika,** Moja ya changamoto kubwa za Wizara hii ni kuongezeka kwa migogoro ya mipaka ya ardhi baina ya watumiaji mbali mbali wa ardhi. Kwa mfano migogoro kati ya wakulima na wafugaji ambayo imeenea katika kila kona ya nchi, migogoro baina ya wawekezaji na wanavijiji, na taasisi za Serikali na wananchi n.k. Migogoro hii, na mingine imesababisha mauaji ya raia na uharibifu mkubwa wa mali za wananchi.

Migogoro hii inachangiwa na sababu mbali mbali ikiwa ni pamoja na kutokupimwa kwa maeneo mengi ya makazi ya wananchi, upatikanaji mgumu wa hati miliki za Kimila, maeneo mengi ya nchi kutokuwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi, na ucheleweshaji wa kulipa fidia pale ambapo wananchi wanatakiwa kuhama na wakati mwingine rushwa, ufisadi na sheria za nchi kutosimamiwa vizuri na ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, moja ya madhumuni ya kuanzisha Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya ardhi ilikuwa ni kupanga matumizi ya ardhi ili kuondoa migogoro baina ya watumiaji wa ardhi. Mipango hii ya matumizi

ya ardhi huongoza utendaji wa sekta zingine kama vile kutenga maeneo ya uwekezaji, kilimo, makazi wanyamapori,misitu, vyanzo vya maji, malisho ya wanyama na shughuli zote zinazotumia ardhi zisigongane.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kuwepo kwa Tume hii bado migogoro ya ardhi imeendelea kujitokeza katika sehemu mbali mbali nchini ikichangiwa na kukosekana kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi.

**Mheshimiwa Spika**,Hadi tunatoa taarifa hii,sehemu kubwa ya ardhi ya nchi yetu bado haijaandaliwa mipango ya matumizi bora ya ardhi. Kati ya Vijiji 11,000 vilivyopo nchini ni ni Vijiji 1,000 tu ndivyo vina mpango wa matumizi bora ya ardhi. Kwa upande wa miji mikuu ya Mikoa, kati ya miji 25 iliyopo ni miji mikuu ya mikoa 10 tu ndiyo ina mipango ( Master Plans)na miji mikuu ya Wilaya yenye mipango ni 20 tu kati ya miji 110iliyopo nchini. Mheshimiwa Spika hili ni tatizo kubwa kwa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali iangalie upya utendaji wa majukumu ya Tume hii kwa lengo la kuiongezea nguvu, lakini pia Serikali iiwezeshe kwa fedha ili iweze kutekeleza malengo yake. Bila fedha za kuiwezesha kupanga ni ndoto za mchana nchi yetu kuandaa na kutekeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi.

**Mheshimiwa Spika**, Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imeshindwa kufanya tafiti kwa wingi kuhusu masuala ya ardhi hasa katika maeneo yenye migogoro kutokana na ufinyu wa fedha. Kwa mfano kwa mwaka wa fedha 2014/15, Tume ilitengewa shilingi billion 1.9 badala ya million 950 waliyopewa katika mwaka wa fedha 2013/14. Lakini hadi kufikia Desemba 2014, Serikali ilishatoa Milioni 308 kwa Tume fedha ambayo haiwezi kusaidia Tume kutekeleza Majukumu yake.

Kamati inaishauri Serikali iache kufanya kazi kwa mazoea na kwa mtindo wa zimamoto wa kupeleka askari polisi wakiwa na mabomu kuzima ghasia za migogoro, badala yake itoe fedha za kutosha kwa Tume ya Mipango ya Matumizi bora ya Ardhi ili ardhi ya nchi yetu itengenezewe mipango kabambe wa jinsi ya kuitumia.

**Mheshimiwa Spika**, sambamba na hilo Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kuanzisha utaratibu wa kuwa na ardhi ya akiba (Land Bank) kwa ajili ya matumizi ya Serikali kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Aidha Kamati inaishauri Serikali itwae mara moja maeneo ya mashamba makubwa yaliyotelekezwa, machache wapewe wananchi na mengi yaingizwe katika orodha ya ardhi ya akiba. Mashamba mengi yaliyotelekezwa yamegeuka kuwa maficho ya majambazi,chanzo cha ugomvi kati ya wenye mashamba na wananchi na wengine yamekuwa vyanzo vya mapato (rushwa) kwa baadhi ya watendaji na viongozi kwa kuyakodisha au kuratibu mipango ya kuyauza kinyemela kwa wamiliki wengine.

**Mheshimiwa Spika**, Mashamba makubwa yaliyotelekezwa kwa miaka mingi yako katika mikoa mingi hapa nchini ikiwa ni pamoja na Pwani,Tanga ,Morogoro,Kilimanjaro, Arusha na Kagera na ndiko kuna vurugu nyingi za wananchi kugombea ardhi.

**Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, miji mingi hapa nchini imeendelea kukua kwa kasi kubwa bila ya kuwa na uwiano na taratibu za mipango miji. Ukuaji huu umechangia kuwepo kwa makazi yasiyo rasmi( Squatter settlements)na ujenzi holela, hasa katika

maeneo ya Mijini ambayo yamekuwa na wahamiaji wengi kutoka Vijijini.

**Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Mipango Miji na 8 ya mwaka 2008 na Sera ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 zinasimamia ukuaji wa miji na majiji na zinatoa dira juu ya namna gani miji ipangwe, kulingana na miundo mbinu ya eneo husika. Hata hivyo, Halmashauri za Manispaa na wilaya zimekuwa zikishindwa kuwapatia wakazi wake huduma mbali mbali zinazotakiwa ikiwa ni pamoja na kupima viwanja kwa ajili ya makazi na kwa mpangilio unaotakiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kusimamia na kutekeleza Sheria ya Mipango Miji kwani mbali na changamoto ya ukuaji wa kasi ya miji, kumekuwepo pia na ukaidi wa makusudi wa wananchi kutotii sheria hiyo.
Aidha ili kurahisisha kazi ya upimaji wa ardhi na hivyo kupunguza malalamiko ya wananchi na wawekezaji na hatimaye kuondokana na migogoro ya ardhi, Serikali ijenge kituo cha kupelekea picha za satellite mjini Dodoma.

Aidha, Kamati inashauri Serikali kwamba uandaaji na utekelezaji wa mipango miji ufuate sheria za Ardhi, zilizopo ikiwa ni pamoja na Sheria ya Ardhi namba nne (4), ya mwaka 1999, sheria ya vijiji namba tano (5) ya Mwaka 1999 na ya mipango miji namba 8 ya 2007 vifungu namba 15, 28 na 29 nasio vinginevyo. Kutozingatiwa kwa Sheria hizi kumesababisha baadhi ya mipango kubadilishwa kiholela kwa masilahi binafisi au watu wachache.

### 5.3 Uendelezaji wa Miji ya Viungani (satellite Cities)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea Mradi wa Luguruni tarehe 16 Januari, 2015 kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa ushauri wa Kamati ulioitaka

Serikali kukabidhi mradi huo kwa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) ili uweze kutekelezwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inayofuraha kulifahamisha Bunge lako tukufu kwamba ushauri wa Kamati yako umetekelezwa na Wizara kwa kukabidhi eneo hilo kwa Shirika la Nyumba kuanza uendelezaji wa Mji wa Luguruni.

Kamati inaipongeza Shirika la Nyumba kwa hatua hiyo stahiki na kwamba liko katika hatua za mwisho za kuanza ujenzi wa Mji mpya wa Luguruni. Miradi mingine inayotekelezwa na shirika hili na ambayo imeanza ni pamoja na ujenzi wa Mji mpya wa Kawe eneo lililokuwa la Tanganyika Packers pamoja na ujenzi wa Mji mpya Usa River Mkoani Arusha, ujenzi wa mji mpya wa Burka Mateves – Arusha na ujenzi wa mji mpya wa Salama Creek Kigamboni.

Kamati inalipongeza Shirika la Nyumba la Taifa kwa kuwa mstari wa mbele kutekeleza malengo ya Nchi na kuyataka mashirika mengine ya Umma kuiga mfano wa Shirika la Nyumba.

## 5.4 SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Nyumba la Taifa lilianzishwa kwa Sheria Na. 2 ya mwaka 1990 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2005. Jukumu la msingi la Shirika hili nikujenga na kuwezesha ujenzi wa nyumba za makazi na majengo ya Biashara kwa ajili ya matumizi ya wananchi na Serikali pia.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza jukumu lake la msingi, Shirika la Nyumba limeendelea na ujenzi wa nyumba katika maeneo mengi hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na jitihada za wazi za Shirika katika kujenga nyumba kwa ajili ya kuuza, bado nyumba hizo zinaonekana kuwa ghali kutokana

na Wanunuzi kulazimika kulipa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT). Kwa mfano, kwa sasa nyumba za bei ya chini zinauzwa **Tsh. Mil 46.9** kujuumuisha VAT, ambapo bila VAT Wanunuzi wangelipa **Tsh. Mil 39.8** ikiwa ni tofauti ya shilling Milion 7.1.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia kwamba Shirika limeweka lengo la kujenga nyumba 15,00 ifikapo mwaka 2015 ili kuwawezesha wananchi wengi hasa wenye kipato cha chini na kati kumiliki nyumba zinazojengwa na Shirika.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mara nyingine tena Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha ione umuhimu wa kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Nyumba za Shirika zinazojengwa kwa ajili ya kuuza kwa wanachi wa kipato cha chini na kati.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na ushauri huo, Kamati inatambua hatua ya Serikali hvi karibuni ya kuondoa ushuru wa Forodha pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa vifaa vya ujenzi vinavyoagizwa na Shirika la Nyumba la Taifa kutoka nje ya nchi. Kamati inaishauri Serikali kuliondolea Shirika la Nyumba VAT Kwa vifaa vya ujenzi vinavyozalishwa hapa nchini.

### 5.6 Mpango kabambe wa Fedha (Financial Master Plan) wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)

Kamati ilipokea taarifa kuhusu mpango Kabambe wa Fedha wa Shirika la Nyumba la Taifa. Kamati ilifahamishwa jinsi Shirika lilivyojipanga kufanya shughuli zake na kwamba lina uwezo wa kufanya kazi za uendelezaji makazi bila kutetereka. Kamati ilifahamishwa kwamba chanzo kikuu cha mapato ya Shirika ni Tozo za pango, mauzo ya nyumba zilizojengwa na Shirika pamoja na vyanzo vingine. Mapato ya shirika yameongezeka kutoka Billioni 33.9 mwaka 2009 hadi kufikia Bilioni 126 mwaka 2014.

Kamati inalipongeza Shirika kwa mafanikio iliyoyapata na kulishauri liweke mikakati endelevu ya kuhakikisha linawezesha watanzania wengi kuwa na makazi bora.

**5.7 Ziara katika mradi wa ujenzi wa nyumba za gharama nafuu za NHC: Mkinga tarehe 29/01/2014:**

Kamati ilitembelea mradi wa Shirika la Nyumba la Taifa wa ujenzi wa nyumba za gharama nafuu wilayani Mkinga mkoani Tanga. Kamati iliipongeza NHC kwa jitihada zake za ujenzi wa nyumba 40 katIka wilaya ya Mkinga. Hadi mwisho wa mwaka Shirika litakuwa limetekeleza mpango huo wa nyumba za gharama nafuu katika wilaya zote.

**5.8 MRADI WA PAMOJA KATI YA JWTZ, WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA NA SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA KWENYE ENEO LA KULENGA SHABAHA (KUNDUCHI RIFLE RANGE)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea taarifa ya kuwekeana saini mkataba wa kushirikiana *(memorandum of understanding)* baina ya Shirika la Nyumba la Taifa kwa upande mmoja na JWTZ na Wizara ya ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa upande mwingine. Mkataba unahusu kufanya kazi kwa pamoja kama wabia katika uendelezaji wa eneo linalojulikana kama Kunduchi Rifle Range lililopo Jangwani Beach Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapongeza jitihada hizi za ushirikiano kati ya NHC na JWTZ na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na kuzitaka Tasisi hizi kuangalia maeneo mengine ambayo wanaweza kuyaendeleza kwa ubia badala ya kuyaacha wazi hivyo kutoa kishawishi kwa wananchi kuyavamia.

## 5.9 Mradi wa viwanja 20,000 mkoani Dar es salaam

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu ulibuniwa mwaka 2002 kutokana na upungufu mkubwa wa viwanja pamoja na kasi kubwa ya ujenzi holela uliokuwa ukiendelea katika jiji la Dar Es Salaam. Kamati iliagiza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuwasilisha taarifa kuhusu mradi wa viwanja 20,000 Mkoani Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika,** kwa bahati mbaya Wizara iliwasilisha taarifa ambayo haikutoa taswira ya maendeleo ya mradi huo, hivyo Kamati kuikataa taarifa hiyo na kuitaka Wizara kuleta mbele ya Kamati taarifa inayojitosheleza.

**Mheshimiwa Spika,** kuna taarifa kwamba katika mradi huu, eneo ambalo serikali ilitumia fedha nyingi kulipa fidia liligubikwa na vitendo vya rushwa vikihusisha baadhi ya watumishi wa Wizara, Watumishi wa Manispaa za miji kujimilikisha viwanja, kuficha baadhi ya maeneo kwa lengo la kuyauza kwa maslahi binafsi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaitaka Serikali kuwabaini viongozi na watumishi wote ambao kwa namna moja au nyingine walihusika katika kuchakachua mradi huu itaweza kupambana na vitendo vya rushwa na matumizi mabaya ya madaraka katika miradi itakayofuata.

## 5.10 ZIARA KATIKA WILAYA YA MAFIA

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ziara katika Wilaya ya Mafia tarehe 22 – 23/1/2015 kwa kutembelea mashamba makubwa ya Utumaini na Ng'ombeni. Aidha Kamati ilipokea taarifa ya Wilaya iliyobainisha migogoro iliyopo katika mashamba hayo baina ya wanachi na wawekezaji.

**5.10.1 Shamba la Utumaini**

**Mheshimiwa Spika**, Shamba la Utumaini la Mafia lenye ukubwa wa ekari 4040 ambalo lilivamiwa na wananchi miaka zaidi ya 40 iliyopita baada ya mwenyewe kulitelekeza na baadaye kuwa msitu, miaka miwili iliyopita shamba hili liliuzwa kwa mmiliki mwingine bila ya kufuata taratibu na sheria za nchi. Mbaya zaidi, hadi Kamati inatembelea shamba hili, si Halmashauri wala ofisi ya mkuu wa Wilaya walikuwa wanajua kama shamba hilo lina mmiliki mwingine. Mipango yote ya kuliuza imefanywa Dar Es Salaam.

**Mheshimiwa Spika**, katika shamba la utumaini Kamati ilibaini migororo ya aina tatu. Kwanza mwekezaji kutelekeza shamba kwa zaidi ya miaka 40. Pili wananchi kuvamia Shamba lililotekelezwa na kufanya maendelezo kwa kulima mazao ya kudumu, kujenga makazi pamoja na kujenga shule na zahanati ndani ya shamba. Tatu kuhamisha ulimiliki wa shamba kutoka kwa mmiliki wa awali kwenda kwa Mmiliki wa sasa bila kufuata taratibu. Shamba limeuzwa Dar ES Salaam bila kushirikisha vyombo, idara na taasisi zinazohusika.

**Maoni na ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** ili kumaliza mgogoro uliopo katika shamba la Utumaini Kamati inashauri yafuatayo:-

- Sheria ya Ardhi ifuatwe

- Ekari 1000 zilizotwaliwa na Serikal mwaka 1967 kwa GN na 983 ziondolewe na kumilikishwa kwa wananchi.

- Serikali ifanye upembuzi yakinifu utakaosaidia kujua mahitaji halisi ya ardhi kwa vijiji vinavyozunguka shamba la utumaini.

- Serikali iwachukulie hatua za kinidhamu watumishi wa Wizara ya Ardhi waliohusika kuuza shamba la Utumaini bila kufuata taratibu.

### 5.10.2 Shamba la Ng'ombeni

**Mheshimiwa Spika**, huko huko Mafia Shamba jingine lenye hati namba 15108 linalomilikiwa na H.J.Stanley ambalo hati ya shamba inaonyesha ni kwa matumizi ya kilimo na ufugaji, shamba hilo ambalo nalo lilitelekezwa kwa muda mrefu limebadilishwa matumizi ya eneo na sasa linazalisha umeme kwa kutumia magogo ya minazi, mikorosho na uoto wa asili wa eneo hilo. Minazi, mikorosho na miti mingi imekatwa katika shamba hilo kiasi cha kuhatarisha mazingira ya kisiwa cha Mafia.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imejionea uharibifu mkubwa wa mazingira hususan ukataji wa miti na minazi katika shamba la Ng'ombeni. Aidha, Kamati imebaini kuwa mwekezaji amebadili matumizi ya Shamba bila kufuata taratibu na kwamba matumizi yaliyopo hayaendani na yaliyoidhinishwa.

Kamati inaishauri serikali yafuatayo:-

- Serikali itekeleze wajibu wake wa kusimamia Sheria ya Ardhi na Sheria ya Mazingira

- Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lifanye tathmini ya athari za ufuaji umeme kwa kutumia magogo ili kuona kama mradi huo ni endelevu.

- Taratibu za kubadili matumizi ya shamba zifuatwe ikiwa ni pamoja na kuishirikisha Halmashauri ya Wilaya ya Mafia.

## 6.0 MKUTANO NA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA)

Kamati ilikutana na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na kupokea taarifa kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Mazingira katika migodi ya dhahabu. Aidha Kamati ilipokea taarifa kuhusu utekelezaji wa agizo la Serikali la kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya Plastiki yenye unene wa micron chini ya 30.

### 6.1 Utekelezaji wa Sheria ya Mazingira

Kamati imebaini mgongano wa kitaasisi ambao unakwamisha utekelezaji wa Sheria ya Mazingira. Pia Kamati inasikitishwa na bajeti finyu ya mazingira inayotolewa kila mwaka hali ambayo inaifanya Wizara na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira kushindwa kufuatilia na kusimamia Sheria ya Mazingira kikamilifu.

### 6.2 Matumizi ya Mifuko ya Plastiki

Kamati ilipokea taarifa kuhusu utekelezaji wa agizo la Serikali kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya Plastiki nchini. Kamati inaishauri Serikali kujifunza kutoka nchi nyingine kama India, Dubai jinsi ilivyofanikiwa katika udhibiti wa matumizi ya mifuko ya plastiki badala ya kupiga marufuku.

**Maoni na ushauri wa Kamati**

Kamati inaishauri Serikali mambo yafuatayo:-

- Kuhuisha Sera na Sheria ya Mazingira. Hii itasaidia kuondoa migongano ya kitaasisi kati ya NEMC na taasisi zingine.

- Kuanzisha mfuko wa Mazingira

- Kuhakikisha kuwa Wizara zote, Sekretarieti za mikoa, Halmashauri za Wilaya, miji, Manispaa na jiji, pamoja na migodi yote inakuwa na afisa mazingira.

- Kufanya marekebisho katika Sheria iliyounda Baraza la usimamizi wa Mazingira (NEMC) ili kulibadili Baraza hilo kuwa Mamlaka. Hii itasaidia kulipa Baraza nguvu zaidi ya kusimamia Sheria ya Mazingira.

### 6.3 ZIARA KATIKA MGODI WA NORTH MARA 27 OKTOBA 2014

Kamati ilitembelea Mgodi wa North Mara tarehe 27 Oktoba 2014 kukagua utekelezaji wa Sheria ya mazingira. Kamati iliridhishwa na hatua zinazochukuliwa na Mgodi kutekeleza Sheria ya mazingira. Kamati imeshauri elimu zaidi kuhusu utunzaji wa Mazingira maeneo yanayozunguka MGODI itolewe kwa wananchi ambao ndio wadau wakubwa.

Kamati inaishauri Serikali ya Wilaya ya Tarime kuchukua hatua za haraka kuzuia ujenzi wa nyumba zinazojulikana kama "Tegesha" katika eneo la mita 200 ambalo Mgodi wa North Mara umepewa. Aidha, Kamati imeagiza tathmini ya eneo hilo ifanyike haraka na fidia zilipwe ili kuepusha migogoro inayoweza kujitokeza.

### 6.4 Ziara katika Mgodi wa Geita Gold Mine

**Mheshimiwa Spika**,Kamati ilitembelea Mgodi wa dhahabu wa Geita kwa lengo la kukagua utekelezaji wa Sheria ya Mazingira pamoja na utekelezaji wa maagizo ya Kamati iliyoyatoa wakati ilipotembelea Mgodi huo mwaka 2012. Kamati iliridhishwa na hatua zinazochukuliwa na Mgodi huo kutekeleza Sheria ya Mazingira.

Aidha, Kamati iliridhishwa na hatua zilizochukuliwa kukarabati bwawa la kuhifadhia maji machafu yatokayo katika kiwanda cha kuchanjua dhahabu (TSF). Kamati imepongeza Mgodi wa dhahabu wa Geita kwa kujenga shule ya Sekondari ya Wasichana ya kisasa mjini Geita.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeelezwa tatizo la uharibifu mkubwa wa misitu mkoani Geita unaotokana na ongezeko kubwa la watu wanaokuja kuchimba dhahabu. Uharibifu wa misitu unasababishwa na matumizi ya miti katika uchimbaji wa dhahabu unaofanywa na wachimbaji wadogo wanaotumia teknolojia duni za uchimbaji dhahabu. Aidha, uharibifu mwingine wa misitu unasababishwa na ujenzi wa makazi. Kamati inaushauri uongozi wa Mkoa kuzuia uharibifu wa misitu kwa kuhamasisha ujenzi wa makazi bila kuharibu misitu. Aidha, Kamati inapinga mpango wa Mkoa wa Geita wa kuchukua hekta elfu kumi za misitu kwa ajili ya kujenga makazi ya watu.

**6.5 Ziara katika Mgodi wa Bulyankhulu tarehe 29 Oktoba, 2014**

Kamati ilifanya ziara katika Mgodi wa Dhahabu wa Bulyankhulu tarehe 29 Oktoba, 2014. Kamati iliridhishwa na hatua zinazochukuliwa na Mgodi huo katika kutekeleza Sheria ya Mazingira, kutekeleza maagizo ya Kamati ilipotembelea Mgodi huo mwaka 2012. Yaliyotekelezwa ni pamoja na kujenga maeneo ya kukusanyia taka za Plastiki sambamba na kujenga vizuizi vya kudhibiti uvujaji wa mafuta ya mitambo (hydro carbons) kuenea katika mazingira.

**6.6 Ziara katika Mgodi wa Dhahabu wa Buzwagi Tarehe 30 Oktoba, 2014**

Kamati ilitembelea Mgodi wa dhahabu wa Buzwagi tarehe 30 Oktoba 2014 kwa nia ya kukagua utekelezaji

wa Sheria ya mazingira pamoja na maagizo ambayo Kamati iliyatoa wakati ilipotembelea Mgodi huo mwaka 2012.

Kamati iliridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Mgodi kutekeleza maagizo ya Kamati, yakiwemo ujenzi wa mabwawa ya kisasa ya kuhifadhia maji taka yanayotoka katika kiwanda cha kuchenjulia dhahabu. Aidha Kamati ilipongeza jitihada za mgodi katika kujenga mahusiano na wananchi wanaoishi kando kando ya mgodi huo ambayo miradi kama ya ujenzi wa kituo cha afya cha kisasa ukarabati wa majengo ya shule, kituo cha afya cha kisasa, ukarabati wa majengo ya shule za msingi, ujenzi wa baadhia ya majengo ya shule ya sekondari.

**6.7 Ziara katika kiwanda cha Falcon cha kuchakata taka za plastiki tarehe 28 Oktoba, 2014**

Kamati ilifanya ziara katika kiwanda cha Falcon kilichoko mjini Mwanza, Kamati ilijionea jinsi taka za plastiki zinavyochakatwa na kutoa bidhaa za plastiki zinazotumika kutengeneza meza, milango, madawati na hivyo kupunguza matumizi ya mbao katika Kutengeneza samani za nyumbani.Kiwanda hiki siyo tu kinalinda mazingira kwa kuokoa misitu na mazao yake, bali pia kinachangia kuliweka jiji la Mwanza katika hali ya usafi kwa kuzitumia taka za Plastiki.

Kamati imeushauri uongozi wa Kiwanda cha Falcon kuongeza ufanisi wa kukusanya taka za Plastiki. Aidha Kamati imeshauri uwezekano wa Kiwanda kama hiki kujengwa katika jiji la Dar es Salaam ambako kuna taka nyingi za Plastiki.

Kamati inaishauri Serikali kuhamasisha matumizi ya bidhaa za Kiwanda cha Falcon ambazo zitaokoa misitu kwa kupunguza matumizi ya mbao katika

kutengeneza samani kama vile meza, milango, madawati na kadhalika.

**6.8 Ziara katika kiwanda cha Falcon cha kuchakata taka za plastiki tarehe 28 Oktoba, 2014**

Kamati ilifanya ziara katika kiwanda cha Falcon kilichoko mjini Mwanza, Kamati ilijionea jinsi taka za plastiki zinavyochakatwa na kutoa bidhaa za plastiki zinazotumika kutengeneza meza, milango, madawati na hivyo kupunguza matumizi ya mbao katika Kutengeneza samani za nyumbani.Kiwanda hiki siyo tu kinalinda mazingira kwa kuokoa misitu na mazao yake, bali pia kinachangia kuliweka jiji la Mwanza katika hali ya usafi kwa kuzitumia taka za Plastiki.

Kamati imeushauri uongozi wa Kiwanda cha Falcon kuongeza ufanisi wa kukusanya taka za Plastiki. Aidha Kamati imeshauri uwezekano wa Kiwanda kama hiki kujengwa katika jiji la Dar es Salaam ambako kuna taka nyingi za Plastiki.

Kamati inaishauri Serikali kuhamasisha matumizi ya bidhaa za Kiwanda cha Falcon ambazo zitaokoa misitu kwa kupunguza matumizi ya mbao katika kutengeneza samani kama vile meza, milango, madawati na kadhalika.

**7.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** mafanikio ya Kamati yangu katika kutekeleza shughuli zake kwa mwaka 2014 yametokana na ushirikiano wa karibu sana na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara hizi, Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa pamoja na Wadau wetu wote, napenda kuwashukuru wote kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** napenda pia kutoa shukrani kubwa kwa ushirikiano tulioupata kutoka kwenye ofisi yako Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Dkt. Thomas Kashililah pamoja na Katibu wa Kamati hii Ndugu Gerald Magili kwa kuratibu shughuli zote za Kamati kwa kipindi chote cha mwaka 2014.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo haya nachukua fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwa kutoa maoni, ushauri pamoja na ushirikiano wao kwenye Kamati, hali ambayo imewezesha kutekeleza na kufanikisha kazi nyingi za Kamati yetu.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

James D. Lembeli, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI,**
**MALIASILI NA MAZINGIRA**

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji.

**MHE. SAID J. NKUMBA (K.n.y. MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):** Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kusoma taarifa yangu, nitumie fursa hii kuwapa pole wakazi wa Wilaya ya Sikonge kwa ajali ya gari ambayo imetokea na kuua baadhi ya Wanakwaya wa Kanisa la Moravian. Mungu awalaze mahali pema peponi na wale waliopata majeraha awape nafuu.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, naomba niwasilishe taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Kamati ya Bunge Kilimo, Mifugo na Maji kwa kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari, 2015.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu taarifa ya shughuli zilizofanywa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji Kwa kipindi cha Januari 2014 hadi Januari 2015.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ina jukumu la kusimamia utendaji wa Wizara za Kilimo, Chakula na Ushirika; Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; na Wizara ya Maji. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Nyongeza ya Nane, Kifungu cha 6(9) kikisomwa sambamba na Kifungu cha 7(1), majukumu ya Kamati hii ni kama yafuatavyo:-

(i) Kuchambua bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati;

(ii) Kuchambua Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa na Wizara ili kujadiliwa na kupitishwa au kuridhiwa na Bunge;

(iii) Kushughulikia taarifa za kila mwaka za utendaji za Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii; na

(iv) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(b) ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, shughuli zilizopangwa Kufanyika katika kipindi cha Januari 2014 hadi Januari 2015. Katika kipindi cha Januari 2014 - Januari 2015, Kamati ilipanga kufanya kazi zifuatazo:-

(i) Kuchambua bajeti za Wizara husika;

(ii) Kuchambua Miswada ya Sheria, Maazimio na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge;

(iii) Kufanya mikutano mbalimbali na watendaji wa Wizara inayozisimamia ili kujadili taarifa za utendaji za Wizara hizo na kutoa maoni, ushauri pamoja na maelekezo;

(iv) Kufanya ziara katika sehemu mbalimbali nchini ili kujionea utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara husika; na

(v) Kufanya ziara za mafunzo nje ya nchi katika sekta za Kilimo, Mifugo na Maji.

Mheshimiwa Spika, shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa Kipindi cha Januari 2014 hadi Januari 2015. Katika kipindi cha Januari 2014 hadi Januari 2015, Kamati ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kuchambua utekelezaji wa Mipango ya Bajeti ya Wizara zote inazozisimamia kwa mwaka wa Fedha 2014/2015;

(ii) Kuchambua Maazimio na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge;

(iii) Kufanya ziara katika sehemu mbalimbali nchini ili kujionea utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara husika; na

(iv) Kufanya ziara za mafunzo ndani na nje ya nchi katika sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na maji.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua utekelezaji wa Mipango ya Bajeti za Mwaka wa Fedha wa 2014/2015 kwa Wizara inazozisimamia. Katika kujadili utekelezaji wa bajeti za Wizara hizo, Kamati ilibaini kuwa Wizara zote tatu zinakumbana na changamoto zinazofanana ambazo ni kutengewa kiasi kidogo cha fedha; kuchelewa kupata fedha hizo hasa za miradi ya maendeleo; na fedha zinazoidhinishwa

na Bunge hazitolewi kwa ukamilifu inapofika mwisho wa mwaka wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu makadirio ya fedha za Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii yaliwasilishwa Bungeni kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2013.

Mheshimiwa Spika, kujadili Maazimio ya Bunge. Katika Kipindi cha Januari 2014 hadi Januari 2015, Kamati ilipokea na kujadili Azimio la Bunge la Mapendekezo ya Kuridhia Makubaliano ya Ushirikiano katika Bonde la Mto Nile "*Agreement on the Nile River Basin Cooperative Framework - CFA*". Pamoja na kwamba Kamati ilichambua Azimio hili na kuandaa maoni na ushauri wake, Azimio hili halikupewa nafasi ya kuwasilishwa Bungeni na hivyo mpaka leo halijaridhiwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, Azimio hili lilikuwa na lengo la kuweka makubaliano yatakayohakikisha nchi 11 washirika wa Bonde la Mto Nile zinapata matumizi yenye uwiano ya rasilimali za maji ya Mto Nile. Hii ingewezesha nchi yetu, pamoja na mambo mengine, kupanua shughuli mbalimbali kama vile uzalishaji umeme, kilimo cha umwagiliaji na miradi ya maji ya matumizi ya nyumbani.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa ni nchi mbili tu za Ethiopia na Rwanda ambazo zimekwisharidhia mkataba huu. Tanzania kutokusaini mkataba huu mpaka leo kunaisikitisha Kamati ukizingatia kwamba Serikali ya Tanzania ilikuwa mstari wa mbele katika kuandaa mkataba huu wa ushirikiano tangu hatua za awali mwezi Januari 1997 wakati Jopo la Wataalam lilipoundwa. Aidha, kuanzia mwaka 2003 hadi mwisho wa majadiliano mwezi Mei, 2010, Tanzania ilikuwa Mwenyekiti wa Nchi saba za Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Ethiopia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kwa ngazi za wataalam na Mawaziri wa Maji katika Baraza la Mawaziri wa Nchi za Bonde la Mto Nile.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa kwa kuzingatia juhudi hizi, Tanzania ingepaswa kuwa nchi ya kwanza kuridhia mkataba huu. Kamati inaishauri Serikali kurudisha Azimio hili Bungeni mapema iwezekanavyo liweze kuridhiwa ili kufanikisha mchango huu muhimu toka kwa Serikali yetu na pia kunufaika na mgao ulio sawa na wa haki wa kutumia rasilimali ya maji ya Mto Nile.

Mheshimiwa Spika, ziara za Kamati ndani ya nchi. Kwa kipindi cha Januari 2014 hadi Januari 2015, Kamati ilifanya ziara ya kukagua miradi iliyo chini ya Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kwa lengo la kuona utekelezaji wa miradi hiyo, mafanikio na changamoto zilizopo. Ziara hizo zilifanyika katika kanda nne tofauti kama ifuatavyo:-

(i) Kanda ya Kaskazini katika Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara;

(ii) Kanda ya Pwani katika Mikoa ya Pwani, Lindi na Mtwara;

(iii) Kanda ya Ziwa katika Mikoa ya Mwanza, Simiyu, Geita na Mara ikiwa ni pamoja na shughuli za uvuvi; na

(iv) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini katika Mikoa ya Morogoro, Iringa na Mbeya.

Mheshimiwa Spika, mafanikio katika miradi ya maji. Baada ya kufanya ziara hizo, Kamati imejiridhisha na juhudi za Serikali na inaipongeza Serikali pamoja na wananchi kwa utekelezaji mzuri wa baadhi ya miradi inayoendelea. Miradi hiyo ni pamoja na miradi ya maji ya Masasi, Arusha, Kilimanjaro, Kilolo, Mamlaka ya Maji Tanga, Iringa Mjini, Kibiti, Ikwiriri, Tandahimba na Mtwara Vijijini.

Mheshimiwa Spika, changamoto zinazoikabili miradi ya maji. Katika ziara hiyo, Kamati ilibaini changamoto nyingi zinazoikabili miradi hii. Changamoto hizi ni pamoja na:-

(i) Ucheleweshwaji/kutopatikana kwa fedha kutoka Serikalini kwa ajili ya Miradi ya Maji na hivyo kushindwa kukamilisha ujenzi wa miradi katika muda uliopangwa. Kwa mfano miradi ya maji ya Fulwe - Morogoro Vijijini, Masoko - Rungwe na mradi wa maji wa Minjingu – Manyara.

Mheshimiwa Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa mwaka wa Fedha wa 2014/2015, Wizara ya Maji ilitengewa jumla ya Sh.488,878,252,000/=. Hata hivyo, mpaka kufikia mwezi Disemba 2014, Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha Sh.105,732,986,191/= tu ikiwa ni sawa na asilimia 21.6 ya fedha zote zilizoizinishwa na Bunge.

(ii) Utaratibu wa kupeleka fedha katika Halmashauri kwa kupitia utaratibu wa *exchequer* pamoja na kusubiri kupata kibali kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kunachangia kuchelewesha utekelezaji wa miradi;

(iii) Halmashauri nyingi zinadaiwa na makandarasi kwa miradi ya maji inayoendelea;

(iv) Uharibifu wa miundombinu ya maji kama vile uvunjaji wa makusudi na wizi wa dira za maji kwa mfano katika Manispaa ya Morogoro;

(v) Uchakavu wa miundombinu ya maji kama vile kwenye miradi ya maji ya Ilula, Gedemar-Manyara, Tukuyu, Rondo-Lindi, na Malampaka-Maswa;

(vi) Upotevu wa maji kwa mfano katika Mji wa Tukuyu;

(vii) Gharama kubwa za uendeshaji wa miradi ya maji kutokana na matumizi ya umeme na dizeli kwa mfano katika miradi ya Bukombe, Rondo na Dareda;

(viii) Baadhi ya Mamlaka za Maji kudaiwa madeni makubwa ya umeme na Shirika la Umeme la Taifa (*TANESCO*);

(ix) Kukatika kwa umeme mara kwa mara na hivyo kuathiri mitambo ya kusukuma maji kwa mfano katika miradi ya Lindi Mjini, Ikwiriri na Kibiti;

(x) Makandarasi wasio na uwezo kwa mfano makandarasi katika miradi ya Mikumi na Dareda;

(xi) Uharibifu wa Mazingira na vyanzo vya maji kutokana na shughuli mbalimbali za binadamu kama vile kilimo, ufugaji na uchimbaji wa madini kwa mfano Geita na Muheza;

(xii) Upungufu wa wataalamu wa maji na vitendea kazi katika Idara za Maji;

(xiii) Utozwaji wa Kodi ya Ongezeka la Thamani *(VAT)* kwenye dawa za kutibu maji na hivyo kuongeza gharama za uendeshaji wa miradi kwa Mamlaka za Maji;

(xiv) Matumizi madogo ya maji yasiyolingana na uwezo wa mradi na hivyo kusababisha Mamlaka za Maji kuelemewa na gharama kubwa za uendeshaji wa mradi kwa mfano katika miradi ya maji ya Ihelele na Masasi;

(xv) Taasisi nyingi za Serikali kutolipa kwa wakati ankara za maji kwa mfano Majeshi, Shule na Hospitali;

(xvi) Mahitaji ya maji, hasa vijijini bado ni makubwa kuliko uzalishaji hivyo wananchi walio wengi wanakosa huduma ya majisafi na salama;

(xvii) Mwamko mdogo wa wananchi katika kuchangia gharama za uendeshaji wa miradi ya maji kwa mfano katika Mji wa Tukuyu.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali katika kusambaza huduma ya maji safi vijijini na mijini na uondoshaji wa maji taka mijini, Kamati ilijiridhisha kwamba, tatizo la maji bado ni sugu hasa katika maeneo ya vijijini. Hivyo basi, kwa kuwa ni ukweli usiopingika kuwa maji ni uhai, Kamati inashauri:-

(i) Kwa kuzingatia kwamba Halmashauri nyingi zina madeni makubwa kutoka kwa makandarasi, Serikali itoe fedha kwa wakati kwa ajili ya miradi ya maji. Hali hii itapunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la maji kwani miradi mingi itatekelezwa kwa muda uliopangwa;

(ii) Halmashauri zitenge bajeti na kuomba vibali vya kuajiri wataalam zaidi wa Idara za Maji kutoka katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma;

(iii) Halmashauri zitunge sheria ndogo na ziendelee kutoa elimu kwa umma kuhusu utunzaji wa mazingira na vyanzo vya Maji;

(iv) Ili kuepukana na tatizo sugu la Taasisi za Umma kutokulipa ankara za maji, Kamati inashauri Serikali ianze utaratibu wa kutumia mita za maji kwa wateja wote wa maji;

(v) Halmashauri zihamasishe uundwaji wa Kamati za Watumiaji Maji na kuanzisha Mifuko ya Maji ili kuweza kukarabati vituo vya maji pale vinapoharibika. Hali hii itachangia kuwa na miradi iliyo endelevu;

(vi) Halmashauri na Mamlaka za Maji ziwe makini katika kuchagua makandarasi wenye uzoefu katika ujenzi wa miradi ya Maji. Aidha, miradi mikubwa iwe na Makandarasi tofauti kwa kila shughuli ya mradi kama vile ulazaji wa mabomba, ujenzi wa matanki na kadhalika ili kuepuka kusimama kwa miradi kwa muda mrefu mara migogoro baina ya Halmashauri na Mkandarasi inapotokea;

(vii) Makandarasi wanaoharibu miradi wachukuliwe hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria zilizopo; na

(viii) Ili kupunguza gharama za uendeshaji wa miradi ya maji, Serikali ione uwezekano wa kutumia nishati mbadala kama vile umeme wa jua (*solar*) na upepo.

Mheshimiwa Spika, ziara za mafunzo nje ya nchi. katika kipindi cha Januari 2014 hadi Januari 2015, Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji walipata fursa ya kufanya ziara katika nchi za Singapore na Sudan.

Mheshimiwa Spika, ziara ya Kamati Nchini Singapore. Ziara ya mafunzo nchini Singapore ililenga kuiwezesha Kamati kujifunza masuala mbalimbali yanayohusu sekta za Kilimo, Mifugo na Maji nchini Singapore. Ziara hii iliandaliwa na kugharamiwa na Ofisi ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika ziara hiyo, Kamati ilitembelea Mamlaka ya Kudhibiti Chakula Kinachoingizwa nchini Singapore. Katika Mamlaka hii, Kamati ilijifunza namna ambavyo Singapore imefanikiwa katika kudhibiti uingizaji wa

chakula toka nchi za nje ili kulinda afya za wananchi na mifugo yao. Mamlaka hii ina jukumu la kuhakikisha kuwa chakula chote kinachoingia nchini kinakuwa salama kwa asilimia 100. Kamati inaishauri Serikali kuwa makini katika kuingiza bidhaa za chakula zilizo salama kwa watumiaji wake.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Kimataifa ya *International Enterprises* Singapore. Katika Kampuni hii Kamati ilijifunza kuhusu shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na kampuni hii ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kufundisha masuala ya kilimo kwa taasisi zinazojishughulisha na kilimo;

(ii) Kuendeleza uwekezaji nje ya nchi zikiwemo nchi za Asia, Ulaya, Amerika na Afrika. Katika nchi za Afrika Kampuni hii imewekeza katika nchi za Algeria, Tanzania na Uganda; na

(iii) Kuratibu utengenezaji na soko la *software*.

Mheshimiwa Spika, katika ziara hii, Kamati ilipendekeza Kampuni iangalie uwezekano wa kuwekeza katika zao la karafuu na viungo vingine hususan katika visiwa vya Zanzibar. Kampuni iliafiki kuwa wazo hili lina tija na kwamba watalifanyia kazi pindi watakapofanya ziara nyingine nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa, endapo nchi yetu itapata fursa hii, Serikali ihakikishe bidhaa zitakazosafirishwa nje ya nchi zinakidhi vigezo vya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kiwanda cha *Hyflux* cha kubadili maji ya bahari kuwa maji safi ya kunywa na matumizi ya kawaida. Kamati ilitembelea eneo hili kwa lengo la kujifunza namna ambavyo wanabadili maji ya bahari kuwa maji safi na salama. Kamati ilifahamishwa kuwa nchi ya Singapore ilikuwa na tatizo la maji kwa muda mrefu kutokana na kutokuwa na vyanzo vya maji vya nchi kavu na hivyo

kulazimika kununua maji kutoka nchi jirani ya Malaysia kwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa, kutokana na gharama hizo, Singapore ilibuni mbinu ya *desalination* ambayo imeliokoa Taifa hili kwa kiasi kikubwa kwa upande wa maji.

Mheshimiwa Spika, kufuatia ziara hii, Kamati ilijifunza kuwa hata kama nchi haina vyanzo vya maji lakini ikawa na bahari tatizo la maji linaweza kutatuliwa**.** Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutumia vizuri vyanzo vya maji vilivyopo ili kutatua matatizo makubwa ya maji yanayoikabili nchi yetu ili tusije tukalazimika kutumia *desalination* kama Singapore.

Mheshimiwa Spika, kukutana na wataalam wanaojishughulisha na uhifadhi wa maji kwenye udongo kwa ajili ya kilimo (*solid rain*). Kamati ilipata fursa ya kukutana na wataalam wanaojishughulisha na namna ya kuhifadhi maji kwenye udongo na kuweza kutumika kwa kipindi kirefu bila kuhitaji maji ya ziada. Kamati ilifahamishwa kuwa, teknolojia hii *(solid rain)* hutumika katika kipindi cha mvua ambapo aina ya poda yenye *potasium* hutumika kubeba kiasi cha maji mara 500 zaidi ya uwezo wake.

Mheshimiwa Spika, katika ziara hii, Kamati ilijifunza namna ambavyo nchi ya Singapore inatumia kiasi kidogo cha maji kwa kuyahifadhi kwenye udongo na kuyatumia kwa kilimo wakati wa ukame**.** Kamati inaishauri Serikali kufanya majaribio ya kutumia teknolojia hii kwenye maeneo yenye uhaba wa mvua. Hata hivyo, ipo haja ya Serikali kujiridhisha kwanza kuhusu jinsi teknolojia hii inavyofanya kazi, madhara yanayoweza kutokea kwa afya ya binadamu na athari kwa udongo katika kipindi kifupi na kwa muda mrefu**.**

Mheshimiwa Spika, ziara ya Kamati nchini Sudan. Ziara ya mafunzo nchini Sudan ilikuwa na lengo la kujifunza jinsi nchi hiyo inavyotumia maji ya Mto Nile katika kutekeleza miradi mbalimbali ya kijamii na kiuchumi. Ziara hii iliandaliwa

na Wizara ya Maji. Katika ziara hiyo, Kamati ilitembelea maeneo mbalimbali yanayonufaika moja kwa moja na maji ya Mto Nile.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Viwanda wa GIAD *(GIAD Industrial City)*. Kamati ilitembelea Mji wa Viwanda wa Giad na kujionea shughuli za viwanda (*industrial activities*) zikiwemo:-

(i) Uundwaji wa zana za kilimo (kama matrekta, vifaa vya palizi na uvunaji);

(ii) Magari ya kubebea mizigo, abiria na magari madogo *(salon cars)*;

(iii) Samani mbalimbali zikiwemo vitanda kwa ajili ya matumizi ya hospitali na nyumbani; na

(iv) Kujihusisha na kilimo cha umwagiliaji na usindikaji wa vyakula (*food processing industry*).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijifunza kuwa, shughuli za viwanda vya *Giad* zinatumia zaidi watumishi ambao ni wazawa na hivyo kuleta maendeleo kwa wananchi kutokana na kuongezeka kwa ajira hususan ajira kwa vijana. Aidha, msisitizo mkubwa unawekwa katika kujiongezea uwezo wa kutengeneza vifaa mbalimbali kwa matumizi ya nchi. Kwa sasa matumizi ya vifaa vinavyotengenezwa ndani ya nchi ni asilimia 25.

Mheshimiwa Spika, Kituo Kikuu cha Kusambaza Umeme *(National Grid Contol Center)*. Kituo hiki kinahusika na usambazaji wa umeme wa *grid* nchi nzima ya Sudan. Kamati ilifahamishwa kwamba Sudan inategemea sana umeme wa maji ambapo kati ya *gig watts* 2.7 zinazozalishwa, asilimia 65 ni ya umeme utokanao na maji yaani *hydro* na asilimia 35 umeme wa joto *(thermal)*.

Mheshimiwa Spika, Bwawa la Merowe (*Merowe Dam Site*). Kamati ilitembelea bwawa la kuzalisha umeme la Merowe ambalo limejengwa katika Mto Nile. Bwawa hili lina urefu wa kilometa 174 na lina uwezo wa kuzalisha takriban megawati 1,250 za umeme kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Sukari ya KENANA (*KENANA Sugar Company*). Kampuni hii ilianzishwa mwaka 1975 ikijihusisha na kilimo cha miwa kwa njia ya umwagiliaji wa maji ya Mto Nile. Kampuni hii huzalisha sukari kiasi cha tani 400,000 kwa mwaka. Kampuni ya KENANA inaiingizia Sudan faida kubwa katika uzalishaji wa sukari pamoja na bidhaa nyingine kama chakula cha mifugo na *ethanol* ambapo asilimia 60 ya *ethanol* huuzwa nje ya nchi. Aidha, umeme unaozalishwa kutokana na maganda ya miwa ni megawati 55.5.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo na Umwagiliaji. Katika ziara hiyo Kamati ilijulishwa kwamba Sudan hutegemea zaidi kilimo cha umwagiliaji ambapo ekari milioni 1.9 hulimwa kila mwaka. Aidha, Kamati ilitaarifiwa kuwa Sudan hulima na kusafirisha mazao kwenye soko la nje. Mazao hayo ni pamoja na pamba ambalo ndilo zao kuu la biashara, mbogamboga na matunda kama ndizi na maembe.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo yote yaliyotembelewa, Kamati ilijifunza kwamba, japokuwa zaidi ya asilimia 50 ya nchi ya Sudan ni jangwa, nchi hii imeweza kutumia vizuri maji ya Mto Nile kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya kiuchumi na jamii**.**

Mheshimiwa Spika, deni la wakulima wa mahindi. Kwa muda mrefu wakulima wa mahindi wamekuwa wakiidai Serikali kiasi cha shilingi bilioni 89. Deni hili linatokana na Serikali kukopa mazao ya wakulima na kushindwa kuwalipa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Serikali kutokulipa deni hili kwa wakati kumesababisha wakulima kushindwa kujiandaa mapema kwa ajili ya msimu mpya wa kilimo

ambao umeshaanza. Aidha, wakulima wengi wanaotegemea zao la mahindi wamekwamishwa katika shughuli za maendeleo ikiwa ni pamoja na ustawi wa familia zao.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha deni hili linalipwa haraka iwezekanavyo ili wakulima waendelee na shughuli msimu za kilimo.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Naomba nikushukuru tena kwa kunipa fursa hii ili kuweza kuwasilisha Taarifa ya Kamati. Aidha, nakupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati hii kwa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu ya Kamati kwa kipindi chote cha mwaka 2014. Michango yao imewezesha Kamati kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa.

Aidha, napenda kuwapongeza Mawaziri na Naibu Waziri wa Wizara zote tatu ambazo zinasimamiwa na Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa ushirikiano walioipa Kamati wakati inatekeleza majukumu yake. Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Waziri hao ni Mheshimiwa Eng. Christopher Kajoro Chiza aliyekuwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Naibu Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Dokta Titus Mlengeya Kamani, Waziri wa Maendeleo ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, pamoja na Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Waziri wa Maji na Mheshimiwa Amos Makalla, Naibu Waziri wa Maji. Aidha, natoa shukrani kwa Watendaji wa Wizara zote tatu wakiongozwa na Makatibu Wakuu kwa ushirikiano mzuri waliouonyesha kwa kipindi kilichopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah, kwa kuiwezesha Kamati wakati wote ilipokuwa inatekeleza majukumu yake. Aidha, nawashukuru Makatibu

wa Kamati hii Ndugu Grace Bidya na Ndugu Angelina Sanga pamoja na msaidizi wa Kamati Ndugu Sophia Vumbi kwa kuihudumia Kamati vizuri kwa kipindi chote na kuratibu kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Mheshimiwa Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, naomba kutoa hoja. Ahsante sana (*Makofi*)

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KAMATI YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI KWA KIPINDI CHA JANUARI 2014 HADI JANUARI 2015 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu taarifa ya shughuli zilizofanywa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji Kwa kipindi cha Januari 2014 hadi Januari 2015.

**2.0 MAJUKUMU YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ina jukumu la kusimamia utendaji wa Wizara za Kilimo, Chakula na Ushirika; Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; na Wizara ya Maji. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Nyongeza ya Nane Kifungu Na.6 (9) kikisomwa sambamba na Kifungu Na. 7(1), majukumu ya Kamati hii ni kama yafuatavyo:-

- Kuchambua Bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati;

- Kuchambua Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa na Wizara ili kujadiliwa na kupitishwa au kuridhiwa na Bunge;

- Kushughulikia Taarifa za kila Mwaka za utendaji za Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii; na

- Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) (b) ya Katiba.

**2.1 Shughuli zilizopangwa Kufanyika katika Kipindi cha Januari 2014 hadi Januari 2015**

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Januari 2014-Januari 2015, Kamati ilipanga kufanya kazi zifuatazo:-

- Kuchambua Bajeti za Wizara husika;

- Kuchambua Miswada ya Sheria, Maazimio na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge;

- Kufanya mikutano mbalimbali na watendaji wa Wizara inayozisimamia ili kujadili taarifa za utendaji za Wizara hizo na kutoa maoni, ushauri pamoja na maelekezo;

- Kufanya ziara katika sehemu mbalimbali nchini ili kujionea utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara husika;na

- Kufanya ziara za mafunzo nje ya nchi katika sekta za Kilimo, Mifugo na Maji.

## 3.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI KWA KIPINDI CHA JANUARI 2014 HADI JANUARI 2015

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Januari 2014 hadi Januari 2015, Kamati ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

- Kuchambua utekelezaji wa Mipango ya Bajeti ya Wizara zote inazozisimamia kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015;
- Kuchambua Maazimio na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge;
- Kufanya ziara katika sehemu mbalimbali nchini ili kujionea utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara husika; na
- Kufanya ziara za mafunzo ndani na nje ya nchi katika sekta za Kilimo, Mifugo, uvuvi na Maji.

### 3.1 Kuchambua Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua utekelezaji wa Mipango ya Bajeti za Mwaka wa Fedha wa 2014/2015 kwa Wizara inazozisimamia. Katika kujadili utekelezaji wa bajeti za Wizara hizo, Kamati ilibaini kuwa Wizara zote tatu zinakumbana na changamoto zinazofanana ambazo ni (i) kutengewa kiasi kidogo cha fedha; (ii) kuchelewa kupata fedha hizo hasa za miradi ya Maendeleo; na (iii) fedha zinazoidhinishwa na Bunge hazitolewi kwa ukamilifu inapofika mwisho wa Mwaka wa Fedha. Maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu makadirio ya Bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii yaliwasilishwa Bungeni kwa Mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2013 .

### 3.2 Kujadili Maazimio ya Bunge

**Mheshimiwa Spika,** Katika Kipindi cha Januari 2014 hadi Januari 2015, Kamati ilipokea na kujadili Azimio la Bunge la Mapendekezo ya Kuridhia Makubaliano ya Ushirikiano katika Bonde la Mto Nile "*Agreement on the Nile River Basin Cooperative Framework- CFA*"

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kwamba Kamati ilichambua Azimio hili na kuandaa maoni na ushauri wake, Azimio hili halikupewa nafasi ya kuwasilishwa Bungeni na hivyo mpaka leo halijaridhiwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Azimio hili lilikuwa na lengo la kuweka makubaliano yatakayohakikisha nchi 11 washirika wa Bonde la Mto Nile zinapata matumizi yenye uwiano ya rasilimali za maji ya Mto Nile. Hii ingewezesha nchi yetu, pamoja na mambo mengine, kupanua shughuli mbalimbali kama vile uzalishaji umeme, kilimo cha umwagiliaji na miradi ya maji ya matumizi ya nyumbani.

**Mheshimiwa Spika,** mpaka sasa ni nchi mbili tu za Ethiopia na Rwanda ambazo zimekwisha ridhia Mkataba huu. Tanzania kutokusaini Mkataba huu mpaka leo kunaisikitisha Kamati ukizingatia kwamba Serikali ya Tanzania ilikuwa mstari wa mbele katika kuandaa Mkataba huu wa Ushirikiano tangu hatua za awali mwezi Januari 1997 wakati Jopo la Wataalam lilipoundwa. Aidha, kuanzia mwaka 2003 hadi mwisho wa majadiliano mwezi Mei, 2010, Tanzania ilikuwa Mwenyekiti wa Nchi saba za Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Ethiopia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kwa ngazi za wataalam na Mawaziri wa Maji katika Baraza la Mawaziri wa Nchi za Bonde la Mto Nile.

**Mheshimiwa Spika,** Ni dhahiri kuwa kwa kuzingatia juhudi hizi, Tanzania ingepaswa kuwa nchi ya kwanza kuridhia Mkataba huu. Kamati inaishauri Serikali kurudisha Azimio hili Bungeni mapema iwezekanavyo liweze kuridhiwa ili kufanikisha mchango huu muhimu toka kwa Serikali yetu, na pia kunufaika na mgao ulio sawa na wa haki ya kutumia rasilimali ya maji ya Mto Nile**.**

### 3.3 Ziara za Kamati Ndani ya Nchi

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kipindi cha Januari 2014 hadi Januari 2015, Kamati ilifanya ziara ya kukagua miradi iliyo chini ya programu ya maji na usafi wa mazingira vijijini kwa lengo la kuona utekelezaji wa miradi hiyo, mafanikio na changamoto zilizopo. Ziara hizo zilifanyika katika kanda nne tofauti kama ifuatavyo:-

- Kanda ya Kaskazini katika Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara ;
- Kanda ya Pwani katika Mikoa ya Pwani, Lindi na Mtwara;
- Kanda ya Ziwa katika Mikoa ya Mwanza, Simiyu, Geita na Mara ikiwa ni pamoja na shughuli za uvuvi; na
- Kanda ya Nyanda za Juu Kusini katika Mikoa ya Morogoro, Iringa na Mbeya.

**Mafanikio katika Miradi ya Maji**

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kufanya ziara hizo, Kamati imejiridhisha na juhudi za Serikali na inaipongeza Serikali pamoja na wananchi kwa

utekelezaji mzuri wa baadhi ya miradi inayoendelea. Miradi hiyo ni pamoja na miradi ya Maji ya Masasi, Arusha, Kilimanjaro, Kilolo, Mamlaka ya Maji- Tanga, Iringa Mjini, Kibiti, Ikwiriri, Tandahimba na Mtwara Vijijini.

**Changamoto zinazoikabili Miradi ya Maji**

**Mheshimiwa Spika,** Katika ziara hiyo, Kamati ilibaini changamoto nyingi zinazoikabili miradi hii. Changamoto hizi ni pamoja na:-

- Ucheleweshwaji/kutopatikana kwa fedha kutoka Serikalini kwa ajili ya Miradi ya maji na hivyo kushindwa kukamilisha ujenzi wa miradi katika muda uliopangwa. Kwa mfano miradi ya maji ya Fulwe- Morogoro Vijijini, Masoko-Rungwe na mradi wa maji wa Minjingu-Manyara;

  **Mheshimiwa Spika**, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015, Wizara ya Maji ilitengewa jumla ya shilingi **488,878,252,000/=.** Hata hivyo, mpaka kufikia Mwezi Disemba 2014, Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi **105, 732,986,191/=** tu ikiwa ni sawa na asilimia **21.6** ya fedha zote zilizoizinishwa na Bunge.

- Utaratibu wa kupeleka fedha katika Halmashauri kwa kupitia utaratibu wa *exchequer* pamoja na kusubiri kupata kibali kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kunachangia kuchelewesha utekelezaji wa miradi;

- Halmashauri nyingi zinadaiwa na makandarasi kwa miradi ya maji inayoendelea;

- Uharibifu wa miundombinu ya maji kama vile uvunjaji wa makusudi na wizi wa dira za maji kwa mfano katika Manispaa ya Morogoro;

- Uchakavu wa miundombinu ya Maji kama vile kwenye miradi ya maji Ilula, Gedemar-Manyara, Tukuyu, Rondo-Lindi, na Malampaka-Maswa;

- Upotevu wa maji kwa mfano katika Mji wa Tukuyu;

- Gharama kubwa za uendeshaji wa miradi ya Maji kutokana na matumizi ya umeme na dizeli kwa mfano katika miradi ya Bukombe, Rondo na Dareda;

- Baadhi ya Mamlaka za Maji kudaiwa madeni makubwa ya umeme na Shirika la Umeme la Taifa (TANESCO);

- Kukatika kwa umeme mara kwa mara na hivyo kuathiri mitambo ya kusukuma maji kwa mfano katika miradi ya Lindi Mjini, Ikwiriri na Kibiti;

- Makandarasi wasio na uwezo kwa mfano makandarasi katika miradi ya Mikumi na Dareda;

- Uharibifu wa Mazingira na vyanzo vya maji kutokana na shughuli mbalimbali za binadamu kama vile kilimo, ufugaji na uchimbaji wa madini kwa mfano Geita na Muheza;

- Upungufu wa wataalamu wa maji na vitendea kazi katika Idara za Maji;
- Utozwaji wa Kodi ya Ongezeka la Thamani (VAT) kwenye dawa za kutibu maji na hivyo kuongeza gharama za uendeshaji wa miradi kwa Mamlaka za Maji;
- Matumizi madogo ya maji yasiyolingana na uwezo wa mradi na hivyo kusababisha Mamlaka za Maji kuelemewa na gharama kubwa za uendeshaji wa mradi kwa mfano katika miradi ya maji ya Ihelele na Masasi;
- Taasisi nyingi za Serikali kutolipa kwa wakati ankara za maji kwa mfano Majeshi, Shule na Hospitali;
- Mahitaji ya maji, hasa vijijini bado ni makubwa kuliko uzalishaji hivyo wananchi walio wengi wanakosa huduma ya majisafi; na
- Mwamko mdogo wa wananchi katika kuchangia gharama za uendeshaji wa miradi ya maji kwa mfano katika Mji wa Tukuyu.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na juhudi zinazofanywa na Serikali katika kusambaza huduma ya maji safi vijijini na mijini, na uondoshaji wa majitaka mijini, Kamati ilijiridhisha kwamba tatizo la maji bado ni sugu hasa katika maeneo ya vijijini. Hivyo basi, kwa kuwa ni ukweli usiopingika kuwa **MAJI NI UHAI**, Kamati inashauri ifuatavyo:-

- Kwa kuzingatia kwamba Halmashauri nyingi zina madeni makubwa kutoka kwa makandarasi, Serikali itoe fedha kwa wakati kwa ajili ya miradi ya maji. Hali hii itapunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la maji kwani miradi mingi itatekelezwa kwa muda uliopangwa;

- Halmashauri zitenge bajeti na kuomba vibali vya kuajiri wataalam zaidi wa Idara za Maji kutoka katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma;

- Halmashauri zitunge sheria ndogo na ziendelee kutoa elimu kwa umma kuhusu utunzaji wa mazingira na vyanzo vya Maji;

- Ili kuepukana na tatizo sugu la Taasisi za umma kutokulipa ankara za maji, Kamati inashauri Serikali ianze utaratibu wa kutumia mita za maji kwa wateja wote wa maji;

- Halmashauri zihamasishe uundwaji wa kamati za watumiaji maji na kuanzisha mifuko ya maji ili kuweza kukarabati vituo vya maji pale vinapoharibika. Hali hii itachangia kuwa na miradi iliyo endelevu;

- Halmashauri na Mamlaka za Maji ziwe makini katika kuchagua makandarasi wenye uzoefu katika ujenzi wa miradi ya Maji. Aidha, miradi mikubwa iwe na Makandarasi tofauti (kwa kila shughuli ya mradi kama vile ulazaji wa mabomba, ujenzi wa matanki n.k) ili kuepuka kusimama kwa miradi kwa muda mrefu mara migogoro baina ya Halmashauri na Mkandarasi inapotokea;

- Makandarasi wanaoharibu miradi wachukuliwe hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria zilizopo;na

- Ili kupunguza gharama za uendeshaji wa miradi ya maji, Serikali ione uwezekano wa kutumia nishati mbadala kama vile umeme wa jua (*solar*) na upepo.

3.4 **Ziara za Mafunzo Nje ya Nchi**

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Januari 2014 hadi Januari 2015, wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji walipata fursa ya kufanya ziara katika nchi za Singapore na Sudan.

**(a) Ziara ya Kamati Nchini Singapore**

**Mheshimiwa Spika,** Ziara ya mafunzo nchini Singapore ililenga kuiwezesha Kamati kujifunza masuala mbalimbali yanayohusu sekta za Kilimo, Mifugo na Maji nchini Singapore. Ziara hii iliandaliwa na kugharamiwa na Ofisi ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Katika ziara hiyo Kamati ilitembelea maeneo yafuatayo:-

**(i) Mamlaka ya Kudhibiti Chakula Kinachoingizwa nchini Singapore**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mamlaka hii Kamati ilijifunza namna ambavyo Singapore imefanikiwa katika kudhibiti uingizaji wa chakula toka nchi za nje ili kulinda afya za wananchi na mifugo yao. Mamlaka hii ina jukumu la kuhakikisha kuwa chakula chote

kinachoingia nchini kinakuwa salama kwa asilimia 100;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuwa makini katika kuingiza bidhaa za chakula zilizo salama kwa watumiaji wake.

**(ii) Kampuni ya Kimataifa ya *International Enterprises* Singapore**

**Mheshimiwa Spika,** Katika Kampuni hii Kamati ilijifunza kuhusu shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Kampuni hii ikiwa ni pamoja na:-

- Kufundisha masuala ya kilimo kwa Taasisi zinazojishughulisha na kilimo;

- Kuendeleza uwekezaji nje ya nchi zikiwemo nchi za Asia, Ulaya, Amerika na Afrika. Katika nchi za Afrika Kampuni hii imewekeza katika nchi za Algeria, Tanzania na uganda; na

- Kuratibu utengenezaji na soko la *soft ware*

**Mheshimiwa Spika,** katika ziara hii Kamati ilipendekeza Kampuni iangalie uwezekano wa kuwekeza katika zao la karafuu na viungo vingine hususan katika visiwa vya Zanzibar. Kampuni iliafiki kuwa wazo hili lina tija na kwamba watalifanyia kazi pindi watakapofanya ziara nyingine nchini Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kuwa, endapo nchi yetu itapata fursa hii, Serikali ihakikishe bidhaa zitakazosafirishwa nje ya nchi zinakidhi vigezo vya kimataifa.

**(iii) Kiwanda cha Hyflux cha Kubadili maji ya Bahari kuwa maji Safi ya Kunywa na Matumizi ya Kawaida**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea eneo hili kwa lengo la kujifunza namna ambavyo wanabadili maji ya bahari kuwa maji safi na salama. Kamati ilifahamishwa kuwa nchi ya Singapore ilikuwa na tatizo la maji kwa muda mrefu kutokana na kutokuwa na vyanzo vya maji vya nchi kavu na hivyo kulazimika kununua maji kutoka nchi jirani ya Malaysia kwa gharama kubwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijulishwa kuwa, kutokana na gharama hizo, Singapore ilibuni mbinu ya "*desalination*" ambayo imeliokoa taifa hili kwa kiasi kikubwa kwa upande wa Maji.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia ziara hii, Kamati ilijifunza kuwa hata kama nchi haina vyanzo vya maji lakini ikawa na bahari tatizo la maji linaweza kutatuliwa**.** Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutumia vizuri vyanzo vya maji vilivyopo ili kutatua matatizo makubwa ya maji yanayoikabili nchi yetu ili tusije tukalazimika kutumia"*desalination*" kama Singapore.

**(iv) Kukutana na Wataalamu wanaojishughulisha na Uhifadhi wa Maji kwenye Udongo kwa Ajili ya Kilimo (*Solid Rain*)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kukutana na wataalamu wanaojishughulisha na namna ya kuhifadhi maji kwenye udongo na kuweza kutumika kwa kipindi kirefu bila kuhitaji maji ya ziada. Kamati ilifahamishwa kuwa, teknolojia hii *(solid rain)* hutumika katika kipindi cha mvua ambapo aina ya poda yenye *potasium* hutumika kubeba kiasi cha maji mara 500 zaidi ya uwezo wake.

**Mheshimiwa Spika,** Katika ziara hii Kamati ilijifunza namna ambavyo nchi ya Singapore inatumia kiasi kidogo cha maji kwa kuyahifadhi kwenye udongo na kuyatumia kwa kilimo wakati wa ukame**.** Kamati inaishauri Serikali kufanya majaribio ya kutumia teknolojia hii kwenye maeneo yenye uhaba wa mvua. Hata hivyo, ipo haja ya Serikali kujiridhisha kwanza kuhusu jinsi teknolojia hii inavyofanya kazi, madhara yanayoweza kutokea kwa afya ya binadamu na athari kwa udongo katika kipindi kifupi na kwa muda mrefu**.**

**(b) Ziara ya Kamati Nchini Sudan**

**Mheshimiwa Spika,** Ziara ya mafunzo nchini Sudan ilikuwa na lengo la kujifunza jinsi nchi hiyo inavyotumia maji ya mto Nile katika kutekeleza miradi mbalimbali ya kijamii na kiuchumi. Ziara hii iliandaliwa na Wizara ya Maji.

**Mheshimiwa Spika,** Katika ziara hiyo Kamati ilitembelea maeneo mbalimbali yanayonufaika moja kwa moja na maji ya Mto Nile. Maeneo hayo ni yafuatayo:-

**(i) Mji wa Viwanda wa GIAD *(GIAD Industrial City)***

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea Mji wa Viwanda wa Giad na kujionea shughuli za viwanda (*Industrial activities*) zikiwemo uundwaji wa zana za kilimo (kama matrekta, vifaa vya palizi na uvunaji); magari ya kubebea mizigo, abiria na magari madogo *(salon cars)*; samani mbalimbali zikiwemo vitanda kwa ajili ya matumizi ya hospitali na nyumbani; na kujihusisha na kilimo cha umwagiliaji na usindikaji wa vyakula (*food processing industry*).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijifunza kuwa, shughuli za viwanda vya *Giad* zinatumia zaidi watumishi ambao ni wazawa na hivyo kuleta maendeleo kwa wananchi kutokana na kuongezeka kwa ajira hususan ajira kwa vijana. Aidha, msisitizo mkubwa unawekwa katika kujiongezea uwezo wa kutengeneza vifaa mbalimbali kwa matumizi ya nchi. Kwa sasa matumizi ya vifaa vinavyotengenezwa ndani ya nchi ni asilimia 25.

**(ii) Kituo Kikuu cha Kusambaza Umeme *(National Grid Contol Center)***

**Mheshimiwa Spika**, Kituo hiki kinahusika na usambazaji wa umeme wa *grid* nchi nzima ya Sudan. Kamati ilifahamishwa kwamba Sudan inategemea sana umeme wa maji ambapo kati ya gigawatts 2.7 zinazozalishwa, asilimia 65 ni ya umeme utokanao na maji (*hydro*) na asilimia 35 umeme wa joto *(thermal)*.

**(iii) Bwawa la Merowe (Merowe *Dam Site*)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea bwawa la kuzalisha umeme la Merowe ambalo limejengwa katika mto Nile. Bwawa hili lina urefu wa **km 174** na lina uwezo wa kuzalisha takriban megawati 1,250 za umeme kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

**(iv) Kampuni ya Sukari ya KENANA (KENANA *Sugar Company*):**

**Mheshimiwa Spika**, Kampuni hii ilianzishwa mwaka 1975 ikijihusisha na Kilimo cha miwa kwa njia ya umwagiliaji wa maji ya mto Nile. Kampuni hii huzalisha sukari kiasi cha tani 400,000 kwa mwaka.

Kampuni ya KENANA inaiingizia Sudan faida kubwa katika uzalishaji wa sukari pamoja na bidhaa nyingine kama chakula cha mifugo na Ethanol ambapo asilimia 60 ya ethanol huuzwa nje ya nchi. Aidha, umeme unaozalishwa kutokana na maganda ya miwa ni megawati 55.5.

**(v) Wizara ya Kilimo na Umwagiliaji**

**Mheshimiwa Spika**, Katika ziara hiyo Kamati ilijulishwa kwamba Sudan hutegemea zaidi kilimo cha umwagiliaji ambapo ekari milioni 1.9 hulimwa kila mwaka. Aidha, Kamati ilitaarifiwa kuwa Sudan hulima na kusafirisha mazao kwenye soko la nje. Mazao hayo ni pamoja na pamba (ambalo ndio zao kuu la biashara), mbogamboga na matunda kama ndizi na maembe.

**Mheshimiwa Spika,** katika maeneo yote yaliyotembelewa, Kamati ilijifunza kwamba, japokuwa zaidi ya asilimia 50 ya nchi ya Sudan ni jangwa, nchi hii imeweza kutumia vizuri maji ya mto Nile kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya kiuchumi na jamii**.**

**3.5 Deni la Wakulima wa Mahindi**

**Mheshimiwa Spika**, kwa muda mrefu wakulima wa mahindi wamekuwa wakiidai Serikali kiasi cha shilingi bilioni 89. Deni hili linatokana na Serikali kukopa mazao ya wakulima na kushindwa kuwalipa kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** kitendo cha Serikali kutokulipa deni hili kwa wakati kumesababisha wakulima kushindwa kujiandaa mapema kwa ajili ya msimu mpya wa Kilimo ambao umeshaanza. Aidha, wakulima wengi wanaotegemea zao la mahindi

wamekwamishwa katika shughuli za maendeleo ikiwa ni pamoja na ustawi wa familia zao.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha deni hili linalipwa haraka iwezekanavyo ili wakulima waendelee na shughuli muhimu za Kilimo.

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba nikushukuru tena kwa kunipa fursa hii ili kuweza kuwasilisha Taarifa ya Kamati. Aidha, nakupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu vizuri.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati hii kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu ya Kamati kwa kipindi chote cha Mwaka 2014. Michango yao imewezesha Kamati kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa. Aidha, napenda kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

1.Mhe. Prof. Peter Mahamudu Msolla, Mb - Mwenyekiti
2.Mhe. Said Juma Nkumba, Mb - Makamu Mwenyekiti
3.Mhe. Prof. David Homeli Mwakyusa, Mb - Mjumbe
4.Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mb - Mjumbe
5.Mhe. Asaa Othman Hamad, Mb - Mjumbe
6.Mhe. Abdulsalaam Selemani Ameir, Mb - Mjumbe
7.Mhe. Abdallah Haji Ali , Mb - Mjumbe
8.Mhe. Haji Juma Sereweji, Mb - Mjumbe
9.Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Namelock Moringe Sokoine, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Dkt. Lucy Sawere Nkya, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Sylvestry Francis Koka, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Kheri Khatib Ameir, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Meshack Jeremia Opulukwa, Mb - Mjumbe

| | | |
|---|---|---|
| 15. Mhe. Philemon Kiwelu Ndesamburo, Mb | - | Mjumbe |
| 16. Mhe. Jitu Vrajlal Soni, Mb | - | Mjumbe |
| 17.Mhe. Sadifa Juma Khamis,Mb | - | Mjumbe |
| 18.Mhe. Donald Kelvin Max, Mb | - | Mjumbe |
| 19.Mhe. Moshi Selemani Kakoso, Mb | - | Mjumbe |
| 20.Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb | - | Mjumbe |
| 21.Mhe. Magdalena Hamisi Sakaya, Mb | - | Mjumbe |
| 22.Mhe. Amina Nassoro Makilagi, Mb | - | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri wa Wizara zote tatu ambazo zinasimamiwa na Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa ushirikiano walioipa Kamati wakati inatekeleza majukumu yake. Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri hao ni Mheshimiwa Eng. Christopher Kajoro Chiza, aliyekuwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, (Mb), Mheshimiwa Godfrey Zambi, Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Dkt Titus Mlengeya Kamani, (Mb), Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele(Mb), Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, pamoja na Mheshimiwa Prof.Jumanne Maghembe (Mb), Waziri wa Maji na Mheshimiwa Amos Makalla (Mb), Naibu Waziri wa Maji. Aidha, natoa shukrani kwa Watendaji wa Wizara zote tatu wakiongozwa na Makatibu Wakuu kwa ushirikiano mzuri waliouonyesha kwa kipindi kilichopita.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuishukuru Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah kwa kuiwezesha Kamati wakati wote ilipokuwa inatekeleza majukumu yake. Aidha, nawashukuru Makatibu wa Kamati hii Ndugu Grace Bidya na Ndugu Angelina Sanga pamoja na msaidizi wa Kamati Ndugu Sophia Vumbi kwa kuihudumia Kamati vizuri kwa kipindi chote na kuratibu kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, naomba kutoa hoja.

Prof. Peter M. Msolla, (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI**
**31 Januari, 2015**

**SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na nia njema ya kupenda kila mtu ajadili hizi taarifa kama kipindi cha bajeti, bado wakati ni ukuta kwa hiyo hakuna namna. Katika Wizara hizi mbili, Wajumbe kumi na sita tu wanaweza kuongea na bahati nzuri Wizara zilizo hapa ni karibu sita na Mawaziri nao watajadili katika Wizara hizo. Sasa hivi kama yupo namuita Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Kangi Lugola, Mheshimiwa Malocha, Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa Dokta Mponda na Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye, kwa asubuhi hii wanatosha.

**MHE. ABDULKARIM E.H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia taarifa za Kamati hizi mbili nikiwa kama Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, naomba kwanza kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote waliokuja Wizara ya Ardhi, karibuni sana na tunategemea ushirikiano mzuri tutakaopata kutoka kwenu. Pia tuwashukuru wale walioondoka kwa heshima waliyotupa na kuweza kuhakikisha kwamba yale yote ambayo walikuwa wakihitaji kwa faida ya nchi na sisi walikuwa wakitupa ushirikiano, yaliyojitokeza mengine Mungu mwenyewe anajua.

Mheshimiwa Spika, naomba niende moja kwa moja kwa kuwa wakati wenyewe mdogo, Kamati yetu ilifanya ziara Mafia na iliweza kwenda kuangalia hali ya mgogoro mzito uliokuwa katika Shamba la Utumaini kule katika maeneo ya Gonge, Chunguruma, Kilongwe na Baleni. Shamba hili lilitelekezwa miaka zaidi ya 40 iliyopita. Leo

anakuja mtu anasema shamba hili ni la kwangu, wananchi wote, vijiji vyote vilivyoandikishwa kisheria, vitongoji vyote, shule zote, zahanati zote na nyumba zao na mazao ya kudumu yaliyokuwa mule mtu anasema hizi mali zote za kwangu. Hili si jambo la kukabalika na bahati nzuri, nawashukuru pia Wajumbe wa Kamati baada ya kuliangalia na kuweza kulitolea maamuzi ambayo naamini Mheshimiwa Waziri jioni atakapokuwa anafanya *winding up* ataweza kuja kutuambia ni jinsi gani wananchi wale waliokaa zaidi ya miaka 40 waweze kupata haki kwa sababu waliishi pale bila ya kupata bugudha. Hakuna mtu aliyejitokeza katika kipindi hicho na kusema shamba hili la kwangu, wala hizi mali za kwangu na ninyi mlipokaa hapa si kwenu. Kwa hiyo, hili tunaiomba Serikali iweze leo kutamka na hivi tunavyoongea wananchi wa Mafia wote wako katika vyombo vya habari wakisikiliza nini Serikali itatoa msimamo wake na hatma ya wananchi hawa. Hili sitaki kulizungumzia sana na naomba wananchi wenyewe leo sikilizeni Serikali itasema nini.

Mheshimiwa Spika, lingine hivi vitu vinavyofanyika hii migogoro kwenye Kamati Mwenyekiti hakuweza kusoma yote. Tulichokuwa tunasema baadhi ya watumishi wetu ambao wanakuwa chanzo cha vurugu, chanzo cha kubeba watu kwa sababu ya hivi viposho posho, naomba sana Serikali isiache kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi wote wa Wizara ya Ardhi na hata Halmashauri waliohusika katika kumfanya huyu mtu anayejifanya kanunua shamba wakati Wizara wala Halmashauri haijui waliuziana vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mtu anapanga katika kuleta hujuma wanafanya mabadiliko ya mashamba, shamba mwenyewe hajulikani. Mimi nimezaliwa mwaka 61 shamba hili limepata hati mwaka 67 nikiwa na umri wa miaka 6, huyo mwenyewe toka nimepata fahamu sijawahi kuliona shamba hilo likitoa mazao au usindikaji wa nazi, mafuta au wa jambo lolote. Sasa leo mtu amekaa amefikia kujukuu anakuja mtu anasema shamba hili lake, hili jambo halikubaliki.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wananchi wa Mafia leo naamini eneo lile mlilokaa kwa zaidi ya miaka 48, amevunja sheria mara nne ya miaka kumi na mbili ya Sheria ya Ardhi Na.9, leo tutakuwa huru baada ya Tangazo la Mheshimiwa Waziri jioni. Nataka atuambie au Serikali itutose kuhusu jambo hili. Kwa hiyo, tunataka haki iweze kutendeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati pia iliweza kupata bahati ya kutembelea katika shamba la Ng'ombeni kule Mafia lakini kwa bahati nzuri maelezo mazuri yaliyotolewa na Serikali kwa upande wa *NEMC,* nasema tunayazingatia. Naomba Baraza leo la Taifa la Usimamizi wa Mazingira lifanye tathmini ya athari ya ufuaji wa umeme kwa kutumia magogo ili kuona kama mradi huo ni endelevu au ni hatari. Mafia ni Kisiwa kwa hivyo, mradi ule endapo tukiwa tunatumia umeme wa kuzalisha kwa kukata miti, jamani Mafia inaangamia. Kwa hiyo, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), naomba sana tathmini izidi kufanyika na iweze kutoa taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nashukuru wenye mashamba sasa hivi wameshaanza kuelewa na kwa bahati nzuri yuko mwekezaji ambaye anataka kwenda kufufua zao la mnazi ili kuweza kuja kujenga kiwanda cha kusindika tui ambalo litakuwa *packed.* Naamini likifanyika hili zile takataka zitakazotoka, umeme wao utaweza kuendelea.

Mheshimiwa Spika, sitaki kupoteza muda mrefu lakini kidogo tu nataka nizungumzie upande wa maji. Mheshimiwa Rais mwaka 2005 wakati anagombea alitoa ahadi ya Kisiwa cha Jibondo kuweza kupata maji, miaka mitano imepita. Kipindi hiki cha mwaka 2010 hadi leo, jamani wananchi wa Jibondo wanateseka. Sasa mimi kila siku kwenda pale kukaa mzigo na kwenda kuwaambia maji yanakuja, maji yanakuja na kuwafanya wananchi wale kama watoto ambapo sina lugha nzuri ya kusema kwa sababu nitakalowaambia ni wazazi wangu. Naomba Waziri wa Maji asimame atuambie, maji yatapatikana au hakuna na kama hakuna uwaambie yale aliyoyasema Rais yalikuwa ni maneno gani? Tunataka utuhakikishie kwamba, miaka kumi ahadi ya Rais Wizara haitaki kutekeleza.

Watu wako visiwani, wanasafiri baharini kuja Kisiwa Kikuu maili kumi, wakati mwingine wanapata ajali wanazama. Tayari tulishawahi kutangaza kwamba, watu walishawahi kufariki kwa kufuata maji katika Kisiwa Kikuu cha Mafia, lakini leo Serikali imekaa, tunabembelezana, tunasema, tufanye nini, tutumie lugha gani kuwaambieni ili wenzetu muweze kusikiliza, halafu na wale Wananchi wa Jibondo waweze kupata stara ya kupata maji safi na salama katika kisiwa chao?

Miradi mizuri, tumetoa mawazo mengi mazuri, lakini wenzetu hamtaki kuyasikiliza. Kwa hiyo, Waziri wa Maji, naomba mtuambie kuhusu suala hilo.

Suala la mwisho kwenye uvuvi, Naibu Waziri tunamshukuru aliwahi kutembelea Mafia kule, ameona matatizo ya wavuvi.

La mwisho, tunasema, yule mzee, Mheshimiwa Ole-Telele, uliyemuahidi kwamba, utampa baada ya kurejesha nyavu haramu, mpaka leo kimya. Hivi Serikali hii haina shilingi milioni nne au sita za kumlipa fidia yule mtu aliyejitolea na kuonyesha mfano. Mbona majambazi wengine wanaporudisha silaha mnakwenda, lakini mtu anayefanya jambo lake kwa haki, anarudisha kwa heshima zote, leo Serikali hii mnataka mumdharaulishe. Hivi sasa anatukanwa, kijiji kizima kinamwona yeye kama vile mtu asiyekuwa na fahamu, au mtu ambaye hakuwa na mwelekeo. Sasa msitirini yule mzee ili aweze kupata haki.

Kutoa milioni nne au sita kwa thamani ya nyavu zake, hivi Serikali hii, Wizara yako, Idara yako ya Uvuvi, inashindwa? Mimi naomba tupate majibu mazuri ili na hawa wananchi waweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba dakika zangu zilizobaki nne hizi, nimpe Mheshimiwa Esther Bulaya, aweze kuendelea. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mimi ndiyo ninayepanga hapa, nani kawaambia! Mchezo huo sina, wale wote waliochangia katika hotuba zingine, hawapewi nafasi hapa. Kwa hiyo, ndiyo hivyo.

Mheshimiwa Kangi Lugola, atafuatia Mheshimiwa Malocha, halafu Mheshimiwa Zitto!

Hivi, mbona unanipotezea muda na wewe!

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, samahani sana, hii laini yetu *mic* hazifanyi kazi.

**SPIKA:** Ahsante sana, tumesikia.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kufanya mabadiliko kwenye Baraza la Mawaziri. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba, wale ambao wamekwenda kwenye zile Wizara ambazo zilikuwa hazifanyi vizuri, sasa tutaona mambo mazuri kwenye Wizara zao, ikiwemo Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Spika, nianze na migogoro ya ardhi. Migogoro ya ardhi katika nchi yetu imekuwa ni historia ya miaka mingi. Waheshimiwa Wabunge, migogoro ya ardhi haitakwisha katika nchi yetu kama Viongozi wa Serikali watakuwa ndiyo wahusika wakuu wa kujihusisha katika migogoro ya ardhi. *(Makofi)*

Wako viongozi wengine ndiyo wanahodhi maeneo na wako viongozi wengine, ndiyo wanaowabeba kwenye mbeleko wawekezaji ambao baadaye wanaleta migogoro baina yao na wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano mdogo, yuko mwekezaji mmoja pale Osterbay Villa na historia inaonyesha alikuja pale akaingia makubaliano ya kuviendeleza viwanja viwili vinavyomilikiwa na Manispaa ya Kinondoni. Historia inaonyesha, wakati Mheshimiwa Lukuvi akiwa Mkuu wa

Mkoa, ndiye ambaye alihakikisha yule mwekezaji anapata lile eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na leo Mheshimiwa Lukuvi huyu huyu ndiyo amepelekwa tena Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ambako yule mwekezaji bado ana mgogoro na Manispaa ya Kinondoni. Mwekezaji yule ana kiburi, aliizuia Kamati ya Bunge isikanyage ardhi ya Wananchi, ya Watanzania, ili tuweze kuona zile *apartments* 17 ambazo ni za Manipaa ya Kinondoni.

Mheshimiwa Spika, mwekezaji yule anahakikisha kwamba, Kinondoni hawatapata bilioni tatu ambazo anadaiwa na Mheshimiwa Lukuvi ndiyo unambeba kwenye mbeleko. Pamoja na kwamba alizuia Wabunge kuingia, lakini nilihakikisha alijifanya yeye ni baunsa katika nchi hii, nikamwambia hapa amefika, nchi hii kuna mabaunsa ambao ni sisi. Nilihakikisha natumia ubaunsa wangu kumdhibiti yule mwekezaji tukaingia kwenye vile viwanja viwili vya Manispaa ya Kinondoni.

Nakuhakikishia Mheshimiwa Lukuvi, ukiendelea kumbeba kwenye mbeleko, nitahakikisha ninaichoma moto na kuhakikisha huyu mwekezaji anadondoka.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nchi yetu itumie risasi, mabomu na virungu, kuwapiga watu kama akina Lipumba, waombolezaji wanaomboleza vifo vya wenzao, badala ya kutumia mabomu kuwatandika wawekezaji fidhuli kama hawa, ili waweze kutoa fedha za Watanzania. *(Makofi)*

Lazima tufike pahala, hawa ambao wanaiba rasilimali za nchi hii, ndiyo tutumie mabomu haya kuhakikisha tunawatandika, waweze kutoa fedha za Watanzania.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye suala la kilimo cha pamba. Nimesoma kwenye Ripoti ya Kamati wamekwenda mpaka Sudani kuangalia umwagiliaji wa zao la pamba. Sasa ilikuwa ni imani yangu kwamba, Mheshimiwa Wasira, unakwenda kwenye Wizara hii ya Kilimo, Chakula na Ushirika,

lakini nenda ukatatue matatizo sugu ya kilimo cha pamba, hususan mbegu za pamba ambazo wakulima wanaletewa ambazo hazioti. Wanaletewa madawa ambayo hayaui wadudu na wengine hawajalipwa fedha zao mpaka leo.

Ninakuamini, huu u-Tyson usiwe ni u-Tyson tu wa kupigana kwenye ulingo wa kisiasa. Nakuomba ukatumie u-Tyson kwenda kupambana na wale wote ambao wanawachakachua wakulima.

Kwa nini mnailinda Bodi ya Pamba? Taarifa nilizonazo ambazo nakamilisha uchunguzi wangu, nitalileta hilo bomu hapa ili tuone ni kwa namna gani fedha ambazo ni za wakulima zinaliwa kwenye Bodi ya Pamba, wakishirikiana na Mawaziri, ambao wanahusika kwenye Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Ninakushauri, utakapofika Kanda ya Ziwa wanakolima pamba, hakikisha unaiita Bodi hii na Wadau na Wabunge, ili tuje tuzungumze matatizo ya fedha ambazo wamekula kwenye Mfuko wa Kuendeleza Zao la Pamba na matokeo yake hawa wafanyabiashara wakubwa, hizi pembejeo wanawapelekea feki, wakati fedha za wakulima ndiyo zinazotumika kununua pembejeo.

Nakuhakikishia nitakupa huo msaada. Nakuhakikishia hata hayo mambo yako mengine unayohangaika nayo, usipotatua matatizo ya wakulima hatutaelewana. Tumia u-Tyson wako kuhakikisha mambo haya yanafanyika. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye suala la migogoro baina ya Hifadhi, Wanyama pamoja na Wananchi wanaozunguka maeneo hayo.

Mheshimiwa Lazaro Nyarandu, nilikwambia hapa Bungeni, wananchi wangu wa Mwibara, wapiga kura wangu, wanateketea kwa sababu ya mamba na viboko, lakini mpaka leo hujafika kule. Wapiga kura wangu wanaendelea kutafunwa, nani atanirudisha Bungeni hapa kama wapiga kura wangu wanaendelea kuliwa na mamba wako hawa? *(Kicheko)*

Sisi tunapopambana na viboko hawa, wananchi wangu wanakamatwa kule kwamba, wanaua wanyama wa maliasili. Sasa endapo hutafanya mkutano na hawa mamba na hutafanya mkutano na hawa viboko, kuwazuia wasile Wanamwibara, wasitafune Wanamwibara, ninakuhakikishia huko unakokimbilia kama umeshindwa kudhibiti mamba na viboko na sasa unakimbilia Ikulu, Ikulu kule ndiko utaweza! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nilishamwambia Mheshimiwa Nyalandu aje aondoe wale mamba na hata juzi hapa wamemla mama mmoja ambaye ndiye alikuwa ananisaidia kwenye kampeni. Nani atanirudisha Bungeni watu wangu wanateketea kwa sababu ya mamba hawa?

Mheshimiwa Spika, nizungumzie maji. Mheshimiwa Maghembe, maji yetu yanayotoka Nyabehu kwenda Bunda, ambapo Vijiji vitatu vya Bulamba, Buzimwe na Mwiseni wanatarajia kupata maji yale. Nashukuru Mheshimiwa Abdallah ulienda Kabainja pale, lakini mpaka leo maji ya Bunda imekuwa kizungumkuti. Hata kwenye Kitabu hiki cha Taarifa yake Mheshimiwa Waziri, hakuna huo Mradi wa Maji ya Bunda, Mradi mkubwa, lakini ukienda kwenye Miradi yake ya Same, Mwanga, ndiyo imejaa kwenye Kitabu hiki. Kwa nini nisiamini kwamba unafanya kazi kwa kupendelea maeneo yako?

Mheshimiwa Spika, tunahitaji maji haya Wananchi wa Bunda, yanatoka Ziwa Victoria, kilomita 20, lakini mpaka leo zaidi ya miaka sita Mradi huu haukamiliki. Wananchi wa Bunda wanaendelea kuteseka, mambo gani haya? Mimi nilishaomba, hawa Mawaziri ambao ni mizigo, Mawaziri ambao wanatupa tabu, kwa nini Mheshimiwa Rais anaendelea kuwakumbatia Mawaziri wa namna hii!

Sisi tunaenda kwenye uchaguzi, ambako naamini CCM tutaendelea kushinda kwa kishindo na Mheshimiwa Rais amefanya mabadiliko haya yawe na tija. Mheshimiwa Maghebe, unao muda wa kufanya marekebisho, Wananchi wa Bunda hatutakubali kukipigia kura Chama cha

Mapinduzi, iwe ni Udiwani, iwe ni Wabunge, hata mimi nitasema wasinipigie kura. Haiwezekani!

Mheshimiwa Spika, zaidi ya miaka sita, Wananchi wa Bunda wanatumia maji taka, mradi ule umekwama, fedha hakuna, halafu unaleta hapa Taarifa unasema umetekeleza, hali ya maji ni nzuri, hamna lolote! Wakati ule ulilidanganya Bunge hapa kwamba, Mradi unaendelea vizuri!

Narudia tena, Wananchi wa Wilaya ya Bunda, Mwibara, Mradi huu Maji unatuhusu na nina Miradi mingine ya Bulamba, Kibara, bado wakandarasi hawafanyi kazi kwa sababu ya kutokuwa na fedha. Wananchi wa Mwibara mnaonisikia, pamoja na kwamba nitakuja kuwaomba Ubunge, Chama cha Mapinduzi, msitupigie kura endapo Miradi yangu ya Maji, ukiwemo na wa Bunda, haitakuwa imekamilika. *(Makofi)*

Tumechoka! Wanatupigia kura nyingi wananchi wale, wanaibusu CCM, wanaikumbatia, wanaimba nyimbo za Komba usiku na mchana … *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Basi, na muda umefika.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tuendelee, nilisema Mheshimiwa Malocha, Mheshimiwa Zitto. Mheshimiwa Malocha yuko wapi?

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika Taarifa za Kamati ambazo zimetolewa mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, mimi naanza na suala zima la kilimo. Kabla sijaanza, kwanza, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Wasira, kwa kuteuliwa tena kushika

nafasi hiyo nyeti na sisi tuna imani naye na hata wananchi wana imani naye.

Mheshimiwa Spika, nazungumzia suala la kilimo kwa sababu, kwa sasa hivi karibu mikoa yote inayojihusisha na kilimo, ina tabu kubwa sana na wananchi wake. Ina tabu kubwa mno na hatujui suala hili tutanasuka namna gani, kwa sababu sehemu kubwa ya Watanzania wanategemea kilimo. Wakulima wadogo wadogo, wafanyabiashara, hata Watumishi wa Serikali, ili kujiongezea kipato nao wanajihusisha na kilimo. Kwa hiyo, lazima tujue kuwa sekta hii ina uzito wa pekee.

Nizungumzie tatizo lililopo katika Mkoa wa Rukwa kwa ujumla. Mkoa wa Rukwa unaotegemea kilimo cha mahindi, zao la chakula, lakini, kilio kilichoko kule ni cha hali ya juu. Wananchi waliouza mazao wengine hawajalipwa fedha mpaka sasa na wengine hawakupata nafasi ya kuuza mazao kutokana na Serikali kutonunua mazao yao au wafanyabiashara kushindwa kukidhi uwezo wa uzalishaji uliopo kwa sasa hivi. Kwa mfano, Mkoa wa Rukwa peke yake, kwa msimu uliopita wa mwaka 2014/2015 ulikuwa na ziada ya tani laki tatu na elfu arobaini. Tani zilizonunuliwa pamoja na zilizokopwa ni elfu sitini na tatu mia moja kumi na nne. Kwa hiyo, unakuta tani karibu laki mbili na sabini na sita elfu na zaidi, ndiyo zilibakia ambazo wafanyabiashara wengine wamenunua, lakini hawajakidhi haja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, lazima tukubali, kwa sasa hivi tatizo hilo ni kubwa na katika tani hizo zilizonunuliwa, fedha ambazo zinadaiwa mpaka sasa hivi na wananchi ni karibu bilioni 22. Juzi tumeambiwa tumepewa bilioni mbili. Karibu bilioni 20, hatujui wananchi hao watalipwa lini. Lazima tukubali kwamba, hii ni hasara kubwa na tumeleta matatizo makubwa kwa wananchi, kwa sababu walio wengi wameshindwa hata kumudu kilimo cha msimu huu. *(Makofi)*

Hata ukitoa fedha mwezi wa tatu, msimu wa kilimo umekwisha. Kwa hiyo, lazima tukubali tumewatia hasara wananchi, tumewakatisha tamaa, tumewaongezea

umaskini na hata ziada ya chakula Mkoa wa Rukwa nina imani kwa mwaka huu itapungua kwa kiasi kikubwa sana, kwa sababu mitaji imekufa na watu wanadaiwa na mabenki. Sasa lazima tujiulize, hivi kweli sisi kama Serikali tumeshindwa kutafuta ufumbuzi juu ya suala hili, kwa kundi kubwa ambalo linabeba watu walio wengi na ndiyo wapiga kura? Ukikidhi mahitaji haya, wala huwezi kuwa na wasiwasi wa uchaguzi ujao kwa sababu sehemu kubwa ya wananchi ipo katika kada hii ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naishauri Serikali, kama kuna mahali pa kuelekeza nguvu, ni katika suala la masoko. Masoko yanasumbua sana, yametia hasara sana wananchi, yametia hasara sana wakulima wadogo wadogo, wakulima wakubwa hata wafanyabiashara, hata watumishi wanaojiongezea kipato chao kutokana na mishahara midogo wanayoipata. Kwa hiyo, lazima nguvu kubwa ya Serikali tuelekeze katika kutafuta masoko.

Nina imani kabisa na Mheshimiwa Wasira aliyeteuliwa hivi karibuni, ninajua atakaa kidete kushirikiana na sekta nyingine kutafuta utatuzi, kwa kusaidiana na Naibu Waziri wake ndugu yangu Zambi, ambaye tunamwona anavyohangaika na suala hili. Kwa hiyo, lazima Serikali iangalie suala hili.

Mheshimiwa Spika, nakuja kwenye suala la maliasili. Katika maliasili, tatizo kubwa tulilonalo, mipaka yetu ya hifadhi haijawekwa alama ya kuonekana na wananchi. *(Makofi)*

Kutokana na tatizo hilo, inatoa nafasi ya wale wanaohusika na mipaka hiyo kuwachapa wananchi viboko kwa kisingizio kwamba wameingilia mipaka kumbe hata mipaka yenyewe hamjaonyesha barabara inaishia wapi. Wananchi wanaingia wanadhani wako salama, kumbe wameingilia hifadhi. Kwa hiyo, Serikali, mambo mengine sisi wenyewe ndiyo tunaosababisha wananchi wetu wapigwe. Kwa hiyo, ninashauri Serikali, sehemu zote za hifadhi, mipaka

ionekane wazi, ya nchi kavu hata ndani ya maji. Kwa sababu hata ndani ya maji kuna hifadhi. *(Makofi)*

Nitoe mfano wa Ziwa Rukwa, kuna sehemu imehifadhiwa kwamba ni mazalia ya samaki, lakini hawajaweka alama kwamba, mipaka hiyo inaishia wapi ndani ya ziwa. Kwa hiyo, wavuvi wanapoingia, bila kuelewa wanashitukia aidha wameingia ndani ya mipaka au hawajaingia na kwa sababu watu wetu siyo wote waaminifu, wanawakamata kwa kisingizio kwamba wameingia kwenye hifadhi, lakini ukiangalia hata mipaka haionyeshi ndani ya maji mipaka ni wapi. Kwa mfano, katika Kambi ya Nankanga na kule Muze, wavuvi wangu wamenyang'anywa vifaa, wamepigwa, kutokana na kutoonyesha alama za mipaka ndani ya Ziwa Rukwa. Kwa hiyo, ninaishauri Serikali ijaribu kuangalia jambo hilo.

Jambo lingine, ni zile hifadhi ambazo mmesema ni za akiba. Ukiangalia kwa undani unakuta hata wananchi wanashindwa kujua faida ya hizo hifadhi za akiba; kwa sababu pori limekaa, wananchi wanateseka na hata Serikali haionyeshi ushirikiano na vijiji vya maeneo yale walau kuwasaidia hata kwenye miradi ya shule, miradi ya zahanati ili kuwapa moyo wananchi watambue kwamba jambo lile wanashirikiana pamoja na Serikali, mmewaachia tu. Sasa unashindwa kuelewa, Serikali hii ipo kutesa wananchi au kuwasaidia, kutoa elimu na kushirikiana nao.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali iangalie zile hifadhi ambazo zimekaa kama mapori, aidha, kuwaelimisha wananchi au kuwaonyesha tija nyingine ambayo italeta faida kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitaka niliseme hilo. Ndugu yangu Lugola amezungumzia suala la mamba, nimelizungumza mara kadha wa kadha. Waziri ametoa ahadi humu zaidi ya mara hatu, hakuna kinachoendelea. Hivi wewe Waziri unadanganya nchi, unawadanganya wananchi! Mamba wanazidi kula wananchi, ambao ni wapiga kura, halafu mara tatu zaidi unadanganya; hivi unajiona uko sahihi kweli!

Aaah, mambo mengine kwa kweli mnatusikitisha na mnatushangaza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, naenda kwenye ardhi. Kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Lukuvi, kwa kuteuliwa; lakini ujue tuna kilio cha ardhi, upande wa Shamba la Malonje. Majibu yamekuwa yakitolewa na Serikali ya kuahirisha ahirisha, sijui hawapimi madhara yanayowapata wananchi! Unapoacha muda mrefu, katika ya mwekezaji na mwananchi, anayeumia ni mwananchi, kwa sababu mwananchi hana *alternative* nyingine ya kujisaidia zaidi ya ardhi.Yule mwekezaji ana mambo mengi. Mnawakalisha wananchi zaidi ya miaka mitatu; jamani, Serikali tuwe na huruma kwa watu hawa. Watu wanakuwa maskini kwa sababu ya jambo dogo la kutoa maamuzi jambo likaisha. *(Makofi)*

Sasa nina imani na Mheshimiwa Lukuvi kwamba, jambo hili utatusaidia kwa haraka zaidi.

Suala la maji; tumekuwa na Miradi mingi ya Maji ambayo inatekelezwa na mingine inamalizika lakini Serikali hamjapeleka pesa. Tuna taarifa kwamba wafadhili walishatoa pesa; sasa ninyi kwa nini hampeleki fedha kwenye Miradi ya Maji ambayo imeshakamilika? Halmashauri zitafikishwa mahakamani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri utuambie fedha zitaenda lini kwenye Halmashauri na hasa kwenye Miradi ambayo imeshakamilika na ile inayoendelea imesimama.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na hayo, nashukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, nakushukuru. Nilisema nitamwita Mheshimiwa Zitto, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mponda, atafuatiwa na Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye! Ikipatikana nafasi asubuhi hii basi Mheshimiwa Mkosamali atafuatia.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru. Jambo la kwanza, ningependa mwongozo wako kuhusiana na Muundo wa Taarifa za Kamati hizi, kwa sababu kwa mujibu wa Kanuni ya 123 inaonesha Taarifa za Kamati zinapaswa kuwa katika sehemu tatu. Sehemu ya mwisho ndiyo ambayo inatoa Maoni na Mapendekezo ya Kamati. Taarifa ambazo ziko mbele yetu hapa hazina sehemu hiyo ya mwisho ya maoni na mapendekezo ya Kamati, wamekwenda kwa mfumo wa kufanya *analysis* na ushauri. Kwa hiyo, mwishoni jioni tutakapokuwa tunapitoa tunafanya maamuzi ya Bunge, hatutakuwa na kitu ambacho tunakifanyia maamuzi. Kwa hiyo, naomba Wenyeviti na Makatibu wao wa Kamati, sasa hivi wakae ili waweze kutuandalia hayo maoni na mapendekezo ili jioni Bunge lako Tukufu liweze kufanya maamuzi inavyostahili, maana kuna wengine tuna mapendekezo ambayo tunataka tuyalete kama sehemu ya maoni hayo.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ambalo ningependa kulizungumzia ni ukurasa wa kumi na saba wa Taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira. Kifungu namba 4.1.8, kesi dhidi ya tozo kwa watalii wanaolala katika hoteli zilizoko katika Hifadhi za Taifa. Taarifa hii inaonesha kwamba, Waziri hajatoa Tangazo la Serikali ili tozo mpya zianze kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, toka wiki iliyopita tunalalamika hapa kuhusu kutokupatikana kwa mapato ya Serikali. Leo hii tuna Taarifa ya Kamati inayozungumzia Waziri kushindwa kutoa Tangazo la Serikali ili mapato yaweze kupatikana. *(Makofi)*

Wiki iliyopita na juzi Jumamosi tulikuwa tunazungumza kuhusu masuala ya Shirika letu la Ndege na Mheshimiwa Waziri Mpya wa Usafirishaji, hongera sana, amezungumza namna gani ya kuweza kufanya kuliokoa Shirika la Ndege. Moja ya mapendekezo ya Serikali yalikuwa, mashirika haya mawili ya utalii, kwa maana ya *TANAPA* na Ngorongoro, yawe ni sehemu ya *shareholders* kwenye Shirika la Ndege, kwa sababu utalii na ndege vinahusiana. Shirika

la ndege linahitaji fedha ya kununua ndege. Leo tunapoteza Shilingi bilioni themanini kwa sababu ya kutokusanya kodi ya tozo za kwenye utalii. Waziri Nyalandu yuko pale, anashindwa kutoa Tangazo la Serikali ili kodi hii iweze kukusanywa. Sasa tutaendelea kulalamika mpaka lini sisi Waheshimiwa Wabunge hatuchukui hatua! *(Makofi)*

Taarifa ya Kamati inaonesha kwamba, Kamati iliitaka Wizara ya Maliasili na Utalii iwe imeshatoa tangazo katika Gazeti la Serikali ifikapo tarehe 28 Januari, 2015. Leo ni tarehe 2 Februari, tangazo halijatoka, halafu Kamati inasema Kamati inataka Serikali itoe maelezo sababu ya kutokufanya hivyo. Kamati umeona agizo lako halijatekelezwa, halafu inaitaka Serikali itoe taarifa ndani ya Bunge! Mimi ninamheshimu sana Mwenyekiti wa Kamati, ni mzee wangu, ni rafiki yangu sana tu, lakini napata ukakasi wa namna ambavyo siku zote amekuwa akishughulikia watu wanaoshindwa kutekeleza wajibu wao, lakini hapa anavuta miguu kushughulikia watu wanaoshindwa kuchukua hatua. Ndiyo maana Mheshimiwa Lema juzi hapa akazungumza kwamba, hii kuna mapacha watatu; maana yake Waziri, Mwenyekiti wa Kamati, Waziri Kivuli wa Wizara, wote hakuna mtu ambaye anaona kwamba kuna tatizo katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe wito kwa Bunge lako Tukufu, itakapofika jioni ya leo, tutakapokuja kufanya majumuisho, kama Tangazo la Serikali kwa ajili ya kukusanya tozo hizi halijatoka, Waziri awasilishe barua yake ya kujiuzulu kwa Rais. Hatutaki kuwa na mchezo na masuala ya fedha za Umma. Tunalalamika hapa kila siku na linalohitajika ni tangazo kwa ajili ya kukusanya *almost two billions* kila mwezi. Tumeshapoteza *eighty billion* mpaka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Nyalandu, kijana mwenzangu na ningependa vijana wa-*perform* vizuri na siku zote naunga mkono vijana, nakuomba tutakapofika jioni haujatoa tamko la Tangazo hili, tusikuone humu Bungeni; kwa sababu hatuwezi kuvumilia upotevu wa mapato ya Serikali kiasi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo ninataka kulizungumzia, Mheshimiwa Sitta, twende tukakusanye hizi hela ndiyo tuifanye *ATCL* ianze kazi. Sehemu ya mapato haya ndiyo ya kuiendesha *ATCL,* tafadhali.

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo ninataka kulizungumzia ni ardhi. Mheshimiwa Kangi ametoka kumpiga kidogo Mheshimiwa Lukuvi hapa, lakini Lukuvi nimefanya naye kazi kwa karibu sana, mmoja wa watu ambao wamejitahidi kuokoa mkataba mbovu ule wa pale Oysterbay Plaza ni pamoja na Mheshimiwa Lukuvi. Ndiye ambaye amesababisha ile hati badala ya kuwa ya miaka 99 imekuwa kwa mujibu wa miaka ambayo imebakia katika hati. Kwa hiyo, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Mheshimiwa Kangi, nakuomba kidogo umwachie mshikaji. *(Makofi)*

Sasa tatizo ambalo lipo katika Wizara ya Ardhi na ninamwomba Mheshimiwa Lukuvi asikilize vizuri, ni kwamba, kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kuna viwanja 263,000 ambavyo vilitolewa hati hivi karibuni, lakini ni viwanja 22,000 tu ndiyo vimo kwenye kumbukumbu za Wizara. Jambo ambalo linapelekea Serikali kupoteza mapato ya zaidi ya Shilingi bilioni mia moja na tatu kwa mwaka wa fedha uliopita. Hapa tunazungumzia mambo ya mapato ya Serikali na huku ndiko kwenye mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha wa kabla ya mwaka huu ambao tumepoteza bilioni mia moja na tatu, Wizara ilipangiwa kukusanya Shilingi bilioni tisini na tisa kama tozo ya ardhi *(Land Rents)*. Wizara ilikusanya Shilingi bilioni ishirini tu, ambayo ni asilimia ishirini na moja ya makusanyo yote. Mwaka wa fedha uliofuata ndiyo hizo bilioni mia moja na tatu zimepotea kwa sababu zaidi ya viwanja 240,000 havimo kwenye kumbukumbu za Wizara.

Mheshimiwa Spika, sasa tuliunda Kamati ndogo na tulikuletea ushauri wetu na ninaamini kwamba utakuwa umeanza kuufanyia kazi. Moja ya ushauri wetu ambao

tuliutoa ni kuanza kutoa hati za ardhi kwa njia za elektroniki, kwa maana ya *digital land titles*. Tukifanya jambo hili kwa ushirikiano na sekta binafsi wala Serikali haitahitaji kuweka fedha ya bajeti, kwa sababu kama sasa hivi kupata *title* ni Shilingi laki mbili na elfu arobaini, tukishirikiana na sekta binafsi hizo laki mbili na elfu arobaini, kwa *title* tu laki nane ambazo ziko Dar es Salaam peke yake ni bilioni mia moja tisini na mbili. Kwa hiyo, Serikali itaweza kujiendesha bila kuhitaji bajeti na bila kwenda kupambana na Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni la kilimo na bahati nzuri Waziri wa Kilimo yuko hapa. Naomba aipitie Taarifa ya *PAC* ambayo tuliijadili juzi kuhusiana na tatizo kubwa la rushwa na ufisadi katika korosho na kuhusiana na namna gani ya kuhakikisha ya kwamba, tunauza nje korosho ambayo imebanguliwa. Naomba Waziri aipitie, atakapokuwa anakuja kujibu hapa aweze kufanya jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, yangu yalikuwa ni hayo tu, nasubiri Tangazo ili tuweze kuona kama tunakula kichwa cha mtu au anabakia.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nilisema nitamwita Mheshimiwa Dkt. Mponda, Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye na nilisema kama atakuwa karibu Mheshimiwa Mkosamali, kama hayupo najua yuko kwenye Kamati ya Bajeti basi ataingia Mheshimiwa Lolesia Bukwimba.

**MHE. DKT. HAJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Taarifa za Kamati zako tatu, lakini nitasisitiza mchango wangu zaidi katika Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, tumeona Taarifa ya Kamati na huko tunakotoka na tukipita sehemu zingine hasa tukielekea Dar es Salaam, tunaona misitu inavyotoweka. Hali ni mbaya sana.

Naungana mkono na ushauri ambao umetolewa na Kamati na ninaomba nichukue nafasi hii kumpongeza aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mwantumu Mahiza na dhamira na kauli aliyoitoa na amri kwamba sasa mikaa basi katika Mkoa wa Pwani. Mkoa wa Pwani misitu yake inateketea kwa sababu ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaungana na Kamati kwenye mambo mawili; kwamba, tuongeze kasi ya kupanda miti na udhibiti wa miti hiyo ambayo baadaye tunaita misitu. Asilimia hamsini na tatu ya misitu tunayozungumza iko chini ya mamlaka ya vijiji na Halmashauri. Sasa bahati mbaya mamlaka hizo hizo ndiyo wanapitisha vibali, mamlaka hizo hizo za vijiji na Halmashauri ndiyo wanawezesha uharibifu wa misitu hiyo.

Mimi ninaomba niwapongeze mamlaka au Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga kwa maamuzi yao ambayo wameyafanya hivi karibuni, kusimamia wale wanaoharibu misitu yetu ya hifadhi ya vijiji. Wamewafikisha mahakamani na ninaomba Serikali ongeeni na mahakama. Hatuwezi kuingilia Mhimili huu lakini unatuumiza, kwa sababu kesi zimepelekwa Mahakamani lakini utaratibu wanaoufanya wenyewe tunaona, hawana *interest* ya *public* Mahakama.

Mheshimiwa Spika, Taarifa imezungumzia sana mambo ya hifadhi, mimi naomba nizungumzie migogoro ambayo inajitokeza kati ya wananchi na mapori tengefu. Mwaka 2009 wakati tunarejea Sheria ya Wanyamapori, Bunge hili lilitoa maelekezo mawili nayakumbuka. Moja, waangalie kama kuna ulazima wa kuwepo na mapori tengefu 42 yaliyopo sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, mapori mengine wala siyo rafiki tena kwa wanyama wala mazingira, lakini bado mpaka leo Serikali hii hawajafanya.

Maelekezo ya pili katika kurejea Sheria hiyo ya Wanyamapori, Serikali walielekezwa warejee mipaka ya hifadhi ya mapori tengefu. Nitatoa mfano wa Pori Tengefu

la Bonde la Kilombero. Mwaka 2012 wamerejea mipaka ile, lakini walichofanya Serikali, badala ya kuyaachia yale maeneo ambayo wananchi wameshaanza kuyatumia, ambayo siyo rafiki tena kwa matumizi ya wanyama, ukirejea Taarifa ya Utafiti wa Wanyamapori ya 2008, walibainisha kuna maeneo hayafai tena kwa matumizi ya wanyamapori. Badala yake sasa waliporejea mipaka hiyo wameendelea kupunguza maeneo mengine ya ardhi za vijiji na wakatengeneza kitu kinaitwa *buffer zone*.

Mheshimiwa Spika, hii *buffer zone* kule kwetu Ulanga katika vijiji 91 vya Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga, vijiji 18 viko ndani ya *buffer zone*. Vijiji hivi vimesajiliwa na vitongoji vyake 15. Sasa tunawaeleza Serikali, Maliasili na Utalii, basi mrejee tena mipaka hiyo, hasa lile eneo mnaloliita *buffer zone*, mrudishe kwenye ardhi ya vijiji; vinginevyo, wananchi wale muwaambie waondoke. Suala la msingi hapa wakiondoka watakwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, nimeeleza sana kwenye mchango wangu wa bajeti ya mwaka huu katika Wizara hii na nimeiomba na bahati nzuri Waziri Mkuu amesikia kilio cha watu wa Ulanga. Kwa kuwa tulikwenda kwake tukamweleza, tukafafanua akalielewa na mwezi wa nne mwaka huu alitoa agizo kwa dokezo kwamba, Wizara nne zikutane, zitengeneze jopo, waangalie watawezaje kutatua suala hili la *buffer zone* kwenye Wilaya ya Ulanga au lile Bonde la Mto Kilombero kwenye Pori Tengefu la Mto Kilombero.

Mheshimiwa Spika, lakini mpaka leo Mawaziri hawa; Waziri wa Maliasili na Utalii, Waziri wa Ardhi, Waziri wa Mazingira na Waziri wa TAMISEMI hawajakaa, angalau wakae wapitie maombi haya, wapitie kero hizi na siyo Ulanga tu peke yake na mapori tengefu mengine 42, je, bado tunahitaji tuendelee kuya-*maintain*?

Mheshimiwa Spika, wananchi wanateseka maeneo yale, wanaishi kwa hofu, hawalimi kama inavyotakiwa. Kule kwetu asilimia karibu 40 ya wakulima wanaishi kwenye maeneo hayo. Kule kuna wakazi karibu 40,000 na kuna hekta

zinazolimwa 90,000. Sasa mpaka leo Serikali bado hawajafanya maamuzi haya kwamba tutafikia wapi. Usumbufu huu unawacheleweshа wananchi kulima kila mwaka, wale wafugaji kila siku wanaisumbua mifugo wakati wananchi wale wanaishi kule kwa sababu vijiji vile vimesajiliwa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba basi wakati watakapohitimisha Wizara watupe kauli moja. Ninamwomba Waziri wa Maliasili na Utalii, yeye amepewa mamlaka katika sheria ya Wanyamapori ya Mwaka 2009, yeye ndiyo ana maamuzi namna gani maeneo ya *buffer zone* yanaweza yakatumika, wakati huo mchakato ukiendelea kuirudisha ile ardhi ya *buffer zone* kwa wananchi wa vijiji vile kumi na nane vya Wilaya ya Ulanga.

Mheshimiwa Spika, nami naunga mkono Taarifa ya Kamati, hii migogoro ambayo iko katika Hifadhi ya Taifa na dhidi ya wananchi; kwa mfano, Tarangire na Ruaha. Ombi langu ninaomba waendeleze na kukamilisha huo mchakato ambao ni wa muda mrefu na majibu ndiyo hayo hayo kila siku kwamba, mchakato, tutaendelea, mazungumzo tutaendelea kuwahusisha wadau, lakini kilio hiki ni cha miaka mingi. Haya ya hifadhi na wananchi, migogoro ya mipaka kila siku inaendelea.

Mheshimiwa Spika, naomba tu nimalizie upande wa ardhi. Migogoro ya mipaka ya ardhi ambayo bado inajitokeza kati ya kijiji na kijiji, mipaka ya ardhi kati ya Wilaya na Wilaya iko ndani ya uwezo wa Wizara ya Ardhi. Bado mpaka leo hawajatimiza lile zoezi la matumizi bora ya ardhi. Vijiji vingi tumejitayarisha, lakini tunapopeleka maombi yetu kwenye Wizara tunaambiwa fedha hakuna au tunaambiwa baadaye. Kwa hiyo, tunaomba hasa kwa Wilaya ya Ulanga, ili tuweze kuondoa migogoro ya mipaka kati ya vijiji na vijiji, kati ya haya mapori tengefu, malizieni hili zoezi la matumizi bora ya ardhi ambayo itaiwezesha sasa kisheria hawa wananchi namna gani watajipanga kutumia ardhi yao.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwenye ardhi. Hawa Wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya jamani ni matatizo. Baadhi ya wilaya Wenyeviti hawa ni matatizo. Wilaya ya Ulanga na Kilombero, Baraza la Ardhi Mwenyekiti wetu ni mmoja yuko Ifakara, amekaa pale zaidi ya miaka mitano sasa, mengi tumesharipoti lakini bado Serikali mmekuwa na kigugumizi. Ombi letu, tunaomba huyu miaka yake imetosha pale mumtoe mumpeleke sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye, atafuatiwa na Mheshimiwa Lolesia Bukwimba!

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na Wizara ya Ardhi. Ningeomba tupatiwe taarifa ya utekelezaji wa Mradi wa Kupanga Matumizi Bora ya Ardhi, Kupima na Kumilikisha Wananchi Ardhi, ambao *G8*, Benki ya Dunia pamoja na Sweden, mwaka wa juzi walikubali kujitolea kwamba watatusaidia kuutekeleza Mradi huo kwa gharama ya Dola za Kimarekani milioni kumi na tano. Tungeomba kupata taarifa ya utekelezaji, umefikia wapi Mradi huo.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Mradi huu ni kuondoa migogoro ya ardhi. Kama ardhi itakuwa imepangwa na imepangiwa matumizi, maana yake mgogoro baina ya makundi ya watumiaji, wakulima na wafugaji, hifadhi, pamoja na wananchi, itakuwa imeweza kuondoka. Kama tutapima ardhi na kuwamilikisha wale wenye haki juu ya ardhi hiyo, basi mgogoro baina ya mtu na mtu au kikundi na kikundi utakuwa umeondoka.

Mheshimiwa Spika, suala la pili kuhusiana na migogoro ya ardhi ni masuala ya mipaka. Mwaka 2014 mwezi Novemba, wakati wa Mkutano wa 16 na 17, Mheshimiwa Waziri Mkuu alimwagiza Waziri wa Ardhi kwamba, aende Arusha, ashirikiane na Uongozi wa Mkoa, kusuluhisha

mgogoro wa muda mrefu wa mpaka baina ya Monduli na Arumeru, Longido na Arumeru. Mgogoro huu ni wa siku nyingi sana, ambao ulianza baina ya iliyokuwa Wilaya ya Arusha na iliyokuwa Wilaya ya Maasai na umeendelea hadi leo hii.

Mkuu wa Mkoa aliyeteuliwa hivi karibuni, Mheshimiwa Daud Felix Ntibenda, yuko tayari kusuluhisha mgogoro huo, lakini anahitaji kusaidiwa, hususan nyenzo muhimu. Ramani ya Wilaya hizo ilipoanzishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1926 na kusajiliwa mwaka 1954 zikipatikana ni nyenzo muhimu za kuweza kusuluhisha mgogoro huo. Wabunge wa Majimbo katika Wilaya hizo kwa maana ya Mheshimiwa Mbunge wa Monduli, Mheshimiwa Mbunge wa Longido na mimi mwenyewe tumeshajadili, tuko tayari kushirikiana kwa ajili ya kusuluhisha mgogoro huo.

Mheshimiwa Spika, tunamwomba Waziri atuambie lini atakuja Arusha ili tushirikiane kusuluhisha mgogoro huo wa muda mrefu, ambao umekuwa ukigharimu maisha ya watu na mali. Tusingelipenda kuona ndugu ambao wana nasaba ya muda mrefu wakiendelea kugombana pasipo sababu za msingi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mgogoro wa mashamba, tunayo migogoro ya mashamba kadhaa kule Arusha. Kwanza, kuna Wananchi wa Oldonyosambu, ambao Ardhi yao ilitwaliwa na Serikali mwaka 1984 kwa madhumuni ya kuanzisha Kambi ya Kikosi cha Jeshi katika eneo hilo. Hadi leo wananchi hao pamoja na ahadi ya muda mrefu ya Serikali, hawajapewa ardhi mbadala. Tunaomba Serikali ituambie ni lini wanapewa ardhi hiyo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, mwaka 2013, ulianza mgogoro juu ya Shamba la Chama Kikuu cha Ushirika Arusha, yaani *Arusha Cooperative Union,* ambao ulitokana na wananchi kutaka kuvamia Shamba hilo. Chama cha Ushirika kilikubali kwamba kingeliwakatia wananchi hao sehemu ya ardhi hiyo ekari zipatazo 1,500. Kabla ya zoezi hilo kufanyika, Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, alikwenda pale na kuwaambia wananchi kwamba, yuko tayari kuwapa

shamba zima badala ya hizo ekari 1,500 ambazo Chama cha Ushirika kilikuwa tayari kuwapa. Tungetaka kujua Mamlaka ya Mkuu wa Wilaya katika ugawaji wa ardhi inatoka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kana kwamba haitoshi, mwezi Novemba, 2014, aliyekuwa Naibu Waziri wa Ardhi, alikwenda Arusha na kwenda ku-*cement* yale ambayo Mkuu wa Wilaya aliyafanya, kwa kwenda kutaka kuligawa Shamba la Chama cha Ushirika. Tunaomba maelezo ya Serikali, kwa nini wamiliki halali ambao wanaendeleza mashamba yao wananyang'anywa bila sababu?

Mheshimiwa Spika, wako wawekezaji ambao kwa kiasi kikubwa mimi ninaweza kusema ya kwamba, wananyanyaswa na Serikali. Kuna Kampuni inaitwa *Tanzania Plantation*. Mwaka 1999 Serikali ilitoa sehemu ya mashamba ya Kampuni hii, Mashamba sita yalitwaliwa na Serikali iliahidi ingelilipa fidia. Hadi leo Kampuni ile haijalipwa fidia hiyo na aliyekuwa Naibu Waziri wa Ardhi, alipotembelea Arusha Novemba, 2014 alikwenda akamwagiza Msajili Msaidizi wa Hati kwamba, asajili hatua iliyochukuliwa na Serikali mwaka 1999 ya kutoa mashamba yale, kabla ya wenyewe kulipwa fidia.

Mheshimiwa Spika, sisi sote tuliomo humu ndani tumekula kiapo cha kuilinda Katiba yetu. Katiba ya Jamhuri ya Mwaka 1977, inaelekeza kwamba, kabla mali ya mtu yeyote kutwaliwa, Serikali inapaswa ilipe fidia kwanza kwa thamani stahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tungeliiomba Serikali iheshimu Katiba, Sera ya Ardhi na isimamie na kutekeleza Sheria ya Ardhi. Mwekezaji huyu wa *Tanzania Plantations*, alipwe fidia stahiki kwa Ardhi yake yote ambayo imechukuliwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Mipango Miji; Miji imekuwa inakuwa holela karibu maeneo yote ya nchi. Tunaiomba sana Serikali, ichukue hatua, iwe *pro-active,* inapoona kuna *settlement* inataka kuanza, ichukue hatua

ya kupima eneo hilo na kuwamilikisha wananchi na kusimamia ujenzi kwa viwango ili kuepuka makazi holela.

Mheshimiwa Spika, Mabaraza ya Ardhi; Serikali imechukua hatua ya kuboresha Mahakama na hususan baada ya kuanzishwa kwa Mfuko wa Mahakama. Tunaipongeza sana Serikali kwa kazi kubwa ambayo imekuwa ikiifanya katika uboreshaji wa Mahakama. Hata hivyo, Mabaraza ya Ardhi ambayo yalianzishwa kwa madhumuni ya kusuluhisha migogoro ya ardhi, yamekuwa yakifanya kazi katika mazingira magumu. Wenyeviti wa Mahakama hiyo hufanya kazi bila vitendea muhimu sana vya kazi. Tunaiomba Serikali ichukue hatua ya kuboresha Mabaraza hayo, ikiwa ni pamoja na kuwalipa Wazee wa Mahakama posho wanazostahili.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa misitu, Serikali tunaomba kama ambavyo Mheshimiwa aliyenitangulia kusema, misitu ya asili inateketea. Tunashughulika kuwalinda tembo, lakini kuna siku itafika tembo hatakuwa na mahali pa kujificha, kwa sababu misitu hiyo inakatwa na kugeuzwa kuwa mkaa. Serikali kupitia Wizara husika, ichukue hatua stahiki kuhakikisha misitu ya asili inalindwa kama ambavyo tunahangaika kuwalinda tembo na simba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2014 wakati tukijadli Bajeti ya Wizara ya Kilimo tulipendekeza na ninakumbuka nilipendekeza tujenge mabwawa ya Kimkakati, yatakayotumika kwanza kutoa maji ya kunywa kwa wananchi, umwagiliaji na kupata maji ya mifugo na ikiwezekana tufuge samaki ili wananchi wetu wapate *protein.* Utekelezaji wa Miradi hii inaelekea pengine kwa sababu hakuna fedha za kutosha zinazotengwa kwa ajili hiyo, haitekelezwi ipasavyo.

Kule kwangu tunalo bwawa ambalo tumeanza kulijenga tangu mwaka 2012, lakini hadi leo hii halijakamilika, kwa sababu ya kutokuwepo kwa fedha. Mradi ule umekwama na matokeo yake, lengo lile ambalo awali ilikuwa ni kwa ajili ya kuzuia mafuriko na pia kwa ajili ya

kuwapatia vijana ajira kupitia kilimo cha umwagiliaji limekwama kufikiwa. Ninaiomba Serikali itusaidie kuweza kupata fedha kwa ajili ya kutekeleza Mradi huu.

Mheshimiwa Spika, kuna wananchi katika Jimbo langu ambao wananyanyaswa na Hifadhi ya Msitu wa Meru. Ng'ombe akiingia kwenye Msitu ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Lolesia Bukwimba!

**MHE. LOLESIA J.M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuunga mkono kwa dhati changamoto mbalimbali pamoja na Maoni ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, hasa walipozungumzia changamoto ambazo zinajitokeza katika Bajeti za Halmashauri. Mara nyingi Serikali inapeleka fedha kidogo kidogo sana katika Halmashauri na hii inapelekea Miradi mingi ya utekelezaji hasa Miradi ya Maji, kutokukamilika kwa wakati.

Halmashauri ya Wilaya ya Geita, ni mfano dhahiri kwamba ni kweli kabisa Bajeti ambazo zimekuwa zikipelekwa, yaani fedha, ni kidogo sana ukilinganisha na Bajeti. Kwa hiyo, niunge mkono kabisa kama ambavyo Kamati imesema na mimi nichukue fursa hii kuiomba Wizara inayohusika ya Maji, iweze kuhakikisha fedha ambazo tumezibajeti zinaenda kwa wakati ili Miradi ya Maji iweze kutekelezwa kama ilivyokusudiwa. *(Makofi)*

Kuna Miradi ile ya Vijiji Kumi. Miradi hii imekuwa ni ya muda mrefu sana, zaidi ya miaka kumi bado haijakamilika na tatizo kubwa ni fedha. Naiomba Wizara, sasa ni wakati mwafaka kwa sababu ni muda mrefu na mwaka huu wa 2015 ni kipindi ambacho ni vyema Miradi yote ikamilike, ili kuwafanya wananchi waweze kuona jinsi ambavyo Serikali inafanya kazi yake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Geita kwa ujumla kuna changamoto kubwa sana ya maji. Nilikuwa nikiangalia taarifa ya Mheshimiwa Waziri, sijaona kabisa akizungumzia Geita. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri azungumzie suala hili wakati anafanya majumuisho kuhusiana na Miradi ya Maji Geita. Ninasema hivyo kwa sababu mara nyingi maji yanatolewa Ziwa Victora kwenda katika mikoa mingine kama vile ya Tabora, Shinyanga, wakati mikoa ambayo tunazungukwa na Ziwa Victoria kama Mkoa wa Geita, kwa kweli tuna changamoto kubwa sana ya Maji. *(Makofi)*

Tukitumia vizuri vyanzo vya maji vilivyopo kama Ziwa Victoria, mimi nina uhakika changamoto ya maji katika Mikoa wa Geita na mingine ambayo imezunguka Ziwa Victoria, haitakuwepo.

Ninachukua fursa hii kuiomba Serikali iweze kuweka mipango mikakati mizuri ya kuhakisha inatumia vizuri vyanzo vya maji vya Ziwa Victoria na kuhakikisha wananchi wanapata maji hasa katika maeneo ambayo tumezunguka Ziwa Victoria ikiwemo na Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna jambo ambalo limezungumzwa katika Taarifa ya Kamati kwamba, mara nyingi shughuli za uchimbaji wa madini zinaharibu vyanzo vya maji. Ni kweli kabisa kwamba, katika Mkoa wa Geita, shughuli nyingi ni za uchimbaji wa madini, kwa hiyo, mara nyingi wananchi wanatumia maji ambayo ni machafu kwa

sababu ya shughuli za uchimbaji wa madini. Ninaiomba Serikali iweke mkakati mzuri, ili kuhakikisha tunapta maji safi na salama katika maeneo hayo. Kwa sababu mara nyingi shughuli za uchenjuaji wa dhahabu na mambo mbalimbali ya uchimbaji wa madini, tunakuta maji mengi ambayo yanatumika katika shughuli hizo, wananchi wanatumia pamoja na mifugo, jambo ambalo ni hatari sana kwa afya za binadamu. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali iweke kipaumbele kuhakikisha tunapata maji safi na salama katika maeneo ambayo yako katika shughuli za uchimbaji wa madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kilimo ni vyema tukaangalia uwezekano wa kupata miundombinu muhimu kwa ajili ya umwagiliaji hasa katika maeneo ya Maziwa kama Ziwa Victoria na sehemu nyingine. Tukiwa na shughuli za umwagiliaji, mimi nina uhakika wananchi wataweza kufanya shughuli zao mwaka mzima na tutaweza kupata mazao ya kutosha. Kwa sababu hii, naiomba Serikali iweke Miradi ya Umwagiliaji katika Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Maziwa mengine hapa Tanzania. Miradi hii itatunufaisha wananchi tulioko kando kando ya Maziwa kuweza kufanya shughuli hizi kwa mwaka mzima.

Nimefurahishwa na Kamati kwamba iliweza kutembelea Sudan na kuona jinsi ambavyo wanatumia Mto Nile. Kwa hiyo, niombe basi na sisi katika Tanzania hii, kupitia Ziwa Victoria na Maziwa mengine, tuhakikishe tunatumia vizuri rasilimali ya maji kwa ajili ya kuwezesha shughuli za umwagiliaji katika mikoa ambayo imezunguka Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile ninaiomba Serikali, mara nyingi nimekuwa nikiomba iwekeze kwenye viwanda vidogo vidogo. Viwanda hivi vitatuwezesha wananchi kuongeza thamani ya mazao. Kilimo kisichoongeza thamani ya mazao tutakuwa hatupati faida ya kutosha. Tukiweka viwanda

vidogo vidogo, nina uhakika tutaweza kunufaika zaidi na wananchi wataweza kupata faida kubwa kutokana na mazao yao kuongezewa thamani. *(Makofi)*

Mkoa wa Geita hatuna Viwanda, Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha viwanda vipya hasa vidogo vidogo ili kuwawezesha wananchi weweze kufanya shughuli zao na kuongeza thamani ya mazao. Tuna mazao mengi, kuna pamba, mahindi na mzao mchanganyiko na yote haya tunahitaji kuwa na viwanda kwa ajili ya kuongeza thamani ya mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ninapenda kulizungumzia ni suala la ulipwaji wa fidia, hasa kwa upande wa ardhi. Katika Kijiji cha Rwamgasa kule Geita, namwomba Waziri wa Ardhi aangalie sasa, wananchi wamefanyiwa tathmini ya kulipwa fidia ili waondolewe katika eneo la Rwamgasa na sehemu mbalimbali jirani na pale.

Tathmini hii imefanyika kwa muda mrefu sana, sasa ni miaka miwili, wananchi hawajalipwa fidia yoyote na hakuna kitu chochote kinachoendelea. Wananchi wanauliza sasa inakuwaje, maana wamezuiliwa kufanya shughuli mbalimbali za kilimo katika maeneo hayo?

Wanaiuliza Serikali sasa wafanye nini, maana hata kulima hawawezi kulima, hawawezi kufanya shughuli yoyote, kwa sababu wanasubiri kulipwa fidia na Shirika la Madini ambalo linatarajiwa kuwekeza katika meneo hayo. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, aangalie utaratibu mzuri wa kuwawezesha wananchi hawa, kama ni fidia waweze kulipwa mara moja ili waweze kuendelea na shughuli nyingine. Wasipolipwa fidia tuangalie utaratibu …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha. Tatizo linaloonekana katika kujadili taarifa za utekelezaji wa Kamati katika kipindi cha mwaka, wachangiaji wanajadili zaidi mambo yao. Matokeo yake sasa inakuwa kama ni Kikao cha Bajeti. Kwa hiyo, maombi hapa yamefika karibu wachangiaji 200 na tutakaporudi kipindi cha jioni watapata nafasi wachangiaji sita tu. Nadhani siku zijazo tutajipanga na kuona ni utaratibu upi mzuri wa namna ya kuzijadili. Kwa sababu kama taarifa zitakuwa *issue oriented* kitu fulani, ndiyo hicho mnachokijadili halafu mnakipigia kura.

Mheshimiwa Zitto katika mapendekezo yake amependekeza kama yalivyoandikwa, yaani hapa wala hakuna wanachojadili. Yale yaliyoletwa na Kamati ndiyo mapendekezo hayo hayo. Hakuna anayejadili hayo mambo, wala anayebadilisha, watu wapo kwenye habari nyingine za mamba huko na mikutano ya mamba. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunalo tatizo, *technically* kwa maana ya taarifa hizi tunalo tatizo, kwa sababu hatujadili hizi taarifa, tunajadili vitu vingine kabisa. Mkikuta majibu hayatoshelezi msimlaumu mtu, kwa sababu hizi siyo hoja za kipindi hiki. Kwa hiyo, kama ingelikuwa *issue oriented,* tunajadili *issue* moja, tuanasema na sisi wote tunakubaliana na mapendekezo ya Kamati au tunaya-*amend,* lakini mna-*amend* vitu gani wala hamzungumzii vitu walivyoleta. Ninyi mko mbali kabisa na mambo yenu.

Tutakaporudi jioni nitamwita Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Saleh Pamba na Mheshimiwa Yussuf Hussein ajiandae.

Ninasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.56 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyowaambia, hoja hizi ni lazima tuzimalize jioni hii. Kwa hiyo, ninao wachangiaji, lakini naangalia wale ambao wanatakiwa kuchangia, Mheshimiwa Mkosamali kidogo amechelewa sijui! Mheshimiwa Saleh Pamba, Mheshimiwa Yussuf Hussein na Mheshimiwa Dkt. Kafumu kama yupo. Tuanze na waliopo, kama wakirudi, basi wamekosa nafasi.

Mheshimiwa Pamba!

**MHE. SALEH AHMED PAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Nami napenda nichukue nafasi hii vilevile nizipongeze Kamati zote mbili kwa taarifa nzuri ambazo wamezitoa na vile vile mapendekezo ambayo yapo katika taarifa hizo.

Mheshimiwa Spika, nitajikita katika maeneo kama matatu ambayo nataka kuyazungumzia. La kwanza, nataka kuzungumzia suala la utalii.

Mheshimiwa Spika, kuna taarifa ya Benki ya Dunia ambayo imetoka hivi karibuni nami nataka ninukuu maneno machache tu ambayo yapo katika taarifa hiyo, yanayohusu utalii wa Tanzania, nayo kwa Kiingereza yanasema kama ifuatavyo naomba ninukuu: Wanasema, "*Tanzania Tourism Sector is the story of a starving man who is surrounded by plenty of food.*" Kwa tafsiri rahisi, maana yake ni kwamba utalii wa Tanzania ni kama mtu ambaye ana njaa kali sana lakini amezungukwa na chakula kingi sana. Ukweli huu nadhani unabaki kama walivyosema Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, tunavyo vivutio vya kutosha vingi kuliko nchi zote duniani, chakula ni kingi lakini bado tunalalamika kuhusu njaa. Moja ambalo linajitokeza ni kwamba hatujaweka mipango ya muda mfupi, mrefu na wa kati wa kuhakikisha kwamba tunafahaidika na sekta hii muhimu.

Kwa tathmini ambazo Benki ya Dunia wamesema, ni kwamba kama Tanzania tungezitumia fursa zote tulizonazo na kuondoa vikwazo katika Sekta ya Utalii, katika kipindi cha miaka 10 ijayo, tungeweza kila mwaka kupata siyo chini ya Shilingi bilioni 16 kutokana na sekta hii. Lakini sasa hivi mchango wake ni Shilingi bilioni 1.9. Maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba, ni lazima tuwe na mpango wa muda mrefu ambao siuoni katika Serikali wa miaka 10 ijayo kuhakikisha kwamba tunafikia na tunaweza kutumia vivutio hivyo.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema kwamba kuna haja sasa kwa Serikali kujipanga vizuri na kuhakikisha kwamba wanakuja na mkakati na mpango mahususi wa kuendekeza sekta hii katika miaka 10 ijayo. Maana yake ni kwamba lazima kuwe na *reform* kwa jinsi tunavyoendesha sekta hii sasa na lazima tuwe na mipango thabiti ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo ambayo ni lazima tuyatekeleze katika mpango ambao tunataka tuuandae. Kwanza, ni lazima tuimarishe na kukuza utalii kwenye Kanda ya Kusini, kwa sababu sasa hivi tume-*concentrate* kwenye Kanda za Kaskazini na tumeacha Kanda za Kusini. Ni lazima tuongeze idadi ya mahoteli na idadi ya vyumba, ni lazima tuimarishe mafunzo kama tunataka kushindana na wananchi, ni lazima tuimarishe utangazaji. Tanzania haijulikani sana huko duniani. Pamoja na kwamba tunavyo vivutio vyote lakini utangazaji wetu ni dhaifu.

Jambo la tatu ni lazima tuhakikishe kwamba tunatumia raslimali za utalii wa ndani. Watanzania sasa hivi wameshaimarika sana kiuchumi na kifedha. Kwa hiyo, kuna Jumuiya ya Kati, yaani *Middle Class* kubwa, tukiwatumia hawa wanaweza wakatusaidia sana katika kukuza utalii wetu. Sasa haya ni maeneo ambayo ni lazima tuyafanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa na ambalo ni muhimu sana ni kuhakikisha kwamba malipo yote yanayolipwa hapa nchini kwa ajili ya Sekta ya Utalii,

yanaingia nchini. Kama tukiyaachia Makampuni makubwa yaliyopo nje yatuletee watalii, halafu fedha zote zinalipwa nje na bila kuwa na mfumo madhubuti wa kibenki wa kuhakikisha kwamba malipo yote yanakuja nchini, tutakuwa tumefanya kazi bure.

Kwa hiyo, haya ni maeneo ambayo katika mkakati wetu na mpango wetu ni lazima yawekwe na kuhakikisha kwamba tunaweza kusonga mbele kama Benki ya Dunia ilivyosema tuweze kupata dola bilioni 16 kwa mwaka. Haya masuala tunayozungumza ya umasikini na kadhalika, tunayo sekta ambayo inaweza kutusaidia na kutuondolea matatizo haya.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia, halihusiani zaidi na utalii, linahusiana na suala la mazingira. Lazima tukubali kwamba hali ya mazingira nchini imekuwa tete, hasa kwa upande wa mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wamezungumzia sana asubuhi hapa masuala ya kupanda miti, uhifadhi, kupunguza idadi ya watu na kadhalika. Haya ni maeneo ambayo lazima tuseme kwamba ni maeneo ya ukweli.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kujidanganya kwamba suala la tabia nchi halipo, tunalo! Tunaona mafuriko, tunaona bahari inapanda, tunaona *landslides* zote hizi, nalo hili kama nilivyosema kwenye utalii, linataka mikakati mizuri, ambayo pia inawekewa raslimali fedha ili kuhakikisha kwamba tunatunza mazingira yetu. Hayo ni maeneo ambayo nataka kuyazungumzia.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano tu katika Jimbo langu katika athari ya mazingira. Kwa mfano, tumepoteza kisiwa kizima pale Pangani ambacho hakipo sasa hivi. Kilikuwepo miaka kumi iliyopita! Lakini sasa hivi Mji wa Pangani unatishiwa na mmonyonyoko. Kuna *project* ya *UNEP* miaka minne *down the line* lakini hakuna kazi iliyoanza. *UNEP* wametoa dola 1,000,000 lakini hakuna kazi yoyote ambayo imeanza mpaka

leo. Maana yake ni kwamba labda Serikali inasuburi hao wananchi wachukuliwe au wasombwe na maji kama Indonesia na maeneo mengine.

Kwa hiyo, Serikali inatakiwa iongeze jitihada zake. Eneo hili ni moja tu, lakini kuna meneo mengi tu ambayo ni mifano hai.

Suala lingine ambalo nataka kulizungumzia haraka haraka ni masuala ya migogoro iliyopo kati ya wananchi hasa masuala ya ardhi, mipaka katika maeneo ya hifadhi na kadhalika. Yamezungumziwa na Wabunge wote kwamba lazima Wizara ya Maliasili ifike mahali iseme kwamba kama maeneo haya hayana tena sifa ya kuwa hifadhi, basi tuachane nayo ili kusudi wananchi waendelee na shughuli zao. Lakini hii migogoro isiyokwisha, itamalizika lini? Tume, tume, tume! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna migogoro katika hifadhi ya Saadani pamoja na wananchi kuhusu mipaka. Huu ni mwaka wa 10 sasa tangu kuanzishwa hifadhi, hakuna *solution,* wanasema Tume itakuja, Tume inakuja. Naiomba Wizara inayohusika kwamba, ni lazima tufike mahali tuone kwamba tumemaliza matatizo hayo.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kuyazungumzia haya nataka nizungumzie lingine la mwisho. Wizara ya Maliasili ina utaratibu mzuri sana wa kuwahusisha wananchi katika kuhifadhi, ndiyo maana katika sera zao kuna maeneo yanaitwa Hifadhi za Jamii, katika sera zao wanasema lazima sisi wananchi tukubaliane ndiyo tuhakikishe kwamba tunawatunza wale wanyama kwa sababu tunaona faida zake.

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi ni kwamba katika maeneo yote ambayo yanazunguka hizi hifadhi, wananchi wanatakiwa waone faida za kweli zinazotokana na hifadhi hizi. Kama hawataona, hawatawasaidia kuwatunza hao wanyama. Kwa sababu majangili ambao mnapambana

nao, wanaishi huko huko vijijini. Lakini kama hamwasaidii wanavijiji katika huduma mbalimbali, hawatawasaidia.

Kwa hiyo, nafikiria kwamba ni lazima Wizara kwamba yale matatizo madogo madogo ambayo mnaweza kuya-*solve* katika muda mfupi, mchukue muda mfupi sana muweze kuya-*solve*.

Kwa mfano, katika Hifadhi ya Saadani ambayo inapakana na vijiji vyangu kule, miaka 10 iliyopita tembo wenu walitoka wakaharibu mazao, minazi na mashamba. Tumekuwa tukifuatilia suala hili la kuwalipa wananchi fidia, sasa ni mwaka wa 10, wananchi wamekuwa masikini, wananchi wanategemea minazi na Korosho; Korosho zao zimekufa na hakuna kifuta machozi.

Mheshimiwa Spika, nimezungumza na Waziri wa Maliasili aliyepita, kuna Mawaziri watatu wamepita sasa hivi na Ndugu yangu Mheshimiwa Nyalandu ameniahidi. Kwa hiyo, nitashukuru kama suala hili litafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, nilimwita Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein halafu Dkt. Kafumu.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, nami nashukuru kwa kupata nafasi jioni hii ili niweze kuchangia katika mjadala ulio mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nataka nianze na Wizara ya Ardhi, Maliasili na Mazingira hasa katika *report* yao kwenye ukurasa wa 25 na 26 alipozungumzia miti ya mikoko.

Mheshimiwa Spika, miti ya mikoko siyo tu kwamba inaleta faida za kiuchumi ambazo amezizungumzia hapa. Miti ya mikoko ina faida nyingi. Tuangalie sasa hivi athari iliyotokea kule Mtwara, Msimbati. Kama eneo lile lingekuwa limepandwa miti ya Mikoko basi athari ya bahari kuchukua

ardhi isingetokea. Kwa hiyo, ile miti ya mikoko inazuia mmomonyoko wa ardhi kwa kiasi kikubwa sana. Kwa hiyo, ni miti ambayo inatakiwa ipandwe katika fukwe zetu zote ili kuzuia bahari kumega ardhi yetu kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, nami naiomba Serikali, kama ambavyo katika miaka ya 80 kulikuwa na miradi ya *HADO* na HASHI ya kuhakikisha kwamba maeneo ya Shinyanga na Dodoma yanapandwa miti kwa mkakati maalum, naiomba Serikali, sasa hivi katika fukwe zetu ipandwe miti ya mikoko kwa mkakati maalum. Lakini siyo kwamba ina manufaa ya kuzuia mmomonyoko wa ardhi tu au faida za kiuchumi, lakini pia ni mazalio makubwa sana ya vyakula vya baharini kama Kaa, Kamba na Chanje ambao wanapatikana wengi katika maeneo ya Mikoko.

Pia kuzuia upepo mkali, (windbreak) Katika hili nitakupa mfano, katika Kisiwa cha Kojani katika miaka ya 1970 na 1980, ilikuwa kila msimu wa Kusi watoto 150 na 200 ikifika msimu huo wanapoteza maisha. Watu wanajiuliza ni nini? Tatizo likawa halijulikani, kumbe ilikuwa ni upepo tu wa Kusi unapovuma na upande wa Kusini wa Kisiwa cha Kojani, hakuna miti, ikawa upepo unakuja katika Mji, watoto wanapata maradhi; *Pneumonia, Anemia*, wanakufa watoto 150 hadi 200 kila mwaka. Lakini baada ya wenyewe kufahamu tatizo hili wakauachia msitu ule ukue, wakapanda na wakaweka sheria zao na tatizo lile Kojani limeondoka. Kwa hiyo, huu ni mfano wa wazi, mtu kama anataka kujifunza, Kojani ni *sample,* ipo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naishauri Serikali kwamba lazima tulione hili, Msimbati pale Mtwara imetupa funzo jinsi gani bahari inaweza ikachukua sehemu kubwa ya ardhi katika muda mfupi. Kwa hiyo, Serikali itoe kipaumbele kama ambavyo ilitoa kipaumbele miaka ya 1980 katika Mikoa ya Dodoma na Shinyanga katika suala zima la upandaji wa miti katika maeneo yale.

Mheshimiwa Spika, pia nataka kuzungumzia suala zima la utalii. Kwa mara nyingine tena wakati Mheshimiwa

Kagasheki ni Waziri na Mheshimiwa Lazaro akiwa Naibu Waziri, *personally* na kwenye *plenary* humu, nikawaomba kwamba jamani Pemba kuna kitu kimoja kikubwa sana ambacho kitatusaidia katika nchi yetu, nawaomba mwende mkaone. Mheshimiwa Lazaro akiwa Waziri nimemwambia tena *personally* kwamba Pemba kuna kitu kikubwa sana, nakuomba uende ukaone. Hadi leo Mheshimiwa Waziri hajafika.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi duniani vyombo vyote vikubwa vya habari kama redio, televisheni na magazeti yanatangaza *under water room* ambayo ipo Pemba Jimbo la Konde la Mheshimiwa Khatib. Ni *under water room* iliyoko pekee katika Bara zima la Afrika. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri leo katika safari zake zote za nje anazokwenda, atakapoulizwa kuhusu *under water room* iliyopo Pemba, atajibu nini wakati hajafika pale? Angeweza kutumia ile kuitangaza tena Tanzania kwa kiasi kikubwa katika sekta hii. Bado, nakuomba Mheshimiwa Lazaro Nyalandu utembelee Jimbo la Konde la Mheshimiwa Khatib ili ukaone *under water room* ili utakapokuwa nje uendelee kuitangaza nchi yetu katika sekta nzima ya utalii ili watalii waje kwa wingi katika nchi yetu tuweze kupata faida kubwa inayotegemewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika suala la zima la utalii, nisizungumzie tu kwamba lazima waje watalii wengi, lakini tunahitaji watalii wale ambao wataleta tija katika nchi yetu. Tulete watalii wa kati na wa kiwango cha juu, siyo watalii hao wanaokuja wakatembee na kula mihogo ya kuchoma humu na kuharibu tu mila na tamaduni zetu. Tunahitaji watali ambao watakuja hapa na wataleta tija na faida katika nchi yetu. Hili naomba tuliangalie vizuri sana na tuweze kuhakikisha kwamba tunapotangaza, tuseme tunataka watalii wa aina gani lakini siyo watalii vishuka tu, lakini hata wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, niendelee hapo hapo katika Sekta ya Utalii, sijui Mheshimiwa Waziri Nyalandu unaliangaliaje suala zima la utaliii wa ndege. Tanzania tuna ndege wengi

ambao duniani kote hakuna. Tuna ndege pia ambao wanapotea katika nchi yetu. Tunasema wale watalii wanaokuja kuangalia ndege, kuna *endangered* halafu kuna ndege ambao hawaonekani.

Je, suala hili Mheshimiwa Waziri umelichukulia katika kiwango gani kuhakikisha kwamba wale ndege ambao wanapotea na wale ambao hawapatikani duniani bali katika maneo yetu, tumeweza kuya-*identify* yale maeneo ambayo yana ndege wale, ili watalii watakapokuja waweze kupelekwa katika maeneo yale na kuona hasa ile faida ambayo inapatikana?

Mheshimiwa Spika, pia kuna wananchi ambao wamejitolea tu katika kukuza mazingira, wanawahifadhi hawa ndege, wanawawekea maeneo maalum na kuyalinda: Je, wananchi kama wale wanapewa kipaumbele gani ambao wanalinda ndege wale kwa faida ya Taifa letu?

Mheshimiwa Spika, kabla kengele ya mwisho haijalia, naomba nimalizie na suala la ardhi. Mwenyezi Mungu ametujaalia ardhi kubwa katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, imani yangu inaniambia kwamba yawezekana kuna ardhi ndani ya Tanzania haijawahi kukanyagwa na unyayo wa mwanadamu, lakini bado tuna tatizo kubwa la migogoro ya ardhi ndani ya nchi yetu. Migogoro hii ya ardhi inakua siku hadi siku.

Mheshimiwa Spika, kuna migogoro ya ardhi, Mheshimiwa Lukuvi nataka unisikilize vizuri sana siyo utikise kichwa. Kuna migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji, baina ya wananchi na wawekezaji, baina ya wananchi na mbuga au sehemu za hifadhi, baina ya wananchi na kwa wananchi wenyewe na baina ya wananchi au watu walio chini au walio ndani ya taasisi yako.

Mheshimiwa Lukuvi una changamoto kubwa katika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofii)*

**SPIKA:** Katika Kamati Teule hayo yote yapo. Taarifa itakuja.

Mheshimiwa Dkt. Kafumu atafuatiwa na Mheshimiwa Mkosamali, halafu Mheshimiwa Grace Kiwelu.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza, naomba niseme mimi ni Mjumbe wa Kamati wa Ardhi, Maliasili na Mazingira na hiyo ndiyo taarifa yetu.

Napenda nisisitize mambo machache kwenye taarifa hiyo. Jambo la kwanza ni suala la hifadhi ya Saadani. Kama Kamati tulivyosema, suala hili ni baya sana kwa sababu Serikali kutoa shamba ndani ya hifadhi, siyo jambo zuri sana, hata kama ni karibu na hifadhi. Shamba lenyewe ni la kulima miwa, na unajua kilimo cha miwa kinapendwa sana na tembo. Kwa hiyo, maana yake tukilima miwa karibu na hiyo hifadhi, tunataka kuwaua tembo hawa, wanapenda sana sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kama taarifa yetu ilivyosema, ni juu ya hifadhi yenyewe kwamba inatunza bioanuai ya kila aina; ya bahari, nchi kavu na majini. Tukiweza kulima miwa pale, maana yake tunaweza tukapeleka kemikali ndani ya bahari na tukaharibu mazalia ya samaki kwenye mikoko, mazalia ya wale kasa wa kijani. Kwa hiyo, siyo jambo zuri sana kujaribu kulima miwa karibu na hiyo hifadhi au ndani ya hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali wasifikirie hata kuleta mabadiliko ya mpaka pale, ni kuacha kabisa huo mradi, tutaharibu mazingira. Dunia hii sasa hivi ni ya mazingira. Dunia yetu kitaalam inazeeka na sisi Wanadamu tumekuja

kuleta *stress* juu ya dunia hii. Sasa tukiendelea kuharibu, tutaharibu kweli kweli! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ningependa kuzungumzia ni uchimbaji wa madini ndani ya hifadhi. Tulipotembelea hifadhi ya Ziwa Manyara, tulikuta uchimbaji wa madini ya vito ndani ya hifadhi ile.

Jambo hili lilitokea wakati nikiwa pale kama Kamishna wa Madini. Kulikuwa na mgogoro pale; Serikali iliamua kupanua hifadhi, ikachukua na maeneo ambayo yalikuwa na leseni za madini na ukawa mgogoro. Mimi niliukuta. Tuliamua miaka ile kwamba leseni hizi zikiisha muda zisihuishwe tena.

Leseni nyingi zilikuwa zinaisha mwezi wa Pili, mwaka 2015 (yaani mwezi huu). Lakini kitu cha kushangaza ni kwamba, tulipoletewa ripoti wakati tumetembelea eneo lile tuliona kuna leseni nyingine imetolewa inayoenda mpaka mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, labda kama ni taarifa tu mbovu, lakini kama ni kweli, Serikali isitishe kabisa leseni hiyo ili tuweze kutunza mazingira, tuweze kuhifadhi wanyama na wachimbaji wakachimbe sehemu nyingine ambazo hazina wanyama au hatuzihifadhi kwa sababu hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ambalo ningependa kusema ni juu ya maji kule Igunga, Tabora, Nzega, Uyui na Sikonge, tuna matatizo kweli ya maji. Tabora ni Mkoa ambao umekaa sehemu ambayo haina ziwa wala chanzo kingine cha maji. Kwa hiyo, tunahitaji sana maji kutoka Ziwa Victoria kama alivyoahidi Waziri wa Maji. *(Makofi)*

Ninakumbuka wakati nachangia nilipokuwa mgeni humu, nilieleza habari za Mkoa wa Tabora, hususan Wilaya ya Igunga kuwa ni kame na Mheshimiwa Waziri aliniandikia ki-*note* akasema, "nimekusikia, nimepata uchungu." Nakumbuka Profesa alisema hivyo na akasema "tutakusaidia."

Mheshimiwa Spika, kati ya mambo ambayo ametusaidia ni kuleta maji katika vijiji sita kwa kuchimba visima virefu. Miradi hii imekamilika isipokuwa vijiji viwili Mkandarasi hajalipwa, tunaomba Serikali imlipe. Pia mradi wa kutoa maji lake *Victoria* upembuzi yakinifu umeishafanyika. Tunaishukuru sana Serikali, nakumbuka kwenye bajeti tuliweka kama Dola 800,000 hivi kwa ajili ya upembuzi yakinifu na umefanyika.

Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Waziri, kitu cha kusikitisha ni kwamba, Mkandarasi huyu kutoka Ethiopia, hajalipwa, anaidai Serikali. Naomba mumlipe ili tuweze kuanza huu mradi. Najua tumepata fedha kutoka Serikali ya India, sasa tusipomlipa huyu na mradi ukakamilika, hatuwezi kuzipata zile fedha za India. Naomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anamaliza hili jambo atupe matumaini sisi watu wa Tabora, huo ni ukombozi wetu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia naipongeza Serikali kwa jambo moja ambalo ililifanya kuhusu huo mradi, imeweza kuhakikisha kwamba tunapata *line* yetu peke yetu watu wa Tabora kutoka Ihelele pale. Mwanzoni mlikuwa mnachukua kutoka kwenye maunganisho ya Shinyanga. Hii ingetusumbua! Nawapongeza na muifanye hii kazi vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ambalo napenda kusema ni juu ya shamba la Utumaini kule Mafia. Kamati ilitembelea kule, kweli tuliona kitu cha ajabu kwamba shamba ambalo liliachwa muda mrefu kabisa na wananchi wakaingia na vijiji vikaanzishwa mle, vikaandikishwa, kuna Shule na Zahanati mle, mwaka jana, 2014 akajitokeza mtu anasema nimenunua shamba hili. Sasa tunamwuliza, wewe umenunuaje? Mkuu wa Wilaya hajui, Halmashauri haifahamu, kila mtu hajui kule? Yeye anasema, mimi nimefanyia Dar es Salaam. Tukawauliza Wizara, ninyi mnauza shamba bila kuwahusisha wadau?

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Kamati tunapendekeza shamba hilo lichukuliwe na Serikali na wananchi wapewe nafasi waweze kujenga na kuishi humo bila kubughudhiwa.

Vinginevyo, mashamba ya namna hii yako mengi na yanawasumbua wanachi wetu badala ya kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naona bado kengele moja, nimalizie kwa kuzungumzia kidogo kuhusu wafugaji. Igunga ni nchi ya ufugaji na wafugaji wanapata taabu sana. Mwaka 2014 tulipata taabu ya wafugaji na wakulima kuuana kwenye eneo la Isakamaliwa, lakini hii inatokana na utekelezaji mbaya wa baadhi ya Viongozi kuchukua maeneo ya kulima ndani ya maeneo ambayo kwa kawaida ni ya kuchungia.

Kwa hiyo, ilitokea baadhi ya Viongozi kule Mkoa wa Tabora, Wilaya ya Igunga na wengine kutoka Dar es Salaam walichukua maeneo ya mashamba ndani ya eneo la Isakamaliwa, wakapeleka wakulima kule. Wale wafugaji wakachukia na wakaanza kufanya fujo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba Serikali tujaribu kuyatenga maeneo haya na kuyapima kwa ajili ya wafugaji. Pia tutenge maeneo ya kilimo, tusichanganye. Tusiende sehemu ambazo *essentially* zilikuwa ni ufugaji, tukatengeneza mashamba. Nachelea kusema, hata Wilaya ya Kiteto inawezekana jambo linalotokea la namna hii, watu wanaenda kuanzisha mashamba ndani ya maeneo ambayo kwa kwaida yalikuwa ni ya ufugaji.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali isimamie hili ili wafugaji wetu hasa hawa ndugu zangu wanaohamahama waweze kupata sehemu za kuchunga.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru, naomba kuunga mkono hoja hii na Serikali itekeleze yale tuliyopendekeza kwenye Kamati. Ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Namwita Mheshimiwa Mkosamali, atafuatiwa na Mheshimiwa Grace Kiwelu na Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, ajiandae.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ili nami niweze kuchangia kwenye Taarifa hizi za Kamati za Ardhi, Maliasili na Mazingira na Kilimo, Mifugo na Maji.

Mheshimiwa Spika, moja ni kwamba sisi ambao hatuongozi Serikali tunawashangaa sana watu wanaoongoza Serikali. Haiwezekani haya mambo ambayo tumeshauri mwaka huu, 2015, mwaka 2014, mwaka 2013, miaka zaidi ya sita iliyopita yanaendelea na migogoro ya ardhi ninyi mmeshindwa, *you have failed compeletely to solve these problems! (Makofi)*

Sasa hivi ukiangalia kila Wilaya, kuna migogoro ya ardhi ambayo inahusisha watu wengi. Tumeangalia hapo Morogoro, watu wanauawa. Kiteto mmekuja, mpaka Rais mwenyewe amekuja, hawezi! *Who are you*? Tuwaeleweje nyie watu kuhusu migogoro ya ardhi? Tunawashauri kwenye bajeti, nini na nini, mmeshindwa! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, pale Kibondo mmeleta *DC* mmoja, amekaa huko Mitaani, hana kazi, baadaye mkamsaidia pale. Amefika, amenyang'anya watu ardhi. Anafuta kijiji, ardhi ya Kijiji. Anahazimisha wananchi wahame kwenye Kijiji, anaitwa Mwamoto. He! Hivi ni sheria gani ya nchi yetu inayomruhusu *DC* anifukuzie wananchi wangu kwa sababu amepata msaada wa u-*DC*? *(Makofi)*

Ukienda kila mahali, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa wanasababisha hii migogoro. Pale Tunduma Afisa Ardhi alisimamishwa na Baraza la Madiwani, baada ya wiki akateuliwa kuwa *DC* wa Arumeru, kwa Mheshimiwa Nassari. Yaani huyu amefukuzwa huku kwa matatizo ya ardhi, ameenda kuwa Mkuu wa Wilaya kwenye Wilaya ambayo ina matatizo ya ardhi. Amefukuzwa na Madiwani, kesho yake ameteuliwa kuwa *DC*. Mnataka tuwaeleweje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ukienda kila Wilaya, Kasulu tumewaambia akina Mheshimiwa Nyarandu, Mheshimiwa Maige na wengine wameenda kule, hawawezi kutatua

matatizo ya Kasulu pale Kagerakandi, hawawezi! Mheshimiwa Mgimwa ameenda, sijui nani, wameshindwa kutatua! Sasa ninyi ni watu gani? Unachoma mafuta, unaenda mpaka kule, lakini matatizo yanaendelea. Tuwaeleweje? Hayo mafuta si bora tungeyatumia kufanya kazi nyingine?

Mheshimiwa Spika, nchi hii ukitaka kupata hati ya kiwanja, ni mgogoro. Unapitia hatua kama nane, tisa, sijui nini! Moja unatakiwa utafute watu uwalipe ili wakupimie ardhi yako. Uwalipe fedha, Shilingi milioni mbili, ngapi, fedha nyingi tu. Wakishamaliza kukupimia, ufuate hatua nyingine, wakuandalie rasimu ya mchoro wa pale walipopima, wachukue miaka kadhaa. Ukitoka hapo ile rasimu ipelekwe kwa Mpima Ardhi wa Mkoa, azunguke nayoooo, akitoka hapo uende kwa Kamishna wa Ardhi. Kote huko unalipa fedha, unahangaika, wanakusumbua miaka na miaka. Ndiyo utaratibu wa kupata hati kwenye nchi hii. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Kamishna akimaliza, unaenda kwa Msajili wa Hati, unazungukaaa, haya hamyajui? Sheria hizi jamani, unazungushwa! Kuna watu wametafuta hati miaka kumi, hapati, nchi hii! Wakati mnafahamu kabisa kwamba ukienda kwenye mabenki huna hati,…! Sasa mna shida gani? Kwanini msibadilishe hiki kitu? Mhesimiwa Lukuvi, umeingia, hebu jiulize, haya mambo ni sahihi kweli?

Mheshimiwa Spika, alipoingia Mheshimiwa Prof. Anna Tibaijuka; kwanza ukipata hiyo hati kwenye nchi hii, hiyo hati ukimuuzia mtu akataka ku-*transfer* ile hati, ukinunua kwa sasa hivi, kama ardhi ni ya Shilingi milioni 100, kodi ni Shilingi milioni 10, ambayo ni asilimia 10, *Capital Gain Tax*. Sasa watu wanachofanya, wana-*forge*. Kwanza wengine hawafanyi *transfer*, kwa hiyo, hampati hata hiyo kodi. Wengine wana-*forge*, mtu anaona mimi nimenunua ardhi Shilingi bilioni moja, nikalipe Shilingi milioni 100! Ni kuandika mkataba wa ku-*forge* ndiyo anafanya *transfer*.

Mheshimiwa Spika, haya ni mambo ambayo ni usumbufu na tuliwashauri mwaka jana, Mheshimiwa Lukuvi

alisimama hapa bado akiwa Chief Whip, nikawashauri kwamba tubadilishe mfumo wa Baraza la Ardhi, mmekaa vile vile!

Mheshimiwa Spika, tumewaambia ni tatizo mtu kutoka Wilaya moja, kilomita 200 kwenda kutatua mgogoro wa Sh. 100,000/= Mkoani. Tukawaambia mrudishe huu mfumo huku. Mkasema aah, tumeliona, ni jambo zuri, tutalifanyia kazi. Miaka inapita tu, miaka inapita! Enhe, sasa kama ndiyo *style* yenu ya uongozi, hata hao wananchi wanaowachagua kwa kweli, nyie mtakuwa ni mabingwa sana wa *propaganda,* kwa sababu wanapata matatizo lakini wako na ninyi. *(Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi hii kodi ya ardhi mwaka 2012 iliongezeka mara nne kwenye ardhi za biashara na makazi. Kwa hiyo, watu kwanza hawaendi kulipa au wanalipa wachache, na hata wale wachache wanalipa wakiwa wanalalamika. Kwa sababu iliongezeka karibu mara nne, tano kulingana na aina ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika mwaka jana tuliwashauri hapa kuhusu mfumo wa vocha na pembejeo. Sisi Kibondo hatujaona pembejeo, sijui imekuwaje! Mmepatwa na tatizo gani? Mlituambia wakati mnahitimisha bajeti hapa, sijui mnadhani tunasahau! Sijui mnakuwaje! Hata Mheshimiwa Waziri Chiza pale jirani yangu na yeye mbolea hamna, mbegu hamna. Mbona wakati mnahitimisha bajeti mlituambia kwamba mtapeleka vocha na pembejeo kwa wakati? Kimetokea nini?

Mheshimiwa Spika, Kibondo sisi hatujapata pembejeo mpaka sasa hivi, tumeshamaliza kupanda na kila kitu. Hatuhitaji hata pembejeo sasa hivi, kwa sababu watu walishamaliza kupanda! Tuambieni nyie Serikali ambao mlituahidi hapa mwaka jana, 2014!

Mheshimiwa Spika, wakati tunatoa maoni haya, tuwe na Kamati ambayo itafuatilia yale maagizo ambayo tunawaagiza ili tusitumie muda wa Bunge kujadili mambo

yale yale kila mwaka. Tumewaagiza moja, mbili, tatu. Mwaka kesho tunaangalia kwanza yale tuliyowaagiza, wametekeleza nini? Kwa sababu hawasikii hawa, wala *they don't work!*

Mheshimiwa Spika, hata hawa Mawaziri, hapa ni kutumalizia tu muda. Mtu yeyote kwenye kazi yoyote ni lazima ujifunze. Sasa mtu anaingia kwenye Wizara siku mbili, umemweka huko. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huyu Rais toka ameingia, ameshabadilisha sijui Mawaziri 200, alianza sijui na 68, huyu ameenda huku, hapa wote mmeshakuwa Mawaziri. Wote! Kama wewe hujawa Waziri, labda hujui kusoma na kuandika, ndiyo sifa zako na nini, mambo madogo madogo. Lakini wote hawa hapa wameshakuwa Mawaziri. Yaani kama umekaa miaka kumi hii ya Mheshimiwa Kikwete hujapata msaada wa kuwa Waziri; na kila anayeingia matatizo ni haya haya! *(Kicheko/Makofi)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mhesimiwa Spika, Mwongozo wa Spika!

**SPIKA:** Mheshimiwa Jenista!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE**): Mheshmiwa Spika, kwa utaratibu wa Kikanuni, Kanuni ya 68 (1) na pia Kanuni ya 64 (g) na (f); wakati mwingine maneno yanayosemwa na Waheshimiwa Wabunge yawe ni yenye staha na uhalisia. Siyo kweli kabisa kwamba hawa Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi toka Mheshimiwa Rais ameshika madaraka nchini eti wote wamekuwa ni Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, unajua maneno mengine yanaudhi, hayana ukweli wala uhalisia wa jambo lenyewe na hasa maneno hayo yanapoingiza madaraka na shughuli

anazozifanya Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu yake kama Kiongozi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, ingetosha tu Mheshimiwa Mbunge ajikite katika hoja ambayo iko mezani, lakini si kuvunja Kanuni ya 64 (g) na (f) kwa kutumia maneno ya kuudhi tu ambayo hayana uhalisia katika utaratibu mzima wa mwenendo wa Serikali na shughuli za Mheshimiwa Rais katika nchi yetu kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako katika haya.

**SPIKA:** Naomba kwanza ukae. Alichofanya Mheshimiwa Mkosamali ni kutia chumvi nyingi kwenye mboga mpaka hailiki. Mpaka hailiki kabisa! Haya Mheshimiwa Mkosamali, una dakika moja. *(Kicheko)*

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Sijui hata ninahii kwa sababu…

**SPIKA:** Endelea na *discussion*, na wewe nitakuzimia sasa hivi!

**MJUMBE FULANI:** Endelea!

**SPIKA:** Nimesema una dakika moja!

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, kwa dakika hiyo moja ni kwamba, kwa muda mfupi kama huu, Mawaziri hawa hawawezi kutatua matatizo yetu. Muda wa miezi sita iliyobaki ni wa kujifunza. Huwezi ukaingia kwenye Wizara ambayo umepewa bado miezi sita ufanye kazi. Utafanya nini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante. Nilisema nitamwita Mheshimiwa Grace Kiwelu, atafuatiwa na Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kusema machache katika hotuba za hizi Kamati mbili zilizowasilisha.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira. Naomba nianze na suala la tozo katika hoteli wanazolala watalii wetu zilizoko katika hifadhi zetu. Suala hili ameliongelea Mheshimiwa Zitto kwa uchungu, lakini tumeliongelea kwenye Kamati yetu mara mbili na tuliishauri Wizara kwamba itoe kwenye gazeti la Serikali tangazo hili ili tozo hii iweze kutozwa.

Mheshimiwa Spika, kinachosikitisha mwaka 2011 wenye mahoteli haya walikimbilia Mahakamani kuzuia tozo hii isitozwe. Mahakama kwa kujali maslahi ya Taifa, mwaka 2014 Septemba tulishinda kesi hii na ilitolewa hukumu kwamba Wizara inayohusika kupitia kwa yeyote anayehusika akiwemo Waziri, watoe tangazo kupitia gazeti la Serikali na ambaye hatafanya hivyo atakuwa amelihujumu Taifa.

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza, mpaka leo tangazo hilo halijatolewa na tulitoa *deadline* tarehe 28 Januari, mpaka leo ninavyozungumza halijafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi hapa Jumamosi, Waziri wa Fedha aliongea kwa uchungu sana kwamba tunatakiwa tuwahamasishe Watanzania waweze kulipa kodi, lakini cha kusikitisha, Mawaziri wenyewe wanakuwa msitari wa kwanza kukwepa, kuchukua hukumu hii ili iweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunachokisikia huko nje ni kwamba Mheshimiwa Waziri wa Maliasili anataka kufanya mazungumzo na wenye mahoteli. Sasa sijui kama kuna ukweli! Ni kwa nini akafanye mazungumzo na wenye mahoteli na huku hukumu ya Mahakama inamruhusu aweze kukusanya tozo hiyo? Ni kwa nini hataki kutoa tangazo hilo? Ana maslahi gani na watu hao wenye mahoteli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina matatizo makubwa sana. Hatuna maji, hospitali zetu hazina dawa, leo tunaona

wananchi wanakimbizwa huku wakidaiwa hela za Maabara, lakini Shilingi bilioni 80 toka kesi hiyo imeanza mwaka 2011 mpaka 2014 ilipomalizika, tumepoteza zaidi ya Shilingi bilioni 80. Kuanzia Septemba, 2014 kila mwezi tunapoteza Shilingi bilioni mbili.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana. Nchi yetu ni masikini, lakini Viongozi mnaopewa dhamana na Rais na Watanzania wa kuongoza Taifa hili mnaendelea kulirudisha nyuma Taifa. Kila siku Watanzania wanalalamika. Leo kulikuwa kuna kipindi *Radio One* wanasema Wabunge tumeacha kujadili shughuli za maendeleo, tunaendelea kulalamika. Sasa kwa mtaji huu, tutaacha kulalamika kweli?

Mheshimiwa Spika, Shilingi bilioni 80 ni bajeti ya Wizara kama Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ni bajeti ya miaka miwili hii, lakini fedha hizi zinaendelea kupotea.

Mheshimiwa Spika, Waziri atakapokuja hapa, tunaomba sana alieleze Taifa ni kwa nini mpaka leo hajachukua jukumu hili la kutangaza ili tuweze kukusanya kodi hiyo? Tunaomba sana.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ninalopenda kuliongelea ambalo limesemwa kwenye taarifa yetu ni suala la migogoro katika mipaka ya mapori ya Akiba. Tulitembelea Wilaya ya Simanjiro na Kiteto kwenye Pori la Akiba la Mkungunero.

Mheshimiwa Spika, hali iliyoko kule ni mbaya sana na niwashukuru Mheshimiwa Lekule Laizer na Mbunge wa Kiteto, walifanya kazi ya ziada. Tulikuta wananchi wamesimama na sime na mapanga na mishale.

Wananchi wamechoka, wanasema wamechoka kuona Tume zinakwenda mara kwa mara lakini hakuna kinachotatuliwa. Mheshimiwa alisimama na kusema kwamba hii siyo Tume bali ni Kamati ya Bunge, na tukawaahidi kwamba tuliyoyaona tutakuja kuyasemea.

Mheshimiwa Spika, kwenye kijiji kilichoko Simanjiro, akina mama wamebakwa, wamepigwa na wanaendelea kupigwa. Tuiombe Wizara ya Maliasili na Wizara ya Ardhi, mnapokwenda kule, tunaomba mshirikishe wananchi kama mnataka migogoro iishe. Lakini kama hamtafanya hivyo, wananchi wataendelea kunyanyasika ndani ya nchi yao na hakuna suluhu yoyote wanayoipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aliongea mama mmoja anaitwa Salome, yeye alisema ni mwanachama mwaminifu wa Chama cha Mapinduzi, ameendelea kukichagua Chama cha Mapinduzi lakini ameendelea kupigwa ndani ya Chama cha Mapinduzi. Akasema mnataka afanye nini? Amekiamini Chama cha Mapinduzi lakini mmeshindwa kuwasaidia. Haya siyo maneno yangu na Mheshimiwa Lekule Laizer ni shahidi. *(Makofi)*

Kwa hiyo tunaomba mwasaidie wananchi hawa. Hii kauli ya kupigwa tu, wanapigwa kweli wananchi huko. Kwa hiyo, naomba sana ndugu zangu, hatupigwi tu sisi wa Upinzani, hata wananchi ambao wanatokana na Chama cha Mapinduzi nao wanapigwa. Kwa hiyo, naomba sana ndugu zangu, hasa Waziri wa Ardhi, nakuomba sana, umeingia kwenye Wizara hii, karibu, lakini migogoro ni mingi sana.

Mheshimiwa Spika, kwenye Kijiji cha Jimbo la Kiteto tulikwenda na Mheshimiwa Mbunge na bahati nzuri ni Mjumbe wa Kamati, kule wananchi wamepigwa bila hatia. Kwanza eneo lililokuwa wanadai kwamba liko kwenye pori la Mkungunero, siyo kweli. Lile eneo lipo kwenye eneo la kijiji, lakini wananchi hao wameendelea kupigwa, wamenyanyaswa na kibaya zaidi wamefunguliwa kesi.

Mheshimiwa Spika, tulipokwenda pia huko tulikutana na hali hiyo hiyo, wananchi wakiwa na jazba kubwa, lakini Mbunge aliweza kuwatuliza. Tulikwenda tukakuta kuna mwananchi mmoja mwanawe alipigwa, amevunjwa mguu na Askari wa Wanyamapori kule. Kule hali ni mbaya na tunavyoongea sasa, Askari wawili wameuawa na wananchi.

Kwa hiyo, msipochukua hatua za haraka wale watumishi na Askari Wanyamapori kule maisha yao yako hatarini, kila mmoja anamvizia mwenziwe. Mwananchi anamvizia Askari na Askari anamvizia mwananchi. Kwa hiyo, naomba sana, suala hili mlitilie maanani na mweze kulifuatilia.

Mheshimiwa Spika, lingine niongelee Shirika la Nyumba la Taifa. Nalipongeza Shirika hili chini ya Mkurugenzi wake Nehemia Mchechu pamoja na wafanyakazi wengine kwa kujenga nyumba na kuweka nchi yetu kwenye mandhari nzuri. Lakini lipo tatizo moja ambalo tuliongea kwenye bajeti iliyopita mwaka 2014 kuhusu *VAT* kwenye nyumba za gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, kama dhamira ya Serikali ni njema ya kuwaondoa wananchi kwenye nyumba za tembe, ni lazima tufikiri mara mbili kwamba ni lazima tuondoe *VAT* kwenye nyumba hizi za gharama nafuu ili wananchi wa kima cha chini waweze kumudu kununua nyumba hizi. Vinginevyo watafaidika wenye fedha, lakini wale wananchi wengi wenye kipato cha chini hawatafaidika na nyumba hizi.

Kwa hiyo namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu wake namwona hapa, hili ni suala la msingi. Kama hatutafanya hivyo, wananchi wa kawaida hawataona umuhimu wa *National Housing.* Tuwasaidie *National Housing* waendelee kujenga nyumba, lakini na Watanzania wa kipato cha chini waweze nao kumiliki nyumba hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee pia suala la mwisho la uchimbaji wa madini kwenye hifadhi zetu. Ameongea vizuri Mheshimiwa Kafumu, tulitembelea hifadhi ya Manyara na tuliona uchimbaji unaoendelea kule. Tunaomba sana Waziri anayeshughulika na Sekta hii ya Madini, kama hatutachukua hatua za haraka na kuzuia zile leseni ambazo zimetolewa nyingine kwa kukiuka taratibu zikafungiwa, hifadhi zetu zinakwenda kumalizika.

Mheshimiwa Spika, mazingira yameharibika, kama tulivyotembelea Hifadhi ya Manyara, tulikuta mashimo

makubwa na Mkuu wa Hifadhi alilalamika akasema maeneo haya wakati wa mvua hasa tembo wanapata madhara makubwa, wakitumbukia kule wakati wa mvua wanafia kwenye maji. Kwa hiyo, naiomba Wizara ya Nishati na Madini wakishirikiana na Wizara ya Maliasili wafuatilie suala hili ili tuweze kunusuru hifadhi zetu.

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho kabisa, niongelee suala la upatikanaji wa maji jiji la Dar es Salaam. Tumegaiwa kitabu hapa kinachoonyesha miradi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilisema baada ya Mheshimiwa Profesa Mwakyusa, atafuatia Mheshimiwa Gekul na baadaye Mheshimiwa Zabein.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Nakiri kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mifugo, Kilimo na Maji. Kwa hiyo, ripoti tuliyoisoma leo asubuhi, nakubaliana nayo kabisa.

Mheshimiwa Spika, katika huduma za jamii ambazo zinamgusa mwananchi moja kwa moja kwa maana ya afya, elimu na maji, huduma za maji ndizo zinazolalamikiwa sana na wananchi. Kama Kamati tumetembelea Wilaya nyingi ili kubaini ukubwa wa tatizo, wiki mbili tu zilizopita tulijigawa katika makundi manne na kwenda katika Kanda nne ili kujiridhisha na ripoti za Serikali lakini vilevile kukutana na wananchi.

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa maji hairidhishi, ni mbaya na hasa vijijini. Katika ripoti zetu tatu za Kamati katika miaka iliyopita, tulileta hapa mbele ya Bunge na hizo ripoti tuliziandika kwa niaba ya Bunge na sisi Kamati

tuligoma kupitisha bajeti ya Bunge. Bunge likagoma na lenyewe na Serikali ikakubali kuongeza pesa. Lakini hizo pesa hazikuonekana, ni bahati mbaya sana kwamba ahadi ya Serikali ilikuwa ni kama funika kombe tu. Kibaya zaidi hela zinapoongezwa, miradi ambayo inanufaika inaorodheshwa na wananchi wanaelezwa. Sasa mwananchi ana matatizo kweli ya maji, akielezwa kwamba watapatiwa maji mwaka huu, inakuwa nderemo, wanafurahi, miradi inaanzishwa, pesa mtiririko wake unakuwa hautabiriki. Hivi sasa Halmashauri nyingi zinadaiwa kwa sababu miradi ilianzishwa lakini pesa hazionekani.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa nane wa kitabu chetu, tumeonyesha pesa ambazo zilipitishwa na Bunge hili ambayo ilikuwa ni Shilingi bilioni 888.8, lakini katika miezi sita ya kwanza ya bajeti, fedha zilizotolewa ni Shilingi bilioni 105.7 ambayo ni asilimia 21 tu na hii inaonyesha hali halisi.

Mheshimiwa Spika, tumetoa mapendekezo yetu ukurasa wa 10, lakini katika ziara yetu huko Singapore, wenzetu tulipowauliza, wanasema, wanapotoa bajeti, inatolewa kwa asilimia mia moja. Kama hawana pesa, basi wanaambia wahusika kwamba pesa tulizonazo ndiyo hizi. Lakini hizo ambazo zinaahidiwa, zote zinatoka.

Mheshimiwa Spika, nataka kuishauri Serikali kwamba isione aibu kama pesa hamna, bora kusema kwamba hatuna kuliko kuorodhesha miradi mingi halafu pesa hazitolewi, tunaonekana kama waongo.

Mheshimiwa Spika, tuna mradi mmoja kule Rungwe unaitwa Mradi wa Masoko ambao ulisainiwa mwaka 2009 na ilikuwa ukamilike Agosti mwaka 2011. Ilikuwa pajengwe matenki manne pamoja na mambo mengine, lakini hadi leo ni tenki moja tu ambalo limefunikwa. Wanufaika ilikuwa wawe 15,300 katika vijiji 15. Sasa huu mradi ulikisiwa kugharimu Shilingi bilioni 4.7 na zimetumika Shilingi bilioni 1.3 ndiyo zilizopatikana. Kama Serikali itaamua kuufufua, nadhani hela itakuwa nyingi zaidi ambapo tungekuwa tumeukamilisha pale awali, mahitaji yangekuwa machache.

Mheshimiwa Spika, sasa wananchi hawatuelewi, wamekosa imani na wamekata tamaa. Mheshimiwa Waziri wa Maji, ni mradi huu wa Maji ambao nilmekuwa nikizungumza nawe karibu mara tano umeniahidi, sasa wananchi wanalia. Imeibuliwa miradi mingi baada ya huu mradi huu na imekamilika, wanashangaa kwamba kwa nini wao hawatimiziwi.

Mheshimiwa Spika, naomba niongee kidogo kuhusu makubaliano ya ushirikiano katika bonde la Mto Nile. Kuna nchi 11 ambazo ni wadau wa hili bonde, baadhi ziko ukanda wa juu, nyingine ukanda wa chini. Hizi za ukanda wa chini, Sudan na Egypt wao hawana maji mengi, wanategemea huo mto tu. Lakini nchi nyingine tisa zilizobaki ikiwemo Tanzania, sisi ndio tunazalisha maji. Tanzania inazalisha asilimia 28 ya maji yote yanayokwenda Lake Victoria ambayo ndiyo chanzo cha *White Nile*.

Mheshimiwa Spika, chimbuko la azimio hili ni kwamba, kuna mkataba wa mwaka 1929 ambao Uingereza kwa upande mmoja na Egypt na Sudan kwa upande mwingine walitiliana saini. Huo mkataba ulikuwa unasema kwamba nchi hizi mbili zitumie asilimia 87 ya maji yote ya Mto Nile. Sasa inajulikana kwamba asilimia 10 ya maji yanapotea kama mvuke, yaani *evaporation*. Kwa hiyo, hii inaacha asilimia tatu tu ya maji ili yatumike na nchi 11.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba hapo nyuma tulipoanzisha mradi wa kuchukua maji kutoka *Lake Victoria* kwenda Kahama kulikuwa na manung'uniko na tunanuniwa sana, lakini tukaendelea. Ndiyo mambo kama haya ambayo nchi hizi nyingine tisa haziridhiki na mgao wa maji ambao siyo sawa.

Mheshimiwa Spika, tarehe 30 Novemba, 1961 siku tisa kabla ya uhuru Mwalimu alitamka kwamba tutakapopata uhuru, hatutarithi mikataba ambayo haina maslahi kwetu. Huu ndiyo mmojawapo; na hii ndiyo inaitwa Nyerere *Doctrine*. Nchi nyingi sana zime-*adopt* hiyo, wanaona ni kinga nzuri

sana. Sasa sisi yametupata. Huu mradi ulisainiwa na Uingereza kwa niaba yetu wakati huo walikuwa Wakoloni wetu na wenzetu kama *Egypt* unaweza tukaelewa hawana mto hata mmoja na wangependa iwe hivyo kwamba maji yote ukitaka kuyatumia uwaombe wao.

Kwa hiyo, baada ya kutoridhika huko, ndiyo kumekuwa na hili Azimio kwamba tuwe na uwiano wa haki katika matumizi ya rasilimali ya Mto Nile. Vile vile tuwe na chombo au *commission* ambayo itakuwa ndiyo inasimamia.

Kwa hiyo, toka mwaka 1997 mazungumzo yamekuwepo, lakini kuanzia mwaka 2003 kumekuwa na vikao vingi sana kwa ngazi ya wataalamu lakini vilevile kwa Mawaziri. Serikali yetu imekuwa ndiyo kinara. Ilikuwa Mwenyekiti wa wataalamu na Mwenyekiti wa Mawaziri kipindi chote hiki.

Mheshimiwa Spika, natambua mchango wa Profesa Mwandosya ambaye alikuwa Waziri wakati huo na alikuwa Mwenyekiti. Kwa hiyo, kumekuwa na haya mazungumzo kwamba nchi ziliridhie ili tuunde *commission* na tupate mgao ambao ni sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vikao vimefanyika, ni nchi mbili tu ya Ethiopia na Rwanda ambazo ndiyo zimeridhia mpaka sasa. Tanzania ilikuwa inategemea kwamba ingekuwa nchi ya kwanza, kwa sababu ndiyo tulikuwa tumeshika bango kwa muda mrefu na nchi nyingine nadhani hazijaridhia kwa sababu wanangojea, wanauliza, Watanzania wanasemaje?

Kwa hiyo, tukumbuke kwamba tulikuwa na Azimio ambalo lililetwa hapa Bungeni lakini likaondolewa dakika ya mwisho. Sisi kama Kamati tulikuwa tumelipitisha, lakini Serikali ika-*withdraw*.

Katika mapendekezo yetu ukiangalia kwenye kitabu chetu, ni kwamba tunaiomba Serikali ilete lile Azimio mapema iwezekanavyo ili tuweze kuridhia kwa sababu manufaa ya kuridhia ni mengi sana katika nyanja zote za kilimo, mazingira na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, ni haya machache ya kuchangia ambayo nilikuwa nayo, nashukuru kwa nafasi uliyonipa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Namwita Mheshimiwa Gekul, atafuatia Mheshimiwa Zabein Mhita.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nitoe mchango wangu kwa taarifa ya Kamati ambazo ziko mbele yetu.

Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, ni mara yangu ya kwanza kuongea katika Bunge hili Tukufu kwa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa najiuliza tu, kwa taarifa hizi ambazo tunazipokea, kwamba hawa wenzetu, Viongozi ambao wanaongoza nchi hii, hivi huwa wanafanya *re-treaty*? Wanakaa wanatafakari jinsi gani ambavyo nchi imefikia katika masuala mbalimbali na jinsi gani ya kuyatatua masuala haya?

Mheshimiwa Spika, nilikuwa najiuliza kama Chama ambacho kinaongoza Serikali, huwa kinakaa kinafanya *re-treaty* ili kuona kama Serikali ambayo wao ndio wameiweka madarakani, inafanya vizuri; na kama haifanyi vizuri, nini wanafanya ili Watanzania wajisikie amani kwa sababu wamekuwa wakiwachagua?

Mheshimiwa Spika, nchi inanuka madeni; kila idara inaidai Serikali, kila Mtanzania anaidai Serikali, wanafunzi wanadai mikopo na hivi tunavyoongea kuna harufu tu kuna migomo kwenye vyuo vikuu huko, wanafunzi hawapewi mikopo. Pia nchi hii imefikia hatua ambapo haijawahi kufika, mimi sijawahi kusikia mpaka umri huu wakulima wakiandamana na wao wanaidaia Serikali.

Mheshimiwa Spika, ninachoona mbele yangu kwa wenzetu ambao wameaminika na Watanzania kuongoza nchi hii, tunaona nchi hii ni *oversize* kwao wameshindwa kuiongoza, kwa sababu haiwezekani, wafanyabiashara hawana amani na nchi hii, wanalalamikia masuala yao hayasikilizwi, wafanyakazi wanalalamikia masuala yao hayasikilizwi, Polisi wanaidai nchi hii hawasikilizwi hakuna kinachokwenda.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kilimo wametuambia, wakulima wa mahindi wanadai zaidi ya bilioni 87 tangu mwaka jana, Serikali kupitia *NFRA* wamechukua mahindi ya wakulima, wamekaa na hayo mahindi wakulima wa Tanzania wakiwemo wa Mkoa wa Manyara, kipindi hiki msimu huu wa kilimo hawajakwenda mashambani, hawajaona pembejeo, lakini Serikali imekaa kimya tu, tunasimama kwenye majukwaa, Vyama vinatoa kauli mbalimbali mahindi ya wakulima yalipwe, hakuna hatua inayochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, ninavyosikia baada ya kelele kuzidi na Bunge linarudi hapa zimetolewa kama bilioni 15 kati ya 87 kuwapoza wale wakulima, wakulima wangu wa Mkoa wa Manyara wanadai zaidi ya bilioni kumi, wamekuwa wao kila siku ni kama wanahudhuria kliniki kwa Mkuu wa Mkoa wanadanganywa njoo wili ijayo, njoo mwezi ujao tangu mwaka jana Mwezi wa Nane Serikali imeweka pamba kwenye masikio hawataki kulipa wakulima.

Mheshimiwa Spika, tuwaelewe vipi viongozi wenzetu? Kwa nini tusiseme hii nchi mmeona ni kubwa sana hamuwezi kuongoza m-*declare* tu muwe waungwana, sijawahi kuona wakulima wakiandamana nchi hii hasa wa mahindi, kwanza

maghala mmeshauza, mahindi yao wanakusanya kwenye viwanja vya mipira huko, wanaweka wananyeshewa, *NFRA* wamechukua hawalipi. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo mlolongo tu wa kuuza yale mahindi wakulima wanavyokwenda kuuza kwanza ni rushwa, nchi imeshindwa kuongoza.

Mheshimiwa Spika, hivi ninavyoongea wakulima wa Mkoa wa Manyara wameshindwa kupeleka watoto wao shule, wameshindwa kulipa kodi za nyumba, wameshindwa kufanya chochote kwa sababu mtu ana magunia zaidi ya 1,000 kauza, anasubiri Serikali inamdanganya msimu wa kilimo unapita, aliyewaambia Manyara tunalima Mwezi wa Tatu ni nani? Sisi tunalima kuanzia Mwezi wa Kumi na Mbili, hamlipi mahindi ya wakulima wa Manyara, hamlipi na wakulima nchi nzima wanalalamika, halafu tunakaa tu hapa tunajadili.

Mheshimiwa Spika, haya mambo yanasikitisha sana na ndiyo maana inafikia hatua tunasema, hivi hawa watu wanafanya kujitafakari kwamba tulikotoka ni wapi na tunaelekea wapi wanakaa wanajiangalia kweli?

Mheshimiwa Spika, niwaombe Watanzania na mara nyingi nimebadilisha *modality* ya kuchangia, niwaombe Watanzania maamuzi yako kwao, haiwezekani nchi hii inanuka madeni kiasi hiki *ATCL* wanadai, sijui wastaafu, sijui wafanyakazi pesa zao hawajui, yaani nchi haieleweki Watanzania tujitafakari, tuchukue hatua, hawa watu tuwapumumzishe tu kwa amani, hatuna sababu ya kugombana nao, wameshindwa na naomba Mheshimiwa Waziri atuambie hawa wakulima anawalipa lini na Bunge Zima tuazimie, hili la wakulima wa mahindi *it's too much* hatuwezi kuendelea tena.

Mheshimiwa Spika, kwanza mwaka huu Mheshimiwa Mkosamali amesema hata pembejeo hatukuona, sisi Babati hatukuziona kabisa, mmeanzisha mfumo mpya kwamba wajiunge kwenye *SACCOS* zao sijui waingie mkataba benki, sijui waende kwa Wakala, wanakimbia na kukimbia yaani mbio wanazopiga ni hizo, sawa na hizo za ardhi ambazo

Mheshimiwa Mkosamali amezisema hapa, yaani sasa hivi wakulima wameingia kwenye riadha hawajui hata hizo pembejeo wanazipata wapi na ndiyo maana wengi hawakupata, hivi ndugu zetu hamjitafakari na hamwoni haya?

Mheshimiwa Spika, kilichonisikitisha zaidi na niombe tu Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira watusaidie, mlikuja Babati, mkaenda Vijiji vya Ayamango, Gedamari, Gijdaboungi mka-*recommend* hapa kuwa kila mwaka zaidi ya miaka minane hivyo vijiji tunazungumza jinsi ambavyo wamedhulumiwa na Hifadhi ya Tarangire. Sasa sikiliza mapendekezo ya Kamati, wanasema ukurasa wa 23, ardhi mbadala ipatikane haraka ili wananchi wa Kijiji cha Hayamango wanaopaswa kuhama wahamie huko.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikilisemea hilo mpaka natajwa kwa haya majina ya Vijiji vitatu. Ndugu zangu Wanakamati mnapofika huko kutembelea mngeuliza na wananchi, ilishashindikana ardhi mbadala na hawa wananchi mwaka jana walilala nje, Mkuu wa Wilaya alikwenda, Mkuu wa Mkoa akaahidi kumwona Rais ili ule mpaka urekebishwe kwa sababu ardhi mbadala kwa Babati haipo tena. Walisema Galapo *Estate,* kule walishajaa watu hawawezi kuwahamisha, sasa miaka nane mtu huruhusiwi kulima, huruhusiwi kufanya chochote halafu tena tunashauri ardhi mbadala itafutwe, wapi?

Mheshimiwa Spika, nchi hii migogoro ya ardhi nimewahi kusema, popote pale unapoishi kuna migogoro ya ardhi, ardhi za wananchi hazipimwi, Serikali mnajitafakari? Maji kwenu ni tatizo, afya tatizo, akinamama wajawazito hawapati matibabu ambayo mmesema ni bure, watoto chini ya miaka mitano hawapati chochote, wanafunzi wamekata tamaa, wafanyabiashara wamekata tamaa, wafanyakazi wamekata tamaa, Jeshi la Polisi mnawakopa, hivi sasa mnafanya nini madarakani?

Mheshimiwa Spika, tukiongea haya mambo ndugu zetu viongozi kaeni chini, Tanzania ni ya kwetu sote mtaongoza leo, lakini Watanzania watawachoka kwa mambo haya…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Waheshimiwa nilisema nitamwita Mheshimiwa Zabein Mhita!

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nichangie hoja zilizo mbele yetu. Naunga mkono Taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira hasa katika kipengele cha migogoro kati uya wananchi na mapori ya akiba, migogoro hii ni mingi na imedumu kwa muda mrefu sana. Sasa kwenye hili naomba nitoe mfano tu, katika Wilaya ya Kondoa kumekuwa na mgogoro wa mpaka kati ya wananchi wa Vijiji 11 na pori la akiba la Mkungunero.

Mheshimiwa Spika, Mgogoro huu umedumu kwa miaka mingi sana baada ya ule mchakato wa kupandishwa hadhi Pori Tengefu kuwa Pori la Akiba kati ya mwaka 1983 hadi mwaka 1996. Madai ya wananchi katika vijiji hivi 11, madai haya ambayo na mimi Mbunge wao nayaunga mkono, kuwa, hawakuhusishwa ipasavyo katika mchakato wa kupandishwa hadhi pori hili na uwekaji wa mipaka ardhini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wenzetu walivyokuja kuweka mipaka waliweka wenyewe lakini hawakuwahusisha wananchi wakati ni muhimu wananchi hawa nao wangehusishwa. Tatizo ni kuwa wananchi waliokuwepo maeneo haya sasa wanatakiwa kuondoka, waende wapi wakati wamekuwa huko kwa miaka yote hiyo?

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa mgogoro huu umedumu kwa miaka mingi sana juhudi mbalimbali

zimechukuliwa hasa na Mbunge wa Jimbo la Kondoa Kaskazini, Zabein Muhaji Muhita katika kuleta suluhisho, lakini suluhisho halikupatikana.

Mheshimiwa Spika, uongozi wa Wilaya pia umechukulia kwa karibu kabisa tatizo hili kutaka litatuliwe tatizo hili bado likawa halijatatuliwa ila naomba niseme, sasa naanza kuona mwanga, mwanga unaanza kuonekana na wananchi wameanza kupata imani.

Naishukuru sana Serikali kwani tarehe 28/1/2015 mpaka tarehe 29/1/2015 Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa; Naibu wa Wizara ya Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Angela Kairuki pamoja na wataalam wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mheshimiwa Chiku Galawa walifika Kondoa na tukashirikiana tukaenda katika maeneo ya pori hili na pia kuwasikiliza wananchi madai yao na kulitembelea pori kuona *beacons* zilivyowekwa.

Mheshimiwa Spika, hili naona ni kama hatua nzuri na wananchi wamepata imani kwa Serikali yao inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi.  Sasa basi naiomba Serikali iharakishe hatua zilizobaki, kwa sababu wametuambia kutakuwa na hatua kadhaa, basi waharakishe hizo hatua ili suluhisho la kudumu lipatikane kwa manufaa ya wananchi wetu ili waweze kuendelea na shughuli za uzalishaji mali kwani mpaka sasa wananchi hawa hawana uhakika wa maisha yao na hawana uhakika wa makazi yao.

Mheshimiwa Spika, nina pendekezo, kwa nini Serikali isikate, isiondoe sehemu ya pori ambako wananchi wamekuwepo kwa muda mrefu sana, kwa mfano, kuna Kijiji cha Kisondoko.  Kijiji hiki kipo hapo kwa miaka mingi, Kijiji hiki kimesajiliwa na kina miundombinu.  Sasa kwa nini Serikali isiamue na kusema hilo eneo waachiwe wananchi, waendelee kukaa humo wafanye shughuli zao? Pia tulivyokuwa kule tulishuhudia hata miundombinu ya maji iko pale wananchi wanachota maji pale.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile lipo pia Pori la Akiba la Swagaswaga, pori hili lilipopandishwa hadhi na kuwa Pori la Akiba mwaka 1988, wananchi waliokuwa wanaishi eneo linaloitwa Simbo walihamishwa tena walihamishwa na gari la Halmashauri kwamba hapa mlipo patakuwa ni Pori la Akiba, sasa tunawaondoeni hapa tunawapeleka sehemu nyingine ambayo siyo pori.

Mheshimiwa Spika, walihamishwa mwaka 1988 Novemba mpaka mwanzoni mwa mwaka 1989, wakapelekwa katika maeneo ya Saruku, Mantembo, Kurubani na Dumi walihamishwa kwa gari la Halmashauri kwamba tunawatoeni hapa tunawapeka nje ambapo patakuwa siyo Pori la Akiba. Sasa wananchi hawa waliohamishwa wakati pori hili limepanda hadhi na kuwa Pori la Akiba wakapelekwa sehemu nyingine nilizozitaja, sasa tena wanatakiwa wahame wanaambiwa kuwa wako ndani ya Pori la Akiba.

Mheshimiwa Spika, unashangaa! Wamehamishwa kuwa muwe hapa sasa, huku hakuna pori, sasa tena wanaambiwa wako ndani ya pori, sasa watu hawa waende wapi? Naiomba Wizara ya Maliasili, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na TAMISEMI wafanye kama walivyofanya katika pori la Mkungunero hebu waende wakaonane na wananchi hawa ambao wamepakana na hili pori la Swagaswaga, wakawasikilize matatizo yao, wananchi hawa wanajua mipaka vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawaomba waende kama walivyofanya katika pori la Mkungunero na wakahakiki ile mipaka ili sasa wananchi waweze kuendelea na shughuli zao za uzalishaji mali kwani wananchi hawa sasa hivi hawana utulivu kabisa kwa kuwa hawa maaskari wanapita mara kwa mara na kuwaambia waache shughuli zao za kilimo na kwamba waondoke, sasa wanakwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri atakapokuwa akichangia tafadhali hebu atupe jibu la ombi ambalo nimelitoa kwamba wananchi hawa katika yale maeneo

ambayo walikuwepo na vijiji ambavyo vimekwishasajiliwa na vina miundombinu hebu waachwe katika hayo maeneo, waondoe kabisa na kusema nyie mnabaki hapa.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena naomba nikushukuru sana sana.

**MICHANGO KWA MAANDISHI KWA HOJA ZA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA NA KAMATI YA ARDHI MALIASILI NA MAZINGIRA**

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mungu.

Mheshimiwa Spika, tunaposema ulinzi na usalama sina hakika kama tunaiona hali inayoikabili nchi yetu kwa sasa, hali ya usalama ni tete kabisa Serikali haijaliona suala la usalama wa ndani wa nchi kama kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, suala la usalama kwa watawala wenye upeo mkubwa ni wa lazima siyo ombi na usalama siyo tu kujaza bunduki na risasi kwenye maghala ya Polisi au mabomu ya moto na machozi ni pamoja na utoaji haki bila upendeleo na rushwa, lakini pamoja na kuangalia shughuli za kufanya kwa raia wake ikiwemo kufungua fursa, kujilimbikizia mali na pengo la walionacho na wasionacho linapoongezeka usalama na amani ya nchi nayo inapungua.

Mheshimiwa Spika, tutakapofikia hatua ya watu wetu kukosa fedha za chakula kwa ajili ya kunusuru familia zao, ipo siku watataka kwa nguvu zote kuchukua kwa walionacho na hapo ndiyo mwanzo wa machafuko na kwa kuwa walionacho hawatakubali kabisa kuporwa kwa kile wanachoamini ni cha kwao hata kama wamekipata kwa halali au haramu.

Mheshimiwa Spika, wakati wa Serikali ya Awamu ya Kwanza inajenga viwanda haikuangalia tu uchumi, lakini pia usalama kwa kuwa watu wengi wanakuwa na shughuli za kufanya. Kujenga Kiwanda cha Nguo Dar es Salaam wakati

Mkoa huo haulimi pamba, haikuwa ni mkakati wa uchumi bali usalama ili kila mtu akiamka aende kazini na hapo kunakuwa na uhakika wa usalama.

Mheshimiwa Spika, leo kuna ujenzi wa mabasi yaendayo kasi katika Mji wa Dar es Salaam, nakubaliana kabisa na Mpango wa Maendeleo, lakini mabasi mtakayoyatoa kwenye mzunguko mnatoa mbadala gani wa maisha ya watu wanaoendesha maisha yao kupitia mabasi hayo ya zamani. Ikumbukwe familia kwa kila daladala moja ni zaidi ya nne: kwanza Dereva; pili Kondakta, tatu Fundi, nne mwenye gari pamoja na muuza vipuri. Kama watu hawa hatutawaandalia kazi mbadala ya magari yao basi ieleweke kabisa huna gereza la kuwaweka na Dar es Salaam inakuwa mashakani kiusalama, ni vizuri mkaliangalia kwa macho angavu.

Mheshimiwa Spika, mbali na niliyosema ni vizuri pia kuangalia hali ya vitendea kazi vya walinda usalama pamoja na maslahi yao, kuna wakati mwingine kazi yao inakuwa katika hali ya kujitoa zaidi kuliko kawaida.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Mawaziri kwa umoja wao wanao wajibu mkubwa wa kuhakikisha kwa kupunguza rushwa, ubadhirifu na dhuluma ikiwemo kutoa fursa mpya kwa wananchi ili watu wengi wapate shughuli za kufanya na kuimarisha usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, hali ya usalama wa raia na mali zao kwenye majanga ya moto; ukuaji wa Miji unakwenda sambamba na *risk,* kwa upangaji miji bado ni holela kwa maeneo mengi. Majanga ya moto yamekuwa mengi sana magari ya zimamoto hayatoshi kuifanya kazi hiyo kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna miradi mingi sana inatekelezwa katika Miji mipya na maeneo haya wamesahau kuweka *fire hydrants,* ni vizuri Baraza la Mawaziri likaweka maelekezo kwa Wizara ya Ardhi na TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Maji ili kuokoa mali za Watanzania na maisha yao.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kuwa yote niliyoyazungumza yatapewa kipaumbele na kufanyiwa kazi.

**MHE. ANNA M. J. MALLAC:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata muda wa kuchangia kwa maandishi taarifa hii ya Kamati ya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Spika, nianze na ulinzi na usalama wa Mipaka. Kumekuwa na wimbi kubwa la njia za panya ambazo zinatumika kupitishia biashara za magendo kama vile vipodozi feki, madawa ya kulevya na wakimbizi wanaovuka kutoka nchi jirani (wahamiaji).

Kamati ya Huduma za Jamii iliwahi kutembelea mipaka ya Kasumulo pia Tunduma mwaka 2012 na kugundua mianya ya panya 13 wanazopita wahalifu hao. Pia kamati iligundua uhaba mkubwa wa Askari wa kulinda mipakani. Nashauri Serikali iongeze Askari wa kutosha katika mipaka ili kuhabiliana na uhalifu wa kupitisha magendo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya Magereza. Magereza mengi nchini ni yale yaliyojengwa miaka ya 50 na mfano ni Magereza ya Mahabusi iliyopo Mpanda Mjini na kadhalika. Vyumba ni vidogo ambavyo vinatosha wafungwa 20-25, lakini wanalala wafungwa 40-45, huko ni kurundikana. Ni hatari kwa afya zao wanaweza kupata magonjwa kama *TB*. Serikali ione umuhimu wa kutanua majengo ya Magereza yaliyojengwa zamani yaendane na wakati tulionao, mabweni yawe makubwa, vyoo vya kisasa, maji yapatikane safi na salama, umeme, uzio kwa usalama wa gereza.

Mheshimiwa Spika, mfano Gereza la Kalilankulukulu Mpanda, Gereza la Kilimo halina uzio wafungwa wanazagaa kama kuli, Serikali haioni hatari kwa uvamizi? Naishauri Serikali iangalie pia usalama wa Magereza yote nchini kuwa na miundombinu imara sana ikiwemo sare za wafungwa ili watambulike popote na pia mablanketi.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa makazi ya Askari. Ni aibu sana Askari kukosa makazi bora ya kuishi, Askari anatakiwa kuishi karibu na Gereza na siyo uraiani, kwanza, kwa heshima yake na pili kwa usalama wa gereza.

Wafungwa wamekuwa wakiripotiwa kutoroka, yote hiyo ni Askari kuishi uraiani mbali na gereza. Serikali ihakikishe Askari wanapatiwa nyumba karibu na mahali pao pa kazi kwa kulinda heshima zao na pia kulinda mali na nyaraka za gereza na wafungwa wao.

Mheshimiwa Spika, malalamiko ya wafungwa na mahabusu. Kumekuwa na tatizo la kucheleweshwa kwa kusomwa kesi za mahabusi katika Mahakama na kuwafanya mahabusu wengine kupoteza maisha na kuacha kesi zao bila kusomwa. Naishauri Serikali ili kuleta haki kwa wote, sheria zifanyiwe marekebisho ili haki itendeke kwa kila anayestahili haki. Upepelezi ufanyike kwa wakati na haraka na siyo kumrundika mtu ndani kwa muda mrefu. Uchunguzi wa kina ufanyike ili kuondoa uonevu kwa wanaobambikiziwa kesi.

Mheshimiwa Spika, pia wajane hasa waathirika wa UKIMWI washughulikiwe mirathi zao ili wasipoteze maisha huku kesi zao zipo Mahakamani. Serikali izingatie hili.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mwenyekiti na Kamati yake kwa taarifa waliyoiwasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Ufinyu wa Bajeti: Inasikitisha sana kuona Wizara nyeti kama hii ambayo inashughulikia Ulinzi na Usalama wa Raia Nchini wanapatiwa bajeti finyu na hata bajeti inayopitishwa hapa Bungeni hawapatiwi kwa muda uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, ningeomba Serikali itoe kipaumbele kwa Wizara nyeti kama hii kupatiwa bajeti iliyopangwa na kwa wakati ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa uhakika na bila kulalamikiwa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, Tatizo la Wahamiaji Haramu: Kuna tatizo kubwa sana la wimbi la wahamiaji haramu na wengine hupitishwa katika mipaka yetu kwenda nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na magereza yetu kukabiliwa na ufinyu wa vyumba vya mahabusu lakini hawa wahamiaji haramu wamekuwa wakiongeza mrundikano mkubwa wa mahabusu hao.

Mheshimiwa Spika, nini suluhisho la tatizo hili? Pengine pangetengwa mahabusu maalumu ya kuwahifadhi mahabusu hao wakati wanasubiri hatima zao ili kupunguza msongamano wa wafungwa na mahabusu.

Mheshimiwa Spika, Msongamano wa Wafungwa na Mahabusu: Tatizo hili ni kubwa sana katika magereza zetu nchini ikiwapo magereza ya Iringa. Nakubaliana kabisa na Kamati kuhusiana wa malalamiko yaliyopo katika magereza yetu kama kesi zao kuchelewa kusikilizwa kutoka na upelelezi kutokamilika mapema, kubambikiziwa kesi, masharti magumu ya dhamana, kesi kuhukumiwa kwa kutumia lugha ya Kiingereza, kitendo cha kutotolewa kwa nakala za hukumu mapema na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, matatizo haya ni ya muda mrefu sana na yapo karibu katika magereza zetu ikiwapo ya Iringa pia. Kwa nini kusiundwe chombo maalumu ili kiweze kushughulikia changamoto hizi ambazo kwa kweli zimeweza hata kusababisha migomo kwa mahabusu kwenda Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, Uhaba wa Vituo vya Polisi: Tatizo hili ni kubwa sana hapa nchini ikiwapo Mkoa wa Iringa. Tatizo hili linawafanya wananchi kutembea muda mrefu kufuata huduma hiyo yanapotokea matatizo.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hayo vipo vituo vilivyojengwa kwa nguvu ya wananchi na vinatakiwa angalau Serikali iunge mkono juhudi hiyo ili kulimaliza viweze kuwasaidia wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuishauri Serikali kuwa ingetoa kipaumbele kwanza kwa vituo vilivyojengwa kwa nguvu ya wananchi ili viweze kwisha kwa wakati na kuwapa moyo hata wananchi wengine wenye kuitakia mema nchi yetu waweze kujitolea zaidi.

Mheshimiwa Spika, Huduma za Zimamoto na Ukoaji: Jeshi hili limekuwa na changamoto mbalimbali za upungufu wa magari ya kuzima moto vifaa vya ukoaji pamoja na magari ya kubeba wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa changamoto hizi kuwepo karibu nchi nzima, lakini Serikali ingeangalia angalau kupeleka magari katika maeneo ambayo yapo nyeti na hatarishi na yanaweza kupata madhara makubwa ya moto endapo moto ukitokea yakapelekwa magari, kama Msitu wa *Sao Hill* Mufindi hakuna gari la Zimamoto na ule Msitu ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu.

Pia Jeshi hili kukosekana kuwa na vifaa vya kazi linaonekana kama linawatoza wananchi bila kuwapatia hduma za uhakika.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mchango wangu katika Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa kipindi cha Februari 2014 hadi Januari 2015 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hali ya Jeshi la Magereza siyo ya kuridhisha kutokana na changamoto nyingi zinazolikabili Jeshi hilo. Bado msongamano ni mkubwa sana ambapo ni hatari kwani maambukizi ya magonjwa huweza kutokea kwa urahisi kama vile magonjwa ya mapafu, ukurutu, UKIMWI na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kesi nyingi kuendeshwa kwa muda mrefu, Mahabusu/ Watuhumiwa wengi husota magerezani kwa miaka mingi jambo ambalo ni uvunjifu wa Haki za msingi za binadamu. Hata hivyo, Serikali inaweza kusimamia haki ili itendeke kwa wakati na hivyo kuondoa usumbufu unaojitokeza Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, wapo pia wanawake wanaonyimwa haki zao za msingi pale wanapojifungulia Magerezani. Watoto husota na mama zao Mahakamani na hukosa haki zao za msingi za kucheza, kusoma na kupata chakula bora kwa afya zao. Napendekeza, wanawake wanaonyonyesha wapewe kifungo cha nje na endapo wapo mahabusu basi wawekwe nje kwa dhamana ili kuwatendea haki watoto wasio na hatia wanaozaliwa Magerezani.

Mheshimiwa Spika, Magereza ya watoto yatupiwe macho kwani yapo ambayo watoto wa kike wamepelekwa gerezani kwa kesi ambazo wengi wanabambikiziwa na walezi au mama wa kambo na kadhalika. Chakula katika Magereza ya watoto hakina ubora kwa watoto ambao kimsingi bado wapo katika hatua ya ukuaji wa miili yao. Magereza hayo yabadilishwe kuwa sehemu ya kutoa elimu kufuatana na umri wao ili wasipoteze haki yao ya msingi ya kupata elimu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa dhaifu katika kupambana na biashara haramu ya dawa za kulevya hali iliyosababisha vijana wengi kuendelea kujiingiza katika uhalifu huo. Hivi karibuni imefahamika kwamba wafungwa wa Kitanzania zaidi ya 130 (mia moja na thelathini) wanatumikia vifungo katika magereza ya Guangzhou, Macau na Hong Kong kutokana na kusafirisha dawa za kulevya. Ni kwa nini Serikali isiingilie kati na kurudisha wafungwa/wahalifu wanaokamatwa nje ya nchi na kuhukumiwa katika nchi zao? Ni kwa nini utaratibu usifanyike kuwarudisha Watanzania waliohukumiwa na kufungwa huko China na katika Magereza mengine ya Macau na kadhalika na kuhukumiwa/kufungwa hapa nchini?

Mheshimiwa Spika, hata hivyo bado Tanzania inaendelea kuwa kichochoro cha wauza dawa za kulevya. Hatuoni mwamko mkubwa wa dhati wa kuwahukumu kisheria wale wote wanaosafirisha dawa za kulevya. Ulinzi uimarishwe mipakani, katika viwanja vya ndege na wakamatwe na kuchukuliwa hatua kali za kisheria wale wote wanaojihusisha na biashara hiyo haramu ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Jiji la Dar-es-Salaam lilipatwa na taharuki kubwa sana ya mtandao wa uhalifu maarufu kama *Panya Road*, kundi lililovamia mitaa mbalimbali na kupora mali na hata kuvuruga amani kutokana na zoezi lao lilivyoendeshwa kwa silaha za jadi yakiwemo mapanga. Ili jambo hilo lisijirudie Dar-es-Salaam na katika miji mingine ya nchi yetu, Serikali inajiwekea mkakati gani endelevu wa kuhakikisha vijana wetu hawazururi mitaani na kukaa kijiweni bila kazi?

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuongelea kuhusu usalama wa raia na mali zao. Suala hili ni muhimu sana katika nchi. Bado wimbi la mauaji ya vikongwe na *Albino* linaendelea katika baadhi ya Mikoa kwa imani za kishirikiana. Maoni yangu ni kwamba Serikali ihakikishe kwa njia moja au nyingine inawachukulia hatua kali za kisheria watakaobainika na vitendo hivyo vya kuua vikongwe na *Albino*.

Mheshimiwa Spika, napenda kuongelea kuhusu uhamiaji. Nakubaliana na ushauri wa Kamati wa kuwarejesha makwao wahamiaji haramu kwa kutumia njia ya miguu kama walivyokuja kwani kuwarundika Magerezani ni mzigo kwa Serikali na pili Magereza yetu yana mrundikano mkubwa wa wafungwa na mahabusu.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali ione sasa kuna umuhimu mkubwa wa kuangalia hali ya Magereza zetu hapa

nchini. Je, kuna haja ya kuwa na mrundikano huo wa wafungwa? Kwa nini kwa wale wafungwa wenye makosa madogo kusiwekwe adhabu mbadala?

Mheshimiwa Spika, matatizo ya Magereza. Tatizo la msongamano wa wafungwa na mahabusu ni kubwa katika Magereza zetu. Je, suala la afya pia tumeliangalia kwani kuna magonjwa na kuna wafungwa wana maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI? Je, Kamati imeangalia hali za wafungwa hao? Mfungwa ni binadamu ambaye anastahili kupatiwa haki zake kwa mujibu wa haki za binadamu. Kwa mfano, mgonjwa wa UKIMWI lazima apate dawa lishe, vipimo kila baada ya miezi sita yaani vipimo vya *CD4*. Ushauri wangu naiomba Serikali itafute adhabu mbadala kwa wafungwa wanaoishi na ugonjwa huu wa UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, kuhusu chakula cha aina moja ugali na maharage, kwa kuwa kuna mashamba ya Magereza tena wanalima vitu vingi sana, kwa nini wasibadilishiwe aina ya vyakula? Juhudi zifanyike tu kwa kuongeza mashamba ya Magereza ili kuondokana na tatizo hili na pia Serikali iongeze fedha katika bajeti ili kuondokana na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa nyumba za Askari. Nakubaliana na Kamati kwamba nyumba za Askari Magereza ni chache na chakavu sana. Jitihada zifanyike ili Askari Magereza wajengewe nyumba au zikarabatiwe ili kuepuka kukaa nje ya kambi zao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vitambulisho vya Taifa, kwa kuwa zoezi hili haliendi kwa kasi sababu ni zana za kusajili walengwa (*mobile enrolment unit*) bado hazijanunuliwa pamoja na bajeti ya kununulia zana hizo kuidhinishwa na Bunge. Serikali isiwe inasuasua katika kutekeleza masuala muhimu ya Taifa kama haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya

leo na pia kuwapongeza wewe na Kamati yako kwa kazi nzuri na ngumu mnayoifanya ya kuishauri Serikali na kutusaidia kusukuma kupata ufumbuzi wa matatizo yaliyoko katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba Kamati yako ije Babati Vijijini kujionea na kutusaidia katika migogoro mbalimbali inayohusu ardhi, maliasili na mazingira. Matatizo haya yako nchini kote ila kwa Babati imekithiri. Babati inaweza kuwa eneo la mfano wa kujifunza migogoro mbalimbali.

Naomba mwendelee kuishauri Serikali na kusaidia kuweka mfumo bora wa malipo ya fidia au kifuta machozi na kifuta jasho kwa wananchi waliopoteza maisha kutokana na wanyamapori na mazao yao kuharibiwa na wanyamapori. Halmashauri ya Babati haijapokea fidia au kifuta jasho wala kifuta machozi leo ni mwaka wa nne, kila siku majibu hayaridhishi. Matokeo yake ni wananchi kutoa hasira kwa wanyamapori, mfano simba saba mwaka huu. Pia tunaomba Kamati yako isaidie wananchi wa Vijiji vya Ayamango, Gedemas na Gidejabong kupata haki yao ya fidia stahiki na ardhi mbadala. Eneo lao limechukuliwa na hifadhi ya Tarangire kutokana na uzembe wa Uongozi wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo mbadala tumependekeza shamba la *Galapo Estate* na shamba la Rivacu Dareda. Haya maeneo yanaweza kutosheleza na Serikali iangalie fidia stahiki. Pia tunaomba Kamati yako isaidie Halmashauri ya Wilaya ya Babati kupata malipo halali ya kisheria kutokana na hoteli na *campsite* za kikatili ndani ya hifadhi za Tarangire na Manyara ambao hawalipi Halmashauri yetu. Eneo kubwa la Tarangire na Manyara lipo ndani la eneo la Halmashauri ya Babati.

Pia tunaomba Serikali kwa kupitia *TANAPA* ifungue mapema geti la Mawire ili utalii uweze kukua kupitia eneo hilo muhimu, itafanya eneo hilo na Wilaya ya Babati kufaidi utalii tofauti na sasa ambapo Mkoa wa Arusha ndiyo unafaidi.

Itaondoa mgogoro sababu eneo kubwa watabadilisha matumizi kutoka kilimo na kufanya shughuli za utalii, hoteli, *campsites*, maeneo ya masoko ya utalii na utamaduni.

Pia tunaomba Serikali iangalie upya suala la tozo ya ardhi *(Land Rent)* kutokana na kazi ya kilimo na mifugo, bei ya tozo ya ardhi iwe *minimal* kwa ajili ya kukuza sekta hiyo isiwe sababu kupandisha kwa ajili ya watu kuhodhi ardhi. Kuna Sheria ya Ardhi kutatua hilo, ya kutoendeleza mashamba na *ranches*.

Pia tunaomba Serikali ilete haraka Muswada wa Sheria ya Kulinda Ardhi za Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Leo hii maeneo mengi ya kilimo, mifugo na uvuvi yanabadilishwa kuwa maeneo ya makazi, viwanda na matumizi mengine.

Pia tunaomba Serikali itoe majibu haraka kuhusu migogoro ya ardhi baina ya vijiji na wananchi, Vijiji na wawekezaji vijijini na hifadhi za Taifa. Pia tunaomba wahanga wa *Operation* Tokomeza waweze kulipwa fidia stahiki mapema.

Mheshimiwa Spika, pia tunaomba Serikali iangalie mfumo wa kutoa vibali vya shughuli nyingine mfano, uchimbaji madini, kilimo, ufugaji katika maeneo ya vyanzo vya maji na maeneo ya vidakia maji*(catchment area)*. Bonde la ufa lenye eneo pekee katika bonde la ufa la kati lenye mito ya kutiririsha maji, uharibifu ni mkubwa.

Pia Serikali iangalie namna ya kutoa taarifa iliyo sahihi kuhusu nishati mbadala ya kupikia. Misitu ya asili na ya kupanda inakatwa na hakuna hata dalili ya kupanda. Hakuna! Tutafika mahali hatutakuwa na nishati hiyo. Suala la mazingira halipewi umuhimu wake.

Mheshimiwa Spika, tunashauri pamoja na kazi nzuri na kubwa mnayofanya, Serikali iangalie namna ya kushirikiana zaidi na Kamati yenu na kupokea ushauri. Kwa sehemu kubwa mnaweza kusaidia maeneo mengi.

Mheshimiwa Spika, tunaishauri Serikali iangalie namna ya kukopa vifaa vya kisasa vya upimaji ardhi ili ardhi ya wananchi ipimwe na wapatiwe hatimiliki.

Naomba pia nishauri Serikali iangalie eneo la *WMA'S* na Vitalu vya Utalii wa kuwinda. Babati tuna kitalu ambacho mwekezaji amebadilisha eneo la uwindaji wa kitalii na kuwa utalii wa picha na kuwa kero kwa wananchi kwa sababu sasa hawaingii katika eneo hilo kupata huduma muhimu mfano, kuni, dawa asili, kuchunga mifugo kwa kipindi maalum, majani ya kuezekea nyumba na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Spika,, kwa kweli suala la migogoro ya ardhi katika nchi yetu ni sugu sasa.

Katika Mkoa wa Tanga tuna tatizo kubwa la mashamba ya mkonge ambalo mengi ya mashamba hayo sasa ni mapori makubwa na ni muda mrefu sasa takriban miaka 30, 40 sasa katika Wilaya ya Pangani tumeathiriwa sana na mashamba hayo. Kuna vijiji havina kabisa maeneo ya kulima, kama yapo, ni Kisiwani napo ni Kijiji cha Ubangaa, kuna shamba kubwa la Kilimangwidu ambalo ni pori kubwa la hekta 3,000, ni hatari sana. Kuna mpaka wanyama wakali! Vijiji vingine ni Langoni, Ushongo, Mwera, Tungamaa, Mikinguni na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, nakuomba Kamati yako ing'ang'anie Wizara kutatua migogoro ya ardhi na wananchi wapatiwe maeneo ya kulima.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maliasili, kuwe na mipaka inayotambulika, kati ya mbuga na vijji vya jirani na wananchi wapewe elimu ili wananchi wasipigwe hovyo na Maafisa Wanyamapori. Wilaya ya Pangani, kuna mbuga ya Saadani ambayo iko karibu na Kata ya Mkwaja na Mkaramo. Wananchi wanateswa sana hata wanawake wanabakwa, kwa kweli sio halali kabisa.

Pia wanyama kama tembo wanaharibu mazao ya wananchi, minazi inaangushwa na wameambiwa kuwa watalipwa fidia. Naomba wananchi wanaoathirika na hizi mbuga walipwe fidia.

Mheshimiwa Spika, Operesheni Tokomeza haikuwaathiri tu Askari, hata wananchi wetu wameathirika, kwani wamenyang'anywa magobore yao ambayo ni silaha wanazozitegemea sana; nazungumzia kwa Pangani, wananchi wengi wamechukuliwa magobore yao na wana vibali halali na wanalipia. Mpaka leo hawajui kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Mwenyekiti akienda kwenye majumuisho, ajaribu kuligusia suala hili.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupewa nafasi. Napenda kumpongeza *CAG* mpya na ninampongeza kwa sababu naamini kazi yake itakuwa nzuri kama ya *CAG* aliyepita. Nasema nzuri kwa sababu ripoti nzuri za *CAG* ndiyo zinatusaidia sana Wabunge kuisimamia Serikali na pia nampongeza Mkurugenzi wa *NHC*.

Mheshimiwa Spika, kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu, naomba tuisimamie Serikali, wakati mwingine katika utekelezaji wa kazi zake Serikali inaburunda. Ninaomba tusimame imara na kamwe tusitetee maovu, tutaonekana wa hovyo kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ardhi ingekuwa imeweka mpango mzuri wa matumizi ya ardhi matatizo tunayoyaona ya vyanzo vya maji kuharibiwa, mazingira kuharibiwa, hifadhi za Taifa kuvamiwa, mapigano ya wafugaji na wakulima na kadhalika yasingekuwepo. Nakubali uongozi ulioteuliwa hivi karibuni hauwezi kutekeleza kwa muda uliobaki katika Bunge hili la Kumi,  lakini Serikali ipo.

Mheshimiwa Spika, hebu fikiria Tanzania ni namba tatu kwa wingi wa ng'ombe katika Bara la Afrika. Fikiria ng'ombe wanatoka Mwanza na Shinyanga mpaka Lindi na Mtwara.

Siku hizi mifugo kutoka Shinyanga wanaingizwa mpaka Bonge la Malagarasi – Kigoma, siku hizi mifugo inaingia katika Hifadhi ya Selous na askari wanyamapori wanauawa na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, kungekuwepo na *good land use plan* madhara haya yangeepukika. Wafugaji wapewe maeneo yao na iwekwe mipaka. Pale ambapo mfugaji eneo halitoshi auze mifugo na iwe sambamba na uanzishaji wa viwanda vya nyama.

Mheshimiwa Spika, *TIC* nakumbuka iliandaa *land bank*. *TIC* hii itafute wawekezaji wawekeze katika viwanda vya nyama. Wawekezaji wafundishe wafugaji ufugaji bora. Kiwanda kimoja Shinyanga kitachukua mifugo yote ya Tabora, Mwanza na Mara na kingine kikiwa Dodoma kitachukua mifugo yote ya Arusha, Manyara na Morogoro. Hii itawapa wafugaji hamasa ya kupata fedha na hivyo kuzungusha mifugo nchi nzima na hatimaye ugomvi wa wakulima na wafugaji utakwisha.

Mheshimiwa Spika, yako masuala ya kurekebisha ardhi (ku-*revoke)*

Mheshimiwa Spika, nasikitika kusikia kuwa wanafunzi hawaendi shule huko Serengeti kisa wameanza biashara ya kwenda kuwinda wanyamapori usiku katika hifadhi hiyo. Tunatengeneza  jamii ya namna gani, hii itakuwa jamii ya majangili?

Ninampongeza Mkurugenzi wa *TANAPA* kwa kazi nzuri ya kulinda hifadhi zetu. Namuomba kwa hili la askari wa wanyamapori kuuawa, kuwindwa na wafugaji na watoto kuacha shule kwenda kufanya ujangili alivalie njuga kwa sababu ni mambo yasiyokubalika.

Mheshimiwa Spika, ukataji miti kwa ajili ya mkaa umezidi na umefika kiwango cha juu. Jamii inayoishi *along* barabara ya Morogoro, barabara ya Dar es Salaam - Arusha,

katika kila Halmashauri ya Wilaya kuna Maafisa Misitu na Maliasili na hutaamini kuna Idara ya Maliasili katika Halmashauri za Wilaya biashara kuu ni kuchoma mkaa.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili mko wapi? Watu wa maeneo hayo wanaweza kulima. Ni maeneo yenye mvua za kutosha, wananchi wa maeneo hayo walime. Lakini lazima maofisa misitu wafanye kazi. Tukiendelea na ukataji miti wa kiasi hicho, mabadiliko ya tabia nchi yatafanya nchi hii iwe jangwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Hifadhi ya Mkomazi Wilayani Same, hifadhi hii ndiyo kwanza Serikali inajaribu kuweka idadi ya kutosha ya wanyama. Ikiwa na wanyama wa kutosha hususan faru weusi tutategemea watalii wengi hasa wale watakaotumia kiwanja cha ndege kinachojengwa karibu na mji mdogo wetu wa Holili. Kwa hiyo kuna uhakika wa kupata Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iache kutoza kodi kwa wafadhili wanaojitolea kutupa wanyama hao. Bunge limepiga kelele kuhusu misamaha ya kodi. Badala ya kodi katika taasisi nyingine za binafsi na makampuni, basi misamaha itolewe katika hili kwa sababu kuna tija kubwa kwa Serikali.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninapenda nichukue fursa hii kupongeza hoja na maoni yalivyotolewa na Kamati hii ya Ardhi, Maliasili na Mazingira pamoja na Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji. Hakika mapendekezo yao ni muhimu katika kuinua pato na uchumi wa nchi hii, ambayo idadi kubwa ya Wananchi wake ni Wakulima na Wafugaji wa kati walioko vijijini.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nielekeze mchango wangu katika baadhi ya maeneo ambayo ni muhimu sana. Aidha, Serikali iyaone kwa hatua za haraka sana. Mfano, kuna suala la Wananchi kulipwa fidia hususan wale walioathirika na Operesheni Tokomeza. Wananchi hawa baada ya kutoa malalamiko yao ya kweli, wamezidi kuzungushwa pasipo jibu

la lini watalipwa fidia ya mifugo yao, lakini hatuoni hatua zinazochukuliwa tofauti na Mawaziri kujiuzulu. Ninaomba Serikali itoe jibu sahihi sasa ni lini watalipwa maana hata Tume ya Majaji bado nayo haijatoa ufumbuzi wa nini kifanyike. Sasa ni muda mwafaka wa kutoa jibu la uhakika kwa hawa Wafugaji walioathirika na operesheni.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi baina ya vijiji na hifadhi, wafugaji na wakulima, wawekezaji na wanavijiji na kadhalika, ipo katika kila kona ya nchi yetu. Leo hii mipaka haiwekwi wazi na matokeo yake ni migogoro. Ni wazi kuwa idadi ya watu inaongezeka na ardhi ipo palepale. Tukumbuke suala la idadi kwa mujibu wa Sensa iliyofanyika mwaka 2012 na jana Wataalam wameliongelea kwa upana mkubwa sana; ni wakati sasa wa kuliona suala hili katika wigo mpana kama suala mtambuka kwa maana ya Wizara zinazohusika mfano; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana suala la migogoro hii ya mipaka ya ardhi lishughulikiwe haraka sana ili kuepusha umwagaji wa damu usio wa lazima. Kutokana na mipaka kutoeleweka kwa wananchi, inafikia mahala Askari wa Wanyamapori hutoka Ushirombo/Bukombe na kuingia Pori la Hifadhi la Nyantakala. Aidha, hata wale wanaotoka Pori la Kigosi nao wanafanya uhalifu kwa kuingia vijijini kukusanya mifugo na kuiingiza ndani ya hifadhi na kuwatoza fedha wananchi pasipo kutoa risiti. Hali hii haikubaliki na haivumiliki.

Mheshimiwa Spika, tatizo la mipaka ya Nyantimba, Kata ya Nyabusozi lipewe ufumbuzi wa haraka ili wapate haki zao za msingi, kwani sasa haieleweki wapo Wilaya ya Chato au Biharamulo kwa *GN* iliyopo sasa.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kutumia nafasi hii ya awali kabisa kukupongeza wewe binafsi kwa kuandaa mpango mzuri wa kuwasilisha Taarifa za Mwaka za Kamati za Bunge.

Mheshimiwa Spika, vilevile ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri; Mheshimiwa Lazaro Nyalandu - Waziri wa Maliasili na Utalii, Naibu Waziri - Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, Waziri wa Kilimo na Mifugo, Makatibu Wakuu wote wa Wizara hizi mbili na Watendaji wote walioshiriki kutekeleza Ilani ya Uchaguzi 2014/2015.

Vilevile ninawapongeza Wenyeviti wote waliowasilisha Taarifa hizi mbili za Kamati kwa kazi kubwa walizofanya kusimamia Serikali kutekeleza vyema Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ninaungana na Kamati kuhimiza Serikali kuwatafutia wananchi nishati mbadala ili kupunguza kasi ya ukataji miti hovyo kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.

Ninatoa pongezi kwa kazi nzuri wanayofanya Askari wa Wanyama Pori Manyoni, kwa kuwakamata Majangili wanaovamia vitalu vya uwindaji kwenye Vijiji vya Kata ya Rungwa na kukamata silaha zao na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Kituo cha Askari wa Wanayapori cha Manyoni kipatiwe gari la uhakika kupambana na ujangili ipasavyo na vilevile askari wa Wanyama Pori waongezwe.

Mheshimiwa Spika, bado azma ya Serikali ya kuvuna miti ya mikaratusi inayokausha vyanzo vya maji haijatekelezwa. Ninaomba kuungana na Kamati kuhimiza Serikali na kuhimiza Halmashauri zenye miti ya mikaratusi kukatwa na kupandwa miti mingine ya kuzuia ukame usitokee.

Niungana na Kamati kwamba, utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Vijiji Kumi kwa kila Wilaya wa *World Bank* ufanyike. Hivyo, ni vyema Serikali kukaa upya na wafadhili hawa kuwaeleza hali halisi inayotokea kwenye Mradi huu wa Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. GOODLUCK J. OLE MEDEYE:** Mheshimiwa Spika, Uongozi wa Hifadhi ya Msitu wa Meru Usa umekuwa ukinyanyasa Wananchi wanaoishi jirani na msitu huo kwa kuwatoza shilingi 250,000 kwa kila ng'ombe atakayeingia kwenye eneo la msitu. Kiasi hicho cha tozo ni kikubwa sana kwani ni karibu sawa na bei ya kuuzia ng'ombe. Hatua hiyo ni sawa na kutaifisha ng'ombe hao.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Wizara itoe maelekezo kwa Uongozi wa Hifadhi ya Msitu kuimarisha mahusiano na majirani zao. Vile vile uwekwe mpaka mpana *(Buffer)* kiasi cha mita 60 ili kuondoa hali ya sasa ya ng'ombe kukamatwa wanapopita jirani na Hifadhi hiyo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema kuanzia asubuhi, wanaaoomba kuchangia ni wengi na bahati mbaya wanapochangia wanaongea kama hawako kwenye Bajeti, wanazungumza habari za kwao tu na wala siyo mazungumzo ya Kamati. Kwa hiyo, tumeamua kugawa nakala za mapendekezo ya Kamati mbili tofauti mtagawiwa sasa hivi, kila mtu awe na kopi mbili. Haya ndiyo mapendekezo yale mengine mliyokuwa mnayasema ni ya kwenu, siyo sehemu ya mapendekezo, sasa msije mkawadai, mkasema tulipiga kelele sana, hapana mapendekezo ya Kamati ndiyo haya hapa. Kwa hiyo, mfahamu hivyo na hiki siyo kikao cha Bajeti.

Mawaziri nitawapa wazungumze lakini na wenyewe ni dakika kumi tu. Kwa hiyo, sasa nianze na Waziri wa Ardhi atafuatiwa na Waziri wa Utalii, Waziri wa Mifugo, Waziri wa Kilimo, Waziri wa Maji na mwisho atamaliza Waziri wa Mazingira. Mheshimiwa Waziri wa Ardhi!

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa muda ulionipa na napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniamini kwa kunipa hii Wizara ili nimsaidie na naahidi kwamba sitamwangusha.

Mheshimiwa Spika, nataka kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kwamba, najua yaliyozungumzwa ni mengi lakini kama kawaida tumeyanukuu na yaliyo mengi tutayafanyia kazi na tutaendelea kukutana na Kamati ili kuhakikisha yote yanakuwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi niseme machache kwanza nianze na shamba la Tumaini la Mafia ambalo limezungumzwa na Kamati kwa nguvu sana na Wajumbe wamezungumza, nataka nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Shah kwamba, Serikali imeshaanza kuchukua hatua na hatua yenyewe ni kwamba, tumeshatoa *notice* hatua za kulichukua hilo shamba lenyewe ukiacha zile hekari 1,000 zilizokuwa zimechukuliwa mwanzo lakini sasa tunataka kuchukua shamba lote.

Mheshimiwa Spika, tumeshatuma kwa anayejifanya anamiliki hilo shamba tarehe 28 mwezi huu *notice* ya kulichukua hilo shamba ambalo tunataka kusubiri kwa muda wa siku 90, zikiisha hatua zinazofuata zitaendelea. Kwa hiyo, nataka Mheshimiwa Shah na wananchi wa Mafia mjue kwamba Serikali imeshaanza kuchukua hatua. Lengo letu ni kuchukua shamba lote ili kama ikiwezekana sehemu kubwa ya shamba lile wapewe wananchi na sehemu ndogo tuweke akiba kwa ajili ya uwekezaji wa Mafia.

Mheshimiwa Spika, kwa hilo tunafanya na siyo hilo tu, tumeamua kama Wizara sasa kwenda kwa kasi zaidi kutwaa mashamba yote makubwa ambayo hajaendelezwa. Mashamba haya najua yako sehemu mbalimbali Wabunge wengi mmesema yako Tanga, yako Manyara, yako Arusha kule Ngorongoro na Morogoro. Tumeshaanza na nitalifuatilia kwa nguvu zangu zote kuhakikisha kwamba, mashamba haya ambayo hayaendelezwi ushauri wa Kamati unatekelezwa kwamba yanafutwa na wananchi wanachukua sehemu yao na sehemu nyingine inawekwa kwenye akiba ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, kwa hilo nataka kuwaomba Wajumbe mliozungumza hasa wa Kamati kwamba Serikali

inachukua lakini pia niwaombe na wananchi vile vile kwamba basi Serikali wakati inachukua hatua hizo msifanye uvamizi, kwa sababu mkiyavamia sana *then* hata tukija wakati wa upimaji na kuwagawia itakuwa sasa wale walioanza ndiyo wanapata haki wakati kuna wengine wana haki zaidi na pengine wana haki sawa na wenzao. Kwa hiyo, Serikali inachukua hatua.

Mheshimiwa Spika, la pili, nataka kusema lingine juu ya wawekezaji wanaoomba ardhi, tumeamua kama Wizara sasa wawekezaji wanaoomba ardhi lazima wawe na *Business Plan*. Tumegundua kwamba wawekezaji wengine wanapewa ardhi, wanakopa, wanachukua zile fedha wanakwenda kufanyia shughuli nyingine, ardhi waliyokopea haiendelezwi.

Mheshimiwa Spika, kwa hilo tutalisimamia ili kuhakikisha kwamba linakuwa na katika marekebisho ya Sheria ambayo tunaleta, tunataka Kamishna wa Ardhi awe sehemu ya watu muhimu watakaoidhinisha *mortgage* ya yale mashamba katika mabenki, maana sasa hivi mortgage zinafanyika kwa kutumia hati lakini Kamishna wa Ardhi hajui.

Mheshimiwa Spika, lingine nataka kusema kidogo juu ya maelezo ya Mheshimiwa Zitto kwamba kuna eneo kubwa sana la viwanja ambavyo havijulikani, kwa hiyo tunakosa kodi. Nataka nikupe *data* kwamba mpaka leo ni viwanja 439,789 ndivyo vilivyoingizwa kwenye mfumo wa kodi. Kwa hiyo, kama Wizara hivi ndivyo tunavyovifamu, sio 22,000 kama ulivyosema, isipokuwa ni 489,000.

Mheshimiwa Spika, vile vile nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wa Sumbawanga. Mheshimiwa Malocha na Mheshimiwa Aeshi, juu ya mgogoro wa shamba la Malonje. Serikali tunalishughulikia na nimekuta kuna maelekezo pale tunafuatilia kwa kasi sana ili kuhakikisha kwamba maelekezo yote yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais yanatekelezwa kuhusiana na shamba lile. Kwa hiyo, nimepokea, lakini tutawashirikisha na kuwaambia hatua ambazo tunataka kuzichukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Medeye vile vile ameomba twende Arusha, tutakuja Arusha kukaa na wenzetu Mikoani ili kuhakikisha mambo yote yale tunazungumza na viongozi wa Mkoa ili kuhakikisha ile migogoro ya Monduli na Wilaya nyingine za Arumeru tunaitatua.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo ambalo alizungumza Mheshimiwa Lugola, lakini nashukuru Mheshimiwa Zitto amemjibu juu ya Osterbay villa. Sio mimi niliyesababisha mgogoro, mgogoro ule ulikuwepo siku nyingi, lakini angenishukuru kama angemsikiliza Mheshimiwa Rajabu na Mheshimiwa Waziri juzi alitolea ufafanuzi. Katika siku kumi hivi nimeshamaliza huu mgogoro na hivi leo kama unaweza kupiga simu kawaulize, wameshaenda kukabidhiwa *apartment* zao.

Mheshimiwa Spika, kiini cha mgogoro Mheshimiwa Lugola hakujua. Waliweka mkataba wa miaka 99, lakini nimeona haiwezekani kuwa mgogoro na wakawekeana maktaba wa miaka 99 wa ubia wa ile ardhi ya Osterbay, kwa sababu hati yangu ile imebakiza umri wa miaka 47. Kwa hiyo, walichokubali ni kwamba sasa mkataba waingie wa miaka 47 sio 99 kama walivyofanya mwanzo. Sasa mimi ndio nashirikiana naye au naisaidia Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Lugola maelezo ni yale aliyosema Mheshimiwa wa TAMISEMI na nitaendelea kumpa taarifa. Kesho sasa wanakwenda kusaini baada ya kuridhika kwamba zile *apartment* zao zipo wazi. Mheshimiwa Zitto nakushukuru sana kwa kulielewa hilo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu tutahakikisha tunapambana sana na watu wote, wakubwa na wadogo, matajiri na watumishi wa Serikali na matapeli wote, wanaoendesha vitendo vya dhuluma na kunyanganya viwanja, majengo na ardhi za wanyonge. Najua Mijini hasa kuna dhuluma nyingi, maskini wanadhulumiwa, yatima na wale wajane wananyang'anywa ardhi na majengo yao. Tunajua baadhi ya wafanyakazi wa ardhi wasio waaminifu

wanashirikiana. Kwa hiyo, moja ya kazi yangu kubwa na Wizara yangu ni kuhakikisha kwamba tunashirikiana ili kuhakikisha tunatokomeza udhalimu huu unaoendelea.

Mheshimiwa Spika, pia tutashirikiana na wananchi wengine na Wizara ya Maliasili na TAMISEMI kuhakikisha tunakaa pamoja, kuhakikisha tunasuluhisha hii migogoro ya ardhi ya vijiji iliyopo, katika maeneo mbalimbali ya Mikoa, inayohusu maeneo ya maliasili na Vijiji.

Mheshimiwa Spika, yaliyosemwa ni mengi siwezi kusema yote, lakini niseme tena kwamba kama mlivyosema migogoro ni mingi. Wanaosababisha migogoro ni watu. Kwa hiyo, tushirikiane na nimeamua sasa badala ya wale watu kuja Dar-es-Salaam kumfuata Waziri na Wataalam Makamishna, sasa nitakuja Mikoani. Nitapanga ratiba, nitakuja huko huko kila Mkoa na wataalam wangu wote muhimu wenye uwezo wa kuamua, ili tuje tutatue migogoro huko huko kwenye *site*. Ile ambayo ipo ndani ya uwezo wetu tutaitatua palepale, ile ambayo itahitaji kutoa majibu ya muda mfupi tutaitolea majibu, naombeni ushirikiano wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Waziri wa Utalii, atafuatiwa na Waziri wa Mifugo.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nami nachukua nafasi hii kwanza kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii, kuweza kuchangia mada iliyo mbele yetu. Aidha, nachukua nafasi hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, kwa taarifa yake iliyowasilishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nichukue tu nusu dakika kuelezea masikitiko yangu makubwa. Siku ya jana nilimtembelea Mzee Kimaro ambaye alifiwa na mtoto wake George. George aliajiriwa Mwezi wa Tisa katika ajira mpya ambazo tulizitoa na alipokuwa katika siku ya kawaida yeye na mwenzake

anaitwa Anthony, walikuwa wamekwenda katika kijiji cha Namonge, nje kidogo ya Hifadhi ya Kigosi, wananchi waliwavamia, waliwapiga kwa mawe, mmoja mmoja mpaka wakafa. Kitendo hiki cha chuki dhidi ya Maaskari wa Wanyamapori kinadhoofisha sana uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii tu kuwaomba, nimeona picha na mwili wa yule kijana. Niwaombe tu wananchi, kama Tanzania yenye upendo na ninayoifahamu, basi tuangalie Maaskari hawa wote wanaotulinda, wanaolinda rasilimali zetu, tuwaangalie kwa jicho la huruma. Jeshi la Polisi wakishikiriana na Maaskari wetu, wanaendelea na msako mkali.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Waziri wa Mambo ya Ndani, kwa sababu mpaka sasa hivi watu 15 wameshakamatwa na ni matumaini yangu kwamba wale wote waliohusika watakamatwa na kufikishwa katika vyombo vya haki ili tuwape morali Maaskari wanaopigana kuilinda nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kwanza na kujibu hoja ya tozo. Nimekubaliana na Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba kama *schedule* ya majibu haitatosha kutokana na muda, tumeandaa majibu ya kila Mbunge na kila hoja na yale ya Kamati, ambayo tungependa kuwagawia Waheshimiwa Wabunge wakati wowote baada ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa tangazo la Serikali namba 50 la mwaka 2002, kipengele chake cha (m) kilitoa maelekezo kwamba, ulipwaji wa tozo ya kitanda, inayojulikana kama *concession fee*, ulielekezwa kama ifuatavyo na nanukuu.

"*Fees of 10 percent per person, on half board, bed, breakfast and meal, shall be payable by the owner or proprietor of the hotel, lodge, in respect of each person who lodges or stays in such a hotel or lodge*"

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwaka 2007 na hii ndiyo muhimu sana watu wafahamu *chronology* ya hili jambo lililofikia mpaka sasa hivi. Tozo za kitanda zilikuwa zikilipwa kwa *TANAPA* kama ilivyokuwa imeainishwa kwa *GN* namba 50 ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007, Wizara ya Maliasili na Utalii baada ya kupokea maombi kutoka *Board of Trustees* ya *TANAPA,* ilikubali kuridhia kiwango cha tozo ya kitanda, itozwe kwa mfumo wa *fixed rate*. Hatua hii ililenga kuziba mianya ya baadhi ya wenye mahoteli, ambao wanakwepa kulipa kodi ya Serikali, kwa ku-*under declare*, kwa ku-*declare* kiwango kidogo cha mapato wanayoyapata na hivyo kuiibia Serikali.

Mheshimiwa Spika, mfululizo wa mambo ulikuwa kama ifuatavyo:-

Tarehe 20 Julai, 2007, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, alitoa barua ikiamuru tarehe hiyo 20 Julai, kuwa ndiyo tarehe ya kuanza kutoza tozo hiyo ya *fixed rate*.

Mheshimiwa Spika, tarehe 8 Novemba, 2007, Katibu Mkuu wa Maliasili na Utalii aliandika barua nyingine,. ambayo iliahirisha au ku-*suspend fixed rates*, baada ya malalamiko kutoka kwa wadau, juu ya *formula* iliyotumika kupanga viwango hivyo kwani vilikuwa tofauti na havikufuata matakwa ya *GN* namba 50, ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, tarehe 7 Agosti, 2008, mwaka mmoja baadaye! Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii aliandika barua nyingine, ambayo sasa barua hii, iliahirisha kabisa tarehe ya kuanza kulipwa kwa tozo hiyo na hiyo inajulikana kama *effective date* ya kuanza kulipa tozo ambayo ilikadiriwa kuwa ya *fixed rate*.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Shamsa Mwangunga, aliunda Kamati ya Kitaifa, iliyohusisha baadhi ya Wajumbe wa Bodi ya

TANAPA, Wawekezaji kutoka *TCT, Hotel Association of Tanzania,* chini ya ushauri ya kampuni ya kisheria ya *REX Attorneys* na mimi nikiwa kama Mwenyekiti wa ile Tume au Kamati ya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii ilipewa kazi ya kutafuta njia bora zaidi na za wazi za kutekeleza tozo hiyo kwa misingi ya *GN* ya namba 50 ya 2002. Makubaliano yalifikiwa na yalitiwa sahihi, tarehe 27 Oktoba, 2010 na makubaliano hayo yalisainiwa na vielelezo vyote nimeviweka kati ya *AG* wa *TANAPA, HAT, CTC,* Wanasheria wa *TANAPA* na Mwenyekiti wa Kamati, kwamba wenye Mahoteli wote na wenye *Lodges* wote, walitakiwa sasa ni sharti wakaguliwe na *TANAPA* kila mwezi, kuonesha kwa uwazi mapato wanayoyapata ili waweze ku-*declare* mapato ambayo lazima Serikali iyapate.

Pili, hoteli na *lodges* zote zilipaswa zilipe kodi kwa mfumo mmoja na ulio wazi. Tatu, wadanganyifu wote walipaswa kuchukuliwa hatua na kamati ya pamoja.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, tarehe 29 Aprili, 2013 na hii ni miaka mitatu baadaye, Waziri wa Maliasili na Utalii alivunja hiyo *flexible rate* na kuamuru *fixed rate* ya mwanzo kabisa iamuriwe na ndipo ambapo kesi iliyokuwa Mahakamani na ambayo Wabunge wamei-*refer* ikaanza.

Mheshimiwa Spika, katika hukumu yake na bila kurejea mfululizo mzima wa kesi, Jaji J Mugasha, aliamuru yafuatayo:- kwamba katika ukurasa wa 13 ya Hukumu ya Jaji, na nanukuu.

*"In the premises the new concession rate is illegal and the valid rate is the one specified in the first schedule namely 10 percent percent per person, on half board and breakfast and meal"*

Jaji akiwalaani Mawakili na Wanasheria wa *TANAPA* kwa kushindwa kuishauri Serikali, ku-*gazzette fixed rates* kwa kipindi cha miaka minane. Waheshimiwa Wabunge wanapozungumzia *loss* ya fedha iliyotokana, ni kwa sababu

ile *fixed rate* haikuwa *gazzetted* kwa kipindi cha miaka nane. Ndiyo maana kile kipindi cha miaka nane isingekuwa *implemented,* kwa sababu haikuwa sehemu ya kisheria kuchaji hizo kodi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jaji vile vile alisema kwamba *the legal concession fee is that payable under the National Parks Regulation GN 50 of 2002,* lakini cha muhimu sana alichokisema, ambacho nataka nifanye na *reference* na Mheshimiwa Zitto alikisema; *" The revised concession fees must be gazzetted by the Ministry of Natural Resources and Tourism to be effective"* na alisisitiza kwamba tozo hiyo iwe *gazetted* mara moja.

Mheshimiwa Spika, baada ya *ruling* hii, Waziri wa Maliasili na Utalii ambaye ni mimi hapa, nilitoa maagizo yafuatayo:-

(1) Kufikia Desemba 31 na wala sio Januari, 2014, niliagiza kwamba *GN* iwe imekamilika na dokezo hilo ni dokezo namba tatu, ambalo ni katika baadhi ya wasilisho ambazo nitaziweka mezani kwako.

(2) Ukokotoaji wa *fixed rates*, uzingatie…

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri nilisema dakika kumi, maana yake *the way you are conducting the discussion* niliona tu hutamaliza. Kwa hiyo, dakika kumi zimekwisha. Naendelea na Waziri mwingine.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika!

**SPIKA:** Aaah msinipotezee muda sasa Waziri wa Mifugo!

**WAZIRI WA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, aHsante sana kwa kunipa nafasi…

**SPIKA:** Wengine wa-*note* ni dakika kumi. Dakika kumi *is nothing* kama hujajipanga vizuri.

**WAZIRI WA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kujibu hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge, wameelekeza katika Wizara yangu ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji safari hii taarifa yao ilijikita zaidi katika miradi ambayo inatekelezwa na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Wizara ya Maji, wakati ujao watatembelea zaidi katika miradi inayosimamiwa na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Kwa hiyo, kuna mambo machache tu ambayo nataka nijikite katika kujibu hoja hizo.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ni ya Mheshimiwa Mbunge wa Mafia, Abdulkarim Shah. Kulikuwa na ahadi, ambayo niliifanya mimi mwenyewe nilipotembelea huko tarehe 22 Oktoba, 2014 na namshukuru kwanza kwa kunipokea na kunitembeza vizuri. Kwa mara ya kwanza, nilipanda boti, nikaenda katikati kabisa kwenye maji marefu huko, nikawa na mashaka sana kwa sababu sijawahi kwa kweli kuingia ndani ya maji namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, lengo lilikuwa ni kuangalia, jinsi ambavyo uvuvi haramu kwa kutumia sumu na baruti, inavyofanya kazi mbaya sana ndani ya bahari. Nilikutana na huyu Mzee ambaye alikuwa ni mvuvi wa kutumia nyavu ambazo hazikubaliki, amekuwa bingwa kwa muda mrefu, wananchi walimsifia sana, lakini baadaye ni kama aliokoka akaachana na kazi hiyo kabisa na akasalimisha nyavu zake.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nilimfurahia sana, nikampongeza, nikasema kiasi hiki cha fedha cha shilingi milioni nne, tutampa ili aweze kufanya chochote anachotaka, tulitaka kumtia motisha ili asiendelee na kazi hiyo. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba ifikapo ijumaa njoo uchukue *cheque* yako, mpelekee Mzee huyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limezungumzwa, ni kuainisha mipaka ya maeneo ya mazalia ya samaki katika Ziwa Rukwa. Jambo hili lilizungumzwa na Mheshimiwa Ignas Malocha na ni kwamba eneo la mazalia ya samaki linaweza kuwekewa alama mbalimbali ikiwemo miamba, mimea iliyokaribu, au hata Maboya, ili kuweza kuwafanya wavuvi waweze kuona kwamba eneo hili haturuhusiwi kwenda na eneo hili tunaruhusiwa. Kwa hiyo, jambo hili tutaendelea kushirikiana na Halmashauri husika, kuwaelimisha wavuvi, ili wasiendelee kukamatwa, kwa sababu ya kutojua mipaka ambayo wanatakiwa wavue.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la Mheshimiwa Ignas Malocha, ni ubinafsishaji wa shamba la Malonje na nashukuru Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Lukuvi ameshazungumzia jambo hili, lakini nataka tu nikazie kwamba tarehe 10 Januari, 2015, Waziri wangu alitembelea shamba hilo na alitoa maelekezo kwa uongozi wa Serikali ya Mkoa, jinsi ya kutatua mgogoro huo. Ni mwezi uliopita tu! Kwa hiyo, tutaendelea kufuatilia kwamba Serikali ya Mkoa nayo wamependekeza nini katika kutatua jambo hili.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka nijielekeze, ni hoja ambayo ililetwa na Dkt. Dalaly Kafumu, Mbunge wa Igunga. Alizungumzia migogoro ya Wakulima na Wafugaji hasa katika Kijiji cha Isakamaliwa na eneo la Wembere. Nilitembelea eneo hili, nilikwenda kutuliza hiyo migogoro, lakini ukweli ni kwamba lazima, kama alivyosema yeye mwenyewe, eneo lile lazima lipimwe na upimaji huu, wa kujaribu kupima maeneo yote yenye migogoro, lilianzia sasa eneo la Wilaya ya Kiteto na nina hakika litaendelea katika maeneo mengine ambayo yamekuwa na migogoro ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, haya ndiyo maeneo yaligusa Wizara yangu. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante, umetumia vizuri muda. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Maji!

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, ili niweze kuzungumzia mambo machache ambayo yameongelewa kuhusu Sekta ya Kilimo kama ifuatavyo:-

Jambo moja kubwa lililozungumzwa hapa linahusu madeni ya wakulima, ambao mahindi yao yalichukuliwa na Wakala wa Chakula. Nilipenda kwa ufupi kusema tu kwamba, Bunge lako Tukufu liliweka bajeti ya sh. 142,234,333.9176 kwa ajili ya kununua tani laki mbili katika msimu uliopita, lakini kwa sababu, zao ni kubwa na wakulima wengi walileta mazao kwenye vituo vya Wakala, wakati fedha ambayo ilikusudiwa kulipwa ikawa haipo. Serikali ilifanya uamuzi kwamba haitakuwa busara kuwarudisha wakulima wale na mazao yao. Kwa hiyo, Serikali iliruhusu yachukuliwe, yahifadhiwe hatimaye zitafutwe fedha za kulipa wakulima hao.

Mheshimiwa Spika, sasa kazi iliyobakia ni kuwalipa na Mheshimiwa Malocha alikuwa anazungumzia jambo hili pamoja na Mheshimiwa Pauline Gekul ingawa katika *tone* tofauti, lakini nataka kusema tu kwamba tumeanza kazi ya kuwalipa wakulima na tutawalipa wote.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Gekul anasema tumepeleka bilioni 15 baada ya kuona Bunge, siyo kweli, tumezipeleka kwa sababu ndiyo zimepatikana, wala hakuna uhusiano wowote kati ya Bunge na kupatikana. Nataka niseme kwamba fedha zile zimeshasambazwa katika vituo vyote hazitoshi, lakini wiki inayokuja Serikali itasambaza shilingi bilioni 40 katika vituo kwa ajili ya kuwalipa wakulima. Kwa hiyo, tutaendelea mpaka itakapofika mwisho wa mwezi huu tutakuwa tumebakiwa na deni la shilingi bilioni 34 ambayo itamalizika wiki ya pili ya mwezi Machi, na tutakuwa tumeshawalipa wakulima wote wanaodai pesa zao.

Mheshimiwa Spika, nimekwenda Songea na nimerudi kutoka Songea jana, tumetazama zoezi la kuwalipa na tumetoa maelekezo kwambam tuwalipe hatua kwa hatuam tuanze na wadogo ambao ni wengi, halafu tunaenda hatua kwa hatua mpaka mkulima wa mwisho atakayekuwa anaidai

Serikali atakuwa amelipwa ifikapo mwezi kesho. Kwa hiyom hii nadhani inajibu hoja ya Mheshimiwa Pauline Gekul anauliza watalipwa lini na mengine aliyosema sitaki kuyasema sanam maana yeye anasema hamuwezim hamuwezi lakini hakuna ushahidi kama Mheshimiwa Gekul naye angepewa angeweza! Kwa hiyom haya mambo ni rahisi kulalamika zaidi kuliko kufanya kama ilivyo ngumu kujenga na rahisi kuvunja. Kwa hiyo, nafikiri tunaendelea tutamaliza tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Malocha alikuwa amezungumzia juu ya masoko na nataka kukubaliana naye. Unajua tatizo hili la masoko ni tatizo la mfumo tulipo-*liberalize* uchumi, tulikubaliana masoko ya mazao ya kilimo itakuwa ni suala la sekta binafsi. Nadharia iliyokuwepo ni kwamba watu binafsi wageshindana, kwa hiyo, wakulima wangefaidika kutokana na mashindano ya watu binafsi wanaonunua.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba hakuna mashindano ya maana katika ununuzi wa mazao ya wakulima na kwa sababu hiyo kumekuwa na matatizo siyo katika zao hili la mahindi tu, hata mazao yale ambayo yana Bodi bado kuna matatizo ya kutokuwepo ushindani, kuna *monopoly* mahali pengine, mahali pengine makampuni yanashirikiana na kupanga bei mahali pengine. Kwa hiyo lipo tatizo katika jambo, lakini nadharia ya uchumi inasema mahali ambapo soko linashindwa, dola ina wajibu wa kuingia.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema kwamba tutajaribu kutazama mfumo wa soko kwa sasa kwa kutazama mambo mengi zaidi ambayo yapo, mojawapo ni *commodity exchange* ambayo inafanyiwa kazi, suala la stakabadhi ghalani na vile vile tutatazama uwezekano wa kuanzisha shirika na nafaka na mazao mchanganyiko na lenyewe liingie sokoni ili mahali ambapo sekta binafsi imefeli basi Serikali au kupitia Shirika lake iweze kuingia.

Mheshimiwa Spika, nadhani wote tunajua *NFRA* si la biashara, ni la kuchukua mazao kwa ajili ya hifadhi ya chakula mahali kunapokuwa kuna matatizo, lakini hili lingine litafanya

biashara, linaweza kusagisha mahindi likauza unga, linaweza kusafirisha nje kama wanavyofanya watu binafsi. Kwa hiyo, mimi nadhani hii itasaidia katika kupunguza tatizo lililopo sasa hivi la ununuzi hasa katika nafaka kama mahindi na mpunga. Tutafanya hayo na naamini yatafanya msimu ujao uwe wa nafuu zaidi kuliko msimu uliopita.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limezungumzwa hapa na Mheshimiwa Kangi Lugola linahusu pembejeo za pamba. Nataka kumwambia Mheshimiwa Lugola kwamba na mimi ni Mbunge wa wakulima wa pamba, kwa hiyo kama Mbunge wa Bunda naelewa matatizo hayo na mengine nimekutana nayo katika sahani yangu kama Mbunge.

Hata hivyo, nataka kuwahakikishia wakulima wa pamba kwamba kabla ya mwisho wa mwezi huu, tutaitisha mkutano wa wadau wote wa pamba na Wabunge wote wanaotoka katika mikoa ya pamba nitaomba wahudhurie ili tutazame tatizo la zao la pamba, tutazame mfumo wa usambazaji pembejeo, masuala ya madawa, mbegu na kila kitu ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na msingi wa kuendelea mbele.

Mheshimiwa Spika, mengine ambayo yamesemwa sitaweza kuyasema yote kwa sababu Viwanda vya Korosho amesema ndugu yangu pale, tutakaa tutatazama namna ya kuboresha na kuleta ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, nakushukuru, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimwite Waziri wa Maji.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili kutoa maelezo mafupi kuhusu ripoti ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono sana pamoja na kuwapongeza na kuwashukuru Kamati hii kwa kufanya kazi

na sisi kwa karibu katika kupanga bajeti, katika kutembelea miradi na kusimamia utekelezaji wake. Nakubaliana na changamoto walizoziona hasa ile ya kutokupatikana kwa rasilimali ya utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Spika, katika hali hii imetuwia vigumu sana kuhakikisha kwamba miradi yote inakwenda kama tulivyokuwa tumetegemea. Mategeo yetu ni kwamba, tupate shilingi bilioni 244 kwa kipindi cha kwanza cha miezi sita lakini kwenye fedha hizo tumepata shilingi 100.7 na kati ya hizo bado shilingi bilioni 23 zipo kwenye mtandao na hazijaingia kwenye akaunti za walengwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo na kwa bajeti ambayo tumepata kama asilimia 16.2, tumepata mafanikio makubwa katika kutekeleza miradi hii kwa sababu katika kipindi hiki na bajeti ya mwaka uliopita miradi 498 imekamilika na watu milioni 4.9 wamefaidika na miradi ya maji. Miradi 740 bado inaendelea kutekelezwa na naamini kabisa kwamba sasa ni nusu mwaka bado tunayo miezi mitano mbele yetu na naamini kabisa kwamba fedha zitatoka na nataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu tukipata fedha hizi ambazo ziko kwenye bajeti, miradi yetu yote ambayo tunaitekeleza sasa tutaikamilisha.

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wetu kuendelea kuwahimiza wenzetu wa Fedha watufikirie kwa jicho la huruma na kuhakikisha kwamba wanatupatia rasilimali ya kuweza kutekeleza wajibu wetu.

Mheshimiwa Spika, sasa nijibu vitu vichache, kwanza katika Wilaya ya Mafia na Kisiwa cha Jibondo, Mheshimiwa Mbunge Abdulkarim Shah amezungumzia suala hili mara nyingi na amekuja ofisini kwangu, mwezi Januari mwaka huu shilingi 150 milioni zimetumwa katika kisiwa cha Mafia, kati ya hizo shilingi milioni 80 ni kwa ajili ya kununua mabomba na kufunga maji katika Kisiwa cha Jibondo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika miradi ya maji ya Wilaya ya Bunda, napenda kujibu baadhi ya hoja za Mheshimiwa

Lugola kwa kumtaarifu kwamba kati ya miradi tisa inayotekelezwa katika Wilaya ya Bunda, miradi minne pamoja na miradi iliyopo kwenye Jimbo la Mheshimiwa Lugola imekamilika na wananchi wanafaidika na huduma ya maji na miradi mingine mitano utekelezaji umezidi asilimia 50 bado tunategemea kuwapelekea shilingi 721 milioni kwa ajili ya kukamilisha miradi hiyo.

Mheshimiwa Lugola ameongea pia kuhusu mradi wa Mjini Bunda, mradi huo unagharimu shilingi bilioni 6.5 na tayari shilingi bilioni 4.27 zimeshatumwa na zimetumika, Mkandarasi yupo *site* amelaza bomba, kati ya kilomita 22 ameshalaza kilomita 20.5 na bomba toka *site* ya ku-*pump* maji mpaka kwenye *intake* kule ndani ya maji tayari limefungwa, *pump* tisa za ardhini za ku-*pump* maji zimeshafungwa, *submersible pump* ya kule kwenye *intake* tayari inaendelea kufungwa na leo walikuwa wanaendelea na kazi.

Mheshimiwa Spika, mabomba yote ya kupeleka maji kutoka kwenye *intake* mpaka kwenye matenki yote yameshafungwa, umeme umepelekwa kwenye *intake* pale *submersible pump* ilipo na kwenye *pump* zote tisa za ardhini na mradi ule wa kusambaza maji Mjini Bunda umeanza kutekelezwa, Mkandarasi anafanyakazi hiyo kuanzia Desemba mwaka jana na ataendelea na kukamilisha kazi mwezi Juni mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Lugola aliona kazi hiyo na bado akasema maneno aliyoyasema hapa asubuhi, nakuomba umsaidie kumpeleka hospitali anahitaji kupimwa. Wakati mwingine tukinyamaza siyo kama hatuna mdomo.

Mheshimiwa Spika, ngoja pia niseme maneno mawili kuhusu Mji wa Geita. Mji wa Geita maji yanatekelezwa kwa vipande vitatu vya kazi, kwanza wenye thamani ya dola milioni 9.7 unaotekelezwa kati ya Serikali na *GGM* na mradi huo ulioanza mwezi Mei, 2013 utakamilika mwezi ujao na watu 68,600 watafaidi. *Segment* ya pili ni mradi wa usambazaji maji wa dola bilioni 1.4, ujenzi ulianza Desemba mwaka jana na

utakamilika mwezi Juni mwaka huu, utaongeza upatikanaji wa maji kwa asilimia 35. *Segment* ya tatu ni mradi unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika ambapo dola za Kimarekani 4.13 zitaongeza upatikanaji wa maji safi na salama, dola 2.27 zitatumika kwa ajili ya shughuli za kuondoa maji taka na taka ngumu.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru pia Mheshimiwa Dkt. Dalaly Kafumu kwa kuongelea juu ya mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Tabora kwamba Serikali ya India imekubali kutupatia *line* ya *credit* nafuu ya dola za Kimarekani 268 milioni ambazo zitapeleka maji Nzega, Igunga, Tabora, Uyui, Sikonge na Urambo kama Msanifu ataona ni njia rahisi kuliko ile ya kutoa maji katika Mto Ugala.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kusema kuwa ni kweli kwamba kuna mradi kule Rungwe ambao unaitwa Masoko na umekuwa na matatizo ya utekelezaji, lakini Mkandarasi aliyekuwa ameteuliwa na Halmashauri ya Rungwe hakuwa Mkandarasi makini, hakuweza kazi yake na aliposimamishwa kazi ili kutafuta Mkandarasi mwingine kumekuwa na mabishano makali katika Halmashauri ya Rungwe, Madiwani wengine wakitaka aendelee kutekeleza na wengine wakitaka afutwe kazi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita Waziri wa Mazingira, nimetangaza kwamba mapendekezo yote yamesambazwa na ni juu yenu na ninyi Serikali kuyaona haya, siyo mje mgombane baadaye haiwezekani kumbe tumepitisha hapa muangalie haya wote mnayo na asiyekuwepo anyooshe mkono aweze kupewa.

Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Mazingira.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika!

**SPIKA:** Ngoja kwanza tumalize, nina utaratibu ninaoufanya.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naungana na wenzangu kuwashukuru sana Wenyeviti wa Kamati hizi mbili pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa kazi nzuri ya kutushauri katika sekta zetu. Naomba niahidi kwamba yale yote ambayo wamekuwa wakitushauri na ambayo wameyasema leo hii tutayazingatia na kuyatekeleza.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo mengi, niahidi kwamba yale ambayo yameongelewa na Waheshimiwa Wabunge tumeyasikia, tumeyachukua, tutaandaa kitabu cha majibu kwa undani zaidi kuonesha nini kinafanyika upande wa sekta ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla nataka niseme jambo moja nini tunafanya Ofisi ya Makamu wa Rais kuhusu suala zima la mazingira. Tumeandaa ripoti ya hali ya mazingira nchini. Hii ni ripoti ya pili; ripoti ya kwanza ilitolewa mwaka 2008, sasa kwenye ripoti hii tumeonesha uharibifu uliopo katika maeneo ya ardhi, tumeonesha uharibifu katika ukataji miti, tumeonesha tatizo kwenye upotevu wa bioanuai, tumeonesha uchafuzi wa mazingira, tumeonesha uharibifu wa ikolojia, kupungua kwa maji safi na salama na mabadiliko ya tabia nchi.

Mheshimiwa Spika, lengo letu katika ripoti hii ni kuonesha uharibifu halisi uliopo sasa hivi, hali halisi ya sasa kwenye eneo husika au sekta husika, athari za uharibifu huo, hatua zilizochukuliwa hadi sasa na mapendekezo kuhusu nini kichukuliwe kwenye sekta husika, lakini kubwa zaidi tumeonesha ni sekta zipi zichukue hatua gani kwenye eneo husika kama nilivyotaja.

Mheshimiwa Spika, imani yetu ni kwamba, kitabu hiki ambacho sasa hivi tunatengeneza nakala za kutosha

kuwaletea Waheshimiwa Wabunge na tutasambaza kwenye sekta zote, kitasaidia sekta mbalimbali kufanya maamuzi kwenye mipango ya kuainisha yale ambayo tumeyapendekeza kwa ajili ya kupambana na tatizo hili la mazingira katika maeneo mbalimbali. Kitabu hiki kitakuwa tayari tutakileta mwezi wa tatu kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo limeongelewa sana ni matumizi ya magogo kama nishati kwenye viwanda. Naomba kutoa taarifa rasmi kwamba msimamo wa Serikali yetu katika karne hii ya 21 tunaona kwamba matumizi ya nishati ya magogo imepitwa na wakati kwenye viwanda, tumeagiza viwanda vyote vianze kubadilisha viondokane na kutumia magogo vianze kutumia nishati nyingine mbadala. Mathalani Viwanda vya Nguo kama *Sunflag*, kwenye *boiler* moja wanatumia tani 25 kwa siku na pale wana ma-*boiler* manne maana yake wanatumia tani mia moja kwa siku.

Mheshimiwa Spika, hiki ni kiwango kikubwa sana ambacho hakiwezi kuvumilika na wote mnafahamu kutokana na mabadiliko ya tabianchi, misitu ni muhimu sana katika kukabili mabadiliko ya tabianchi kwa maana kwamba inafyonza ile hewa ukaa *carbondioxide*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nimwahidi Mheshimiwa Shah kwamba tunayo taarifa kwamba kuna kiwanda kinachozalisha umeme pale Mafia, kinatoa megawati moja, tutakitembelea, tutafanya tathmini ya athari kwa mazingira na tutashauriana na sekta zingine kama je, inafaa waendelee kutoa hiyo megawati moja kwa manufaa ya mazingira au vipi na tutatoa maamuzi baada ya kulifanya hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la tatu ni kuhusu miradi ya kuhimili na kukabili mabadiliko ya tabianchi ambayo inasimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais. Tunayo miradi katika Wilaya ya Pangani, Bagamoyo, Rufiji na pale Dar es Salaam na kule Zanzibar. Sasa kwa pale Pangani tunao mradi wa ujenzi wa ukuta ambao ukuta ule ulijengwa na Wajerumani miaka 100 iliyopita.

Mheshimiwa Spika, ni kweli mradi huu umechukua muda mrefu, lakini mradi huu uliibuliwa kama wazo mwaka 2009 na mwaka 2013 ndiyo umekubalika kuwa mradi kwenye taasisi zinazotoa fedha yaani *GEF (Global Environmental Facility)*. Kwa hiyo, tarehe 12 mwezi April, 2013 ndiyo ulisajiliwa na ukaanza kutekelezwa na mwaka jana mwezi wa tisa *base line study* ilikwisha kamilika kwa maana ya tathmini ya hali halisi ya mradi pamoja na mambo mengine yote ya takwimu na juzi tarehe 29 ndiyo umesainiwa na Katibu Mkuu kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Spika, mkataba huu ni wa Kimataifa, taasisi iliyopewa kusimamia ni *UNOPS, (UN Operation Program Services)* ndiyo wataanza ujenzi mara moja baada ya kusaini huu mkataba.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru na niendelee kuahidi kwamba yote ambayo mmetuagiza tutayatekeleza na tutayafanyia kazi na tutaleta majibu hapa Bungeni. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa vyovyote vile itabidi wakati ukifika nitumie Kanuni kuongeza muda, ambapo uwezo huo ninao kikanuni. Baada ya saa mbili kasoro robo nitaongeza nusu saa.

Wale wote wanaotaka kujibu wamejibu. Sasa nataka nianze na Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo. Lakini, tutakavyofanya ni kwamba mtoa hoja atatoa hayo maelezo kwa dakika zake hizo 30, halafu naomba asome maneno kama yalivyo kwenye *Order Paper*, akishasoma yale maneno naomba achukue nafasi pale kusudi tuweze kutoa ruhusa

kwa wale wanaotaka kufanya *amendment* katika mapendekezo yao.

Kama nilivyosema *extract* ya mapendekezo imeletwa. Kamati ya Mambo ya Kilimo bahati nzuri wame-*number* mapendekezo yao. Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira haiku-*number*. Kwa hiyo, baadaye ikifika kila mtu namwomba aandike namba moja, mbili, zile *bulleting* zipate *number,* kwa sababu vinginevyo itakuwa vigumu kuweza kuwasiliana.

Namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo!

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nianze kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuhitimisha taarifa ambayo tumeitoa leo hii, asubuhi.

Kwanza, nianze kwa kuwashukuru sana wote Waheshimiwa Wabunge waliochangia. Tulipata Wabunge 14, 11 wamechangia kwa kuzungumza na watatu wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu kuwatambua hawa ambao wamechangia. Kwanza ni Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah.

**SPIKA:** Naomba usiwatambue, tafadhali muda hautoshi.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Basi, vile vile nichukue nafasi ya kuwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri ambao wametoa maelezo ya kina katika maeneo yaliyokuwa yanawahusu juu ya mambo kadhaa.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwashukuru hawa Mawaziri kwa kuyaweka bayana baadhi ya mambo ambayo yalijadiliwa na Waheshimiwa Wabunge. La kwanza kabisa lilikuwa ni kuhusu uvuvi haramu ambao Naibu Waziri wa

Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ameyatolea maelezo na nimpongeze sana kumwahidi huyo mzee ambaye alitupa nyavu zake ambazo zilikuwa hazifai kwa shughuli za uvuvi na kwamba atalipwa hiyo shilingi milioni nne na amemwomba Mbunge wa Mafia ifikapo Ijumaa aweze kuchukua cheki hiyo.

Nishukuru vile vile kwa maelezo yaliyotolewa na Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kuhusu madeni ambayo wakulima wa mahindi wamekuwa wakiidai Serikali, kwamba hawa wakulima wanaidai Serikali jumla ya shilingi bilioni 89. Tayari Serikali imeshalipa bilioni 15 na imetueleza ifikapo katikati ya mwezi Machi kwamba wataweza kuwa wamewalipa hao wote.

Ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba utaratibu wa namna hii basi iwe tumejifunza na kwamba tusirudie tena kuwakopa wakulima kwa sababu athari zake zinakuwa kubwa zaidi kuliko tunavyofanya. Hivyo, wanaolipwa wakati huu na wanaolipwa mwezi ujao ni kwamba uwezo wao unakuwa umepungua na hawezi kutumia hizo fedha kama alivyokuwa amepanga mara ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, pili ni soko, inaonekana kwamba hatutajitayarisha kikamilifu juu ya upande wa masoko. Namshukuru Waziri kwa kuzungumzia juu ya *commodity exchange market* ambayo ingesaidia sana na kwamba katika utaratibu huo mara nyingi wakulima hawakopwi. Mkulima anayepata fedha ndiye yule anayenunua anachukua mazao hayo. Najua liko katika hatua mbalimbali ya utekelezaji ikiwa wanashirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika pamoja na Wizara ya Viwanda na Biashara. Jambo hili tuliomba liletwe Bungeni haraka ili kusudi liweze kupata Baraka ya Bunge.

Vile vile tatizo la shamba la Malonje ambalo Waziri wa Ardhi, Nyumba na Makazi ameitolea maelezo. Tatizo limekuwa la muda mrefu, nafikiri kwamba nalo hili linaingiliana, kuna upande wa unaogusa kilimo, kuna upande unaogusa ardhi kama ardhi tu. Lakini, ingekuwa vizuri kama

jambo hili nalo lingepata utatuzi na Waziri ameahidi kwamba atakwenda yeye mwenyewe afike huko kwenye *site* na aweze kuona nini kinaweza kufanyika.

Wengi wamechangia sana juu ya upande wa maji, wakizungumza kwamba juu ya fedha hazitoshi. Mheshimiwa Waziri ameeleza na yeye vile vile, ameliona hilo tatizo kwamba kati ya bilioni 488.8 ni bilioni 105 tu ambazo zimepatikana ambayo ni asilimia 21.6.

Tunaiomba Serikali tunapopitisha bajeti hapa Bungeni, Serikali ijitahidi kutimiza zile ahadi ambazo imezitoa kwa sababu tukitoka hapa na bajeti, Wabunge wengi wanakwenda kueleza maeneo yao kwamba mwaka huu tunategemea kutekeleza mradi huu, mradi huu na watu wanapata imani. Sasa bila kufanya hivyo, ni kwamba watu wanapoteza imani na Serikali yao. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali iweze kutekeleza haya.

Kumekuweko vile vile na ushauri kwamba kilimo cha umwagiliaji kipewe kipaumbele. Na hii hata *agency* yake, Wakala wa Umwagiliaji ilishaanzishwa. Lakini, kazi kamili inaonekana kwamba haijaanza. Tunaishauri Serikali na Wizara ifuatilie kwa karibu zaidi ili kusudi kilimo cha umwagiliaji kipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, ilikuwa imepangwa kwamba ifikapo mwaka huu Tanzania iwe na eneo la kumwagilia karibu hekta milioni moja, lakini sasa hivi eneo linalomwagiliwa ni hekta 450,000 tu. Hii ni sehemu ndogo sana, hatujafika hata nusu ya lengo ambalo lilikuwepo. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali na hususani kupitia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwamba hili liweze kutekelezwa ili kusudi tuweze kuwa na kilimo cha uhakika na hasa ukizingatia kwamba kuna hili tatizo kubwa la mabadiliko ya tabianchi. Hii ndiyo ingekuwa suluhisho peke yake ili kusudi watu wawe na uhakika wa chakula.

Mheshimiwa Spika, kumezungumzwa juu tatizo la maji Dar es Salaam, nafikiri Mheshimiwa Waziri hakupata

nafasi ya kuweza kuelezea zaidi, lakini hili nalo lina mambo mawili; moja ni ukosefu wa fedha. Lakini, vile vile mipango yake imeishapangwa, kuna mradi wa maji wa Ruvu Chini ambao karibu unakamilika na mradi wa maji wa Ruvu Juu nao karibu unaanza kutekelezwa. Tungeomba Serikali iipatie Wizara fedha za kutosha ili kusudi kazi hii iweze kuendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo hili tulilolizungua juu ya mkataba wa Mto Nile, watumiaji nchi 11, nchi mbili tu zimeshatia saini. Tunaishauri Serikali, kwa sababu ule waraka ulikuwa tayari, lile azimio, sasa naiomba Serikali katika vikao vya karibuni vinavyokuja hiyo iweze kufikishwa Bungeni na iweze kujadiliwa.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na matatizo mengine, yanayohusu Bodi za Maji. Kuna maeneo kama Babati ambako kumekuwa na Bodi za Maji ambazo zinahusisha zaidi ya miradi miwili au mitatu na hii imekuwa ikileta matatizo. Nimempa Mheshimiwa Waziri ili alitazame hili kwa makini ili kuona ni namna gani hilo linaweza kujibiwa.

Tatizo la kilimo cha pamba limezungumzwa sana ikiwa ni pamoja na mbegu ambazo hazioti. Hili tatizo limekuwepo kwa muda mrefu. Lakini namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika ambaye amesema ataitisha mkutano kwa wadau wote ili waweze kujadili jambo hili na kuona ni namna gani wanaweza kufanya.

Vile vile tunashauri kwamba Bodi ya Mazo Mchanganyiko haijaanza kufanya kazi. Kuna maghala mengi, kwa mfano, hata kule Iringa kuna iliyokuwa *National Milling Corporation,* kuna vinu vizuri vinafanya kazi, na mahindi hayo pale ingekuwa ni moja ya soko japokuwa haingekuwa ni kubwa sana, lakini ingeweza kusaidia wakulima kuweza kuuza pale kukatengezwa unga.

Mheshimiwa Spika, lakini, kwa siku za mbele tunapofikia kwenye tatizo kama hili, tunaishauri Serikali

iangalie uwezekano wa kutumia mahindi hayo hayo kuweza kukamua mafuta nay ale mabaki baada ya kukamua mafuta, unaweza kutengeneza chakula cha mifugo na ikaweza kusaidia zaidi.

Mheshimiwa Spika, maelezo mengi yameishatolewa na Mawaziri wanaohusika. Mimi niwashukuru tu wale ambao wamechangia katika hoja yetu na kuweza kuiboresha na najua Wizara husika zimsikia.

Kulikuwa na pendekezo la Mheshimiwa Zitto kwamba tuweke maoni ya jumla, lakini vile vile na mapendekeo, hilo limefanywa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naliomba Bunge lako sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. JUMA S. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante. Naomba Mheshimiwa ukae kidogo hapo tuendelee kidogo. Tuchukue ile karatasi ambayo Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji imewekwa, ukiangalia, Mapendekezo yao yako kwenye *page* ya pili mpaka ya tatu. Kwa hiyo mimi nawahoji.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*

*(Hoja ilitolewa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Kwa hiyo, Kamati hii tumeishamaliza, waliosema ndiyo wameshinda. Wewe Kamati yako imemaliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira! Naona sijui mbadala wake, Mheshimiwa kwa niaba ya Mwenyekiti! Haya!

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru sana Jehova kwa neema zake. Pili, nakushukuru wewe binafsi kwa jinsi unavyoendesha Bunge lako tukufu vizuri. Tatu, nawashukuru sana wapiga kura wangu wanawake wote wa Mkoa wa Mbeya. Lakini, vile vile namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati hii Mheshimiwa Lembeli kwa kuniamini ili niweze kufunga mjadala huu.

Mheshimiwa Spika, kwa fursa ya kipekee kabisa naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia, lakini kutokana na muda kuwa finyu nitaomba nisiyasome majina yao ingawa tunatambua michango yao yote yenye tija. Naomba tu niseme kwamba Wabunge waliochangia kwa maneno wako 15 na waliochangia kwa maandishi wako watano.

Mheshimiwa Spika, nikianza na Wizara ya Maliasili na Utalii. Mimi naomba niseme tu kwamba Wizara hii siyo siri, ina urasimu ambao sasa umekuwa ni ugonjwa.

Mheshimiwa Spika, sasa sijui nini kifanyike! Na hua tunashangaa kwa nini utaratibu huu wa *PPP* ambao unawahusisha wadau mbalimbali una-*base* upande mmoja tu wa wafanyabiashara kunufaika. Maana kuna hizi *WMA's* hatuelewi wananchi kila siku huwa wanalalamika.

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye Kamati yetu na hata Wabunge wengi hapa ukumbini wamesema pia, katika ule ukurasa wa 17, Wizara ya Maliasili na Utalii kuna nini?

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ilipokea taarifa kuhusu hukumu ya kesi, Mheshimiwa Waziri amesema kwa kirefu hapa, Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia. Hii hukumu ya kesi ilifunguliwa mwaka 2011 na baadhi ya wamiliki wa hoteli zilizoko ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro kutangaza tozo mpya ambayo hii tozo ni *fixed concession fee*.

Tangu Mahakama Kuu ya Kanda ya Arusha itoe hukumu ya Kesi Namba 25 ya mwaka 2011 ambapo Mahakama hiyo ilitupilia mbali kabisa makampuni yote 17 yenye mahoteli ndani ya Hifadhi za Taifa kupinga ongezeko hili la tozo.

Mheshimiwa Spika, hivyo Kamati hii, alichosema Mheshimiwa Zitto ni sahihi na ndiyo msimamo wa Kamati kutaka Serikali kwa maana ya kwamba Wizara itekeleze hili jambo mara moja. Haya yalikuwa ni maagizo ya Mahakama na Kamati ndicho ilichosema alichozungumza Mheshimiwa Zitto na ndiyo msimamo wa Kamati mpaka dakika hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niisome hiyo hukumu ya Mahakama Kuu, Kanda ya Arusha ambayo ni *revised version*. Na yenyewe maana, haya mabadiliko ya tozo za malazi zinaleta migogoro mingi na kuchafua taswira ya mabadiliko ya Serikali na za wawekezaji. Hapa chini nanukuu sehemu hiyo ya uamuzi wa Mahakama Kuu ukurasa wa 15 na wa 16 kama ifuatavyo:-

"*In view of the aforesaid, the Ministry of Natural Resources and Tourism, which is the parent to the defendant, should gazette the revised concession rates with immediate effects, so as to enable the defendant to collect concession fees and perform the obligations efficiently.*

*A continued stance of not gazzetting the revised concession rates is indeed against public policy and public interest which is paramount duty to a person entrusted and holding a public office which in this particular case includes the Minister responsible with Natural Resources and Tourism. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Kamati yetu imesikitishwa sana. Hiki kigugumizi cha Wizara hii kinatoka wapi? Kuanzia mwaka 2011 mpaka Septemba, 2014, Taasisi ya *TANAPA* na Ngorongoro mapato yao bilioni 80, mapato ya taifa yamepotea. Hadi hivi leo tarehe ya leo tunavyoongea

Bunge lako tukufu, Serikali kupitia *TANAPA* na Ngorongoro inapoteza bilioni 2 kila mwezi, zinapotea. Je, hii halali kweli kwa mapato ya taifa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania wengi na nchi yetu ni maskini, mahospitalini hakuna dawa, wagonjwa wanafariki, mashuleni hakuna vitendea kazi, watoto wanasoma chini, hakuna madawati, walimu wanapata mishahara midogo, kwa kweli hii haieleweki, haikubaliki na haitakiwi.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako ni muhimili unaoisimamia Serikali, sasa mimi nilikuwa naomba tu kuuliza kwa heshima na taadhima, hivi Kamati yako ya Bunge inatoa maelekezo na mwongozo kwa Serikali na Serikali inakaidi, nini hatima yake? Tunaomba tuambiwe, maana huu ni muhimili unaoisimamia Serikali, sasa unapotoa maelekezo na miongozo na Serikali inakaidi tunaomba utuambie nini hatima yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri sana Kamati hii inasimia Wizara tatu na kwa njia moja au nyingine Wizara hizi zinaingiliana. Nikija katika suala la Wizara ya Ardhi na Maliasili hapo, Hifadhi ya Saadani ilitangazwa na Serikali kuwa ni *National Park* mwaka wa 2005 pamoja na mipaka yake yote, lakini cha ajabu Wizara ya Ardhi mwaka 2008, miaka mitatu baada ya hifadhi hii kutangazwa ikatoa hati juu ya ardhi ambayo iko chini ya sheria nyingine.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii inasikitishwa sana na jinsi Serikali inavyofanya kazi. Taasisi moja ya Serikali, tena kwa jeuri kabisa inatoa hati juu ya ardhi ambayo inamilikiwa kisheria na taasisi nyingine pia ambayo nayo ni ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, hivi kipi bora; kilimo cha miwa na sukari, Mheshimiwa Dokta Kafumu pale amezungumza, Mjumbe mwenzangu wa Kamati, maana sukari inayozalishwa hapa nchini nyingi iko bado kwenye maghala. Hivyo, tunaitaka Serikali kuheshimu sheria iliyoanzishwa juu ya Hifadhi ya Taifa ya Saadani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi hapa wamezungumza matatizo mbalimbali juu ya ardhi. Ardhi imetelekezwa na imekuwa ni tatizo sugu hapa nchini. Mheshimiwa Amina Mwidau amesema, Mheshimiwa Malocha, Mheshimiwa Shah, Waheshimiwa wengi sana wamechangia tena wamezungumza kwa uchungu sana juu ya suala zima la ardhi. Hata mfano kule Mafia, lile Shamba la Utumaini ambalo sisi Wajumbe pia tuliweza kulitembelea na wengi hapa wanasema, limeuzwa kienyeji-enyeji tu bila mpangilio!

Mheshimiwa Spika, lakini mimi namshukuru sana Waziri wa Ardhi na naomba nisiseme sana juu ya hili kwa sababu amesema na ameahidi kwamba vyote, hati zote zitafutwa na Serikali iweze kuchukua hatua na wananchi waweze kupata faida kwa manufaa ya nchi. Kwa hiyo, tunafurahi sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi alivyosema hivyo na maadam ametuhakikishia, sisi kazi yetu kama Kamati itakuwa ni kuhakikisha yale aliyoahidi Mheshimiwa Waziri, je, yanatekelezwa ipasavyo kama alivyoahidi?

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kabla sijamaliza, kwa kweli, Shirika la Nyumba la Taifa linafanya kazi nzuri, kazi ya ziada. Mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shirika hili kwa kweli, pamoja na kwamba limekuwa likijenga nyumba nyingi za kipato cha chini, cha kati na cha juu, lakini limekuwa likitwishwa mzigo. Tunaishukuru sana Serikali kupitia Wizara ya Fedha kwamba wana mpango wa kuwaondolea *VAT* kwa bidhaa zile za ujenzi ama vifaa vya ujenzi vya kutoka nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, lakini kama Kamati tulikuwa tunaomba hivi vifaa vinavyozalishwa nchini pia, shirika liweze kuwaondolea *VAT* kwa sababu, inakuwa ni mzigo mkubwa sana. Na nimeangalia michango ya Waheshimiwa wengine ya maandishi kwamba, Shirika hili linatoza kodi zake kwa kiwango kikubwa sana, lakini vilevile ukiangalia mambo yote

yanayohusu maji, yanayohusu barabara, yanayohusu umeme ni mzigo kwa shirika, Serikali haiwasaidii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali kupitia Wizara ya Fedha, wajaribu kuangalia hivi vifaa vya ujenzi ambavyo vinazalishwa nchini kuwaondolea *VAT* Shirika la Nyumba, ili na wenyewe Shirika la Nyumba baada ya hapo watajaribu kupunguza kodi na wananchi watafaidika sana kwa Shirika lao la Nyumba kwa bei ambazo zitakuwa zinaridhisha.

Mheshimiwa Spika, naomba nisiongee sana, muda wangu ni mfupi, muda wangu ni mchache, lakini nikushukuru wewe binafsi tena kwa kunipa nafasi hii. Na vilevile naomba sasa Bunge lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, pamoja na Mapendekezo na Maoni yaliyomo kwenye Taarifa hii. Nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante. Kama nilivyowaomba Waheshimiwa Wabunge kwamba, ile *extract* ya mapendekezo ya Kamati wameweka *bulletins.* Sasa naomba kila mmoja wenu alipo, kila *bulletin* aipe namba kuanzia ya Kwanza mpaka… itakuwa *bulletin* mpaka ya 22. Nadhani mmeandika wote!

Mheshimiwa Zitto! Niliona ulisimama mara mbili kabla ya hapo?

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, ndiyo nilisimama! Mwanzo nilikuwa nataka nitoe taarifa ambayo bahati nzuri Mjumbe wa Kamati ameshaitoa kuelezea hukumu, kama jinsi ambavyo Mheshimiwa Waziri alivyokuwa anaeleza. Lakini pili, sasa naomba kwa sababu marekebisho haya tumeyapata humu ndani ya Bunge, kwa hiyo, taratibu zile za kawaida za kupeleka maoni kupitia ofisi ya Katibu na Mheshimiwa Spika, naomba uzi-*suspend* ili tuweze kutoa

mapendekezo yetu sasa hivi. Na ninaenda *bullet* namba 8 ambapo…

**SPIKA:** Ngoja kwanza! Nilikuwa nataka kuelewa yale uliyosimama, sio haya, hatujaanza kazi! Naomba ukae.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Sawa!

**SPIKA:** Kwa hiyo, naanza ukurasa wa kwanza, kuna mtu mwenye maoni ukurasa wa kwanza? Mheshimiwa Soni!

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, ahsante!

**SPIKA:** Hatu-*edit!* Tunaangalia tu maudhui yake, hatu-*edit.*

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kwenye hiyo, ya namba 4 na namba 5. Namba 4, kwenye eneo ambalo wamezungumzia suala la kurudisha eneo la Hifadhi ya Mkungunero; tunaomba na eneo lile la vijiji ambalo liko kwenye taarifa yao, vijiji ambavyo walivitaja vya Ayamango, Gedamar na Gidejabon, ambavyo viko Babati Vijijini na vyenyewe viongezwe humo ili lile eneo wale wananchi ambao sasa waliwekwa pale kisheria na *Operation Vijiji* kipindi hicho, wamekaa sasa wana karibu miaka 9 wanasubiri kufidiwa na kupewa eneo mbadala, basi na wao hilo eneo waendelee kupewa liwe ni halali yao.

**SPIKA:** Umesema *bulletin* namba 4?

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, namba 4.

**SPIKA:** Unaongeza nini?

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, kwamba, eneo kutoka lile eneo la hifadhi, lile eneo ambalo sasa lina mgogoro na Hifadhi ya Tarangire. Eneo la vijiji vya iliyochukuliwa kutoka vijiji vya Gadamar, Ayamango na Gidejabon liongezwe katika kipengele hicho, ili hili eneo liendelee kuwa la wananchi.

**SPIKA:** *Are you sure* unasemea eneo hili, maana pale hakuna kijiji kingine chochote?

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba yaani baada ya hapo tu, pawe na…

**SPIKA:** *Bulletin*, ume-*number* vizuri? Kuna *bullet* 1, 2, 3, 4, 5!

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba yaani baada ya hiyo ya 4, pawe na *bullet* mpya ya Namba 5 ambayo itataja vijiji hivyo na huo mpaka wa…

**SPIKA:** Wenzio wanasema *bullet* ya 3 inatosha!

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, naomba basi niiandike mara moja na kuileta, ili iwekwe yaani kimaandishi ikae vizuri hapo. Hata kama ni kwenye hiyo ya 3 inaweza kuingia hapo kwa sababu, ni jirani kabisa na hapo, basi iingie hapo.

**SPIKA:** Naomba na Serikali, mnasimama kuzungumza, sio kama wakisema wao ndio tuna- *endorse*.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu?

**MWONGOZO WA SPIKA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naona *concern* ya Mheshimiwa Mbunge katika ku-*address* matatizo yanayohusu mipaka ya vijiji na maeneo mbalimbali labda katika matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, sina uhakika sana kama azimio hili tutakapolipitisha…

**SPIKA:** Mapendekezo hayo!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, Mapendekezo haya tutakapoyapitisha yana-*reflect* vipi sheria ambazo labda mpaka sasa zipo zinazoongoza maeneo hayo ambayo tunayo.

Mheshimiwa Spika, sasa nilichokuwa naomba tu ni Mwongozo wako; je, mapendekezo haya yanaagiza Serikali sasa ikatizame kwanza sheria zile ambazo ndizo zinazoongoza maeneo haya ama ndio maagizo ya kiutekelezaji baada ya mazimio haya? Sasa hicho kinachoazimiwa ndicho kinachoenda kuwa ama kufanyiwa kazi?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuna masuala mengi yanayotakiwa kufuata sheria kama ya kodi na mambo mengine. Kwa hiyo, nilikuwa naomba mwongozo wako kusudi sisi kama Serikali, maazimio haya yanapopitishwa na sisi tuwe tunajua nini hasa tunachokipitisha na sisi wajibu wetu ni kufanya nini na hasa katika masuala ambayo yanaingiliana kisheria?

**SPIKA:** Mheshimiwa, kama umenisikia vizuri, ndio maana niliwataka Wenyeviti wasome, kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, pamoja na Mapendekezo na Maoni yaliyomo kwenye Taarifa hiyo! Haya sio maazimio! Haya ni mapendekezo.

Mapendekezo maana yake mnaweza kuyafanyia kazi mkakuta kwamba, kuna mikwaruzo fulani, mkarudi kusema kwamba, ahaa, pendekezo hilo tulishindwa kulitekeleza kwa sababu ya matatizo haya, ndio maana hayajakaa ki-maazimio, kwa hiyo, imekaa kimapendekezo ndio maana hii nikasema someni hivyo. Sasa kama Waheshimiwa Wabunge wanatoa, mnaweza ku-*react* pia kwamba, hii haiku hivi, lakini bado yanabakia haya ni mapendekezo sio maazimio.

Mheshimiwa Gekul?

Mheshimiwa Gekul, kidogo! Naomba ukae kidogo.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, tulichokuwa tunajadili hapa kinatokana na Taarifa ya Kamati hii. Na mapendekezo haya yanafafanua maelezo ya Kamati yenyewe yaliyopo ukurasa wa 12, kifungu cha 4.1.5 kuhusu mgogoro wa Mkungunero.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ukiyachukua kwa ujumla yaliyopo kwenye taarifa nzima yanazungumzia Vijiji vya Kimotoroko, Irkushoboro sijui na yaliyopo hapa. Sasa nina mashaka kwamba, hivyo vijiji anavyovitaja ni vipya kabisa havipo hata kwenye taarifa ya msingi iliyoletwa na taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, sasa tukisema kila mgogoro unaongezwa tu, mimi nilifikiri tungechukua vijiji hivi, hapa kimeandikwa kimoja, tungechukua vijiji vyote kama ambavyo taarifa ya Kamati ilivyoandika badala ya kuongeza vijiji ambavyo, havimo hata kwenye taarifa.

**SPIKA:** Na uzuri wa Kamati wamefika huko, na msidhani kama huu ndio mwisho wa safari ya kazi, bado kazi zipo, mtaendelea kufanya na wanaohusika wanafanya; tena nijibu na ile aliyosema Mheshimiwa Dokta Mwanjelwa, kama Serikali mliiagiza kitu mkakaa pamoja hamkuelewana, mnarudi kwa Spika, eeh! Sio mkishagombana huko mkashindana, basi mnaendelea; kama mmejadiliana kitu fulani na mkakubaliana na hawakutekeleza, mnarudi kwa Spika, ndio utaratibu ulivyo.

Ehee, Mheshimiwa Gekul?

Kwa hiyo, sio tunaongeza! Haya ni mapendekezo yao, hatuna nafasi ya kuongeza. Anasema sasa ipokee na kukubali Taarifa ya Kamati na Mapendekezo na Maoni yaliyo kwenye Taarifa hiyo.

Ehee, Mheshimiwa Gekul?

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Labda tu nimpe Taarifa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi kwamba, vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Jitu vipo kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, wakati wa mchango wangu nilizungumza kwamba, kwa sababu ni muda mrefu sasa miaka *almost* 9 hakuna ardhi mbadala, basi Serikali au Bunge tupendekeze kwamba, sasa maeneo yale ya Vijiji vya Gijedabon, Ayamango na Gedamar, ule mpaka sasa ubaki kwa wale wananchi kwa sababu ni miaka 9 ardhi mbadala hawapewi!

Mheshimiwa Spika, ipo kwenye taarifa yao na nikanukuu na ukurasa. Kwa hiyo, mimi nipendekeze…

**SPIKA:** Nukuu ukurasa! Ukurasa gani?

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 22.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa haraka Mheshimiwa Jitu asome!

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, ni Mgogoro wa Mpaka wa Hifadhi ya Tarangire, Ukurasa wa 12, *Bulletin 4.1.12* ambapo ndio ina taarifa nzima na mapendekezo yako hapo na sisi tunapendekeza tofauti na hayo, yaani eneo hilo mbadala kama Mheshimiwa Gekul alivyosema, halipo! Na wale wananchi waliwekwa pale kisheria na *Operation Vijiji*. Kwa hiyo, bado wanaendelea kuteseka pale na hawajahamishwa bado wako ndani ya eneo hilo, waendelee kuhalalishwa pale.

**SPIKA:** Ukurasa wa kwanza tunakwenda kama mapendekezo yalivyo hapa, hayo ya kwenu ni mapya, hayakubaliki.

Ukurasa wa pili? Kuna mtu kwenye ukurasa wa pili? Mheshimiwa Zitto, ukurasa wa pili?

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 2 ile *bullet* ya 2; Kamati inaitaka Wizara ya Maliasili na Utalii…

**SPIKA:** Umeandika kama 7? Maana tunataka tuwe tunaweka!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, itakuwa 7; Kamati inaitaka Wizara ya Maliasili na Utalii kutoa Tangazo katika Gazeti la Serikali mara moja ili viwango vipya vya tozo kwenye Mahoteli yaliyoko ndani ya Hifadhi za Taifa vianze kutumika. Naomba lisomeke kwamba, kutoa tangazo katika Gazeti la Serikali mara moja na kabla ya mwisho wa mwezi huu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nilitaka nimhakikishie kwanza Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati na Mheshimiwa Zitto kwamba, mchakato mzima wa sisi kukamilisha Tangazo hili la Serikali umefanyika kwa kasi. Na tatizo ambalo alilisema Jaji mwezi wa 9, akifanya *reference* ya kutokutangaza katika Tangazo la Serikali ilikuwa ni hatua mfululizo ya miaka 9, miaka 8 ya nyuma ambayo aliielezea. Na sisi baada ya kufika ofisini kwetu mwezi Oktoba, tumefanya mambo mawili ambayo nadhani ni muhimu sana Waheshimiwa Wabunge…

**SPIKA:** Mheshimiwa, naomba unielewe, tuko kwenye mapendekezo! Wewe unasema nini hilo? Alivyosema vile ndivyo, ama unasema nini?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nasema kwamba sisi tunakamilisha mchakato huo tarehe 15 mwezi wa Februari, na saa yoyote baada ya tarehe 15 tutalitangaza Tangazo la Serikali. Na nikasema vilevile kwamba, Tangazo ambalo lilikuwa ni *draft* la nyuma na hili ni muhimu sana, lilikuwa na *hotels* na *lodges* 27 wakati katika *TANAPA* nzima kulikuwa na *hotels* na *lodges* 30 ambazo zilikuwa zimeachwa nje ya hili Tangazo. Nimeagiza kwamba, zote 57 lazima ziingizwe kwa sababu, kama tutatoa tangazo linalohusisha *hotel* na *lodges* 27 peke yake, Serikali itakosa mapato kwa *hotels, lodges* na *tented camps* zingine 30, na

hizi zote kwa kuziweka zitakuwa zimeondoa mwanya kabisa wa kutokupata mapato ya Serikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunachokisema basi, kumbe pendekezo la Mheshimiwa Zitto linatosha. Na hiyo haichukui mamlaka ya Serikali kufanya kazi yake kama inavyostahili. Kwa hiyo, pendekezo alivyofanya Mheshimiwa Zitto ndio tutakalopitisha.

Ukurasa wa 3. Mheshimiwa Soni?

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. *Bulletin* ya 16, ile ambayo inasema Kamati inaishauri Serikali kwamba, uandaaji na utekelezaji wa mipango miji ufuate sheria za ardhi.

Mheshimiwa Spika, tukirudi kwenye ukurasa wa 4 kwamba, naomba pale tuongezee na sheria ile ya kulinda ardhi zinginezo kwa mfano za kilimo, mifugo, uvuvi na mengine, yote basi ile sheria ije haraka. Kwa sababu leo hii tunabadilisha matumizi ya ardhi kiholela na maeneo mengi haswa hizi za kilimo, mifugo na uvuvi zikibadilishwa matumizi ndio maana panatokea sasa migongano na hizi vurugu zote ambazo tunaziona sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba kwamba, hizo sheria tuliahidiwa siku nyingi na mpaka leo bado hazijaletwa. Kwa hiyo, tuongezee pale kwamba, sheria ya kulinda ardhi za kilimo, mifugo, uvuvi na mengineyo iletwe haraka.

**SPIKA:** Hii haiwezi kukubalika, sivyo walivyotaka wao! Walitaka mipango miji. Kwa hiyo, kuna mtu mwingine katika ukurasa wa 4? Ee, nani? Mheshimiwa Kessy! Mheshimiwa Kessy?

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, *bullet* ya 4…

**SPIKA:** Mheshimiwa Kessy, mko wawili mwingine akae!

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, *Bullet* 19 hapa…

**SPIKA:** Mheshimiwa! Vipi?

Mheshimiwa mwingine akae! Mheshimiwa Kessy, ndio ameitwa

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kessy ni ukurasa wa 4! Huu ni wa 3!

**SPIKA:** Ahaa! *Ok!* Ukurasa wa ngapi wewe?

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, wa 3.

**SPIKA:** Ukurasa wa 3, ndio?

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, ile *bullet* ya kwanza pale…

**SPIKA:** Ngoja, tulisema *mzi-renumber,* ukisema ya kwanza, unatuchanganya sisi!

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, ndio ya 11. Inasema Kamati inaishauri *TANAPA* na wananchi wa Kimotoroki wakae pamoja na wajadili jinsi gani watamaliza mgogoro huo.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa napendekeza sentensi iishie "huo", iwe *full stop* kwa sababu, tayari tumeshawashauri wao ndio watafute jinsi gani watamaliza mgogoro. Sasa tukiendelea na maneno yale tena, njia pekee iwe kuanzisha *Wildlife Management Area,* maana yake tunawakatalia tena wasikae pamoja ila sisi ndio tunawaambia sasa kwamba, njia pekee itakuwa kuanzisha hiyo *WMA.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naona kwamba, pale kama tumeamua sisi kwamba, wao

wenyewe ndio wakae na *TANAPA* watafute namna gani; basi iishie kwenye lile neno huo.

**SPIKA:** Sawa.

Mheshimiwa Mwanjelwa! Mheshimiwa Mwanjelwa, ndio pendekezo lenu! Kwani mlimaliza kazi, mbona bado?

**MHE. D.K.T MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikubaliane na marekebisho yake.

**SPIKA:** Haya, tunaenda ukurasa wa 4, Mheshimiwa Keissy!

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, namba 19, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha ione umuhimu wa kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa nyumba za shirika zinazojengwa kwa ajili ya kuuza kwa wananchi wa kipato cha chini na kati.

Mheshimiwa Spika, hii si kweli. Ni wachache watafaidika labda asilimia mbili au tatu ya nyumba zinazojengwa katika nchi hii. Nchi yetu ni wananchi wenyewe wanajenga majumba, sasa hawa wanaojenga watasamehewa na wenyewe *VAT,* hii itanufaisha wachache na tunasema Serikali yetu idhibiti kodi. Hii itakuwa ni njia moja ya kutorosha vifaa kwa ajili ya ujenzi wa majumba ya watu wachache wakaao mijini. Wakulima na wafugaji na wavuvi wanakaa vijijini hawa hawatanufaika na hiki kitu.

Mheshimiwa Spika, hii haiwezekani, hii ni ujanja wa kutaka kuiibia kodi Serikali yetu kwa watu wachache. Wananchi hii kweli kusema kweli wataandamana nchi nzima. *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mimi nilikuwa na hoja hiyo ya 19, lakini naanza na 18 halafu nitakwenda na hiyo ya 18. Kwenye ukurasa wa kwanza suala la kwenye 18 tumeambiwa kwamba Kamati inaishauri Serikali

kufuta kodi zote kwenye maeneo hayo kama magari, magreda, silaha, mavazi ya askari.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba tuongeze kwa mujibu wa taratibu, sheria na miongozo iliyopo. Kwa sababu tukisema tunafuta kodi zote kwenye magari, magari yanayokwenda kwenye uhifadhi yana *multi-use* yanaweza yakatumika kwingineko, magreda yanatumika kwingineko. Sasa lazima miongozo na sheria na taratibu zilizopo zifuatwe kuhakikisha kwamba kile kinachoingia kweli kinakwenda kutekeleza lile jambo ambalo tumetaka lifanywe. Na isitoshe kodi hizi zote ni kodi za *East Africa,* kwa hiyo sisi kama Serikali hatuwezi kwenda kama ambavyo inavyoishia hapa.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine hili la 19, Mheshimiwa Keissy amezungumza, lakini suala hili tumejadili sana wakati tunajadili Muswada wa Sheria ya *VAT,* tumejadili na tumeelewana na tulisema kwamba sisi Serikali tutaandaa utaratibu mzuri zaidi wa kuwawezesha kwa mfano wafanyakazi wetu wa kipato cha chini kuweza kupata *access* ama kuweza kupata unafuu wa vitu kama hivi. Sasa tukiandika hivi tutoe *VAT* kwenye Shirika la Nyumba, kwanza Muswada wetu wa Sheria ya *VAT* hau-*target institutions,* hiyo tumeondoa na ndiyo ilikuwa mantiki nzima ya kuleta Muswada wa Sheria hapa, tunakwenda ku-*target product* zenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili halitawezekana kufanyika, isipokuwa sisi tulitoa *commitment* kwamba tutaangalia utaratibu mzuri wa kuwawezesha sasa wananchi kuweza ku-*afford* nyumba kama hizi ambazo sio kwa shirika tu kwa sababu wako vile vile watu binafsi ambao wanajega nyumba za mkopo nafuu. Kwa hiyo, mimi naomba hii ibadilike lakini labda tutekeleze yale kama tulivyokuwa tumeahidi kwenye Sheria yetu ya *VAT*.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, kwanza *the writing* yenyewe ya pendekezo inaenda kinyume kabisa na mfumo mpya wa *VAT* kwa sababu Sheria ya *VAT* imefanya marekebisho ya namna gani ambavyo nafuu za namna hii

zinatolewa. Lakini pili, huwezi ukatoa msamaha wa *VAT* kwa shirika moja, kwa sababu siyo *National Housing* peke yake wanaojenga nyumba za gharama nafuu, *PSPF* wanajenga nyumba za gharama nafuu, *PPF* wanajenga nyumba za gharama nafuu, *NSSF* wanajenga nyumba za gharama nafuu.

Kwa hiyo ni mambo mawili; ama turekebishe hili pendekezo ili Kamati ishauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha ione umuhimu wa kuweka unafuu wa kodi katika ujenzi wa nyumba za gharama nafuu. Ikishawekwa hivyo, kwa hiyo, watu ambao wanafanya shughuli hiyo ya kujenga nyumba za gharama nafuu wanapata ile *access* ya moja kwa moja. Lakini kwa namna ambavyo pendekezo hili lilipo maana yake ni kwamba utapata nafuu kwa shirika moja peke yake. *(Makofi)*

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, na mimi nilitaka kuzungumzia hapo kwenye nyumba za *National Housing*. Ukiangalia kusudi la kujenga nyumba hizi tunasema ni kwa ajili ya gharama nafuu ili watu wasio na uwezo waweze kununua nyumba hizi.

Mheshimiwa Spika, ukipewa gharama za nyumba zikiwa na kodi na nyumba ikitolewa kodi, utaona kwamba watu ambao hawana uwezo, ambao wamekusudiwa ili nao waweze kununua hizi nyumba, hawatanunua tena na nafahamu kwa sababu zimejengwa Longido. Wananchi wanajaribu kuulizia, wakiambiwa bei, wanakimbia wanasema kwamba hizi haiwezekani ni nyumba za watu matajiri ndiyo wamejengewa hizi nyumba.

Mheshimiwa Spika, mimi nakubaliana na Mheshimiwa Zitto, kama kuna shirika lingine ambao wamejenga nyumba hizi, za aina hii kwa ajili ya kuwawezesha watu wasio na uwezo, nakubali ipunguzwe, wananchi waweze kununua. Lakini siyo vizuri nyumba hizo zikajengwa katika Wilaya zetu watu wengine kutoka Dar es Salaam, kutoka Moshi, kutoka maeneo mengine ndiyo wanakuja kuchukua katika ardhi ambayo Halmashauri zetu wametoa bila fidia ili wajengewe nyumba waone kwamba wanafaidi hizo nyumba.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba na naomba Wabunge wenzangu hizi nyumba isiwekwe kodi kabisa na kama zitawekwa ifutwe hii ya kusema kwamba kwa bei nafuu kwa sababu haitakuwa na unafuu tena.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu kodi namba 19, *VAT* kwa ajili ya vitu…

**SPIKA:** Si ndiyo hii ulikuwa unajadili, ndiyo uliyokuwa umeanza kujadili ndiyo hiyo 19.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, kuna *VAT* ya *Caterpillar* na hiyo hiyo18. Hii iliyosema ya *Caterpillar* pamoja na magari na vifaa vingine ni magari ambayo wamepewa *TANAPA* kwa msaada pamoja hata faru wameandikwa hapa ambao nao wanalipishwa *VAT,* faru ambao wamepewa *TANAPA* na Uingereza.

Sasa, Serikali ikipewa msaada halafu wanakuja tena kulipisha *VAT* kumwambia yule mfadhili ailipie *VAT* itakuwa ni jambo la ajabu kama umesaidiwa, halafu unamdai tena yule aliyekusaidia kwamba lipa *VAT,* haiwezekani, hiyo ndiyo inawanyima watu watusaidie na siyo kwamba inakwenda kwa shirika lingine inakwenda kwa shirika la umma.

Mheshimiwa Spika, nilitaka tu kuongezea haya.

**SPIKA:** Ndiyo maana Waziri amesema kwa mujibu wa sheria na taratibu. Mheshimiwa Mnyika! Mheshimiwa Mwanjelwa, unabakia utajibu.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira; na pendekezo hili Kamati inalirudia kila mwaka kwa sababu ahadi ya Serikali kuleta marekebisho ya sheria ili kuweza kupunguza mzigo wa gharama kubwa ya nyumba zinazoitwa za bei nafuu uweze kupungua, Serikali haiitekelezi. Kamati inarudiarudia kwa Shirika la Nyumba kwa sababu limekuwa mstari wa mbele katika ujenzi, na kama tutaanzia hapa maana yake mashirika mengine yatafuata.

Mheshimiwa Spika, lakini sasa kama tutatumia rai ambayo Mheshimiwa Waziri ameisema, napendekeza tuliboreshe hili azimio lisomeke:-

**SPIKA:** Pendekezo tu, sio azimio!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Pendekezo! Lisomeke:- "Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha ione umuhimu wa kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa nyumba za gharama nafuu zinazojengwa na mashirika ya umma kwa ajili ya kuuza kwa wananchi wa kipato cha chini."

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii hofu ya Serikali ya kwamba tusiwe na pendekezo linalogusa shirika moja peke yake la umma wakati kuna mashirika mengine itaondoka.

Mheshimiwa Spika, na umesema vizuri, kama Serikali inaona ugumu katika utekelezaji, Serikali itakuja sasa na pendekezo kwamba tumeshindwa kutimiza hili katika eneo hili kwa mashirika yote badala yake tumekuja na jambo hili mbadala. Lakini, kuacha bila azimio, kila mwaka tutarudi hapa, tutaimbiwa wimbo wa Serikali ikiahidi kwenda kupunguza mzigo wa bei kwa nyumba za gharama nafuu, lakini hakutakuwa na utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasisitiza tu kwamba safari hii tusiondoke bila azimio hapa. Kama Serikali haikubaliani na *wording* ya azimio hili, tupewe *wording* ya azimio hapa inayokubalika, tupitishe azimio hapa ili utekelezaji ufanyike.

**SPIKA:** Naomba, sio maazimio haya, haya ni mapendekezo. Waliosema mara moja hawasemi tena. Mheshimiwa Soni!

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, kwenye hili la *VAT* lilijadiliwa kwa undani kwenye Kamati ya Bajeti kwa kupitia Kamati zote na suala la *zero rating* kwenye sheria hii mpya tuliyopitisha haipo. Na utakapofanya *zero rating* ukiondoa hiyo kodi ya *VAT* ambayo tunataka ku-*charge,* ina

maana hata ile kodi ya *input tax* na *output tax* utayokusanya kwenye vifaa itaondoka, hizi nyumba zitapanda bei badala ya kuteremka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ukiondoa hii kodi, nyumba zitapanda bei kwa sababu kwenye nondo, *cement*, bati, ile yote ya *package* wakati *NHC* inanunua inaiweka kwenye *input tax,* inaondoka inakuwa *output tax balance* inayobaki, kwa hiyo, hizi nyumba zitapanda kodi kwa sababu ile wakati wanapodai ile *cement*, nondo na nini yote itaondoka, bei kwa ujumla itakuwa juu, hayo tulielimishwa vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuje na mfumo mwingine wa kuangalia namna ya kusaidia kama Mheshimiwa Waziri alivyoelekeza, lakini kwa hii sheria mpya, labda sasa Sheria hii ya *VAT* irudishwe tena hapa Bungeni, tuanze kuijadili upya ndiyo itakuwa na mabadiliko, lakini kutokana na hii sheria tuliyopitisha juzi haitawezekana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, mjadala huu una malengo mema tu. Lengo jema katika mjadala huu ni kusaidia tu Watanzania kuweza kupata makazi bora.

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Waziri wa Fedha, na naomba tu nichukue tu ushauri uliotolewa na Mheshimiwa Zitto Kabwe wakati akijenga hii hoja kwa kusaidiana na maneno yaliyozungumzwa na Mheshimiwa Jitu, haya mambo yote kwetu sisi kama Serikali yanaongozwa na sheria, lakini pia yanaongozwa na Katiba ya nchi yetu.

Sasa kama tutafikiri tu kwamba mapendekezo haya tunayoyatoa yanaweza kujibu matakwa hayo ya kimahitaji kwa wananchi wetu, nadhani sisi kama Serikali utaratibu wa kiutekelezaji unaweza ukatupa shida na tutatakiwa kurudi tena kuja kutoa taarifa, na tusingependa kurudi tena mara nyingi katika Bunge lako na kusema kwamba hayawezekani hayawezekani, ni boa tuwe tumeelewa na kuelimishana kama tunavyoelimishana hapa.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kifungu cha 138 cha Katiba ya Nchi kinatupa kabisa muongozo sisi kama Wabunge ni namna gani masuala yote yanayohusu kodi katika nchi yetu yatafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napenda kushauri ili na sisi Serikali tukapata nafasi nzuri ya kufanyia kazi haya, ni bora maazimio haya ama yakaondolewa ili sisi tukaweza kwenda kuyafanyia kazi vizuri ama azimio hilo linalohusiana… siyo azimio samahani, pendekezo linalohusiana na nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa likaondolewa ili tukapata nafasi nzuri ya kuweza kuona ni namna gani sekta hii ikaweza kuboreshwa kwa ujumla wake na kuwasaidia na kuwafaa Watanzania wote, siyo tu wanaokopa hizi nyumba hata wale wanaojenga vijijini na kadha wa kadha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nafikiri twende hivyo.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, sasa hatutaki kubishana. Mheshimiwa Mwanjelwa, ndiye uliyeleta hoja hii.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Tumesikiliza maelezo ya kutoka Serikalini, lakini kama Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa Mnyika na Mheshimiwa Lekule Laizer walivyosema, ile *concept* nzima ya kuwasaidia wananchi wa kipato cha chini na kuhakikisha kwamba hizi nyumba za gharama nafuu zinaondolewa *VAT* lilikuwa ni la msingi sana.

Mheshimiwa Spika, labda Mheshimiwa Waziri ambacho anaweza kusema na tukamuelewa na Watanzania wote hususan wananchi wa kipato cha chini ni kwamba, hili azimio siyo kwamba likataliwe, haya mapendekezo siyo azimio, samahani, kwamba twende tena turudi tujadiliane ni jinsi gani ya kuliweka vizuri, lakini vile vile naomba nikubaliane na masahihisho ambayo wenzangu wameyasema kwamba lisomeke kama ifuatavyo:-

Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha ione umuhimu wa kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* kwa mashirika yote ya umma yanayojenga nyumba za gharama nafuu kwa wananchi wa kipato cha chini" Naomba kuwasilisha. Ahsante.

**SPIKA:** Tusiendelee kubishana. Kwa mujibu wa taratibu zetu mambo yanayohusu fedha hasa katikati ya safari ni vizuri yakafanyiwe kazi na ziko Kamati nyingi, iko Kamati ya Bajeti, iko Kamati ya *Finance*, ipo Wizara yenyewe.

Ukiangalia mapendekezo ya Kamati hii ni mengi mno halafu yapo tu jumla jumla, siamini kama yalifanyiwa kazi ipasavyo. Kwa hiyo, naagiza pendekezo namba 18 na 19 kwa sasa hivi yaendelee kufanyiwa kazi na Kamati inayohusika wakishirikiana na Kamati nyingine na kuangalia sheria zinazohusika, maana tunaweza tukafanya kosa moja kubwa kabisa hapa likawa kubwa kuliko tunavyotegemea.

Kwa hiyo, baada ya kusema hivyo sasa nawahoji.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira Katika kipindi cha Januari, 2015 Ilipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Kwa hiyo mapendekezo ya Kamati tumeyapitisha kasoro *bulletin* 18 na 19, Kamati iendelee kufanya kazi na kufanya utafiti zaidi kuliko huu waliofikisha.

Waheshimiwa Wabunge sina matangazo mengine. Kwa hiyo naahirisha kikao cha Bunge…

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, ningeomba mwongozo wako!

Mapema tumemaliza kupitisha mapendekezo yanayohusiana na Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, sikulisema hili wakati wa kupitishwa kwa mapendekezo kwa sababu ingekuwa ni nje ya maudhui ya mapendekezo. Lakini sasa hivi tunavyozungumza, Dar es Salaam ina matatizo makubwa sana ya maji ambayo yamekuwepo kwa takribani wiki mbili sasa.

Mheshimiwa Spika, uliombwa mwongozo hapa na Serikali ikaahidi katika Mkutano wa Bunge uliopita kwamba, kwenye Mkutano huu wa Bunge iliunda Kamati ya Uchunguzi juu ya kujirudiarudia kwa mara kwa mara kwa matatizo ya maji kwa mtambo wa Ruvu Juu na kwa upande wa Ruvu Chini na Serikali ikasema tayari uchunguzi umekamilika na ikaahidi kwamba taarifa ingeletwa Bungeni katika Mkutano huu.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kuwa matatizo yamejirudia tena, ningeomba mwongozo wako, ni lini hasa Serikali italeta taarifa Bungeni kufuatia uchunguzi uliofanywa juu ya kujirudiarudia kwa matatizo ya maji katika maeneo yanayohudumiwa na mtambo wa Ruvu Juu.

Kwa hiyo, ningeomba mwongozo wako ili jambo hili litekelezeke kwa sababu Serikali iliahidi kuleta kwenye Mkutano huu wa Bunge na matatizo yamerudia ambayo yana sura ya dharura hivi sasa ninavyozungumza.

**SPIKA:** Kwa mujibu wa Kanuni sina sababu ya kujibu kitu ambacho bado sijakielewa. Kwa hiyo, watakueleza wakati mwingine. Kwa hiyo naahirisha kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.56 Usiku Bunge Liliahirishwa Hadi Siku ya Jumanne Tarehe 3 Februari, 2015 Saa Tatu Asubuhi)*